Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Thealathini na Sita – Tarehe 29 Julai, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 328

**Kupandisha Hadhi Kituo cha Afya Mlandizi**

**MHE. ABUU H. JUMAA** aliuliza:-

Kituo cha Afya Mlandizi licha ya kuhudumia wananchi wa wilaya, vijiji na wilaya za jirani pia kimebeba jukumu kubwa zaidi ya uwezo wake la kuhudumia watu wanaopata ajali mbalimbali katika barabara kuu ya Morogoro.

Na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni zake za uchaguzi mkuu wa 2010 aliliona jukumu hilo na kuahidi kituo hicho kipandishwe hadhi na kuwa hospitali ili kiweze kuhudumia watu kulingana na ukubwa wa kazi waliyonayo.

Je ahadi hiyo itatekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha afya cha Mlandizi kilichopo kwenye Halmashauri ya wilaya ya Kibaha, kilianza kama Zahanati kwenye miaka ya 60. Kituo hiki kinatoa huduma za wananchi zaidi ya 71,088 wa wilaya ya Kibaha pamoja na wananchi wa maeneo ya jirani ya vijiji vya Halmashauri ya Mji wa Kibaha pamoja na Bagamoyo na kuhudumia wahanga wa ajali za barabara yaani barabara kuu inayotoka Dar es Salaam kwenda Morogoro. Aidha, kituo hupokea wagonjwa wa rufaa kutoka zahanati 23 zilizoko wilayani. Kituo kina vitengo mbalimbali vya huduma kama vile vitengo vya wagonjwa wa nje yaani OPD, tiba afya ya uzazi na mtoto, maabara, kitengo cha macho, kinywa na meno, ushauri nasaha na upimaji wa hiari wa maambukizi ya VVU, kifua kikuu na ukoma. Kituo kina watumishi wapatao 56 wa kada mbalimbali. Idadi hii inazidi mahitaji ya watumishi wa vituo vya afya ambayo ni 29.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia ahadi ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 5 Oktoba, 2009 Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kupitia Kamati ya Huduma za Jamii ilijadili na kuamua kuwa kituo cha afya cha Mlandizi kipandishwe hadhi kuwa hospitali ya wilaya. Maombi ya kupandisha kituo hicho yamewasilishwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa hatua zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abuu ameridhika, swali la nyongeza Mheshimiwa.

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yamenipa matumaini makubwa lakini pia maswali ya nyongeza.

Kwa kuwa kituo hiki kinafanya kazi na kutoa huduma nje ya malengo yake na ikiwa uwezo wake ni mdogo na kwa kuwa ahadi hii ya Mheshimiwa Rais na kwa kuwa Naibu Waziri anakiri kwamba maombi yetu tayari yalishakuwa katika Wizara yake. Je, ni lini sasa ahadi hii ya Mheshimiwa itatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, anachosema Mheshimiwa Jumaa ni sahihi. Eneo hili tunalozungumzia hapa pamoja na kwamba liko karibu na Tumbi hospitali ambayo ndiyo inaangalia hao wahanga wa ajali mbalimbali.

Lakini bado kituo hiki anachosema kimeshalemewa, ni kweli na hivi tunavyozungumza ukishapita tu pale kwenye kambale yaani unapita unatoka Dar es Salaam unakwenda wewe Morogoro, ukipita kwenye lile daraja kubwa pale ukienda pale ni Bagamoyo, lakini wale wote wanahudumiwa na kituo hiki hiki anachokizungumza. Ukitoka hapo ukienda kidogo Kibaha kule tayari umeshaingia tena kwenye eneo lingine ni nje ya hii. Na nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji hili jambo linalozungumzwa hapa ni kweli tusipowasaidia wenzetu kituo kile kimelemewa.

Lakini *issue* hapa ni kwamba kituo hiki sasa kimekubalika kwamba kiwe hospitali ya Wilaya. Na *in addition to that* kuna maelekezo ya Mheshimiwa Rais yanayosema kwamba tujenge, wameomba maombi maalum ya shilingi 800. Nimefuatilia tumekwenda mpaka tumepanda kwa Mheshimiwa Mustafa Mkulo, tumekuta mpaka sasa hivi hawakupata kiasi chochote pale.

Nimemwahidi mkurugenzi Mtendaji pamoja na TAMISEMI, kwamba tutafuatilia hizi hela na Serikali ipo hapa inasikia tukisema hivyo, ili tupate angalau hizo milioni 800 zikishapatikana tuweze kufanya kazi ambayo imeagizwa na Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba hospitali hii inakuwa hospitali ya wilaya badala ya kuwa ni kituo. Niombe nichukue nafasi kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyofuatilia jambo hili.

Na. 330

**Mashirika yanayosaidia Katika Janga la UKIMWI Nchini**

**MHE. AMINA C. ANDREW (K.n.y. MHE. MARIAM R. KASEMBE)** aliuliza:-

Yapo Mashirika ya nje yanayosaidia kutoa msaada kwa nchi yetu kupambana na janga la UKIMWI:-

(a) Je, Mashirika hayo ni mangapi na yapi na yanatoa msaada gani?

(b) Je, hali ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI nchini ikoje, sasa kitakwimu?

**NAIBU SPIKA:** Tutalirudia tuendelee, Mheshimiwa majibu ya swali hilo, tutalirudia lile lingine kwa makosa tu bahati mbaya.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jumla ya Mashirika ya nje 16, ambayo yapo nchini kusaidia katika vita dhidi ya UKIMWI. Mashirika hayo ni Elizabeth Glacer *Pediatric AIDS Foundation (EGPAF), International Centre for AIDS Program (ICAP), Department of Defence (DOD*), yaani *water reeds, Family Health International (FHI), Pharmacies International Foundation (PAI), Clinton Health Access Initiative (CHAI),* Engenderhealth, *JHPIEGO, MDH, AIDS Relief, Baylor* Tanzania, *AFRICARE, AMREF, PATHFINDER, MILDMAY* na *Supply Chain Management System (SCMS).*

Mashirika haya hutoa misaada ya fedha na kiufundi katika kutekeleza afua mbalimbali zinazolenga kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI yaani VVU, na kutoa huduma kwa wale ambao wanaishi na VVU.

Baadhi ya afua zinazotekelezwa ni pamoja na uzuiaji wa maambukizi ya VVU, kutoka kwa mama kwenda mtoto *(PMTCT),* huduma na ushauri nasaha na upimaji VVU, kuelimisha jamii katika masuala mbalimbali ya UKIMWI, huduma za maabara, matibabu ya magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya ngono, kusambaza kondomu na kutoa huduma ya tohara kwa wanaume.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti ya taifa ya tafiti ya viashiria vya VVU na malaria ya mwaka 2008 yaani *Tanzania HIV* and Malaria *indicator survey* inaonyesha hali ya maambukizi ya VVU kwa ujumla ni asilinia 5.7. Hali ya maambukizi inatofautiana miongoni mwa watu katika makundi tofauti. Mathalani, maambukizi yako zaidi kwa wanawake asilimia 6.8 kuliko wanaume ambao ni asilimia 4.7, mijini ni asilimia 8.7 kuliko vijijini ni asilimia 4.7.

Aidha, kijiografia, mkoa wa Iringa ndio wenye maambukizi ya juu ukiwa na asilimia 14.7. Mikoa iliyo na maambukizo ya chini ni mkoa wa Kigoma, Arusha, Kilimanjaro, Manyara ikiwa ni asilimia 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia hupata misaada ya kupambana na UKIMWI kutoka kwa Mashirika mengine ya nje, kama vile mpango wa dharura wa Rais wa Marekani wa kupambana na UKIMWI, mfuko wa dunia wa kupambana na UKIMWI, kifua kikuu na malaria yaani *Global Fund*, mashirika ya umoja wa kimataifa, mashirika ya nchi mbalimbali kama vile Japan, nchi za *Scandinavia*, na Canada. Mashirika haya mara nyingi hutoa misaada ya fedha na wataalam katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya kupambana na UKIMWI.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza, kwa kuwa jimbo la Masasi wananchi wengi hujitoa wakaenda kupima UKIMWI wao wenyewe na halafu baadaye wakipatikana waathirika huwa wanatengeneza vikundi wakakaa pamoja ili kujikimu kiuchumi. Je, Serikali itawasaidia nini kupitia haya mashirika hivyo vikundi vya waathirika?

Je, Serikali haiwezi kuwashawishi haya mashirika ili kuwajengea mazingira bora hawa watoto yatima walioachwa na waathirika wakaweza kuwalea? Ahsante sana.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mbunge kama ifuatavyo:-

La kwanza Serikali itawasaidia nini katika vikundi hivyo, Serikali kupitia mpango wa kudhibiti ugonjwa wa UKIMWI yaani *TACAIDS* ina mikakati mbalimbali ikiwa mojawapo ni kusaidia vikundi hivi pamoja na kutoa elimu.

Vile vile katika Halmashauri zetu tuna idara maalum ambayo inashughulikia kupitia Wizara ya Afya, ile idara ya Afya nao wanajishughulisha moja kwa moja na shughuli za kuweza kuwasaidia vikundi hivyo. Wito wangu Wabunge kwamba vikundi hivi kama vipo basi mvisaidie

kuwasilisha au kujitambulisha kwenye idara ya afya pale wilayani, wao wilayani watajua namna gani ya kuweza kuwasaidia hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nimelipokea ombi au ushauri kwamba haya mashirika yaweze vilevile kuwashawishi na kuwashirikisha hivi vikundi ambavyo vinajitokeza.

**MHE. MARIAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kumwuliza Waziri swali la nyongeza, kwa kuwa elimu hii ya UKIMWI haitolewi vijijini na kwa kuwa hata kondomu hazifiki vijijini na imekuwa kondomu hizi hata vijana wanakuwa wanazifua kondomu na kubadilishana kondomu. Je atanihakikishiaje huduma hizi za UKIMWI zinafika vijijini?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu, swali la nyongeza Mbunge Mariam Msabaha, swali lake kama ifuatavyo. Labda naomba nitoe maelekezo ya ziada kwamba labda nitofautiane kidogo na Mbunge Mariam Msabaha, kwamba elimu haifiki vijijini.

Takiwmu tulizokuwa nazo kwamba Watanzania wengi sasa hivi zaidi ya asilimia 90 wana ufahamu mkubwa sana kuhudu ugonjwa huu wa UKIMWI. Na tayari vikundi na wana harakati mbalimbali wanaojihusisha na kampeni za UKIMWI wako mpaka huko vijijini. Na huduma zetu zinafika mpaka kwenye kijiji pale kuna Kamati za afya na hizo Kamati nazo zinazojishughulisha mojawapo wanachofanya ni kutoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo kila mara au kila siku kupitia redio, kupitia *Television*, huwa tunatoa elimu ya kutosha kuelimisha jamii ikiwemo hao wanaoishi vijijini namna gani ya kuzuia au kudhibiti ugonjwa wa UKIMWI. Lakini vilevile suala la kondomu na kubaliana naye kama maeneo ya Masasi kama haipatikani basi nitawasiliana namna gani ya kuweza kuwasaidia nao wapate hizo kondomu kwa urahisi zaidi.

Lakini nina uhakika kwamba kondomu zinasambazwa kila tarafa, kila kata na vilevile siyo tu Wizara au Serikali lakini hata sekta binafsi nazo wanajishughulisha na kondomu wale ndugu zetu wa PSI kwa kutumia hiyo wanaita *social marketing* nao wanasambaza hizi kondomu kwa wananchi wakiwemo walioko vijijini.

**NAIBU SPIKA:** Tuvuke toka kwenye vifungashio, twende Wizara ya Maji sasa naomba nimwite Mheshimiwa Highness Samson Kiwia, Mbunge wa Ilemela.

Na. 329

**Mpango wa kufikisha maji ya Ziwa Victoria Ilemela**

**MHE. REGIA E. MTEMA (K.n.y. MHE. HIGNESS S. KIWIA)** aliuliza:-

Maji ya Ziwa Victoria sasa yanatumika kwenye mikoa jirani ya Kahama na Shinyanga lakini kata za Ilemela, Kirumba, Bugogwa, Sangabuye na Buswelu zilizozunguka ziwa hilo hazina maji safi na salama kwa sababu ya kukosa pampu kubwa za kuweza kusukuma maji, na kukosekana kwa tanki kubwa la kupokelea maji hayo ili yaweze kusambazwa kwa wananchi:-

(a)Je, Serikali ina mkakati gani ya kupata pampu zenye uwezo wa kusukuma maji, pamoja na tanki kubwa la kupokelea hayo maji ili yaweze kusambazwa kwa wananchi?

(b)Kama Serikali inao mkakati kufanya hivyo. Je, utekelezaji wake utaanza na kukamilika lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Highness Samson Kiwia, Mbunge wa Jimbo la Ilemela, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza programu ya maendeleo ya sekta ya maji iliyoanza mwaka 2006/2007. Mamlaka ya majisafi na majitaka Mwanza ilimwajiri Mhandisi mshauri wa kusanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni ya miradi ya majisafi na majitaka Jiji la Mwanza na miji ya Misungwi, Sengerema, Magu, Geita, Nansio, Ngudu na Ukerewe.

Usanifu ulianza mwezi Mei, 2010 na utakamilika mwezi Desemba, 2011 ambapo gharama halisi za ujenzi zitajulikana. Ujenzi utatekelezwa kwa awamu ya pili ya programu ya maendeleo ya sekta ya maji itakayoanza mwezi Julai, 2012.

Sehemu za Kata ya Ilemela, Kirumba, Buswelu, zinahudumiwa na mamlaka ya majisafi na majitaka Mwanza ambazo zipo katika usanifu ambao unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia katika programu niliyoitaja inatekeleza mradi wa vijiji 10, ambapo Halmashauri zote nchini zimechagua vijiji 10 vya kipaumbele.

Halmashauri ya jiji la Mwanza ilichagua vijiji 10 kutoka katika kata za Sangabuye, yaani vijiji vya Nyafula, Sangabuye, Kabusugu na Kayenze; Kata ya Bugogwa Vijiji vya Igogwe na Nyamwilolelwa, kata ya Ilemela kijiji cha Kahama; kata ya Buswelu kijiji cha Nyamadoke; Kata ya Buhongwa kijiji cha Lwanhima; na Kata ya Igoma kijiji cha Fumagira.

Mwezi Februari, 2011, wale wanaotokea Mwanza mniwie radhi kama nakosea maji haya ninayoyasoma hapa. Februari, 2011 Halmashauri ya Jiji la Mwanza, ilisaini mkataba na Maswi *Drilling Company Limited*, kwa ajili ya kuchimba visima katika vijiji nilivyovitaja. Uchimbaji kwa visima ulianza katika vijiji vya Nyafula, Sangabuye na Kabusugu ambapo visima sita vilichimbwa.

Hata hivyo, kati ya visima hivyo ni viwili tu vilivyokuwa na maji n a vinne havikuwa na maji. Kutokana na hali hiyo, Halmashauri ilimwagiza mtaalam mshauri kupima upya maeneo ya kuchimba visima. Tayari kazi ya upimaji imeanza na itakamilika mwezi Agosti, 2011. Baada ya hapo uchimbaji wa visima utaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na sera ya taifa ya maji, vijiji huchagua teknolojia wanayoitaka kupata maji na ambayo itakuwa rahisi kwao kuiendesha. Kati ya vijiji nilivyovitaja hapo juu ni kijiji kimoja tu cha Kayenze ndicho kimechagua kutumia maji ya Ziwa Victoria, vingine vimechagua kutumia visima virefu.

Matumizi ya maji ya visima virefu yana gharama ndogo kwa kuwa maji yake ni safi na hayahitaji dawa za kusafisha. Kwa kutumia maji ya ziwa Victoria, wananchi wangelazimika kulipa gharama kubwa za umeme au dizeli kwa ajili ya kuendesha mitambo ya kusukuma maji na ununuzi wa dawa za kusafisha na kutibu maji. *(Makofi)*

**MHE. LEGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, amesema kwamba Mhandisi Mshauri mradi ulianza wa kuchimba visima sita lakini kati ya hivyo ni viwili tu ndiyo vilikuwa na maji na vyote vinne vilivyobaki havikuwa na maji. Ninapenda kujua tatizo lilikuwa ni nini ina maana Mhandisi alikuwa feki au tatizo liko wapi?

Pili, amesema kati ya vijiji vyote vilivyotajwa hapa ni kimoja tu ndiyo kimechagua kutumia maji ya Ziwa Victoria, anataka kutuambia watu wa Ilemela kwamba ni kijiji kimoja tu ndiyo watafaidika na maji ya kutoka Ziwa Victoria?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Legia E. Mtema kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niiweke vizuri, ni hivi tunapokwenda kuchimba visima kwanza unampelekea mtu anayeitwa Consultant, unamwambia nenda kaangalie pale uangalie kama mimi nitapata maji. Consultant anakwambia hali halisi inaonekana kwamba hapa pana maji na hili jambo ninalolizungumza hapa Waheshimiwa Wabunge wanalifahamu. Akishakwambia ni sawa ndipo sasa unamtafuta Mkandarasi wa kuchimba kusima huyo ni mtu mwingine.

Mkandarasi huyu anayekuja pale kuchimba akakuta maji hakuna atakwambia nilipe pesa yangu hata kama maji hayapo pale kwa sababu generally imeonyesha pale maji yanapatikana na hili jambo siyo jambo la ajabu hakuna cha habari ya kwamba huyu Mkandarasi ni feki, unachimba maji kama uko kwenye mount Kilimanjaro pale slopes ukachimba visima maji yana run through yanakwenda lakini indication inaonyesha kwamba maji yanapatikana pale. Kwa hiyo, kilichotokea ni kwamba mchimbaji yule alipokwenda pale vilivyopatikana pale vikawa ni vijiji sita na vingine vikawa vimekosa.

La pili, hili analozungumzia kuhusu vijiji, nimetaja hiki kijiji ambacho kiliomba maji. Naomba niseme kwamba hawa wananchi kama wanaamua kwamba watavuta maji kutoka Ziwa Victoria kwa kutumia huu utaratibu wa pump unaozungumzwa hapa, Wizara ya Maji inachofanya ni kwamba wakishakuwekea *installation* na kila kitu zile *running cost* wanaziacha kwenye Halmashauri na Halmashauri inapeleka kwa kijiji. Nimpe tu hapa *figures* kwa hiyo anayoisema hapa ni shilingi milioni 500. Kwa hiyo, maana yake ni nini ? Ni kwamba ukisha *install* pale na hapa hata sijui kijiji kiko mbali kiasi gani inaweza ikawa zaidi ya hapo mpaka shilingi bilioni moja, itamaanisha mambo yafuatayo.

Itamaanisha kwamba sasa wakati wa kwenda kuchukua maji yale kwa sababu lazima kuwepo na *sustainability* kwa maana ya kwamba mradi uwe endelevu utatakiwa uwatoze wale wananchi wa Ilemela kwamba lipeni haya maji. Ndoo moja inaweza kuwa ni shilingi 400 au 500 wale wananchi bei ikipanda pale ndiyo sasa kelele itaanza kwamba tunataka haki zetu, tunaonewa na vitu vingine vya namna ile.

Kwa hiyo, nataka nielewe vituo hapa *as much as* mimi nakubaliana na hoja anayoisema kwamba wananchi walio wengi wameamua kwenda kwenye vile visima vya kuchimba chini kwa sababu bei yake ni nafuu na ndiyo maana Wizara ya Maji na *World Bank* wamesisitiza kwamba twende kwenye hiyo *technology.* Lakini kama Mheshimiwa Mbunge anadhani kwamba *technology* hiyo kubwa wanaiweza *I have got no problem, D by D* maana yake ni kupeleka madaraka kwa wananchi ili waamue wao wenyewe kama wakiamua hiyo *technology* wajue madhara yake ni haya niliyoyasema. (Makofi)

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, sana kwa kunipatia nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Maji kutoka Ziwa Victoria wakati yanapelekwa Shinyanga yalipitishiwa katika Tarafa ya Mwamashimba ambayo iko Wilaya ya Kwimba. Cha kushangaza mpaka leo wananchi wa Kwimba wana matatizo ya maji. Naomba maelezo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leticia Nyerere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bomba linalosemwa hapa ni lile bomba kubwa ambalo lilipeleka maji yakaenda mpaka Shinyanga na yakaondoka yakaenda mpaka Kahama, ndiyo analolizungumza hapa.

Sasa waliokuwa pembeni nao wamekuwa wanapiga kelele hizo hizo, sasa mimi naomba *technically* ukisema unaanza ku-*temper* na lile bomba kubwa maana yake kwa Shinyanga na Kahama hawapati yale maji. Sisi tuje tuzungumze habari ya hili eneo analoliita Mwamashimba analolizungumza hapa. Nitakwenda na nita- *touch base* na watu wa Kwimba ili niweze kujua tatizo lipo wapi.

Mheshimiwa Leticia Nyerere naomba tukutane tuzungumze na tuone kwamba tutakusaidiaje katika hilo.

Na. 331

**Mfumo wa Uchangiaji Huduma za Afya**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA (K. n. y. MHE. MOZA ABEID SAIDY)** aliuliza:-

Serikali imeanzisha mfumo wa uchangiaji wa huduma za afya lakini katika kutekeleza sera ya kuwapatia wananchi matibabu na hasa dawa, Serikali imeanzisha mfuko wa afya ambao wananchi wanatakiwa kuchangia.

Je, Serikali ina habari kuwa huduma hiyo haitekelezwi kama ilivyokusudiwa hivyo kusababisha wananchi kukosa dawa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moza Abeid Said, Mbunge wa Viti Maalum, kama lfuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuanzisha mfumo wa uchangiaji wa huduma za Afya kwa lengo la kuboresha huduma za afya kwa wananchi lakini kumekuwepo na changamoto katika utekelezaji wa mfumo huo.

Changamoto hizi zikiwa ni pamojana upungufu wa dawa na vifaa tiba na vitendanishi kwenye ngazi husika. Upungufu huo unatokana na baadhi ya Halmashauri kushindwa kutumia fedha zinazotokana na uchangiaji katika muda uliopangwa ili kununulia dawa, vifaa tiba na vitendanishi au kutokana na kuchelewa kwa taratibu za manunuzi ya umma, kuchelewa katika kutoa maamuzi ya kutotumika fedha hizo kwa manufaa ya wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kuboresha huduma za Afya katika Halmashauri hasa katika kutoa ushauri na miongozo ya matumizi sahihi ya fedha zitokanazo na michango mbalimbali iya huduma za afya iliyoanishwa. Aidha, napenda kuzipongeza baadhi ya Halmashauri zilizofanya vizuri katika kukusanya na kusimamia matumizi mazuri ya michango ya wananchi, Wilaya hizo ni lgunga, Chamwino, Rombo na lramba.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Je, Serikali inawezaje kutoa sera kabla ya kuandaa mwongozo kwa ajili ya watumishi wanaofanya kazi hizo?

Pili, kwa kuwa mwananchi anapochangia pesa yake huamini kabisa kwamba atapata huduma kama alivyokusudia. Je, Serikali inawaeleza nini wananchi wanaochangia fedha hizo katika mfuko wa *CHF?*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba michango hii ya kuchangia afya inapitia kwenye vikao mbalimbali katika Halmashauri. Kuna Kamati za afya ambayo ndiyo wanakaa kwenye Halmashauri ili kuweza kupanga kwamba wananchi wachangie kiasi gani kwa ajili ya kuongezea zile juhudi za Serikali za kuwapa wananchi dawa na huduma zilizo bora.

Kwa hiyo, miongozo mingi ni lazima itokane na vikao hivyo lakini sisi kama Serikali tuna *desk* linaloshughulikia michango na lile *desk* kazi yake ni kwamba kila panapoanzishwa mfuko kwa ajili ya kuchangia afya wanakwenda kutoa mafunzo kwa wale wahusika na wanapanga kwamba zitumikaje.

Lakini kipaumbele kwenye mwongozo unaotolewa ni kwamba kwanza ziongezewe lile pengo la kununua dawa na pengo la pili ni la kununua vitendanishi, vitendanishi maana yake ni kwamba ni zile *re-agent* zinazotumika kwenye maabara kuweza kugundua kwamba mgonjwa anaumwa nini ili aweze kupata tiba sahihi na miongozo ipo. *(Makofi)*Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu Serikali inawaambiaje wale ambao wanachangia pesa zao na hawajapata huduma.

Serikali inawaambia hivi kwa sababu kwenye kila kijiji ambako kuna Zahanati ambayo ndiyo inachangiwa ile *Community Health Fund,* wai-*challenge* kwa sababu wao ndiyo ambao wanachagua hizo Halmashauri.

Kwa hiyo, ninaomba sisi kama Viongozi tusaidie kuwakumbusha Madiwani ambao ndiyo Wenyeviti wa Baraza la Maendeleo ya Kata, wanakutana na Viongozi wake wote wa vijiji wawakumbushe kwamba kuna wajibu wa kuhakikisha kwamba kwenye *dispensary* zao kunakuwepo na dawa kwa sababu pesa zipo na siyo kwamba hizo hela zimeliwa na mtu yeyote, ukienda kule ambako hawajazitumia hilo pesa utazikuta.

Kwa hiyo, naomba nitoe mwongozo tena kwa taifa zima kwamba katika ngazi zote zile pesa zitumike kwa ajili ya kununua dawa pamoja na vitendanishi na siyo kwamba zitumike kwenye masurufu ya safari au ujenzi katika ngazi za Halmashauri.

**MHE. RAYA IBRAHIM HAMISI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi.

Kwa kuwa, imekuwa ni utaratibu kwamba hata dawa zinapopatikana katika hospitali zetu wagonjwa hawapatiwi dawa zinazotakiwa wanapokwenda wanaambiwa dawa zimekwisha. Mheshimiwa Waziri katika jibu la msingi amesema kwamba Serikali imeendelea na jitihada za kujitahidi kuhakikisha kwamba dawa zinapatikana.

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha dawa zinapopatikana na zinapofika hospitalini, kama Serikali kuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wagonjwa wanaoandikiwa dawa wanapata dawa zinazostahili na kutokupewa *Panadol* kama livyokuwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raya Ibrahim Hamis, ambaye leo ndiye Kiongozi wa Upinzani hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba inatokea wakati mwingine kwamba dawa hazipo katika vituo vyetu vya afya, na inategemea na kwamba wale Viongozi kwenye ngazi ya dispensary na vituo vya afya ndipo ambapo mara nyingi dawa zinakuwa hazipo. Sisi tulianzisha huo mfuko ili kuweza kusema kwa kingereza nasema: *to supplement the efforts* za Serikali za kuweza kupata dawa kwenye ngazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huo ni mtindo mpya tunahitaji kuwafundisha na wale unakuta kwamba, na ninaomba niseme Daktari wa Kituo cha Afya hajafundishwa uhasibu. Kwa hiyo, anakuwa mwoga sana kutumika pesa bila kuomba ruhusu.

Sasa naomba niseme hivi kwamba sisi tumeanza kutoa tena mwongozo upya kwa *DMO* awe anapita na kuwapa *autonomy* kwa sababu wana Kamati za afya, zile Kamati za afya ndizo ambazo zinaamua kwamba dawa ambazo hazipatikani ni hizi na jambo muhimu ni kwamba tuweze kuweka takwimu na takwimu zitatoa mwongozo wa madawa ambayo yanahitajika kunuliwa kwa ajili ya ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutafuatilia na ninakuhakikishia kwamba kwa sababu ni jambo jipya litachukua muda kwa kujifunza lakini dawa zitapatikana tu.

Na. 332

**Ujenzi wa Maabara kila Sekondari**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Tatu iliahidi kujenga maabara kila Sekondari. Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Yale maswali ambayo huwa nayasifu ya kibunge ni kama hili lilivyoandikwa.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jitihada mbalimbali zimefanyika katika kutekeleza ahadi ya Serikali ya kujenga Maabara katika shule za Sekondari nchini. Jitihada hizo zilihusisha utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mpango wa maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES I) ambapo vyumba vya Maabara 311 vilijengwa kati ya mwaka 2005 hadi mwaka 2010.

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2001-2005 vyumba vya maabara 108 vilijengwa katika Shule za Sekondari 36 kupitia mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na kupatiwa vifaa katika kipindi husika.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizo zinaendelea kutekelezwa ambapo kupitia mpango wa maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES II) shule 264 zitajengewa maabara na kuwekewa vifaa.

Aidha, Serikali inaendelea kuwasiliana na wadau wengine na mashirika ya maendeleo katika sekta ya elimu ili kuhakikisha shule zote zinakuwa na maabara zinazofanya kazi.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa vile Sekondari za Longido hazikubahatika kuingia katika awamu ya kwanza na ya pili, shule 429 zilizojengwa je, katika awamu hii ya pili mtakumbuka shule za Longido kuzipa maabara?

Swali la pili, kwa vile Sekondari ambazo hazina maabara, Serikali itakubaliana nami kwamba itasababisha tofauti kubwa ya taaluma kati ya shule zilizo na maabara na zile ambazo hazina maabara na kufanya watoto wengine wafaulu mitihani na wengine wasifaulu kwa ajili ya tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuhusu shule nyingi za Longido ambazo hazina maabara, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba shule ambazo hazina maabara kule Longido ni Namanga, Ketembwene na Ingelenaibo na shule hizo zipo katika mpango wa ndani ya zile shule 264 kwamba zitajengewa maabara maana yake tayari tuna fedha dola za Kimarekani milioni 150 ambazo tumetenga na tayari Wataalamu wetu wa Wizara ya Elimu wako katika mchakato wa kuandaa mpango wa kuanza kuzijenga shule hizo.

Swali la pili, kwamba shule ambazo hazina maabara katika mitihani ziweze kutofautishwa kimatokeo nataka tu nisema kwamba kuna mitihani ya aina mbili, kuna wale wanaofanya *actual practical* kwenye shule ambazo zimekamilisha maabara na kama kuna shule ambayo haina maabara kuna *alternative practical* huwa wanafanya watoto wanapomaliza kidato cha nne.

**MHE. SAID MOHAMED MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mkoa wa Lindi ni miongoni mwa Mikoa ambayo shule zake karibu zote hazina maabara ikiwemo katika Jimbo langu la Mchinga.

Naomba kufahamu kutoka Serikalini kwamba je katika awamu hii sasa ya ujenzi wa maabara 200 shule ya Sekondari Mchinga, Kitomanga na Mvuleni zitazingatiwa kwa kuwa Jimbo zima hakuna maabara hata moja?

**NAIBU SPIKA:** Majibu Mheshiwa Naibu Waziri, Mchinga hakuna shule yenye maabara hata moja!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Mchinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema tulizingatia sana hizi shule za Mikoa ya pembezoni kama Kigoma, Mtwara, Lindi na Rukwa. Kwa Mkoa wa Lindi kuna Halmashauri ya Kilwa, Nachingwe, Ruangwa na Liwale, hizi shule zimezingatiwa na ningependa kwa haraka haraka kwamba kuna Mitole Sekondari, Kilwa Sekondari, Mkonge Sekondari, Lindi Sekondari, Mahiya Sekondari, Mchinga Sekondari, *Farm 17* Secondari, Nachingwea Sekondari, Mwekenyera Sekondari, Ruangwa Sekondari, Kibutuka Sekondari na Liwale Sekondari. Shule hizi zote ziko katika mpango wa zile shule 264 zitakazojengewa maabara katika kipindi hiki.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa takribani asilimi tisini (90%) ya shule za Kata kote nchini hazina maabara. Mfano Mkoa wa Manyara, wilaya ya Babati, jimbo la Babati Vijijini ni shule moja tu ya Galapo ina maabara, Babati Mjini ni shule moja tu ya *Babati Day* ina maabara, shule zingine zote hazina maabara na kwa kuwa ni juzi tu katika Bunge hili eneo la utawala tulionyeshwa *mobile laboratories* ambazo zina- *cost* kama shilingi milioni sita (6).

Je, Serikali iko tayari katika mwaka wa fedha ujao kutenga fedha za kupeleka hizo *mobile laboratories* katika shule za Kata? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sina majibu mengine zaidi ya haya niliyoyatoa kwamba Serikali imezingatia zile shule zote ambazo hazina maabara maana yake ni kama nilivyosema kwamba tutajenga maabara 264 katika awamu hii ya mpango wa pili wa MMES. Nadhani nilipokuwa nasoma takwimu hapa mkoa wa Manyara katika hizo shule alizozitaja Mheshimiwa Mbunge zimo katika mpango huu. Kwa hiyo, Mheshimiwa awe na subira tunajenga. *(Makofi)*

Na. 333

**Ujenzi wa Barabara**

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIDOGA** aliuliza:-

Barabara ya Korogwe – Handeni – Dumila na ile ya Mkata Handeni zimeshaanza kujengwa kwa lami.

(a) Je, ujenzi huo hadi sasa umefikia hatua gani kwa kuzingatia muda uliopangwa wa kukamilisha kazi?

(b) Je, ni lini ujenzi utakamilika?

(c) Je, ni lini fidia za wananchi wanaopaswa kulipwa itakamilika ?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hadi kufikia mwezi Mei, 2011, ujenzi wa sehemu ya Korogwe – Handeni umefikia asilimia ishirini (20%), sehemu ya Turiani – Magole, ujenzi umefikia asilimia ishirini na tano (25%) na sehemu ya Handeni – Mkata umefikia thelathini na mbili (32%).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi hii mitatu umepangwa kukamilika kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa barabara ya Korogwe – Handeni umepangwa kukamilika mwezi Oktoba, 2012.

(ii) Ujenzi wa barabara ya Handeni – Mkata umepangwa kukamilika mwezi Novemba, 2012.

(iii) Ujenzi wa barabara ya Magole – Turiani umepangwa kukamilika mwezi Machi, 2012.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, ulipaji wa fidia siku zote utazingatia Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007. Hivyo wale wote wanaostahili kulipwa fidia kwa mujibu wa Sheria watalipwa na wale ambao hawastahili kwa kweli hawatalipwa.

Hadi sasa fedha zilizokwisha lipwa kama fidia ni shilingi milioni 400 kwa mradi wa Korogwe – Handeni, shilingi bilioni 1.0 kwa mradi wa Handeni – Mkata na kwa mradi wa Magole – Turiani kiasi cha shilingi bilioni 1.0 tayari kimepelekwa kwa Meneja wa Mkoa Wakala wa Barabara Morogoro ili aweze kulipa fidia.

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIDOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri.

(i) Swali la kwanza kwa vile wananchi wa vijiji vingine katika barabara hizo husika tayari wamekwishalipa fidia zao.

Je, ni lini wale wananchi wa Mazingara, Mkata, Vibaoni watalipwa hizo fidia?

(ii) Kwa vile hivi sasa yupo Afisa wa *TANROADS* anazunguka katika maeneo haya, Mzingara, Mkata, Vibaoni, Kilole, Bagamoyo na kuwaeleza kwamba wananchi hawatalipwa fidia ambao walikwishaahidiwa kwamba watalipwa fidia hizo.

Je, haoni kauli hiyo inafanya wananchi wawe na hisia kwamba maamuzi ya Wizara hayatabiriki na vilevile kuwapa wasiwasi kwamba Wizara haina *moral obligation* ya kuwafidia hawa watu ambao ni maskini na wana nyumba zao wamekwishakujenga?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa suala la fidia ni suala linaloendelea barabara ikiwa kwenye mchakato wa kujengwa. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba fidia kwa wengine ambao wataendelea kubomolewa nyumba zao na vilevile uhakiki ukiishakamilika tutawalipa. Tunamwomba tu Mheshimiwa Mbunge atusaidie tu kupitisha Bajeti yetu kesho kutwa, atuunge mkono ili fidia ipatikane ya haraka kumalizia malipo hayo.

Lakini kuhusu huyu Afisa wa *TANROADS* anayepita kuwaambia wananchi watalipwa naomba nitoe msimamo wa Serikali kwamba wale walioifuata barabara na kujenda ndani ya mita ishirini na mbili na nusu (m 22.5) toka katikati ya barabara kwenda kushoto au kulia hao hawatalipwa fidia yoyote.

Lakini wale ambao walikuwa nje ya mita ishirini na mbili na nusu (m 22.5) wakati tunapitisha mabadiliko ya sheria mwaka 2007, naomba kuwahakikishia kwamba watalipwa fidia yao kikamilifu kwa sababu hifadhi ya barabara imewafuata baadaye. Ningependa nionane na Mheshimiwa Kigoda baadaye atuelezee afisa huyo wa *TANROADS* anayesema maneno hayo ni nani, na ameyasemea wapi.

**MHE. DUSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Suala la ulipaji wa fidia kwa barabara za Handeni linafanana sana na barabara ya Tanga – Horohoro. Mheshimiwa Rais alipokuja kuzindua ujenzi wa barabara ya Tanga – Horohoro aliahidi kwamba wananchi waliobomolewa nyumba zao watalipwa.

Je, Serikali inatuhakikishia ni lini suala hili litakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dustan Kitandula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia kwa barabara ya Tanga – Horohoro Serikali imefanyakazi nzuri sana mpaka sasa kwa sababu mbali na majengo mengine tuliyobomoa, misikiti 21 na madrasa 4 tulizibomoa na tumezirejesha kwa kuzijenga kwa kisasa kwa zaidi ya shilingi bilioni 1.4 na wananchi wameridhika sana.

Ningeomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba kama kuna madai mengine kama nilivyosema suala la fidia ni endelevu barabara inapojengwa, yanapojitokeza madai ya wananchi tunayasikiliza na kuyahakiki. Tunaomba awasiliane nasi tuweze kuhakiki madai hayo na tuweze kuyalipa vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachomwomba tu ni kwamba keshokutwa tutakapoleta Bajeti yetu atuhsante sana. *(Makofi)*

Na. 334

**Kujenga kwa Kiwango cha lami Barabara ya Mkoa wa Njombe**

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE** aliuliza:-

Barabara ya Mkoa wa Njombe – Makete – Kikondo ndiyo inaunganisha Mkoa mpya wa Njombe na Mkoa wa Mbeya (Isyonje). Barabara hiyo ni muhimu sana kwa sababu inapita kwenye vitega uchumi vya nchi kama vile mradi wa kuzalisha umeme wa MW. 222 utakaojengwa kwenye maporomoko ya Mto Rumakalya, Shamba la Ng'ombe la Kitulo, Hifadhi ya Kitulo na Milima ya Livingstone.

Je, ni nini mkakati wa Taifa wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Bilithi Mahenge, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mkoa wa Njombe – Makete – Kikondo yenye urefu wa kilomita 183 ni barabara inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS).* Wizara yangu inatambua kuwa barabara hii ni muhimu kiuchumi na kijamii.

Kwa kutambua umuhimu huo, barabara hii imekwishafanyiwa matengenezo mbalimbali kama ifuatavyo:-

(ii) Mwaka wa fedha 2008/2009 matengenezo ya maeneo korofi kwa kiwango cha changarawe kati ya Njombe na Makete kwa gharama ya shilingi bilioni mbili (2). Ujenzi kwa kiwango cha lami nyepesi '*Single Surface Dressing* ' kati ya Mang'oto na Ikonda urefu wa kilomita tano (5) kwa gharama ya shilingi bilioni 1.525.

(iii) Mwaka wa fedha 2009/2010 matengenezo kwa kiwango cha changarawe yalifanyika kwa lengo la kuimarisha maeneo korofi yenye jumla ya urefu wa kilomita 34 kwa gharama ya shilingi milioni 668.510. Aidha, ujenzi wa kiwango cha lami ulifanyika katika kipande cha barabara chenye urefu wa kilomita 4.5 katika eneo la Mang'oto. Kazi hii iligharimu shilingi bilioni 2.988 ikijumuisha gharama za usimamizi.

(iv)Mwaka wa fedha 2010/2011 uimarishaji wa maeneo korofi uliendelezwa kwa urefu wa kilomita 22 kwa gharama ya shilingi milioni 396.395 Ujenzi wa kiwango cha lami katika kipande cha barabara chenye urefu wa kilomita mbili (2) kwenye maeneo ya Mang'oto na kazi hii iligharimu shilingi bilioni 1.3 ikijumuisha gharama za usimamizi.

(v)Lengo la mwaka wa fedha 2011/2012 ni kuendeleza uimarishaji wa maeneo korofi ndani ya Wilaya ya Njombe na Makete ili kuepusha kujifunga kwa barabara wakati wa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kwamba barabara hii ipo katika Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo mbalimbali katika barabara hii ili kuhakikisha inaendelea kupitika wakati wote wa mwaka.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, na niishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri ambayo inaifanya Makete kuhusu barabara.

(a)Naiomba Serikali inipe ratiba ya utekelezaji wa ahadi iliyoko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 – 2015 sehemu ya Njombe – Makete ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Inipe utaratibu wake huo namna utakavyotekelezwa. Anaweza akanikabidhi baadaye siyo sasa hivi *schedule* ya *activities* zake.

(b)Kwa kuwa barabara hii kipande cha kutoka Mbeya – Makete kinapita kwenye sehemu za vitega uchumi kama nilivyoanisha kwenye swali la msingi yaani Shamba la Ng'ombe la Kitulo, Hifadhi ya Kitulo na Mradi mkubwa wa umeme wa pale Bulongwa, na kwa kuwa barabara hii ndiyo inayowawezesha watalii hasa Wajerumani wanaokwenda kutembelea *Matema Beach,* wanaenda mpaka Makete na baadaye kwenda kwa mguu *Matema Beach,* lakini wanashindwa kwa sababu barabara hii siyo nzuri, siyo ya lami.

Je, ni kwanini Serikali haiweki kipaumbele cha kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ikizingatia kwamba miradi inayohitaji kuhudumiwa na barabara hii ambayo ni mikubwa ya kitaifa na inabeba uchumi wa nchi yetu ?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Bilithi Mahenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu ratiba, kwamba apewe ratiba ya utekelezaji wa ahadi. Ningependa kumpa ratiba ifuatayo; tutatekeleza ahadi ya Rais kuanzia sasa mpaka mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatambua sana umuhimu wa barabara hii na azma ya Serikali kuijenga kwa lami pale ambapo mfuko utaturuhusu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu muda uliobaki ni mdogo sana nawaomba radhi tuendelee na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 335

**Kituo cha Polisi Mkokotoni Kuungua Moto**

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS** aliuliza:-

Je, Serikali inatambua kwamba kituo cha Polisi Mkokotoni Kaskazini 'A' Unguja kimeungua moto na kusababisha usumbufu kwa askari kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu**:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuungua jengo hilo na ina mpango wa kujenga kituo kipya cha Daraja 'A' katika eneo hilo katika mwaka huu wa fedha 2011/2012.

**NAIBU SPIKA**: Hili jibu ni jibu la kitaalam kabisa. Mheshimiwa Yussuf, nilidhani umeridhika! Swali la nyongeza.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante! Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini pamoja na majibu mazuri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwanza nataka kujua ujenzi huo utaanza lini?

(ii) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri katika jibu lake la msingi kwamba kituo hicho kitajengwa katika Daraja 'A' pamoja na kituo hicho kujengwa katika Daraja 'A' nyumba za Polisi zilizopo Mkokotoni pale ziko katika hali mbaya sana, atanijibu vipi kuhusu suala hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza nimesema katika mwaka huu wa fedha 2011/2012. Kwa hiyo, tunasubiri leo tukijaaliwa jioni mkiishapitisha bajeti yetu basi hapo tutakwenda katika utaratibu wa kutekeleza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu majengo. Hili ni tatizo ambalo tunalo katika taifa zima, lakini nataka kusema kwamba litazingatiwa kwa sababu kituo cha Daraja 'A' pia kina mahitaji yake zikiwemo nyumba za askari.

Naomba tu niseme kitu kimoja kwamba tunashughulikia vituo lakini pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge msiwe wa kwanza katika kuwashawishi wananchi kushambulia vituo vya polisi kwa sababu pesa ambazo tunatumia kujenga vituo hivyo tunazitafuta kwa taabu.

Raslimali fedha inakuwa taabu kuipata, kwa hiyo ni kitu ambacho naomba tuelewe kwamba tutajitahidi kujenga vituo lakini pia tusiwe wa kwanza kuwashawishi wananchi kwenda kuvamia vituo vya polisi.

**NAIBU SPIKA**: Wenye maswali yao leo ndiyo siku ya Wizara hii tuyahifadhi kidogo. Naomba tuendelee na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Mbunge wa Bumbuli.

Na. 336

**Mradi wa Umeme Kata ya Mgwashi**

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA** aliuliza**:-**

Mradi wa kuepeleka umeme kata ya Mgwashi umesimama kwa muda mrefu, pia gharama za kuwaunganishia wananchi umeme ni kubwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mradi huo unaendelea?

(b) Je, Serikali haioni vema kwa wananchi kupatiwa umeme, halafu kukatwa kidogo kidogo huku tayari wakiwa na umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa January Makamba, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, kata ya Mgwashi ina Vijiji vya Wanga, Kwemkole, Malomboi, Sagara, Mkongoi na Mgwashi. Kati ya vijiji hivyo ni vijiji vya Mgwashi na Mkongoi vinavyotegemea kunufaika na mradi huo unaoendelea kupeleka umeme katika kata ya Mgwashi.

Mradi huo ulisimama mwezi Desemba, 2010 kutokana na ukosefu wa vifaa vya ujenzi wa mradi na mahitaji mengine kwa ajili ya kupeleka umeme katika Kata hiyo na ulianza tena mwezi Juni, 2011 mara baada ya kupata vifaa. Hivi sasa mafundi wa *TANESCO* wapo kijijini Mgwashi wakiendelea na kazi ya ujenzi wa njia ya umeme ambapo nguzo za njia ndogo zinaendelea kusimikwa kwenye kijiji cha Mgwashi pamoja na maandalizi ya kuvuta nyaya za njia ndogo na kuweka transforma.

Vilevile *TANESCO* wanaendelea kuvuta nyaya za njia kubwa kuelekea kwenye kijiji cha Mkongoi. Mradi unatarajiwa kukamilika ndani ya mwezi mmoja na nusu kuanzia sasa.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapa Bungeni tarehe 5 Julai, 2011 wakati tunajibu swali la Mheshimiwa Dkt. Seif Selemani Rashidi, Mbunge wa Rufiji, Serikali inatoa punguzo la kuunganisha umeme katika baadhi ya miradi inayofadhiliwa na washirika mbalimbali wa maendeleo.

Pamoja na miradi inayofadhiliwa na Wakala wa Nishati Vijijini *(REA),* na kama tulivyosema baadhi ya maeneo yaliyofaidika na unafuu huu ni pamoja na jimbo la Rufiji, Ukerewe na maeneo mengine 16 yanayofadhiliwa na *REA* kulingana na makubaliano ya awali ambapo wananchi wamehitajika kulipia asilimia kumi na nane (18%) tu ya gharama za kuunganishiwa umeme kwa ajili ya kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT).*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *TANESCO* inaruhusu wateja wa umeme kulipia kwa awamu tatu kwa miezi mitatu mfululizo malipo ya kuunganishiwa umeme katika utaratibu mbadala. Mara mteja anapomaliza kulipia awamu zote, huunganishwa mara moja katika kipindi kisichozidi siku thelathini (30). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia upo utaratibu wa kulipia gharama za kuunganishia wateja umeme kupitia benki. Mpaka sasa benki yenye mkataba na *TANESCO* kwa ajili ya huduma hii ni *Akiba Commercial Bank.* Utaratibu ni kwamba mteja anachukua gharama za kuunganisha umeme *TANESCO* na kuziwasilisha *Akiba Commercial Bank,* halafu benki inalipa moja kwa moja *TANESCO* na kisha *TANESCO* wanamuunganishia umeme mteja.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukiri kwamba ni kweli kazi imeanza baada ya kusimama mwezi Desemba mwaka jana, lakini Serikali wamepeleka nguzo chache, nguzo thelathini (30) tu na zinahitajika *transforma* ambazo hazikupelekwa. Kwa hiyo kazi imeanza lakini itasimama muda si mrefu kabla mradi haujaisha.

Je, Serikali inatoa maelezo gani kuhusu upatikanaji wa nguzo zaidi na nyaya zaidi na *transforma* zaidi, ili kazi isisimame tena na mradi huo uendelee ukamilike na watu wapate umeme kwa gharama nafuu?

(ii) Kwa kuwa kata ya Vuga imezungukwa na maeneo yenye umeme ya Mombo, Soni, na Mponde, lakini yenyewe haina umeme na kwa kuwa Vuga kwetu sisi Wasambaa tunaita 'Kitala Kikuu' ndipo alipokuwa anakaa Chifu Kimweri ambaye alitawala mpaka Mkuranga.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme kwenye Kata ya Vuga?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa January Makamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua kwamba kazi imeanza na ni kweli na mimi katika kufuatilia majibu leo asubuhi nimeambiwa nguzo zilizokwenda ni chache na bado kuna mahitaji ya nguzo za ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hili ni tatizo ambalo limewaathiri watu wengi pamoja na kule Kasulu na Kibondo na maeneo mengine ambapo miradi imesimama simama kwa sasa hivi tulipewa *priority* kusema kwamba ile miradi iliyosimama lazima iongezewe nguzo ili isisimame kwa sababu ikisimama ina gharama kubwa ya ziada ambayo inakuwa haikukadiriwa.

Kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa January Makamba na katika kanda ile pia kuna maeneo pale ya Mheshimiwa Maji Marefu kule Magoma na kadhalika kwamba zile kazi zote zilizokusudiwa ambazo zilikosa vifaa hivi tutahakikisha kwamba vifaa hivi *tranfoma,* nyaya na nguzo vinakwenda kwa wakati ili kazi isisimame na lile lengo la kukamilisha ndani ya mwezi mmoja au miwili ijayo ifikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili suala la pili, ni kweli kwamba pale Vuga panazungukwa na Mombo na Soni ambapo sio mbali ni kama kilomita 4 au 5 kwa maeneo yote, sio mbali lakini kuna matatizo kidogo ya namna ardhi ilivyokaa Tereni pale ni ngumu kidogo, lakini pamoja na hayo pana watu wengi Vuga ni mji mkubwa na kama alivyosema ni kitalu kikuu na pale pana Chifu aliyefika mpaka Mkuranga.

Kwa hiyo naomba nimhakikishie tu kwamba Vuga panakidhi vigezo vyote vya kupata umeme tutaliangalia na tunalipatia ufumbuzi haraka iwezekenavyo. *(Makofi)*

Na. 337

**Mashauri ya Ardhi Kuwa Chini ya Mahakama**

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY** aliuliza:-

Sheria iliyoanzisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba (Na. 2 ya 2002) iliondoa Mamlaka ya Mahakama za Wilaya na za Mwanzo kusikiliza mashauri ya ardhi, na kuipa Mahakama Kuu (Kitengo cha Ardhi); Sheria hiyo imerekebishwa kwa kuondoa Kitengo cha Ardhi Mahakama Kuu:-

Je, Serikali haijaona haja ya kuvunja Mabaraza hayo na kurejesha Mamlaka ya kusikiliza mashauri hayo kwa Mahakama za Mahakimu ili haki ipatikane kwa uhakika na chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa Mahakama Kuu?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuvunja Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na kurejesha Mamlaka za Mahakimu kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri ya ardhi na nyumba. Hii ni kutokana na sababu kuwa mfumo anaoupendekeza Mheshimiwa Mbunge uliwahi kutumika kabla ya kutungwa kwa Sheria ya Mabaraza ya Ardhi ya Na. 2 ya Mwaka 2002. Mfumo huo ulibainika kuwa na mapungufu mengi ya kisheria na kiutawala yaliyosababisha ucheleweshaji mkubwa wa kusikiliza na kutoa maamuzi kwa kesi zinazohusu masuala ya ardhi na nyumba.

Pia, Mahakama hizo zilibainika kuwa na mlundikano mkubwa wa kesi zilizohusu masuala ya ndoa, jinai, mirathi na mikataba ambayo yalichukua muda mrefu hadi miaka 12 bila ya kutolewa maamuzi; na kulikuwepo na gharama kubwa za kuendesha kesi hizo ambapo ilikuwa ni mzigo kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utafiti makini kufanyika na Tume kuundwa (Tume ya Prof. Issa Shivji) Serikali ilishauriwa na ikakubali kuwa ni muhimu kufuta Mamlaka za Mahakama za Mwanzo na za Wilaya kusikiliza na kuamua migogoro ya ardhi na nyumba. Badala yake, kazi hizo zifanywe na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kama ilivyoelekezwa kwenye kifungu cha 167(1) (c) ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999 na Sheria ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba Na. 2 ya Mwaka 2002 na Kanuni zake.

Kwa mujibu wa Sheria Na. 2 ya Mwaka 2002 watumishi wenye mamlaka ya kusikiliza na kuamua mashauri katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ni Wenyeviti ambao kitaaluma ni Wanasheria walioteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yaanzishwe mwaka 2004 yamepunguza migogoro ya ardhi na nyumba iliyokuwepo kwa muda mrefu; na inayofunguliwa inashughulikiwa ndani ya miezi miwili. Hivyo kwa kuzingatia mafaniko yaliyopatikana tokea kuanzishwa kwa Mabaraza hayo, Serikali inaendelea kuyaboresha Mabaraza yaliopo na kuanzisha mengine mapya kwenye Wilaya ambazo hayajaundwa.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa Mabaraza hayo yalikuwa yameanzishwa kutatua tatizo la wananchi ambao walikuwa na matatizo ya kusafiri Mahakamani mara kwa mara. Na kwa kuwa Baraza hizo zimeanzishwa katika Kata ili kurahisisha kuamua kesi kwa haraka na wakapewa mwisho wa kiwango cha thamani ya kuamua kesi ni shilingi 3,500,000/= Je, Serikali sasa imeona kuna sababu ya kuongeza kiwango hicho ifike hata shilingi 50,000,000/= ili kesi hizo ziweze kuamuliwa badala ya kwenda kwenye Baraza la Mikoa?

Swali la pili, kwa sababu sera ya Serikali ni kuanzisha Mabaraza ya Wilaya katika sehemu ambazo hazijaanzishwa. Na kwa vile sera ya Serikali ni kutokuvunjwa Baraza hizo je katika sehemu ambazo Mahakama zilizoanzishwa hasa Wilaya ya Mbulu Serikali inaweza kuanzisha hapa karibuni? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezwa kwa kiwango cha juu ambacho Mabaraza ya Ardhi ya Kata yamepewa ni kweli ni shilingi 3,000,000/= kwa mujibu wa sheria. Hivi sasa Wizara yangu inafanya rejea ya sheria zote zilizo katika sekta ya ardhi kwa lengo la kupendekeza marekebisho ili kwanza kuweza kukidhi haja ya wakati tuliopo. Moja ya sheria ambayo tunatazama ni sheria hii ya Mabaraza ya Ardhi. Nakubaliana naye kabisa kwamba ni kweli kwa wakati huu tokea mwaka 2002 hadi leo hii kiwango cha shilingi 3,000,000/= ambazo Mabaraza haya yalikuwa yamepewa ni kiasi kidogo na hivyo tutapitia sheria ili kuona uwezekano wa kuongeza kiwango hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuanzishwa kwa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Mbulu, napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mbulu imo katika orodha ya Wilaya ambazo hazina Mabaraza hayo na ambayo mara Bajeti yetu itakavyoruhusu basi tutaipa kipaumbele.

Tatizo linalokabili sasa hivi uanzishwaji wa Mabaraza haya ina kesi ya Bajeti. Lakini tunayo matumaini kabisa kwamba uchumi wetu unavyozidi kuboreka basi na Bajeti ya Mabaraza Ardhi na Nyumba itaongezwa ili kuhakikisha kwamba kila Wilaya ina Mabaraza ya Ardhi kama ambavyo imeainishwa na kuelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2010.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yana msongamano mkubwa sana wa kesi na hii nazungumza kwa sababu ni Wakili nafanya kazi kwenye Mabaraza haya.

Sasa naomba Mheshimiwa Waziri aliambie Bunge hili kama kuna uwezekano wa ile sheria inayozuia Mahakama za Kawaida kusikiliza kesi za ardhi inaweza ikaondolewa ili kuruhusu Mahakama za Kawaida ama ilivyofanyika kwa Mahakama Kuu vile vile kusikiliza kesi hizi za ardhi ili kupunguza msongamano mkubwa ulioko katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa sasa hivi *considering* kwamba si kila Wilaya iliyoko nchi hii ambayo ina Mabaraza ya Ardhi na Nyumba wakati kila Wilaya ya nchi hii ina Mahakama ya Wilaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama nilivyoeleza katika jibu la swali la msingi ni kweli kwamba tuna upungufu na sio kila Wilaya ina Mahakama, au Baraza la Ardhi la Nyumba. Tumesema kwamba tunachofanya sasa hivi ni jitihada za kupata fedha za kutosha ili kuanzisha Baraza kwa kila Wilaya. Marekebisho ya sheria ili kwamba kuruhusu Mahakama za Kawaida kusikiliza mashauri haya tutayafikiria pendekezo lake tutakapokuwa tunapitia na kupendekeza marekebisho kwa sheria hii ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge muda wetu wa maswali umetuishia na maswali yote yamepata nafasi ya kusikilizwa. Kwa wale ambao hatukupata nafasi ya kuuliza maswali tuwiane radhi ni kwa sababu ya muda tu.

Nianze na matangazo, lakini kabla ya matangazo ili watu wajiandaye wakati wa uchangiaji leo shughuli hapa itaanza na Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, kama mchangiaji wetu wa kwanza na mchangiaji wa pili atakuwa Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

Wageni walioko Bungeni asubuhi hii ya leo ni pamoja na Walimu 17 kutoka Uingereza ambao wapo hapa nchini wakijitolea kufundisha shule mbalimbali mwenyeji wao ni Mheshimiwa Leticia Nyerere. Wameenda Mtera. *(Makofi)*

Pia wako wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ambayo ni wanafunzi 50 na walimu 4 wa Shule ya Sekondari Jitegemee Mgulani JKT, Dar es Salaam. Nadhani watakuwa *basement.*

Aidha waki Wanafunzi 40 na walimu wa Shule ya Sekondari Mtakatifu Denis. Wanafunzi 39 wa Chuo cha Biashara *(CBE) Dodoma,* ahsanteni sana karibuni majirani zetu. Pia wako Wanakwaya 50 kutoka Mbeya *Moravian Town* Kwaya Ushariki wa Mbeya. Karibuni sana Wanakwaya kutoka Mbeya hapa Dodoma. Wanafunzi na walimu wao kutoka Mtakatifu Joseph *Millenium* Dar es Salaam. Karibuni sana wanafunzi na walimu kutembelea Bunge lenu hapa Dodoma.

Mgeni wa mwisho ni mgeni wa Mheshimiwa Dustan Kitandula, ambaye ni mama watoto na mtoto. Kule mwisho kabisa karibuni sana Bungeni Dodoma.

Liko tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Raya Ibrahim, Msadizi wa *Chief Whip* wa Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, anawatangazia Wabunge wote wa CHADEMA kwamba wakutane saa 9.00 jioni leo kuna kikao katika Ofisi za Kambi.

Kuna tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir *Super* Kibonge. Kwamba ameokota saa ya kike hapo nje ya ukumbi huu anaomba atangaze kwa aliyepoteza saa hiyo aende kuichukua kwake. Amesema saa hiyo ameiokota, sijui kama ameipata pataje hiyo saa ya kike. Aichukue hapo alipo kwa Mheshimiwa *Super* Kibonge. *(Makofi/Kicheko)*

Tangazo la mwisho kwanza nimtambulishe Ndugu Ansibert Ngurumo, Mkurugenzi Mtendaji wa *Voxs Media* Kituo cha Habari na Uongozi Dar es Salaam ambaye ni Naibu Mhariri wa *Free Media*, Wachapishaji wa Tanzania Daima na Sayari. Ahsante Bwana Ngurumo, karibu sana. *(Makofi)*

Tangazo la mwisho ni la Mdahalo, Mdahalo huo utafanyika kesho tarehe 30 Julai, 2011, utafanyika *Saint Gasper Conference Centre* Dodoma saa 12.00 jioni hadi saa 1.50 usiku. Mdahalo huu utakuwa *live* kupitia *Star TV*. Mwenyekiti wa Mdahalo ni Ndugu Rosemary Mwakitwange. Mdahalo huo unahusu:

"*The Tanzania We Want*". Mada inasema Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tanzania tunayoitaka.

Wazungumzaji wa Mdahalo huu ni Mheshimiwa Job Ndugai Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Tundu Lissu, Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Katika mechi hii naomba kulitangazia Bunge kwamba Mheshimiwa Naibu Spika ameshashinda tayari. *(Makofi/Kicheko)*

Liko tangazo la semina bado halijawekwa vizuri kama nikiletewa badaaye kidogo nitawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na kesho, lakini bado sijalipata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadiriio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012
### Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimelazimika sasa kuwajulisha wapiga kura wangu wa Jimbo la Maswa Mashariki kwamba kazi sasa ndio imeanza. Nawashukuru sana kwa kura zao nyingi walizoweza kunipa na ninawahakikishia kwamba nitasimamia haki zao zote na mambo yote yaweze kuwezekana pamoja na kuwa yamechukua miaka hamsini (50). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hoja hii nitajadili suala la ujenzi wa vituo vya Polisi pamoja na makazi ya Polisi. Nilikuwa nina matarajio makubwa sana kwamba katika Makadirio ya Wizara hii nitaona ujenzi wa makazi ya askari Polisi wa Wilaya ya Maswa.

Wilaya ya Maswa ni kati ya Wilaya kongwe zilizoanzishwa na Wakoloni mwaka 1927, cha kusikitisha Wilaya hii haijajengewa Kituo cha Polisi cha Wilaya. Wilaya hii Polisi hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Kituo wanachotumia yalikuwa ni maghala madogo madogo ya Wizara ya Kilimo, kwa maana hiyo *OCD* analazimika sasa akajibane kwenye chumba kingine mbali. *OC CID* naye anaenda kufanya kazi maeneo mengine mbali. Kwa maana hiyo wakubwa hawa wanashindwa hata kusimamia vizuri utendaji wa askari walioko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine cha kusikitisha majengo haya wanayoyatumia kama Kituo cha Wilaya cha Polisi ni majengo ya zamani, yamejengwa mwaka 1927 hivi sasa yanawa-*bip* askari wetu hawa. Majengo hayo yana-*bip* yanasema niue nisiue. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni mazingira magumu tunawakatisha tamaa pamoja na kwamba askari hawa wana moyo sana. Nilitarajia kabisa katika Makadirio haya watakuwa wameingiziwa kwenye mpango wa kujengewa makazi yao na kituo chao cha kisasa cha Polisi cha Wilaya.

Lakini nilichoshangaa nimeangaliwa kwenye kitabu hiki hakuna hata yale matumaini yanayoashiria yaliyowekwa baada ya Serikali kufikisha miaka 50 imeipangia Wilaya hii kuwajengea makazi bora Askari wa Polisi na Askari wa Magereza na kuwajengea kituo cha Polisi kwa vile kituo kilichopo hakina hadhi ya kuhifadhi nyaraka na vifaa vingine muhimu, kwa kuwa kituo hiki kimeshachakaa ukilinganisha vibanda hivyo vilijengwa miaka 84 iliyopita.

Wakati huohuo Serikali inajisema ni makini, ni Serikali sikivu! Sasa kama kweli Serikali ni makini na kama ni sikivu, naomba basi watu wa Maswa, kwa kuwa waliikosa huduma hii kwa kipindi kirefu sana, wakati umefika sasa Serikali ianze kujua kabisa kwamba ina deni kubwa, iwatendee haki askari walioko Maswa, wajengewe kituo chao cha kisasa. Kwanza askari nilionao ni wasomi, wanashindwa kuutumia usomi wao katika vyumba vidogo vilivyopo pale, havina hata hadhi ya kuitwa vyumba vya Polisi aliye na *degree*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kama tunapenda kuwafanyia kazi Watendaji wetu, askari hawa wanahitaji sasa wajengewe kituo angalau cha kwanza na cha kisasa. Nilitegemea kuona Kituo, kama siku moja nilikwenda Kahama, kuna Kituo cha Polisi Bugarama kwenye mgodi wa madini. Kituo hicho ni cha Kata lakini ni cha kisasa. Nikawa najiuliza, kwanini Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Maswa kinakuwa kama kibanda cha kuku tena wale wa kienyeji ambao mwenye kuku hawajali? Katika hali ya haki, huwezi ukawaweka askari wako ambao wanakufanyia kazi ngumu katika Kituo kama kile.

Naomba basi Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho yake aweze kuhakikisha kwamba kuna deni Wilaya ya Maswa kuwa hajawajengea Kituo cha Wilaya tangu miaka 84 iliyopita. Kwa hiyo, pana haja sasa ya kukumbuka kwamba pamoja na upole wa Wasukuma hawa, ambao huwa hawana maneno mengi zaidi, ndiyo taabu, sasa umefika wakati Wasukuma nao wanahitaji watendewe kama zinavyotendewa Wilaya nyingine. Naomba hili, Serikali inayojisema ni Serikali makini, iliingize sasa kwenye mpango wa ujenzi wa Kituo cha Makazi ili maneno haya yaonekane Serikali inatembea juu ya maneno inayodai kwamba ni Serikali sikivu. Ninaomba tuwatendee haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye makazi ya askari hawa, nyumba ambazo wanalala ni za kizamani sana na zenyewe zina hali mbaya kweli kweli. Askari hawa wanafanya kazi ngumu ya kupambana na matatizo mbalimbali ya kuwalinda wananchi, lakini anapolala askari huyu hawezi hata kupata nafasi ya kuweka luninga yake. Nyumba fupi, imebanana, ndogo na askari akiwa kama mimi, basi atagusa kwenye paa. Kwa hiyo, nimesimama hapa kutetea watu hawa, waangaliwe kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na matumaini makubwa, *IGP* alifika kule kushuhudia wale askari walivyoweza kupambana na majambazi mwaka 2009. Majambazi waliivamia Benki ya *NMB* lakini vijana hawa kwa sababu wana uchungu na nchi yao, waliweza kulinda na kuweza kuyaua majambazi yale. *IGP* alifika, alitembelea makazi ya askari wale na kutembelea kituo hicho na wananchi akakaanao kikao na wakaanza hata kuchangia fedha zao ili waweze kujengewa Kituo cha Wilaya kilicho bora. Lakini nimeshangaa kutokuona kwamba huu mpango ameufikisha Serikalini ili ione haja ya watu hawa kujengewa kituo cha kisasa. Alifika mwenyewe na wananchi wakajitolea kuchangia pesa mbele yake wakapata mifuko ya saruji 80 na watu walijitolea zikapatikana karibu shilingi milioni tano papo hapo. Nilitegemea kabisa kwa msimamo huo na kwa tamaa hiyo ya wananchi kupata kituo kizuri ili kuwaenzi askari wao, angeweza kulipeleka jambo hili kwa Waziri ili liingizwe kwenye mpango. Lakini nimeona kimya na hakuna habari tena kwamba hawa watu wana matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uzito wa jambo hili, naomba sasa hao watu ambao wamelala muda mrefu, wameshaamka na kwa kupitia mimi, nadai haki hiyo iweze kuwaendea watu wa Maswa Mashariki na Maswa kwa ujumla. Nimeondoka kwenye hiyo sehemu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kazi moja ambayo askari wetu katika Mkoa wa Shinyanga hutumika kwenda kulinda migodi ya wawekezaji. Katika Mkoa wa Shinyanga, migodi ambayo inatambulika ya madini, ni mitano. Kuna mgodi wa Kakola, kuna mgodi wa Buzwagi, kuna mgodi wa *New Almasi*, kuna mgodi wa *Elhilaly Diamonds*, kuna mgodi wa *Williamson*. Sasa askari hawa katika Wilaya za Mkoa wa Shinyanga huwa wanatumika kwenda kulinda mgodi. Lakini ambacho kinashangaza, katika posho wanazolipwa zinatofautiana. Wanaolinda Kakola na Buzwagi wanalipwa kwa siku Sh. 25,000/=, wanaolinda *Williamson Diamonds* na *New Almasi* pamoja na *Elhilaly* wanalipwa Sh. 10,000/=. Wakiuliza, eti wanaambiwa hawa wanaolinda *Williamson Diamonds*, *Elhalaly* na *New Almasi* ni migodi ambayo bado inafanya uchunguzi. Sasa mimi nashangaa, *Williamson Diamonds* ni mgodi umeanzishwa mwaka 1944, leo eti wako katika upembuzi wanafanya kwa hasara. Kweli inaingia akilini? Vijana wetu wanaokwenda kujitafutia madini kwenye mgodi ule wa *New Almasi* ambao wala hauko kwenye himaya ya yeyote wanakamatwa. Sasa wanawakamata kwanini kama hawajajua kwamba pana almasi pale? Kuna sababu gani ya kuwakamata vijana mpaka inafikia hatua ya kuwaua?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo inakuwa ni nini? Ninaomba nipewe majibu, kwanini askari wanaofanya kazi katika mazingira magumu wanalipwa posho zinazotofautiana? Wengine wanalipwa Sh. 10,000/=. Hivi Sh. 10,000/= hata ungepewa wewe, unakwenda kulinda eneo ambalo unaweza hata kupoteza maisha yako, unaweza kweli ukakubali? Huu utii tunaomba sasa tuuwekee ile haki yake ya msingi. Askari wetu wapewe posho zinazofanana na kazi kubwa wanayoifanya. Ni askari waaminifu na wanahitaji kuheshimiwa na wanahitaji kuthaminiwa. Nimetoka hapo*. (Kicheko/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna utaratibu wa mgao wa mafuta yanayotumika kwenye magari ya Polisi, katika Mkoa wetu askari wanapewa kwenye Kituo cha Maswa lita 200 kwa mwezi. Lakini kituo cha Maswa pande nne za dunia kuzunguka Wilaya nzima kina umbali wa zaidi ya kilomita 100. Lakini sasa mafuta yanatolewa Shinyanga, *OCD* analazimika ayafuate Shinyanga kwa kutumia lita 50 kuyafuata mafuta ambayo mgao wake ni lita 200, maana yake ni kwamba tayari mafuta yanaanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajiuliza, hivi ni busara gani *OCD* tuliyemkabidhi kulinda watu na mali zao, amesoma, msomi, tena vijana wa kule ni wasomi, lakini inakuwaje asiingiziwe hela yeye mwenyewe kwenye Wilaya yake lita zake 200 akakaanazo yeye mwenyewe na aanze kuzitumia? Sasa anarudi na mafuta lita 150, ni sawa na kusema kwamba amepewa kwa siku atumie lita tano. Kumbuka wanakwenda kupambana na majambazi, ameitwa labda mwisho kabisa wa Wilaya, huyu askari umempa lita tano, sijui hata hilo gari litangurumaje! Mimi nashindwa hata kuelewa! Tanki ya gari ni zaidi ya lita 50 mengine ni 100, sasa umempa lita tano, basi tukubali limenguruma, limekwenda, sasa anaowafuata ni majambazi wale watakuwa wametulia. Si maana yake lazima atapambana kuwafuata na gari lazima litembee maili nyingi? Sasa inakuwaje mchezo huu wa kisanii? Unampa lita tano, kweli una makusudi atulinde huyu? Kuna nia ya kweli? Kuna Serikali makini kweli pale? Kuna umakini gani askari unampa mchezo ambao leo na kesho kutwa anaanza kulaumiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwahurumia watu wa Maswa, mimi mara nyingi najitolea sana kuwalipia mafuta askari ili waweze kufanya kazi yao. Mimi ni kati ya Wabunge masikini kweli kweli. Kama kuna Mbunge amepambana kwenye uchaguzi akiwa choka mbaya ni Kasulumbayi. Lakini kwa upendo kwa wananchi wangu, huwa namega kaposho kadogo ninakokapata, nawasaidia askari waweze kuwalinda watu hawa. Sasa wakati umefika, Serikali inayojiita ni makini iweze kutenga fungu la kutosha ili watu hawa waweze kufanya kazi yao vizuri. Natoka kwenye hilo. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa matumizi ya posho, endelea.

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuja kwenye polisi jamii. Kuna vijana wazuri wamepangwa na *OCD* wa kuweza kusimamia Kata. Kila Kata imepewa askari Polisi kwa ajili ya Polisi jamii. Wilaya ya Maswa ina Kata 26...

*(Hapa kengele iligonga kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**WABUNGE FULANI:** Endelea!

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Livingston Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Zuberi.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukushukuru sana na kwa kweli kama ninavyosema siku zote, tunamshukuru Mungu aliyetuwezesha kufika hapa. Nisiwe mchoyo wa fadhila, Mheshimiwa Kasulumbayi ni mmoja wa Wabunge bora sana wa CHADEMA na amechangia vizuri sana. Nampongeza, maana isije ikaonekana kila Mbunge wa CCM akisimama ana nongwa. Mtu mzuri sana Mheshimiwa Kasulumbayi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara kwa kufanya kazi nzuri ambayo hata baadhi ya Wabunge wenzetu wa Upinzani sasa wanakiri kwamba kuna askari wasomi kwenye maeneo yao waliyosomeshwa na Serikali hii makini. Maana hawakujisomesha wenyewe, walisomeshwa na Serikali makini ambayo imepeleka wasomi mpaka Wabunge wanasimama hapa kusifu jitihada nzuri ya Serikali yetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mkuu wa Jeshi la Polisi na niwaambie, mkisikia watu wanapiga kelele, kamateni hapo hapo. Kwenye habari ya dola inatakiwa ionekane kwamba inasimamia haki na kusimamia haki kunawafurahisha wale wanaodhulumiwa haki vilevile. Tusije tukafikiri kwamba pande zote hizi utazifurahisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia uboreshaji wa Magereza, Magereza yaliyoko tu pamoja na hali mbaya iliyoko huko, bado kuna watu wanavunja sheria kila siku na ukienda unawakuta ni hao hao. Yakiboreshwa zaidi itakuwa taabu vilevile. Lazima tukubali kwamba katika Afrika hatujafikia huko kuweka Magereza yetu yawe na nyota tatu za hotel. Yakifikia hapo, itakuwa ni taabu. Kuna watu watashinda huko huko. Hivi yalivyo watu wanatamani kwenda: Je, yakiwa na hali nzuri, itakuwaje? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza kwamba CCM ni Chama dola hata wenzetu hawa wanayoitaka Serikali wanaitaka iwe chama dola vilevile. Wala hawaitaki kwa sababu ya kuja kufanya kazi za Kanisa. Hawa wanajua ukitaka kwenda Mbinguni ingia kwenye dini yako, mwabudu Mungu. Huku wanafuata nini? Wanatafuta kutawala nchi, wanatafuta kuongoza, wanatafuta kumiliki Jeshi na kumiliki Polisi na ndiyo maana hata kwenye Vyama vyao kuna kanuni na huwa zinafanya kazi kwa mujibu wa kanuni, na kwamba asiyefuata kanuni yetu, huyu anaadhibiwa; na kwa mujibu wa kanuni za nchi wanaokosea wanaadhibiwa. Hatuwezi tukaja hapa tukazungumza vitu ambavyo wala havipo kwenye Wizara hii. Mtu anasimama anaanza kuzungumza, ooh, sungura huyo miaka 50 hakui, hivi sungura huwa anakua? Mnataka kudanganya watu! Sungura hata miaka mia anabaki kuwa sungura, au sungura wa kichina? *(Kicheko)*

Maana sungura atabaki kuwa sungura, tusiwadanganye Watanzania kwamba eti sungura miaka 50 hakui. Kuna sungura gani anakua kupita kimo alichonacho sungura? Sungura anabaki kama alivyo. Kwa hiyo, kama Waziri angeleta hapa bajeti imendikwa sungura, tungejadili sungura. Lakini kwenye bajeti sijaona sungura. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunang'ang'ania kwamba boresha Jeshi, imarisha askari wawe watiifu kama Sheria zinavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mtera lina Kata 19 lakini lina Kituo kimoja cha Polisi kati ya Tarafa tatu. Kwa hiyo, naomba sana Serikali itupatie Kituo cha Polisi kila Tarafa ili Tarafa tatu ziwe na Vituo vitatu vya Polisi ambavyo vimekamilika. Pia tunaomba mtupatie askari wa kutosha, vilevile mtupatie na usafiri. Wilaya nzima ya Chamwino ina gari sijui moja ambalo ni zima. Wilaya yenyewe ina zaidi ya Kata 30 na kitu, ina umbali mkubwa. Kwa mfano, kutoka mwanzo tu wa Jimbo la Mtera mpaka mwisho, kuna Kilomita karibu 246. Kwa hiyo, unaweza kuona gari likienda

mpaka mwisho wa Jimbo inachukua muda mrefu sana. Kwa hiyo, nawaomba sana Serikali itupatie vitendea kazi vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna vitu vingine vinachekesha kidogo. Watu wanazungumzia usalama kana kwamba hawaujui. Hivi magari ya thamani waliyonayo Wabunge hapo nje, dhahabu wanazotupia baadhi ya Wabunge akina mama, bila Polisi nyie mngevaa hizo? Isingewezekana, wangeporwa hawa. Hebu vaa hizo halafu pita sehemu ambazo hakuna usalama kama utavaa. Lazima tuheshimu kwamba Polisi wametufikisha mahali hii nchi watu tunaishi kwa amani. Polisi wamefanya kazi nzuri sana. Maana Tanzania sasa kumeingia chuki. Kuna baadhi yetu sisi Wabunge tunaendesha magari ya *V8* yako hapo nje, hawa wananchi wanayaona lakini tunataka Mawaziri wapande Bajaj, inawezekana? Hakuna kitu cha namna hiyo! Wabunge tuishi maisha mazuri, tutupie dhahabu karibu za malaki, halafu tunajifanya tuna uchungu na Majimbo yetu. Sijui tulikotoka makamanda, mbona huuzi dhahabu ukasaidia watu wanaolala na njaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie habari ya wabishi. Wabishi ndiyo waliosababisha mpaka Polisi wanapiga. Mtu anaambiwa, twende Kituoni, anasema siendi. Haya sasa, unampelekaje? Maana hata barabara ukikuta ina tuta kubwa, ujue hapo kuna madereva wabishi. Tuta ndiyo Polisi wa dereva mbishi. Mtu anaambiwa endesha taratibu, anatoa macho. Wakaweka tuta. Akija mwenyewe anakutana na tuta ambalo ni bishi zaidi ya yeye, anazima sigara, anapita kiustaarabu. Kwa hiyo, Polisi akifika akamwambia mtu twende, haendi; twende kituoni, haendi; anafanyaje? Kibao kimoja, nakwenda! Yule yule aliyekuwa anabisha!

Mheshimiwa Naibu Spika, habari ya kuandamana, acha waendelee kuandamana. Kwa sababu niliwaambia siku ile wanafanya mazoezi ya sukari na wala siyo kweli kwamba hayo ni mazoezi ya kupunguza miili na nini. Maandamano yanayochukua masaa mawili siyo maandamano ya kututisha CCM. CCM ni Chama kilichokomaa, hakiwezi kuondolewa na maandamano bwana. Maandamano acheni wapige, porojo acheni wapige, lakini iko siku Watanzania wataamua. Huo ndiyo ukweli bwana. Hatuko hapa kuja kusema eti, ooh, maandamano yanapokelewa na watu wengi; na yakipokelewa na watu wengi inakuaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani jana alipongeza Malawi, akasema, kule makamanda wanafanya kazi. Wale makamanda wa Malawi wanatoa Serikali ya upinzani ile kama hujui. Ile Serikali ni ya Upinzani wanayoitoa pale, wamegundua hawana uwezo. Maana kuna vitu vingine unatoa tu *data* hawa watu hawazielewi vizuri. Ile Serikali siyo Serikali iliyodai uhuru, ni Serikali iliyoingia kwa mageuzi, imeonekana haifai, watu wanaandamana. Kwa hiyo, hata ninyi mtakuja kutolewa katika Majimbo yenu kwa mtindo huo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke kwamba unapomtaja Rais, uzito wa Rais unakuja pamoja na vyombo anavyovimiliki. Jeshi, Polisi na Usalama wa Taifa. Hivyo ndivyo vinavyompa nguvu ya kumpa Mheshimiwa Rais hadhi ya kuitwa Rais, anatawala nchi. Hakuna nchi ya namna hiyo, hata Mungu alikuwa na askari wake. Imeandikwa kwenye vitabu vya dini. Nenda kwenye vitabu vya Kiislam unakuta akina Omar Bin Hatwabi. Sisi wasomi wa dini hiyo tunajua, ukija kwenye vitabu vya Kikristo utawakuta akina Daudi waliopambana na akina Goliati, wasomi tunaelewa. Kwa hiyo, ndugu zangu, habari ya Jeshi kwenda pale nalenale askari wanakwenda wanaringaringa kumkamata mhalifu, hata aliyekuja kutoa taarifa atakuwa hana imani. Askari lazima awe mkakamavu na sisi raia tuwafundishe watu wetu waheshimu vyombo vya dola.

Tumemfundisha askari kwa kodi, tumemsomesha askari kwa kodi ya Watanzania, tumempa *uniform*, tumemwajiri kazi, tumempa silaha halafu wewe hutaki kumheshimu, kwanini? Maana ya huyo askari itakuwa ni nini sasa? Itakuwa haipo! Lazima tuwaheshimu. Sisi hapa tuko, tunaongea kwa amani na utulivu, nje kuna askari. Lakini kama tukivurugana humu tukazima taa kukawa hakuelewiki, wakiingia *FFU* ni mkong'oto. Hawajali kuna Mbunge, kuna Naibu Spika, hawawezi kuelewa hilo. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde hata ndani kuna askari vilevile.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Unaona Bwana! Kukurukukuru humu, wakiingia humu ndani ni mkong'oto. Hawawezi kujua huyu ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, huyu ni Waziri, huyu ni nani. Maana yake nini? Wanatafuta mahali hapo pawe na amani. Kwa hiyo, askari wetu tunapozungumza tuwajengee heshima kwa wapigakura wetu, tuwajengee heshima kwa wananchi wetu. Askari akisema ondoka eneo hili, ondoka. Unabishana naye nini sasa? Maana yeye kaja kukwambia, kwa sasa eneo hili hamtakiwi kuwepo. Wewe unasema, sisi tutakuwepo! Halafu aje aanze kukuchekea! Akikuchekea, hiyo kazi ya uaskari ataifanyeje? Haiwezekani! Lazima ifike mahali tuheshimu vyombo vyetu vya dola kama tunavyotaka kuheshimiwa sisi. Tukiwa wa kwanza sisi kuwahamasisha watu. Maana nimeshangaa jana linatolewa tangazo eti kuwaambia askari msitii. He! Sisi CCM hatuwezi kusema eti wananchi msitii kwenda kwenye maandamano!

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaotaka kwenda kuandamana si waende tu! Kwa hiyo, na askari nao wawatii wale wanaowaongoza, na wanaowaongoza kwa sasa ni Chama cha Mapinduzi, ndiyo kilichopigiwa kura nyingi. Kuna Mbunge anasimama hapa anatupa takwimu kwamba kuna watu wameondoka Upinzani wameingia CCM kwa sababu ya kutishwa. Walioondoka Vyama vingine kwenda Vyama vingine vya Upinzani nao wametishwa na nani? Maana wapo! Wapo watu walioondoka CHADEMA wakaenda Vyama vingine wakafanikiwa. Nako wametishwa na nani? Jamani, acheni siasa za uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mifano iko wazi wazi hata hapa Bungeni. Wewe unasema ooh, wale ambao walikuwa wanasimamia vizuri wametishwa, wamekwenda huku. Wametishwa na nani? Wewe mwenyewe uko kwenye Chama cha nne karibu, unatumia uhuru wako vizuri. Nchi ina uhuru, mtu anahama dini, itakuwa Chama bwana! Kama dini inayompeleka mtu Mbiguni, anabadilisha, anajiunga na dini nyingine, itakuwa Chama cha siasa! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, miongoni mwa vitu vizuri vilivyofanywa na Chama cha Mapinduzi ni kusimamia Dola, kusimamia Majeshi, kutawala nchi vizuri na kuweka sheria nzuri zilizosababisha na baadhi yenu muwemo humu Bungeni, sasa, hata nyie wenyewe ni makosa jamani? Maana kila kinachosemwa ni kibaya tu. Ukiangalia ubaya unaotamkwa wa Jeshi la Polisi na Serikali yetu, huwezi kuamini, yaani ni kama vile watu wanatukana kwamba wananchi hawaelewi, wanachagua Chama ambacho kinawatesa kiasi hicho. Mbona mmepitiliza jamani? Ninyi wenyewe mpo hapa kwa sababu ya matunda mazuri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ndiyo maana mmeitwa Wabunge. Ndiyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, sheria hiyo imepitishwa na Serikali ya CCM. Unajua kuna watu wengine unaweza ukasema mabaya, lakini ukafika mahali ukasema Mungu nakushukuru hata kwa kuniumba tu, ukaishia hapo. Eeh! Maana inawezekana huna viatu vizuri, huna chakula, lakini mshukuru Mungu kwa kukuumba tu. Basi na ninyi muishukuru CCM kwa kuwaunda tu! Walikutana humu Wabunge wote wa CCM wakasema nchi hii iwe na Vyama vingi. Wote walikuwa wa CCM. Hata hilo mnashindwa kushukuru jamani! Asiye shukuru kwa kidogo, hata kikubwa hawezi kushukuru! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafika mahali tunasema tunapitiliza, hivi hata tukitoka hapo nje, unaweza ukasema labda kuna kampuni gani iko hapo nje. Magari mazuri ya fahari na Watanzania wanaona magari ya Wabunge wa Vyama vyote yako hapo. Mbona sioni Mbunge anayekuja na Bajaj hapa ili kuonyesha kwamba sisi tuna uchungu na nyie, hatupandi magari ya thamani? Watanzania msikubali kudanganywa, pamoja na kuwateteeni, lakini vile vile mmetupa maisha wote tuliyoko hapa. Tumepata ugali ambao hatukuwa nao. Sasa tunakuja hapa tunasema mpaka tunapitiliza, utafikiri hakuna kitu tunachopata humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndugu zangu, nataka niisihi sana Serikali, boresheni maisha ya askari, lakini vile vile nchi hii lazima utawala wa sheria usimamiwe. Msisikilize porojo. Tukishindwa kusimamia watu na haki zao, nchi hii itakuwa siyo mahali pazuri pa kuishi. Tusimwangalie mtu sura yake, tusimwangalie mtu kabila lake wala dini yake, anayekosa achukuliwe hatua, *full stop.* Hizi mbwembwe za kuja kusema tunaonewa, tunaonewa, wakati mwingine mtu anayelia msibani ujue yeye ndiye kaua, ndiye mchawi. Hao wanaopiga kelele humu ndiyo wavunjaji sheria wakubwa, tusiwaonee aibu. Tuanze na hao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani tunapiga kelele hapa, tunapanga bajeti, Polisi waongezewe silaha, wewe unafikiri mabomu ya machozi yanapiga nyoka? Si utakuwa huna akili! Mabomu ya machozi wanapigwa watu, dunia yote, hawapigwi samba wala hawapigwi nyoka. Kwa hiyo, tunapoyapitisha humu Bungeni, maana yake Wabunge wote tunapitisha yanunuliwe ili yaje yatulize fujo. Wewe uliona wapi askari wanafundishwa mafunzo yote yale, halafu baadaye wanaambiwa sasa nendeni mkapambane na simba, acheni watu? Ha! Itakuwa jeshi gani hilo? Jeshi linafundishwa kukabiliana na fujo zinazofanywa na watu na watu wenyewe tukiwepo sisi Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa Mbunge, huna *exemption* ya kufanya fujo mahali popote, eti ooh, mimi Mbunge. Ha! Habari ya kusema kwamba tunakwenda Tarime, sijui Polisi wamekimbia na maiti, leo hii Tarime wamekufa watu, mbona hamjakwenda kuzika kama ninyi watu kweli mnawapenda watu wa Tarime? Watu wanafiki kabisa nyie! Tarime watu wamekufa leo, hamjakwenda kuzika, mnangojea mpaka msiba utokee kwenye dhahabu ndiyo mnatimka mbio!

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE SAID M. ZUBERI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na mwenye kurehemu kwa kutupa afya njema siku hii ya leo Ijumaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, kwanza kabisa, kabla muda wangu haujakwisha, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri husika pamoja na Naibu wake kwa kutuletea hotuba nzuri. Nawapongeza na watendaji wa Wizara hii na niwaambie kabisa kwamba hotuba imekamilika, inachohitaji ni kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu dhana ya utawala bora. Hili nalo niishukuru Serikali kwa ujumla wake kwa kuwa tayari tuna Wizara hizi na hata kule kwetu Zanzibar haya masuala tunayo. Katika dhana ya utawala bora, kuna mambo lazima tukubaliane nayo, tukitaka tusitake. Dhana ya utawala bora pamoja na kukabiliana na matatizo yanayojitokeza, ghasia zinazojitokeza, haya yote ni sawa sawa na kusema kwamba dhana ya utawala bora inakamilika kwa kuleta amani na utulivu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee wa zamani wamesema, mtu mzuri au kitu kizuri huwezi kukielewa ama kukifahamu wakati unacho. Unaweza ukaelewa wakati kile kitu kimeishakutoka au yule mtu ameishakutoka. Kwa hiyo, jamani kuna watu inawezekana kwa kuwa amani bado tunayo, umuhimu wake hawauelewi, lakini itakapotutoka, wataielewa. Sasa tusije tukafikia huko. Mheshimiwa Waziri Shamsi, nakuomba u-*carry on* na masuala haya, twende nayo hivi hivi ili amani hii iendelee kuwepo na tuweze kusema tunachotaka, wala usije ukakubali hata siku moja kusema kwamba ule ushahidi wa Kinyamwezi kwamba tusubiri tuone. Mmepewa kazi hii, mnaimudu vizuri na nafasi mnayo ya kufanya. Fanyeni watu tutulie ili tuendelee na shughuli zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mazuri siku zote huwa hayaachi kuwa na dosari ndogo ndogo. Hizi dosari ninaomba sana zirekebishwe ili tukamilishe hii dhana ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kule Zanzibar kulikuwa kuna masuala ya kesi hizi. Hii nayo ni kuthibitisha kwamba bado nchi yetu tunatawaliwa na utawala bora. Kuna kesi ya mtu ambaye ni mwasisi kule kwetu na imekwenda kwa muda mrefu sana. Sasa hivi imefikia hatua ya utekelezaji na utekelezaji wa dhana ya utawala bora ni Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, bado mna dhamana ya kuhakikisha kwamba jambo hili ambalo tayari limetolewa *ruling* kwa mara ya sita na *ruling* hiyo imefanana kabisa. Zote, za nyuma zikija na hii ya mwisho zinaonyesha kwamba kuna mtu ambaye tena ni mwasisi wa Taifa hili kwa kule kwetu Zanzibar, Said Dibavuai, Marehemu, Mungu amlaze mahali pema. Kesi imeonyesha kwamba inabidi apewe haki zake za ardhi, lakini mpaka leo usimamiaji haujawa mzuri. Haya ni matatizo madogo madogo ambayo ni wajibu wetu kuielekeza Serikali ama eneo husika waweze kusimamia vizuri haya masuala.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna suala la wastaafu wetu hawa. Hili ninalolizungumza mimi sihitaji hata saa mbili, ni dakika tu kwa sababu ushahidi ninao hapa hapa. Kuna suala la wastaafu wetu ambao hawa nitasema walifanyiwa kama kiini macho. Wana kama miaka minne hawajalipwa. Sasa nao vile vile wako kule Zanzibar na wao wako tayari kuonana na Mheshimiwa Waziri ili waeleze matatizo yao. Ninao hapa kwa majina hasa, wengi sana hawa, wana miaka minne hawajalipwa na kuna wengine waliwahi kufungishwa mikataba ambayo sasa mimi nitasema ni mikataba *fake*, kwa sababu huwezi ukamwambia mtu akubali bakshishi baada ya kufanya kazi kwa muda wa miaka 30. Akubali bakshishi ama akubali kwamba alipwe malipo ya uzeeni, tena ukamsainisha. Huu ni uonevu! Naiomba sana Serikali yangu, haya matatizo madogo madogo, basi iweze kuyaweka sawa ili tuendelee vizuri. Tusiwadhulumu hawa, hawa wamepigania nchi, walikuwa ni askari watiifu na sasa hivi ni watu wazima sana, kwa hiyo, bado wanahitaji haki zao. Wako tayari kuonana na wewe ili wakueleze matatizo yao na mengine bila shaka utakuwa unayafahamu. Kwa hiyo, wanakusubiri ili muweze kukaa pamoja na kujua jinsi gani, bado wao wanaendelea kuwa watiifu, wanaweza kupata haki zao. Pensheni zao hawajapata kabisa na kuna wengine ndiyo wamedanganywa danganywa kwa masuala haya ya mkataba ambao ninao hapa, unaonyesha kwamba fedha zao za mafao yao hawakulipwa na hawalipwi kwa mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, mimi nipongeze Jeshi la Polisi hususan kule Zanzibar kuhusu kazi za kuzuia dawa za kulevya. Hivi karibuni tu, *airport* pale kuna mtu alikamatwa. Serikali imefanya kazi nzuri au nitasema Jeshi la Polisi limefanya kazi nzuri. Kwa upande wetu kule Zanzibar suala hili sasa hivi limepungua kwa asilimia kubwa na wale waliokuwa wanajishughulisha na masuala haya ya dawa za kulevya, wengi wao sasa hivi wanaepukana nayo na kuna vitengo maalum vya kuwashughulikia. Hili nawapongeza, lakini naomba Wizara kwa pamoja kwamba wahakikishe kwamba, basi hawa watu kuwe kuna *incentives* maalum kwamba wanapofanya mambo kama haya mazuri, kwa sababu pale inawezekana wakawa wanalaghaiwa, wanaaihidiwa kwamba niachie, nitakupa kitu fulani, na hawa watu wanaofanya hii biashara, ni watu wenye fedha nyingi. Lakini inawekana mtu akaweka uzalendo mbele, akaacha umaskini wake akasema kwamba huyu namkamata. Basi lazima tuwe na motisha kwa watu kama hawa, tuweze kuwasaidia ili tuweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, majukumu yako kumi. Alizungumzia suala zima la ulinzi shirikishi, vile vile akazungumzia katika majukumu hayo kumi suala la ujenzi na ukarabati wa vituo. Kwa upande wa Jimboni kwangu, Fuoni, tuna kituo pale ambacho unakijua vizuri sana kwa sababu Jimbo langu na la kwako limepakana na hiki kituo kiko mpakani. Wenyewe wananchi pale wamejitahidi vya kutosha kuhakikisha kwamba wanasimamisha kituo. Ulinzi shirikishi kwa upande wetu walikuja watu wako na wakahamasisha na watu wote wamehamasika sana. Hivi sasa wanalinda wenyewe maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba hicho kituo basi, ili kuwaongezea *morality*, kimaliziwe. Kimekwisha, kimeshaezekwa, lakini kuna mambo madogo madogo tu. Nakuomba sana Mheshimiwa na kwa vile najua ni mdau pale, na bado unaendelea kulihitaji lile Jimbo na nafasi ya kusema huna, basi hili suala usije ukaacha kulisema, watakuwa wanakusikiliza utalijibu vipi. Nakuomba sana uhakikishe kwamba kile kituo kinamalizwa ili watu waweze kufanya shughuli zao. Pale pana watu wametoka mpaka kwenye eneo lako Mheshimiwa Waziri, Uwanja wa Magrisi pamoja na Taveta, wote wanashirikiana kwa pamoja na watu wa juu huku wa Nyarugusu kuhakikisha kwamba eneo lile lina usalama. Na sasa hivi ukienda utagundua kwamba kweli lile eneo sasa hivi ni zuri sana na lina usalama wa kutosha. Kwa hiyo, hiki kituo chao au kituo chetu, nakuomba sana utusaidie kimalizike. Sadaka huanzia nyumbani. Kwa hiyo, na wewe pale ni nyumbani, lile ni Jimbo lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe suala la ujenzi ama ukarabati nilitegemea labda na kituo chetu kikubwa cha Fuoni tungekiona humu. Lakini ukweli, sijakiona. Nacho vile vile, naomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi vya kutosha kuhakikisha kwamba, kwa sababu kile kituo sasa hivi ni kibovu sana, kimechakaa, nyufa tupu, basi *at least* kiweze kupanuliwa kiwe kikubwa na kifanyiwe ukarabati wa hali ya juu ama kivunjwe kabisa kwa sababu kisije kikaja kikawaangukia hao askari kama alivyosema mwenzangu kule. Kituo kina nyufa kabisa, hakikidhi haja, eneo limekuwa kubwa sana. Kwa hiyo, naomba na hiki kituo chetu cha Fuoni kifikiriwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uhamiaji, naiomba Serikali hii Tukufu, Serikali hii sikivu, tuwe tuna utaratibu wa kurahisisha haya mambo, kwa sababu mtu kutaka *passport* sasa hivi kwa kweli imekuwa hali ngumu. Mtu anaweza akaenda akarudi na kumbe ni haki yake kabisa. Wakamilishe watu taratibu, lakini wanapokamilisha taratibu, basi tena kusiwe na mizunguko ya huku na kule. Wapewe watu, hii ni haki yao.

Kama tunavyosema kwamba Serikali haiwezi kuajiri watu wote, kuna watu wanatoka wanakwenda kuajiriwa sehemu nyingine. Lakini, ukweli wanakuwa wanashindwa kufika huko kwa sababu ya mlolongo wa upatikanaji wa hizi *passport*. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, watu wakishakamilisha vigezo, basi tena kusiwe na tatizo la kupata *passport* ama mtu kuchukua muda, na huku ndiyo kurahisisha mwanzo wa rushwa. Sasa ili tuepukane na mambo haya, tujue kwamba hii ni haki ya mtu, na tukishaelewa kwamba huyu mtu ni mwananchi halisi, hana matatizo, ana vigezo vyote, basi hili suala likamilike ili hawa watu watoto wetu, vijana wetu wendelee huko kwenda kuomba ajira huko mbele. Huku kwetu hatuwezi kuwakamilishia wote, basi haya mengine ambayo yako kwenye uwezo wao, tuwakamilishie ili waweze na wao kwenda kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, linguine ni kuhusu suala la posho na pamoja na *transfer* wanazopewa askari wetu. Mimi nakiri kabisa kwamba askari wetu ni wavumilivu, watiifu sana na kazi yao huondoa ghasia. Sasa tusiwatengenezee mazingira ya kuwafanya wao ndio wakaanzisha maandamano, tuwawekee mazingira ya kuhakikisha kwamba wao kazi yao ni kutuliza hizi ghasia ama kutuliza maandamano. Kama hatujawa na utaratibu mzuri, tusiwahamishe, tuache. Kama kuna ulazima wa kuwahamisha, basi kuwe kuna fedha, zitengwe za dharura ili linapotokezea tatizo hilo ziweze kutumika, wanapokwenda kule wasiweze kupata matatizo. Hili naomba sana tujitahidi ili Jeshi letu mpaka sasa hivi kama tunavyozungumza, sote tunakiri kwamba linatii sana, lina uaminifu mkubwa sana. Sasa, tusiwanyanyase kwa utiifu wao huu. Haya matatizo yao tujitahidi kuyatatua na hususan hili la kuwahamisha, kuwatoa huku, ukawapeleka huku, halafu tena mtu akawa hajijui, anaambiwa wewe utasubiri mwaka mmoja, utapata labda fedha, ameshatumia, mwaka unapita na hakuna chochote kinachotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili naomba sana Serikali hii sikivu na Mheshimiwa Waziri tabia yako naijua sana tangu ulipokuwa Waziri Kiongozi, ni mtu ambaye anapenda sana kuhakikisha kwamba kila mtu anapata haki yake kwa wakati muafaka. Basi naomba hawa askari wanaopata haya masula ya *transfer* waweze nao kupata fedha zao kwa wakati ili kuepusha mlolongo. Maana tukifikia hatua tena na wao wakisema sasa waje kuandamana, sijui hii hali itakuwaje. Kwa hiyo, hili naliomba sana. Ikifikia muda, tuhakikishe kwamba hawa tunapowapa *transfer* na hili suala tunalikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kabisa, mimi tu nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Jeshi lake hususan *IGP* Said Mwema kwa ukakamavu wao walioonyesha. Mambo haya madogo madogo kwenye utendaji hayawezi kuepukika, lazima yatatokezea tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kuchangia hoja iliyopo Mezani sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake kwa kuleta hotuba hii nzuri kabisa ya Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Jeshi letu la Polisi kwa kazi nzuri linalofanya ya kutulinda sisi raia na mali zetu. Wote tunajua jitihada za Jeshi hili, linapambana vikali katika kuleta ulinzi wetu sisi wote. Kwa hiyo, nasema, Jeshi la Polisi msirudi nyuma. Kazeni buti, songeni mbele, achana na kusikiliza maneno ya hapa na pale, fanyeni kazi zenu vizuri, endeleeni kutulinda mradi mnafuata sheria na taratibu za kazi zenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uhalifu nchini kwetu wote tunaona kawa umepungua. Lakini, kuna uhalifu wa aina mpya ambao umejitokeza duniani. Kwa hiyo, na sisi kama nchi ni lazima

tujipange vizuri kupambana na uhalifu huo. Uhalifu huo ni ule uhalifu ambao ni uhalifu kwa njia ya mtandao *(cyber crimes).*

Mheshimiwa Naibu Spika, uhalifu huu umeletwa na ukuaji wa maendeleo ya sayansi na teknolojia katika ulimwengu. Uhalifu huu kwa kweli umeenea duniani na sisi Tanzania kama sehemu ya dunia tusipojiandaa vyema utatuumiza. Uhalifu wa kimtandao unaingia katika wizi wa mabenki, wizi wa takwimu na *information* mbalimbali, na unaweza ukasambaza taarifa hizo mbalimbali kwa watu mbalimbali duniani, tujiandae vizuri kama si hivyo tutaumia. Tuweke bajeti ya kutosha ya mafunzo ya watu wetu ili tupate watalaamu wa kutosha wa kupambana na uhalifu huu, vinginevyo tutaachwa nyuma na tutaumia kama nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano tumeuona, kuna wizi wa fedha zimeibiwa kupitia *ATM's*, fedha zinapotea, tujitahidi nchi yetu isije ikakumbwa na maafa makubwa kupitia uhalifu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matatizo ya madawa ya kulevya, nchi yetu imeathirika, vijana wetu wameathirika sana, na kama wazazi tunaumia kabisa kuona tatizo hili bado linaendelea, hili ni tatizo sugu kweli, wote tunakubali, lakini Serikali ipange mikakati na mbinu tofauti za kupambana na tatizo hilo kwa sababu wahalifu hawa wanageuza mbinu kila uchao, kwa hiyo na sisi tuwe makini kuweza kupambana nalo ili watoto wetu wasiendelee kuathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kule Zanzibar wamejaribu kurekebisha Sheria za Kupambana na Madawa ya Kulevya, wameingiza kipengele kwamba kijana yeyote anayekutwa anasinzia ovyo ovyo hata kama hakukukamatwa na madawa ya kulevya mkononi, akienda akipimwa choo kidogo akionekana kuna alama za madawa ya kulevya anakwenda kufungwa miezi sita. Hili linasaidia kiasi fulani. Lakini vile vile kimewekwa kipengele kwamba yule kijana anakoishi na wazazi wake au wapangaji wa ile nyumba, yule kijana anayeuza yale madawa, na kama wale watu itathibitika kuwa wanajua lakini wamemficha, wale wazazi au wapangaji na wao wanakwenda jela miaka saba. Kwa hiyo, sasa hivi wapangaji wanasaidia kuwafichua wauza unga, na wauza unga wanakimbia katika majumba yao kwa sababu wanaona watawahatarisha wazee wao na watakwenda kufungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile askari wanapita katika vijiwe vyote kuchunguza nani anakula unga na nani anauza unga na zaidi wanahangaikia katika maeneo ya pale mjini Unguja, kwa hiyo, uhalifu sasa umeanza kuhama katika maeneo yale ya mjini, wanaenda pembezoni mwa mji. Kwa hiyo, Jeshi la Polisi lisiwe linafanya kazi mijini tu, lakini vile vile na maeneo ya pembezoni mwa Mji waendelee kufanya huo msako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi au Ulinzi Shirikishi, wenzangu wengi wamezungumza, ni kitu ambacho ni cha kupongezwa sana, ni kitu kizuri kinasaidia sana ulinzi katika maeneo yetu. Kwa hili napenda nimpongeze Kamishna wetu wa Polisi Ndugu Mussa, amefanya ziara katika Shehia zote kutoa elimu, kupanga mikakati ili kulifanikisha hili. Nampongeza sana na ninaomba liendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Nyumba za Polisi na vituo vya Polisi, wenzangu wengi wamezungumzia lakini na mimi nimeguswa, kwa sababu katika Mkoa wangu wa Kaskazini Unguja, ni Askari Polisi wachache tu wanaoishi ndani ya ule Mkoa, lakini wengi wao wanaishi mitaani huko mijini na maeneo mengine. Kwa hiyo, inakuwa taabu hata kupata usafiri kuja katika shughuli zao za kazi, kwanza usafiri wenyewe hawana, hawana pikipiki, hawana baiskeli, Wabunge wengine pia wameongea kuhusu hili. Vile vile kunajengeka urafiki katika Mitaa wanayoishi, kwa hiyo, kama askari inakuwa taabu, wanadharaulika kwa vile wanakaa vijiweni, wanakuwa ma-*brother men* na *sister women.* Aidha, wanajenga udugu wa karibu na raia. Kwa hiyo, hata uhalifu ukitokea watu wanakuwa na ile kusema kwamba huyu mimi ni rafiki yangu wa pembeni, huyu mimi ni dada yangu wa pembeni, huyu mimi ni kaka yangu wa Mtaani. Kwa hiyo, hii inakuwa haisadii katika kupambana na uhalifu. Tujenge nyumba za maaskari, tuna maeneo mengi kule Mkoani, Mahonda pale pana eneo la kutosha, Mfenesini kuna maeneo na hati tayari wanazo.

Mhehsimiwa Naibu Spika, sikuona katika bajeti hii kutajwa Mkoa wa Kaskazini kama kutajengwa kitu chochote, kwa hiyo, naomba Waziri afikirie na Mkoa wa Kaskazini. Vile vile kuna vituo vingine ambavyo vipo hatarini kwa mfano kituo chetu cha Malindi. Nimeambiwa kituo kile

kinadidimia, na wahalifu sasa hivi hawawekwi pale mahabusu, wanatafutiwa vituo vingine kupelekwa. Naomba kituo kile kiangaliwe, ni kituo kimoja muhimu sana kule Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kukatika kwa umeme mara kwa mara, naomba sana vituo vyetu hivi vya Polisi vipatiwe angalau majenereta. Unapokatika umeme vituo viwashwe jenerata, umeme upatikane na kazi ziendelee. Hata pale Makao Makuu ya Polisi Zanzibar iwekwe jenerata kubwa tu inayoweza kusaidia kituo kile kufanya kazi, bila hivyo umeme ukikatika kazi zinasimama, na kazi ya Polisi ni kazi ya muda wote, askari wanatakiwa wawepo kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti zilizopita, nilizungumzia kuhusu kikosi cha mbwa pale Makao Makuu Zanzibar. Nashukuru Mbwa wapo, lakini gari ya kuwasafirishia wale mbwa kwenda sehemu ya tukio hawana, sasa watafanya nini? Watabeba mbwa kwenye baiskeli, itawezekana kweli? Mbwa siyo kiti moto kama unamweka kwenye susu unampeleka sokoni ama unampeleka machinjioni kwenda kumchinja. Wale ni mbwa wa askari wanatakiwa wawe na gari maalum ya kufikishwa wanakotakiwa kufanya kazi. Kama siyo hivyo, watafikaje? Sasa hivi kuna matukio mbalimbali, yapo ya madawa ya kulevya na mambo mengine ambayo yanataka ithibati ya mbwa yule aseme hiki ni kitu fulani. Kwa hiyo, naomba sana wapatiwe gari la mbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kasulumbayi amezungumza hapa, mafuta wanayopewa vikosi katika Wilaya kwamba ni kidogo mno kuwawezesha kwenda katika shughuli zao katika kipindi cha mwezi mzima. Wakipewa lita 100 za mafuta, kama kule kwenye kituo changu cha Mahonda cha Wilaya, kuna gari mbili ya *OCD* na gari ya operesheni, lita 200 hizo wanagawana kila gari inapata 100. Sasa hivi kuna matukio mengi tu yanatokea ambayo yanataka kukimbilia. Sasa ukiwapa mafuta kidogo hivyo, halafu tutawalaumu kweli hawakufanya kazi? Watafikaje? Kwa mguu hawawezi kufika, gari ikiwekwa mafuta lita mbili tatu au nne inazimika njiani, ni aibu pia kwa Serikali. Gari ya Polisi kuzimika njiani, haiwezekani hasa katika kipindi hiki tulichonancho ndugu zangu. Waongezewe mafuta ili wafanye kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasisitiza sana ajira ya Polisi zipitie katika makambi yetu, *JKU* na *JKT* ikikosekana watu wenye sifa wanaohitajika katika Kambi hizo ndiyo wachukuliwe kutoka maeneo mbalimbali. Katika mgawo wa Mkoa, sisi kule Kaskazini kipindi hiki tumeletewa nafasi kwamba anatakiwa mwanamke mmoja tu kwenda kwenye mafunzo ya uaskari. Lakini linaloshangaza, wakimaliza mafunzo, wanarudishwa zaidi ya watano, wale wengine wametokea wapi na sisi tumetoa mmoja tu katika mgawo wetu? Ina maana Mikoa mingine wanapata mgawo mkubwa kuliko Mikoa mingine na hatimaye tunaletewa sisi kuajiri katika Mkoa. Hili tunaomba liangaliwe.

Mhehsimiwa Naibu Spika, Idara ya Uhamiaji Zanzibar ni Idara yatima, Idara ambayo haina pesa za kutosha, wanatengeneza bajeti wanaleta Makao Makuu, lakini hawarudishiwi bajeti yao kwa kisingizio kwamba wanakusanya mapato. Mapato yenyewe mangapi wanayokusanya? Wanakusanya mapato machache tu na wanagawana na *SMZ*. Wana mambo chungu nzima ya kufanya, yamesimama hayaendelei kwa kuwa hakuna pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri aangalie Idara ya Uhamiaji Zanzibar. Mimi nimepitia katika Kitabu chetu cha bajeti katika sehemu ya Wizara, nimeona Idara ya Uhamiaji ina bajeti *line* tatu tu, ni mshahara, posho na *contingency.* Lakini ukiangalia kwenye Ofisi za Mikoani Bara zina *item* karibu 23 ikiwemo mafuta, mavazi, madudu gani yamejaa tele, kwanini Idara ya Uhamiaji Zanzibar ifanywe kama mtoto mdogo? Kwanini isipewe bajeti yake ya kutosha kuendesha shughuli zake? Kuna majengo ya ofisi yanavuja, ni aibu. Ikinyesha mvua, Maafisa wanasogeza meza pembeni. Mambo hayaendi namna hii! Wana viwanja chungu nzima vya ku-*develop* nyumba za kukaa Maafisa, hawana hela za kujengea. Kwa hiyo, naomba Wizara ifikirie sana Idara ya Uhamiaji Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni ajali za barabarani. Ajali za barabarani zimekithiri, watu wetu wanakufa, madereva ni wazembe. Naomba iwekwe sheria kali kuzuia hili, vinginevyo watu wetu watakuwa wanapoteza maisha yao kila siku kwa ajili ya ajali za barabarani. Hapa kuna kitabu mmetupatia wenyewe kuhusu taarifa ya hali ya uhalifu kuanzia Januari hadi Desemba, 2010. Taarifa inasema kwamba ajali za barabarani mwaka 2010 zimeongezeka kwa

asilimia 13.2 ikilinganishwa na mwaka 2009. Mwaka 2010 tu, ajali zilikuwa 24,926. Ni nyingi mno! Hiki ni kitu ambacho kinazuilika, kila siku watu wetu wanakufa kwa sababu ya ajali za barabarani. Watu maelfu kwa maelfu wanakufa. Naomba sana Wizara mliangalie suala hili na muweke adhabu kali ili kuwazuia madereva kuua wenzao bure. Dereva anaendesha gari kwa kasi ya kupindukia, hatumii hata akili yake kuona humu ndani ya gari amepakia binadamu wenzake, anafanya fujo barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Waziri aliangalie suala hili ili watu wetu wasipotee kwa mambo ambayo yanaweza yakazuilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ole, kwanza nataka niipongeze Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo karibuni itatimiza umri wa mwaka moja. Katika hili vile vile nampongeza Waziri wetu wa Mambo ya ndani ambayo kwa wakati huo wa Uanzishwaji wa Serikali hii yeye alikuwa ni Waziri Kiongozi. Ninaamini kwamba mchango wake ulisaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kidawa alianza kuhusu habari za ajali za barabarani, hata mimi nataka nijikite moja kwa moja katika suala zima la ajali za barabarani. Katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 12 na 13 ameeleza kwamba Jeshi la Polisi limekusudia kupunguza ajali za barabarani kwa asilimia kumi katika mwaka huu wa 2011/2012. Unaposema kwamba unataka kupunguza ajali kwa asilimia kumi, hapa tunaanza kupata mashaka kwamba bado Wizara haijataka kuliona suala hili la wananchi wetu ambao wanapoteza maisha kwa ajili ya ajali za barabarani. Takwimu zilizopo ni kwamba watu kumi wanapoteza maisha kila siku kwa ajili ya ajali za barabarani. Sasa unaposema kwamba utapunguza kwa asilimia kumi, ina maana kwamba umepunguza kifo cha mtu mmoja. Hapa inaonesha ni namna gani Wizara haijawa tayari kuji-*commit* katika suala hili la kupunguza au kuondoa kabisa ajali za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1998 Gazeti la *Daily News* liliandika kwamba Taifa limechoshwa na kupata habari za ajali za barabarani. Hiyo ilikuwa mwaka 1998, sasa leo Waziri anapotueleza kwamba ana mikakati hii, ni takribani miaka zaidi ya kumi tangu hili suala limeanza kupigiwa kelele, leo tunasema bado tuna mikakati ya kupunguza ajali za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Waziri, roho za wananchi, roho za Watanzania zinazidi kuteketea, leo asubuhi tumepata taarifa ya ajali ya basi lililokuwa linatokea Moshi kwenda Arusha wananchi kumi na moja wamepoteza maisha na wengine wengi wamejeruhiwa. Hali hii ni mbaya, inatisha na hili sasa hivi ni janga la kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya hali ya uhalifu ambayo imetolewa na Jeshi la Polisi, inaonyesha kwamba zaidi ya asilimia 45 ya makosa ambayo wameyagundua ya uhalifu, basi asilimia hiyo imekuwa *covered* na makosa ya ajali za barabarani. Taarifa hii imeonesha ni namna gani ukubwa wa ajali za barabarani ambavyo zimewaelemea wananchi wetu sasa hivi. Tufikie pahali suala hili tulione ni janga la kitaifa, tusilichukulie tu kwamba ni suala dogo, wananchi wetu wanapotea. Wananchi kwa kweli kama tutaipitisha bajeti hii bila ya Waziri kutoa mikakati halisi, kwa kweli tutakuwa hatujatenda haki juu ya usalama mzima wa barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Waziri inasema kwamba Jeshi la Polisi limekuwa likiwahimiza wamiliki wa mabasi ya abiria yanayokwenda Mikoani kufunga mitambo ya kutoa taarifa za mwendo. Jamani, siyo mabasi peke yake ambayo yanasababisha ajali za barabarani. Malori makubwa ya mizigo yanasababisha ajali za barabarani, pikipiki zinasababisha ajali za barabarani, kwa hiyo, tusichukulie mabasi tu peke yake kwamba yanasababisha ajali za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo Mkoa ambao unaongoza katika ajali za barabarani. Mabasi yanakwenda nje ya Dar es Salaam, lakini zaidi ya hapo, Waziri

anasema kwamba ameshauri kutumika kwa *car tracking*. Lakini katika taarifa ya hali ya uhalifu katika mikakati iliyopo katika kukabiliana na tatizo la ajali za barabarani, ukurasa wa 40 sentensi ya mwisho inasema kuhimiza doria za barabarani na kudhibiti mwendo kasi kwa magari kwa kutumia ratiba za mabasi ikiwa ni sambamba na kuhamasisha na kuimarisha utumiaji wa teknolojia ya kisasa ya *car tracking system*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachomwambia Waziri hapa, watendaji wake wamemwongopea, teknolonojia ya *car tracking* inayotumika sasa hivi Tanzania haina uwezo wa kuzuia ajali, haina uwezo wa kupunguza ajali, ile ni biashara ya watu na ni biashara ya kitapeli ambayo ndani yake kama ataifuatilia atakuta ni namna gani ilivyo na harufu mbaya ya ufisadi. Hii *car tracking system* ambayo katika mchakato wa tenda wamepewa kampuni inayoitwa *U-track,* kampuni hii ya *U-track* ndiyo ambayo imekabidhiwa kazi hii. Sheria iliyotumika *section 51 subsection (5) of the Road Traffic Act, Cap 168* ya 2002, inasema kwamba: *"the person shall drive a public vehicle other than a taxi cab on public road unless that vehicle is fitted with a speed governor, or any other similar divice designed to regulate and or record the speed of the vehicle."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ambayo imepewa kazi hii, inarekodi tu, haina kitu kingine chochote ambacho inaweza kufanya, *just* ku-*record* tu. Wakati tumepitisha bajeti hapa ya Wizara ya Sayansi na teknolojia, nilimwuliza Waziri wa Sayansi na Teknolojia hapa, kuna teknolojia mpya ambayo wafanyabiashara au wamiliki wa mabasi wanatakiwa waitumie. Je, Waziri teknolojia hii una taarifa nayo katika Wizara yako? Akasema yeye hana taarifa.

Ninachotaka kukwambia Mheshimiwa Waziri kupitia kwa Wakuu wako wa Vitengo vya Jeshi la Polisi ambao walihusika moja kwa moja katika mchakato mzima katika kuileta hii *car track* na *documents* zipo na sahihi zao tunazo, hawakutaka kukaa kitako wakaangalia ukubwa wa tatizo na ajali za barabarani. Wamejiingiza katika huu mradi, sasa hivi kilichobaki ni wewe Waziri uwalazimishe watu wa mabasi wafunge hii *car track. Car rack* yenyewe ikoje? Ni chombo kidogo sana ambacho ndani kinatumia *chip* ya simu hii hapa, kwa sababu hicho chombo ninacho na nilitaka niingie nacho humu ndani lakini sikuruhusiwa. Inatumia *chip* ya *VODACOM*. Mheshimiwa Zungu wakati anachangia hapa katika Wizara ya Sayansi na Teknolojia alisema kwamba lazima hii mitandao ya simu iangaliwe na ichunguzwe. Hapa kuna mapato mengi ya Serikali yanapotea. Hiki chombo, mtu wa mabasi anatakiwa akinunue, siyo chini ya Sh. 700,000/=. Pamoja na kukifunga, anatakiwa anunue vile vile na *camera* ambapo *cost* yake inakuja siyo chini ya Shilingi milioni tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi Shilingi milioni tano, huyu mmiliki wa mabasi hazitambana yeye, haya malipo yatawaelemea wananchi. Sasa baada ya kupunguza ajali, sisi tunatafuta miradi ya kifisadi kwa ajili ya kuwakomoa wananchi. Kweli wananchi watatuelewa Mheshimiwa Waziri wakati ajali zinazidi kuendelea kutokea? Nakuomba Mheshimiwa Waziri, hili suala liangalie upya, ni bomu ambalo umeshatiliwa mfukoni. Litakuja kukulipukia pabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha ziada wakati wa mchakato wa kuipata hii kampuni kwa ajili ya kufanya kazi hii katika mchanganuo, hii kampuni inaonekana haina *CV*, hii kampuni haina *experience,* wanasema *experience in similar management past of three years now.* Hii kampuni *deliver schedule* haina, hii kampuni *ability of train* haina. Sasa leo tunakwenda kuchukua mzigo huu, fedha chungu nzima tunawabebesha wananchi wakati ajali zinazidi kuendelea. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna tatizo sisi Watanzania na zaidi Wizara na Watendaji. Mwaka 2007 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilifanya *research* ya ajali za barabarani na nikatoa taarifa kwa Serikali kupitia *SUMATRA* na kimetoa mpango wa kupunguza ajali wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu, lakini imepuuzwa, haiangaliwi na wala haiulizwi. Hapa tuna tatizo. Hebu tukubali kurudi tuangalie, jamani wasomi wamekaa kitako wametengeneza, wametupa mpango kamili wa namna gani ya kupunguza ajali. Leo mnakuja kutuambia tutapunguza kwa asilimia 10, tena ni mwaka 2007 na kabla ya hapo katika mwaka 1998 mtaalam wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Profesa Tilebangila akishirikiana na *T. Pilis and BSC Moaner* kutoka katika Kitivo cha *Transit Research Laboratory* ya Uingereza, walifanya utafiti wa ajali za barabarani Tanzania na wakatoa ripoti yao. Lakini hakuna ambaye kakaa anaiangalia, ajali zinazidi kutokea, watu wetu wanazidi kufariki katika ajali za barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *car tracking.* Hii polisi sasa hivi wanayo na wanaitumia. Nataka nitoe mfano mdogo, juzi wakati natokea Dar es Salaam niko Morogoro hapo katika eneo la Mkambalani baada ya kuona Askari Polisi wamekaa na ile darubini ya kuchunguza *speed,* mimi nikaongeza *speed* ili kuangalia watafanya nini. Polisi wale walinipiga mkono wakanisimamisha sikutaka kukwaruzana nao kwa sababu nilifanya makusudi ili niangalie uwezo wao. Walichokifanya, waliniambia, umeongeza *speed,* sikuwakatalia kwa sababu kweli niliongeza *speed*. Lakini wakaniambia itabidi tukupige faini. Sikujieleza kwamba mimi ni Mbunge, nikakubali wakanipiga faini ya Sh. 20,000/=. Kwa hiyo, hivi vyombo tunavyo, kwa nini tutafute mzigo tuwaelemeze wananchi? Kuna sababu gani ya kuwaelemeza mzigo wananchi? Nikalipa shilingi 20,000 na nikaridhika kabisa. *(Makofi)*

Sasa kama hili tunalo, jamani Mheshimiwa *Inspector* Mwema katoa rai nzuri kabisa ya suala zima la maboresho. Anasema Jeshi la Polisi, maboresho yanaongozwa na mihimili mikubwa mitatu ambayo ni Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi. Kwa nini sasa hivi tusichukue vyombo hivi tukatumia Ulinzi Shirikishi katika barabara zetu ili ku-*control speed* za mabasi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua muda wangu umemalizika. Ninachosema ni kwamba siungi mkono hoja hii mpaka Waziri atakaponieleza kwamba hii *car tracking* ambao ni mzigo kwa wananchi ameondoa. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Naomba mwongozo wako, kwa mujibu wa Kanuni 64(g), naomba nisome: “Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayowadhalilisha watu wengine.” Humu ndani kumekuwa na tabia sasa imejitokeza, ni mara ya pili leo kuna baadhi ya Wabunge, wanasimama na kuwaita Wapinzania wanafiki. Mara ya kwanza Mheshimiwa Sitta alisimama akawaita Wapinzani wanafiki, Meza ikamlinda. Mara ya pili leo Mheshimiwa Lusinde wakati anachangia akawaita Wapinzani wanafiki. Naomba mwongozo wako kama hili linaruhusiwa na je, upande wa pili tukijibu humu ndani kutakalika? Naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Nitatolea mwongozo baadaye.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kuwa kunipa nafasi fursa hii nyingine ya kuchangia katika Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani. Lakini pia ningependa nitumie fursa hii kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii tena. Pia ningependa kutumia fursa hii kwa kushukuru wananchi wangu wa Jimbo la Ilemela ambao wananiombea usiku na mchana ili niweze kuifanya kazi hii sawa sawa na matarajio yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, safari na mtazamo mzima juu ya suala la amani na suala zima la safari ya kuingiza Bungeni, mimi binafsi huwa nalinganisha na nchi mbili zilizopata uhuru kwa njia tofauti. Nchi moja ikipata uhuru kwa amani kama zawadi ya *X- Mass* na nchi nyingine ikapata amani kwa kudai kwa kupigania hatimaye vita ndio ikapata uhuru, hakika ukihoji watu hawa wawili wanaotoka katika hizi nchi mbili tofauti, historia ya namna nchi zao zilivyopata uhuru na namna ninavyoelezea hakika kutakuwa na tofauti kubwa. Nitatoa mfano wa pili ili nieleweke vizuri zaidi. Ukiwaita akina mama wawili waliojifungua mmoja kwa njia ya kawaida na mwingine kwa njia ya operesheni ukawahoji kwa habari ya uchungu hakika kila mmoja atakupa maelezo yasiyofanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitachangia. Kwangu mimi tunapozungumzia suala la amani, tunapozungumzia suala la maandamano, kimsingi machungu ninayopata ni ya tofauti. Hii nitaelezea uchaguzi wa mwaka 2010 Jiji la Mwanza, kwa jinsi na utaratibu uliokuwepo hatukuhitaji wagombea kwa kipindi hicho kusubiri kuingia kwenye chumba cha majumuisho ili uweze kujua kwamba wewe umeshinda Ubunge au umeshindwa. Kwa sababu kulikuwa na utaratibu ambao katika kila kituo cha kupiga kura muda ulipofika majumuisho yalibandikwa ukutani. Wabunge Wagombea waliokuwa makini kama mimi haikuhitaji kwa wakati huo nifike katika chumba cha majumuisho ili niweze kujua kwamba nimeshinda Ubunge. Kwa hiyo, kwa wakati naingia kwenye chumba cha majumuisho saa 1.00 jioni siku ya uchaguzi sikuwa naingia kama mgombea, nilikuwa naingia kama Mbunge anayekwenda kutangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha, siku ya kwanza haikuwezekana kutangazwa bila sababu za msingi, siku iliyofuata maandamano yalianza kwa kuwa wananchi walikuwa wanajua kwamba wamepiga kura za kutosha na nani wanayemtaka aweze kuongoza kwa nafasi ya Ubunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Serikali ikitazama maandamano yale katika chumba kile, hali ikawa ni mbaya sana, kimejaa moshi wa mabomu ya machozi. Hali nje haifai, magari yanachomwa moto, bado hawataki kutangaza matokeo, nani ameshinda Ubunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine ni vyema tukaelezea yaliyotukuta ili tunapozungumzia suala la maandamano, watu wajue kwa nini Wabunge wa Upinzani tunakasirika na kwa nini hatutaacha maandamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kunisikitisha zaidi, siku hiyo ya pili baada ya hali kuwa mbaya hata watumishi wa Jiji sasa wanatapika. Chumba kilipata giza kwa ajili ya moshi wa mabomu. Kitu hiki sitasahau katika maisha yangu. Cha kunisikitisha, Mkurugenzi wa Jiji anasimama anaongea na simu mbele yetu wote, anasema: “Mheshimiwa, nimejitahidi kwa kadri ninavyoweza (sijui walikuwa wanaongea na nani, sitaki huyu aliyekuwa anaongea naye ni nani), hali imeshindikana, naomba uniruhusu nitangaze matokeo.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu aliyekuwa anaongea naye kwenye simu, nimesema sitaki kumjua, lakini hiyo ndiyo hali halisi. Kwa Ubunge huu ambao leo hii unanipa fursa ya kusimama hapa, ni Ubunge ambao umezaliwa na maandamano, siyo haki itokanayo na Serikali. Tunapozungumzia maandamano, kwangu mimi au Waziri ni sawa sawa au Wabunge wanaobeza maandamano siyo hivyo. Nitanukuu ukurasa wa 11 katika hotuba hii katika hali ya usalama na matukio ya uhalifu. Kwa ujumla, hali ya nchi yetu imeendelea kuwa ya amani na utulivu. Hata hivyo, mara baada ya kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu Oktoba mwaka 2010 zimeanza kujitokeza dalili za uvunjifu wa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uvunjifu wa amani haijaanza kujitokeza baada ya uchaguzi, hata kabla ya uchaguzi. Nitaendelea, baadhi ya viongozi wa kisiasa wanaandaa maandamano na Mikutano ya mara kwa mara pamoja na siasa kutumia haki yao ya kidemokrasia. Hali hii inawanyima wananchi fursa ya kushiriki katika shughuli za maendeleo na miradi ya kuwapunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, walioandamana, ili kutaka mimi nitangazwe kuwa Mbunge katika Jimbo la Ilemela, hawakuwa CHADEMA walikuwa wananchi wa Jiji la Mwanza. Kwa hiyo, viongozi wanapobeza maandamano kwangu mimi ni sawa sawa na kumbeza mama yangu na baba yangu. Maana baba na mama wa Ubunge wangu ni maandamano. Hii imeshajengeka kwangu na imeshaingia kwenye damu. Kwa hiyo, leo hii hata tunapozungumzia suala la madawati, ikibidi nitaandamana. Tayari imekuwa hivyo. Hili hata kwa wananchi wangu wa Wilaya ya Ilemela ndivyo wanavyoamini. Nikisoma *message* wanazonitumia hapa wanasema tuje, tuanze nawaambia tutulie kwanza. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge waambie hawaruhusiwi kabisa Dodoma. Endelea.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme kitu kimoja, kimsingi maandamano yanayofanywa na CHADEMA hatujaanza, hii ni *warm-up* tu, siku Bunge hili na Watanzania watakaposikia sasa Wabunge wa Mwanza na wananchi wanakuja Dar es Salaam, watu wa Arusha Mjini wanakuja Dar es Salaam, watu wa Singida wanakuja Dar es Salaam ndiyo wajue kwamba CHADEMA tumeanza maandamano. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI :** Hii nimeipenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, turudi kwenye hali ya usalama na matukio ya uhalifu. Nitazungumzia suala laumaskini kwa mujibu wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Nahodha, nanukuu katika ukurasa ule wa 11, kuanzia hapa. Baadhi ya viongozi wa kisiasa wanaandaa maandamano

ya Mikutano ya mara kwa mara pamoja na wasiasa kutumia haki yao ya kidemokrasia. Hali hii inawanyima wananchi fursa ya kushiriki katika shughuli za maendeleo kwa miradi ya kuwapunguzia umaskini. Kwa bahati mbaya, viongozi wanaamini kuwa Watanzania ni maskini sana ni hao hao wanaotia shime watu umaskini washiriki katika maandamano yasiyokuwa na tija. Nitanukuu maneno ya Waziri Mkuu aliyoyasema hapa jana asubuhi alipokuwa akijibu maswali ya papo kwa papo kutoka kwa Mheshimiwa Magdalena Sakaya alisema, tatizo kuna watu humu ndani wanafikiri kwamba Serikali ni mbumbumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme hivi, tatizo humu ndani kuna watu wanafikiri Kambi ya Upinzani ni mbumbumbu. Kwa faida ya wananchi na Wabunge katika Bunge hili, nitanukuu kwa mara ya pili Hotuba ya Baba wa Taifa kwa faida ya Waziri pia. Nazungumzia hali ya umaskini kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani. Baba wa Taifa alisema, Kikao cha Thelathini na Tatu cha Bajeti kama hiki, tarehe 17 Mei, 1960 alisema: "Ufisadi na rushwa ni adui mkubwa wa zaidi ya maslahi ya watu wakati wa amani kuliko vita." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kusema kwamba haya maandamano yanayozungumzwa hapa kwamba yanapotezea muda wananchi kufanya shughuli za maendeleo, umaskini wa Mtanzania ni wa miaka 50 na ningesema kwa nini tumefika hapa. Tumefika hapa tulipofika kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi, imeshindwa kupiga vita ufisadi na rushwa na matokeo yake ni kwa sehemu ya huo ufisadi, ndiyo tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningemshauri Mheshimiwa Waziri, badala ya kutumia muda wake mwingi kujadili maandamano, njia ambayo imethibitika kitaifa, tuna *successful proven method* ya kushurutisha Serikali zisizo sikivu, ni maandamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia suala la rushwa. Kwa hili, nimetafakari sana, chombo ambacho tunakitegemea kuwa cha kwanza kupiga vita rushwa na ufisadi katika nchi hii, ndiyo kimebainika kuwa chombo kinachoongoza kwa rushwa katika taasisi za umma.

**MBUNGE FULANI:** Aibu!!

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili nitamtaka Waziri atupe ufafanuzi wa kina, kwa kuwa ndiyo ameingia kwa mara ya kwanza kwenye Wizara hii sitaki kumhukumu. Katika majumuisho, atupe ufafanuzi ni namna gani atalibadilisha Jeshi la Polisi kutoka katika chombo ambacho kinaongoza kwa rushwa na kuwa chombo kinachoongoza kwa kupiga vita ufisadi na rushwa, nitaomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri kwa hili na kimsingi kabisa kama majibu yake yatakuwa hayajitoshelezi, basi ni vyema akaungana na waungwana wengine katika suala zima la kufikiri kujiuzulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa narudi Jimboni kidogo. Jeshi la Polisi, hali ilivyo, bila ya kusahau, pamoja na yote, ni pamoja na adha zote wanazozipata, makazi mabovu, nyumba ambazo hawezi hata kukaribisha mgeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi umeshawahi kufikiria hali na jinsi utakavyojisikia ukiishi kwenye nyumba ambayo huwezi ukamkaribisha mgeni? Maana yake ni kusema hata rafiki yako uliyesoma naye shuleni huwezi kumkaribisha nyumbani kuona hali ya nyumba yenyewe. Ni dhahiri kwamba Polisi wetu wanavumilia kuwa Watanzania, wanavumilia kuwa Askari Polisi kuliko kufurahia kuifanya kazi hiyo. Tuna kila sababu ya kuwatia moyo na ninaiomba Serikali kwa mujibu wa hotuba ya Kambi ya Upinzani, iangalie suala hili la makato ya Sh. 5,000/= kwa kila mwezi kwa ajili ya mazishi, siyo wajibu wa Askari hawa. Ni jukumu la Serikali na ni mambo kama haya ndiyo yanafanya tunaandamana.*(Makofi)*

Serikali ina wajibu wa kujua kwamba jukumu la kumzika Askari Polisi ni la kwake, siyo jukumu la Askari mwenyewe. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwarudishie Polisi wote zile Sh. 5,000/= ambazo imekuwa ikizikata tangu ilipoanza kuzikata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yamezungumzwa mengi, lakini pia suala la mshahara ni vyema Serikali ikafahamu kwamba Watanzania wote wana haki ya kunufaika na raslimali za Taifa hili. Kazi

wanayoifanya ya kulinda raslimali zetu na sisi wenyewe, lazima iendane sambamba na kipato wanachokipata, la sivyo tutajikuta *automatically* tunawafundisha kuwa majambazi. Huwezi kulinda Benki kwa mshahara wanaopata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie hali ya vituo vya polisi katika Jimbo langu la...

*(Hapa kengele iligonga kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**NAIBU SPIKA**: Ya pili hiyo Mheshimiwa.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. VICENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza napenda kuwashukuru sana Askari wa Jeshi la Magereza na Jeshi la Polisi walioko Musoma Mjini kwa kura zao nyingi sana walizonipa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na Ubunge, mimi ni Diwani wa Kata ya Mkendo, Kata ambayo wanaishi Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza na raia wachache sana, lakini waliamua kwa pamoja wakaniambia siyo Ubunge peke yake na Udiwani tunakupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Magereza walioko Musoma wana shida sana. Gereza la Musoma limejengwa tangu enzi za ukoloni. Nimekuwa na kawaida sana ya kutembelea Gerezani, mahabusu waliofungwa wamelundikana na hakuna tofauti kati ya mfungwa na Askari Magereza. Wakati mfungwa amelala Gerezani, askari anakesha Gerezani humo humo. Wakienda shambani au kwenye kukata kuni na kuvunja mawe, wako pamoja. Askari Magereza wamenituma niwaombee na sintaacha kufanya hivyo. Ni mita chache kutoka kwenye Kambi zao, nyumba za Polisi zinajengwa, wao hakuna lolote. Hakuna nyumba zinazojengwa pale. *(Makofi)*

Salaam za Askari Magereza, hawasalimiani habari za asubuhi, wanaulizana umelalaje? Hali ni mbaya. Wapo Askari Magereza wanaoishi katika Kata tofauti na Gereza lilipo na inawalazimu kuja usiku, hawana gari. Tukumbuke hawa ni askari ambao wanakaa na watu ambao wamekuwa majambazi, pengine wamemaliza kifungo, wana vinyongo vyao kutoka Gerezani, wanaweza kuwavizia. Kwa hiyo, nilikuwa nataka leo katika majumuisho ya Waziri, aniambie hawa Askari Magereza wa Musoma wanaotoka Kata ya Nyasho kuja Kata ya Mkendo Gerezani saa nyingine usiku kwa baiskeli anawasaidia vipi na ni wajibu wa Wizara kuwapatia usafiri. Hawa watu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Magereza wanahitaji kutoa mafunzo kwa wafungwa, sio tu kuwapa adhabu. Kumekuwa na matatizo ya wafungwa kujirudia kwa makosa yale yale kwa sababu hawana kitu cha kufanya na dhumuni la Magereza limepotea sasa, kwa maana ya kwamba badala ya Askari Magereza kuwafundisha wafungwa namna gani watakaporudi uraiani baada ya kumaliza kifungo wawe na kitu cha kufanya mbadala, wamekaa nao kwa sababu fedha hazitoshi, hawawapi wafungwa mafunzo ili wakitoka wakafanye kazi mbadala. Nchi nyingine, mfungwa akiwa pale anafundishwa ujasiriamali, uzalishaji mali na ufundi kupitia askari au watu wengi wanaokuja kutoa Mafunzo Gerezani. Kwetu haipo, na hii ndiyo inasababisha mfungwa akienda uraiani hana kazi ya kufanya, anafanya makosa, anarudi Gerezani. Mbunge mmoja anasema wanatamani, hawatamani kurudi pale, isipokuwa tu hawana cha kufanya. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali sasa iangalie upya namna gani ya ku-*handle* Magereza na wafungwa.

Sasa hivi tunakwenda kujenga maabara kwenye shule nyingi, kazi hizo wangezifanya wafungwa baada ya kuwa wamepewa mafunzo, fedha zikaenda Gerezani, wakazitumia kiasi kidogo kwa chakula nyingine wakawawekea wafungwa wanapotoka wawe na kitu cha kuanzia ili wasirudi Gerezani. *(Makofi)*

Mimi nina uhakika, mnasema Serikali ni sikivu, inaweza ikawa ni sikivu, lakini kipofu katika hili. Nilikuwa naomba sana sasa ifumbue macho, hatuhitaji kuwa na wafungwa wa kujirudia. Pia

nilikuwa napenda tutakapofikia kwenye sheria, turekebishe baadhi ya sheria. Kuna watu wanakaa pale mahabusu kwa miaka mitano, akisubiri kesi, siku akihukumiwa, anahukumiwa miaka sita, anakaa tena miaka sita. Basi ikifikia hapo, kama amehukumiwa miaka sita akae mmoja tu maana yake mitano yote amekaa Gerezani ili imsaidie arudi akaungane na familia yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Polisi kuna shida. Kama alivyotangulia kusema mwenzangu, Polisi wanachangishwa Sh. 5,000/= kila mwezi kwa ajili ya mazishi yao na wategemezi wao. Hawa ni wafanyakazi wa Serikali. Mimi nilikuwa nadhani Wizara sasa ichukue jukumu hilo, na zile fedha zilizokusanya kama alivyosema mwenzangu warudishiwe. Hawafurahi kwa sababu wao hawawezi kuandamana, wamenituma mimi nije hapa, ikishindikana tutaandamana na watatu-*support*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kingine ambacho kinawakera sana wananchi, kimetokea sana wakati wa uchaguzi. Hata mimi peke yangu kiliwahi kunitokea, suala la *PF3.* Mtu anajeruhiwa, aidha, amepata ajali au amepigwa, kitu cha kwanza cha wasamaria wema huwa wanafikiria kumpeleka hospitali. Akifika hospitali anaambiwa alete *PF3.* Ina maana arudi Polisi. Kama anavuja damu, mtu huyu atafia njiani. Sasa nilikuwa naitaka Serikali na katika majibu ya Waziri, anapotoa majumuisho, ahakikishe basi katika hospitali za Wilaya tunakuwa na askari kwa ajili ya kuandika *PF3,* siyo kumtoa mgonjwa aliyejeruhiwa kwenda kukitafuta Kituo cha Polisi akaandikiwe *PF3.* Watu wengi sana watapoteza maisha na wanaendelea kupoteza maisha kwa sababu ya kwenda kutafuta *PF3,* na wakati mwingine kituo kiko mbali sana na hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la umilikaji wa silaha. Ni sheria zinazowaruhusu watu kumiliki silaha kwa ajili ya kujilinda binafsi, lakini hapa sasa kuna shida. Umewekwa utaratibu mtu anapotaka kumiliki silaha anajadiliwa na Mtaa husika, anajadiliwa na Wilaya, baadaye Mkoa, kisha anamilikishwa silaha. Lakini sasa hivi imekuwa tofauti. Kuna watu wanaishi Musoma, anamilikishwa silaha Shinyanga na maeneo mengine ya nchi. Nina uhakika Waziri ana taarifa, majina yapo, nilikwishampa, nasubiri tu ufuatiliaji na watu hao wamekuwa wakifanya matukio ya ajabu ajabu, imefikia hatua wanatishana kwa silaha *Bar*. Sidhani kama ni utaratibu mzuri. Nataka katika majumuisho yake pia aniambie hatua hii inakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nashauri *at least* sasa waangalie utaratibu upya, kwa watu wanaomiliki silaha ni watu wa aina gani, wamezipata vipi na wanaishi wapi na wamejadiliwa wapi na kuwe na utaratibu wa kuzikagua kila mara. Yamezuga maduka mengi tu ya silaha, yapo kisheria ndiyo, lakini sasa kuna watu wanatumia vibaya na bahati mbaya pale kwetu silaha imekuwa kama kitu cha kawaida Musoma. Mimi nadhani msiangalie sana maandamano, mliangalie hili, siku mambo yakiharibika, sijui itakuaje!

Nilikuwa napenda sana, kama mnavyopenda amani na mimi naipenda kweli kweli. Sipendi yatokee mabaya kwa sababu yaliyotokea wakati wa uchaguzi, nayajua. Watu wangu sio kama mnavyowafikiria, nashukuru, kuna baadhi ya watu wananiambia mbona umetulia sana? Yaliyofanyika wakati wa uchaguzi yalinifanya nitulie, sitaki yatokee tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa wa kwanza kutangazwa kabla ya mtu yeyote hapa ndani, mimi najua nini kilitakiwa kifanyike. Basi nilikuwa naomba, sipendi mambo hayo yatokee, tumeamua kutulia, hatuhitaji sasa vurugu zinazotokea hapa ndani ziendelee kwa sababu watu wangu hawatakuwa wavumilivu wakiona tunaendelea kunyanyaswa kwa sababu wametutuma hapa tuwatumikie. Sasa nilikuwa napenda pia Kiti kijitahidi sana ku-*balance*. Mimi nina uhakika wala siyo siri, yanayofanyika kwa Wabunge wenzangu yakifanyika kwangu, wala hawatahitaji niwapigie simu, watayaanza huko, ninajua. Kwa hiyo, nilikuwa nakuomba sana… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vicent, nakukumbusha tu, usije ukavuka msitari.

**MHE. VICENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi ndiyo maana nacheza katikati ya msitari, nakukumbusha pia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sipendi sana nigongewe kengele ya pili, ninayasubiri sana majibu ya Waziri katika haya niliyoyasema, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Niseme tu kwa hatua hii, Kiti kinatenda haki, tena haki kabisa. Mahali popote pale haki inapotendeka, wako watakaoona kwamba inatendeka na wako watakaoona kwamba haitendeki. Hilo ni jambo la kawaida, lakini Kiti kinatenda haki na ningependa kuwaambia Watanzania wote kabisa, Kiti kinatenda haki na anayefuata utaratibu, hatapata matatizo hata kidogo.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi pia niweze kuchangia kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwanza naomba nianze kwa kutoa salamu za pongezi kwa askari wa Jiji la Mwanza wakiongozwa na Kamanda Simon Siro ambaye nimepata taarifa kwamba ameondolewa Mwanza katika hizi siku za karibuni. Siro amefanya kazi kubwa Mwanza na hata kama mnakumbuka, hivi karibuni na katika miezi michache iliyopita kulikuwepo na tukio la ujambazi maeneo ya Kisesa, askari wetu kule Mwanza walifanya kazi kubwa sana kuwadhibiti na nafikiri waliua wachache. Sasa hii ni kazi kubwa askari wanafanya na napenda nichukue fursa hii kuwapongeza sana askari wa Jiji la Mwanza chini ya Kamanda Simon Sira ambaye sasa ameondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba fursa ya Watanzania kwenda kusoma wakiwepo Askari Polisi na hata fursa ambayo pia mimi Wenje niliipata ya kusoma sio *privilege*. Hili ni suala ambalo Serikali lazima ifanye, kwa sababu ni kodi za baba zetu ndiyo Serikali inakusanya ndiyo imefanya sasa tukasoma. Kwa hiyo, sio *privilege* sisi kwenda kusoma. Lakini pia hiyo hiyo Serikali ime-*deny* watu wengi nafasi ya kwenda kusoma akiwemo Mheshimiwa Lusinde. Hiyo hiyo Serikali imemnyima fursa ya kwenda kusoma, ambaye alikuwa anasema kwamba sisi kwenda kusoma ni *privilege*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee. Nianze kwa kutoa ushauri kwamba leo takwimu za ajali za barabarani zimeongezeka kwa kiasi kikubwa na hizi ni kwa sababu katika magari yetu kwa mfano usafirishaji wa barabarani mabasi, *safety*, usalama ndani ya haya mabasi ni kidogo kweli. Leo mtu anapanda *bus* kutoka Mwanza kwenda Dar es Salaam, *bus* haina hata mkanda, haina *safety belt* kwamba dreva peke yake ndiyo anayepigwa faini akikosa kufunga mkanda. Sasa ajali inapotokea, *bus* imebeba watu wengi, hawana hata mkanda, lazima watu wengi wafe. Kwa hiyo, naomba Serikali kupitia hii Wizara, iangalie sasa upya hali ilivyo kwenye mabasi yetu wanavyosafirisha watu. Tuanze kwa kuweka sheria kwamba lazima iwepo *safety belt* kama nchi nyingine na mtu asipofunga *safety belt*, isiwe kosa la mwenye gari, faini iwe kwa abiria ambaye amekosa kufunga *safety belt*. *(Makofi)*

Hii, hata kama ajali itatokea, lakini itapunguza vifo vingi kwa kiasi kikubwa, nafikiri hii itatusaidia kupunguza vifo vingi pale ambapo ajali inapotokea. Lakini kuna kitu kingine, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye hii Wizara alitoa takwimu jinsi gani Magereza yalivyo leo. Magereza yalijengwa kipindi cha ukoloni, Gereza moja limejengwa kubeba watu 200, leo inabeba watu 1,500. Hiyo ni *over capacitated*. Sasa kwa nini mtu akiiba hata kuku tu apelekwe Gerezani, tumpeleke afanye *community service.*

Kwa mfano, kwenye Majiji Dar es Salaam tunafanya kitu kinaitwa *PPP,* hata Mwanza, *Public Private Partnership* kwenye hata usafi, sasa mtu amekamatwa kwa mfano ni machinga, amekamatwa na mizigo, ameuza kwenye eneo ambalo halitakiwi. Kwa nini huyu mtu apelekwe Gerezani? Apelekwe afanye *community service* ili kwenye Halmashauri zile pesa tunazotoa kuwapa hawa watu wanaotufanyia usafi ipungue ile pesa ikaenda kufanya kitu kingine kwenye hospitali. Siyo kila kosa akina mama wanagombana nyumbani wanapelekwa Butimba kufungwa, ya nini? Wapelekwe wafanye *community service* Magereza yapungue, kwa sababu idadi ya watu kwenye Magereza ni kubwa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaku-*challenge*, u- *think outside the box*. Leta *proposals* kwenye Bunge, namna gani tunavyoweza kupunguza malundikano kwenye Magereza. Kwa hiyo, siyo kila kosa. Shirikiana na Waziri wa Mahakama, Waziri wa Katiba sijui na Sheria muangalie namna mnavyoweza ku-*harmonize.* Siyo kila kosa mtu apelekwe Gerezani. Watu wamenyimana uwanya, gerezani; kosa sijui la nini, gerezani. Hebu kuweni *creative* basi ili tupunguze msongamano kwenye Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme kwamba katika Sheria ya Faini za barabarani, mimi napendekeza haya yafuatayo na nafikiri ni muhimu sana kwa Tanzania.

Mtu ana daladala anakamatwa kwamba gari yake imeharibika, haina taa. Kwa nini huyu mtu apigwe faini? Kwa nini gari yake isipelekwe kituoni iwekwe pale aambiwe kwamba mpaka ununue hiyo taa uweke hapa hapa ndiyo gari yako inatolewa kwa sababu Serikali ina nia ya kusaidia Watanzania wapate kipato kingi waondokane na umasikini. Sasa taa imeharibika, gari mbovu. Sasa kama gari ni mbovu, huyu mtu akishapigwa faini hata ile *saving* kidogo aliyo-*save* itaondoka, gari ile itarudi barabarani kuendelea kufanya kazi kukusanya ili apate hela ya kwenda kuitengeneza. Kwa nini gari isiwe *confined* pale Polisi, aambiwe kwamba badala ya wewe kulipa faini, hakikisha hii gari unaitengeza, hapa inatoka ikiwa nzima, ndiyo tunakukabidhi.

Kwa hiyo, sio kila kosa mtu apigwe faini, lakini kuna makosa kama haya ya mtu kutofunga mkanda, mara mtu kuvuka taa, taa inawaka yeye anavuka na gari. Hawa watu pia wasipigwe faini. Hawa watu wafanye *community service*, hawatarudia. Anachukuliwa mtu amevaa koti kama mimi, amevuka taa, awekwe pale barabarani afagie barabara siku nzima, hatarudia. Lakini kwa sababu ya Sh. 20,000/= siyo tatizo, Sh. 30,000/= siyo tatizo. Mtu analipa tena hapo hapo, anaondoka anakwenda haimuathiri kiasi kikubwa. Kesho pia atavuka tena taa.

Sasa makosa haya ya *repeatedly* ya kuvuka taa barabarani, mtu kutofunga mkanda, haya *traffic offence* ya kawaida. Haya siyo mpaka mtu apigwe faini, tuwawekeni hawa watu wafanye *community service*, afagie barabara pale Mwanza, pale katikati amevaa koti kama mimi siku nzima hata ofisini hajakwenda, hatarudia makosa kama haya. Tukifanya hivyo, mimi nakwambia *traffic offences* nyingi za barabarani tutapunguza kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Waziri, mimi nafikiri sheria tulizonazo, haziko *static*, ziko *dynamic*, *at any point in time* nafikiri tunaruhusiwa kuangalia namna tunavyoweza kuzibadilisha ili angalau tupunguze hizi *minor traffic offences* ambazo zinatokea barabarani.

Leo kuna Wabunge wengi wamechangia kuhusu rushwa kwa Polisi. Mimi nina mawazo tofauti kabisa, naogopa tu kusema kwamba mimi nawaunga mkono wachukue rushwa, naogopa kusema hivyo lakini sababu inayopelekea watu kuchukua rushwa ni kama ifuatavyo:-

Leo hata tukizungumza hapa mpaka tukavua mashati ili *Traffic* asichukue rushwa, wakati anaona katika Serikali kuna Mawaziri wanapiga dili. Dili inapigwa moja kama *Kagoda Agricultural,* mtu anaondoka na bilioni 40. Dili inapigwa moja kama ya Rada mshikaji anakula *commission* bilioni kadhaa. Dili inapigwa moja kama ya Richmond watu wanagonga mabilioni. Sasa kama huku juu tunapiga dili, watu wanakula mabilioni halafu tunakuja kumlaumu huyu *Traffic* anayekula 20,000? Lazima kama kweli tunataka rushwa ikome nchi hii, hili suala la sisi leo tunataka kuiangukia *Traffic* wakati huku juu watu wanapiga dili tena wanaondoka na mabilioni ya fedha, hii siyo haki na kama tuna machungu sana na nchi hii, ngoja nitoe mfano. Hivi yupi bora kati ya kichaa anayepiga kelele kutetea maslahi ya nchi yake na yule mtu mpole, mstaarabu anayeiba rasilimali za nchi yake, yupi bora? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kichaa!

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Ni yupi bora?

**MBUNGE FULANI:** Kichaa!

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Kwa hiyo, niko tayari, hapa bora lawama kuliko hasara. Nipo tayari kuitwa kichaa Bungeni hapa kusimamia rasilimali za nchi hii kuliko kuwa na ustaarabu wa kuiba rasilimali za Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama kweli tunataka tusilaumu sana Polisi hapa kwamba wanakula rushwa, wanakula rushwa kwa sababu wanaona wakubwa wa nchi hii wanakula rushwa. Wanaona ufisadi umeenea kila kona. Sasa kama mnataka ustaarabu kiasi

hicho, hizi nguvu mnazotumia hapa kupiga kelele mnataka ustaarabu, pigeni basi kelele nchi isiibiwe, tumieni *energy* hiyohiyo mpige kelele nchi isiibiwe lakini hivihivi haki ya mama mimi Askari kuchukua hela barabarani sioni kama tatizo ni kubwa kama huku ukubwani watu hawatajirekebisha na wao waache kupiga madili. Mkiacha kupiga madili, nchi itakuwa salama hata huku barabarani hakuna atakayepiga dili tena kwa sababu wakubwa wameacha kupiga dili lakini kwa staili hii, mtaongea mpaka mtavua mashati haki ya mama barabarani watu wataendelea kuchukua fedha. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe *serious* kiasi hicho, tusiwe huku juu tunachukuachukua tu, tunavuna halafu wa huku chini tunawapiga mkwara. Kwa hiyo, isiwe *double standard,* iwe *spade a spade,* hata uwe mkubwa kiasi gani. Kuna nchi zingine mtu akiteuliwa kuwa Waziri ni masikitiko kwa sababu anajua yuko karibu na kwenda gerezani lakini hapa kwetu watu wakiteuliwa kuwa Mawaziri wanafanya sherehe kwa sababu amepewa nafasi ya kwenda kula. Sherehe, washkaji wanapongezana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nchi kama Rwanda ukiteuliwa kuwa Waziri *is nightmare* kwa sababu Kagame *is nonsense man*, huko ukichaguliwa karibu unakwenda gerezani, huku watu wanapongezana, kisa amepewa Unaibu Waziri. Kwa nini wanapongezana? Ni kwa sababu sasa kuna fursa ya kusaini mikataba ya kijanja. Sasa umepewa fursa ya kupiga dili upate mamilioni mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba hili suala la watu kutolewa nje hapa na *Sergeant-At-Arms* siyo *issue*, siyo *big deal.* Kama juzi mimi Wenje nimetolewa, nimesimama naomba Mwongozo wa Spika...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje, nakutahadharisha tu usije ukaanza kujadili maamuzi ya Kiti, nayo ni kinyume cha Kanuni *unless* unachangia tu katika mambo yako mengine lakini kama ni maamuzi ambayo yalikwishafanywa hapa, ni wajibu wangu kukukumbusha kwamba unakaribia mstari. Endelea Mheshimiwa.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachoweza kusema ni kwamba sisi kutolewa humu ndani na *Sergeant-At-Arms* siyo *big deal,* hii ndiyo *Parliamentary Democracy, in fact* kuna nchi zingine watu wanapigana hata makonde, kwa hiyo, hapa sisi kutoka siyo tatizo kubwa. *It is not a big deal. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichukue fursa hii kupongeza Wabunge wote wa Upinzani ambao wamepata fursa ya kulala selo. Ni ujasiri mkubwa na msiogope na hii inaonyesha kwamba *the freedom is coming tomorrow,* kwa hiyo, msiogope. Katika nchi zote za Afrika ambazo zilipata uhuru lazima kuwepo na *second liberation for African countries and what we are doing today is the fight for the second liberation,* msiogope. Wakoloni walikuwa ni wakali kweli, watu walikatwa mpaka mikono mpaka na miguu kipindi wanapigania haki za nchi zao, sasa sisi leo kulala tu selo sio tatizo kubwa na mimi Wenje pia niko tayari hata nikitoka hapo nje mje mnikamate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niendelee kusema kwamba maandamano ni suala la msingi na ni haki ya kila Mtanzania. Serikali iliahidi kwamba bei ya sukari kwa mfano inaenda kupungua leo Mwanza bado wananunua sukari kwa sh.2,000/=. Sasa kama watu wameandamana Malawi kwa sababu maisha ni magumu, sisi leo nchi iko kwenye giza tukiandamana mnaona noma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ieleweke katika mchango wangu wote Bungeni nimewahi kusema kwamba kama ni maandamano, Mahatma Ghandi aliwahi kusema *demonstration is the language of un-have, and indeed we will continue demonstrating, we will demonstrate, we will demonstrate tomorrow.* Tutaandamana kesho na keshokutwa mpaka kieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewasikiliza wenzangu wote waliochangia hoja hii na nimegundua kwamba hakuna hata Mbunge mmoja ambaye haoni thamani au umuhimu wa Jeshi la Polisi katika nchi yetu. Vilevile nimegundua kwamba sote kwa pamoja tunatambua kwamba Askari wa MaJeshi yote, Askari wa Jeshi la Ulinzi, Askari wa Jeshi la Magereza, Jeshi la Polisi hata ndugu zetu wa Usalama wa Taifa, ni vijana ambao wamejitoa mhanga maisha yao kwa ajili ya Taifa. Ni kwa sababu hii tu kwamba mimi kwa niaba ya wananchi wa Rombo, nataka niwapongeze Askari wote kwa kazi wanayofanya kwa ajili ya ulinzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingi zilizozungumzwa ni dhidi ya Jeshi la Polisi. Mimi namfahamu vizuri sana Kamanda Saidi Mwema tangu akiwa *OCS* pale *Central* baadaye *RPC* Mbeya na kadhalika. Nafahamu juhudi zake na namna anavyochapa kazi. Kwa sababu hiyo, naijua dhamira ya Jeshi la Polisi katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, niseme tu kwamba mengi yaliyozungumzwa ni kuhusu malalamiko ya Askari juu ya mafao yao na maisha yao. Siko mbali na waliozungumza kwa ajili ya kuwaombea Askari maboresho ya mafao mbalimbali wanayopata ili kuweza kutenda kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Mkutano wetu wa Tatu, nilipokwenda Jimboni, niliomba nafasi ya kukutana na Askari Polisi wote wa Jimbo langu pale Wilayani Rombo ili kusikiliza matatizo yao kama ambavyo nafanya kwa ajili ya kusikiliza matatizo ya wananchi wengine wote. Kama walivyosema wenzangu, matatizo makubwa ya Askari wa Rombo ni makazi. Miaka 32 ya uhai wa Wilaya ya Rombo, Askari wa Wilaya ya Rombo, Askari Polisi pamoja na Askari Magereza katika Wilaya ya Rombo wanaishi kwenye vibanda vilivyotengenezwa kwa mabanzi. Mabanzi hayo yameliwa mchwa na sungusungu wanaingia ndani. Kwa kweli ni aibu ya hali ya juu sana. Tena mabanzi hayo yamegawanywa katika vyumba, chumba kimoja Askari, kingine Askari. Sasa unajaribu kufikiria huyu kijana amesoma, kazi zake anazifanya katika mazingira magumu sana, pengine jua lake, mvua ni yake lakini ikifika usiku anapotakiwa naye apumzike, anapumzika kwa shida kiasi hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Makamanda, Kamanda wa Jeshi la Polisi na Kamanda wa Jeshi la Magereza wajaribu kufanya chochote kwa ajili ya Wilaya ya Rombo. Bahati nzuri Kamanda Mwema unatoka Kilimanjaro, hebu tumia muda wako mchache tu ufike pale Rombo, ni aibu kubwa, miaka 32 hakuna jengo hata moja la Polisi ambalo limekwishajengwa katika Wilaya ya Rombo na tukumbuke Rombo ni Wilaya ya mpakani na changamoto ambazo zinatokana na kuwa mpakani ni nyingi. Kuna ujambazi unaotoka nchi za jirani na kuna ujambazi unaotoka ndani ya Rombo yenyewe. Kwa hiyo, ni dhahiri Askari wa Rombo wanahitaji msaada mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, utashangaa na nimeshangaa wenzangu wanasema kwamba wamepewa mgao wa lita 100 za mafuta ya dizeli katika Wilaya zao kwa ajili ya Jeshi la Polisi na wengine wamesema 200. Mimi niseme kwamba kwa miaka minne iliyopita, Jeshi la Polisi Wilaya ya Rombo halijawahi kupata mgao wa hata wa lita moja wa dizeli. Sasa mimi nashangaa wale ndugu zangu wanafanya kazi namna gani? Niliongea na *OCD* akaniambia mara ya mwisho mgao waliopata ni lita 400 ambazo walipewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa ajili ya shughuli za Uchaguzi. Sasa hili ni tatizo kubwa. Naomba sana Waziri asaidie katika kuhakikisha kwamba tatizo hili limepata ufumbuzi. Wakati naongea na Askari pale Wilayani waliniomba kama ikiwezekana niiombe Serikali iruhusu tozo ambazo zinatokana na makosa ya usalama barabarani nusu yake zitumike kwa ajili ya kusaidia Jeshi la Polisi pale Wilayani, liweze kupata mafuta kwa ajili ya kuendesha shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine linalowakabili Polisi pale Rombo ni kama walivyosema wenzangu, wana madai ya miaka mingi sana ya fedha za uhamisho. Nawaomba sana vilevile Makamanda na Wizara ijaribu kuangalia jambo hili kwa sababu linawavunja moyo Askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Magereza Rombo pana msongamano mkubwa sana wa wafungwa na kwa sababu Mahabusu ni moja basi wakati mwingine watoto wanachanganywa na watu wazima katika Gereza moja. Eneo la Gereza ni kubwa vya kutosha, lakini halina uzio. Kwa hiyo, Askari wanapata shida sana kwa ajili ya kuwalinda wafungwa. Mara nyingi kadri walivyoniambia ni kwamba mfungwa anapotoroka inakuwa ni wajibu wa Askari kutozwa kiasi fulani cha mshahara wake kama adhabu kwa ajili ya uzembe. Kwa hiyo, naomba Jeshi la Magereza kufanya mkakati wa kuangalia namna ambavyo wanaweza kusaidia ili kuweza kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, msongamano mkubwa wa wafungwa pale Wilayani kwa kiasi kikubwa unatokana na uhaba au uchache wa Wapelelezi kwamba kesi zinaahirishwa mara kwa mara na nyingine mapya zinazaliwa, zinachukua muda mrefu kuamuliwa na hasa tena kutokana na uhaba wa Mahakimu. Kwa hiyo, msongamano ni mkubwa na naungana na wenzangu waliopendekeza kwamba adhabu zingine zingetumika ili kuweza kupunguza msongamano wa wafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Gereza la Rombo nimewakuta akinamama fulani watatu wameshikiliwa. Mmoja anashikiliwa kwa takribani mwaka mmoja sasa akiwa na mtoto wa miaka miwili. Sababu ya kushikiliwa ni kwamba mume wake anatuhumiwa kwa kesi ya mauaji. Sasa mume hapatikani, wamemshikilia huyu mama pamoja na mtoto wake. Mama mwingine alijifungulia kule Gerezani, alikamatwa akiwa na matatizo ya kawaida tu ambayo yangeweza kutatuliwa kijamii. Nilienda kule baada ya Mkutano wa Tatu, mtoto alikuwa na wiki mbili tu. Sasa vitu kama hivi vinawafanya Mahabusu na hata wale Askari wajisikie kwa kweli kuna kitu cha kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uhamiaji. Kuna jengo la Uhamiaji pale Tarakea na Holili. Yale majengo ukiangalia ni tofauti kabisa na majengo ya wenzetu nchi jirani ya Kenya. Hayana kompyuta za kufaa, hayana kamera na mambo kama hayo. Naomba Jeshi la Uhamiaji nalo litafute namna ya kuboresha Ofisi za Uhamiaji pale Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nasema kwamba kuna matatizo kadhaa yamezungumzwa lakini ukiangalia kazi ambayo inafanywa na Jeshi la Polisi na matatizo tuliyozungumza, mimi nasema kwamba kazi inayofanywa ni mzuri, matatizo yaliyopo ni matatizo yanayoweza kutatulika na kwa sababu hiyo tuna wajibu wa kuwatia moyo Polisi wetu ili waendelee kufanya kazi ambayo wanatakiwa waifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekuwa nikijiuliza na naomba Mwenyezi Mungu aepushe jambo hili kwa mfano Polisi wangeamua kugomba kufanya kazi kwa siku moja, *Traffic* wakaondoka barabarani, Polisi wote wakaondoka vituoni, vituo vikafungwa, *Detectives* wote wakaondoka kwa muda wa siku moja, wabakaji wakafanya kazi yao, majambazi wakafanya kazi yao na magari barabarani yakaenda ndivyo sivyo, nchi ingekuwa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na lawama ambazo zinaweza zikatolewa kwa Jeshi la Polisi, tunao wajibu wa kuwapongeza kwa kazi wanayofanya na pale ambapo tunaona mambo hayaendi sawasawa tuwaite na tukae pamoja ili kutatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nilishakumbana na mkono wa Polisi katika maandamano ya Arusha, silaumu. Walifanya kazi yao, kama ninavyosema silaumu lakini kazi waliyoifanya hata kama ningelaumu ukilinganisha na wajibu mwingine wanaoufanya Kitaifa na kama nilivyosema ni watu ambao wamejitolea, wame-*risk* maisha yao kwa ajili ya amani yetu, hatuna sababu ya kupambana nao kiasi cha kuwakatisha tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe tu Polisi na Majeshi mengine wakati wanapokuwa wanatekeleza yale maagizo ambayo wanapaswa wayatekeleze kwa mujibu wa sheria basi katika hali ya kibinadamu waongozwe pia na ubinadamu. Kwa sababu unapomkamata mtu na akakubali kutii amri ya kukamatwa kwake basi muache. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema nilikumbana na tatizo hilo Arusha kwa sababu wakati ule nilikuwa naning'iniza mkono wangu na nilikamatwa nikakubali. Nikaambiwa nipande kwenye

gari, nikaomba jamani taratibu mkono wangu una matatizo na una vyuma. Nilipigwa kofi juu ya mkono mbele ya *OCD* Arusha. Nilipoomba nafasi ya kwenda kuucheki mkono wangu hospitalini nilikataliwa. Sasa hili ni jambo la ajabu. Mtu amekamatwa, amekubali, ameingia kwenye gari, unampiga kwa sababu gani? Kwa hiyo, jinsi ambavyo raia wanakatazwa kuchukua Sheria mkononi hata Askari Polisi pale inapobidi msiamue kuwahukumu raia kwa kuwapiga. Tena kwa kuwapiga kwa namna ambayo inapitiliza! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nilishuhudia mama mmoja alikamatwa katika maandamano, akapigwa virungu na Askari nane! Askari nane wanampiga mtu mmoja tena mwanamke! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndio nasema katika utekelezaji wa kazi zenu, basi mimi naomba busara itumike, vinginevyo narudia kusema nawapongeza sana kwa kazi mnayofanya, vinginevyo Taifa hili amani tuliyonayo, kazi tunazozifanya, maisha ambayo ni ya kawaida tunayoendeleanayo, yasingewezekana kama sio kwa kazi nzuri mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nawaomba sana, Kamanda Mwema, tafadhali sana pale Rombo upaangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuamka salama siku ya leo na ndio maana niko hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ulinzi wa wananchi na mali zao ni jambo la msingi sana ili kutoa fursa kwa wananchi wetu kujishughulisha na shughuli mbalimbali za maisha pamoja na kushi kwa usalama bila ya wasiwasi. Kama Taifa, kazi hii ngumu katika utekelezaji tumewakabidhi ndugu zetu wa Jeshi la Polisi pamoja na kuwa sisi wananchi wengine tuna wajibu mkubwa wa kuwasaidia katika kuetekeleza wajibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina masikitiko makubwa sana kwa ndugu zetu wa Jeshi la Polisi wa Wilaya ya Micheweni, jinsi wanavyopata tabu kutokana na kukosekana kwa makazi kwa muda mrefu jambo ambalo limefanya baadhi ya Askari hawa wanatoka katika kituo chao cha kazi Micheweni kila siku na kurejea makwao ikizingatiwa kwamba, wengi wao hawana usafiri binafsi wa kurudi majumbani kwao. Vilevile Mheshimiwa Waziri, anafahamu vizuri Wilaya ya Micheweni kuna tatizo kubwa la kukosekana kwa usafiri wa uhakika wa kurudi Wete na maeneo mengine, hivyo tunawasumbua sana ndugu zetu hawa na hii si haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha Polisi cha Wilaya ya Micheweni, kilifunguliwa mwaka 1979, hadi sasa ni miaka 32! Miaka 32 ni miaka mingi sana na niseme kwamba miaka 32 ni sawa na maisha ya mtu mzima! Mimi niseme kwa uchungu kabisa Serikali ifikie mahali ione haya! Wilaya ya Micheweni ni Wilaya sawa na Wilaya nyingine Tanzania, hivi ni kwa nini mpaka leo haiangaliwi? Wilaya ya Micheweni ni Wilaya kongwe, mpaka leo Askari hawajajengewa makazi na wala hatujasikia kwamba, kuna mpango wa kujengewa makazi ya Askari hawa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kujibu hoja aniambie ni kwa nini na ni lini Askari Polisi Wilaya ya Micheweni watajengewa makazi ili waepukane na izlali ya kwenda na kurudi kila siku?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru yapo magari ya kazi kwa ajili ya Askari hawa, lakini ni jambo la kusikitisha, mara nyingi kunapotokea tukio lolote, Askari hawa wanashindwa kufuatilia mara moja na kwa kina kutokana na uhaba wa mafuta kwa ajili ya magari haya! Ifahamike kwamba, Micheweni ni eneo ambalo lina bandari ndogondogo nyingi, kuna uwezekano mkubwa wa wengine kujipenyeza na kuweza kufanya lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla, kuona uwezekano mkubwa wa kuwapatia makazi Askari hawa Polisi lakini pamoja na Maafisa wa Uhamiaji wa Wilaya ya Micheweni, kwani na hata wao wana tatizo kubwa ambalo linafanana na la Polisi. Jambo ambalo kwa upande wa Maofisa wa Uhamiaji wa Wilaya ya Micheweni, hata

usafiri wa aina yoyote ile, hawana. Ikiwa Maofisa wa Uhamiaji hawana hata usafiri wa aina yoyote ile, ni vipi wataweza kufanya kazi yao kwa ufanisi? Mimi niseme kwamba, huku ni kuitelekeza Micheweni na ni kuwatelekeza vijana wetu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, wananchi wangu wa Jimbo la Micheweni, wana kilio kikubwa na wamenituma nije niwaombee kwa Serikali kwa ujumla. Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Jimbo langu la Micheweni, hawana ajira! Ajira yao wanajitegemea na Mheshimiwa Waziri, pamoja na wananchi wa Jimbo langu la Michweni kukosa ajira, basi wana mchango mkubwa kuanzia mwezi wa tisa mpaka mwezi wa pili, wananchi wa Jimbo langu la Micheweni, wanaingiza kipato kikubwa kwa Wizara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, awasiliane na Ofisi hii ya Uhamiaji ya Wilaya ya Micheweni, aongee nao, awaruhusu wawapunguzie masharti! Wawapunguzie malipo ya *Passport,* kwa sababu Mheshimiwa Waziri, wananchi wangu wa Jimbo la Micheweni, ni wasafiri wakubwa kuelekea nchini Kenya, kuanzia mwezi wa tisa mpaka mwezi wa pili. Hivyo, wamenituma nije kuwaombea kwa Serikali, wapunguziwe malipo ya *Passport* hizi ambazo wanalipa shilingi 15,000/= ambapo baadhi na wengi wao hawana uwezo wa kulipia *Passport* hizi. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, uwaruhusu watumishi wako wa Wilaya ya Micheweni wa Ofisi ya Uhamiaji, basi angalau wawafanyie kwa shilingi 5,000/= kwa kila *Passport* moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, aweke mazingira mazuri katika Ofisi hii, ili waweze kupata *Passport* za *East Africa.* Kwa sababu, inavyoonekana wananchi wangu wa Jimbo la Micheweni wanaposafiria *Passport* hizi *temporarly* inaonekana kwamba, hazina uzito na wanapata usumbufu wanapofika nchini Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba, kutowaimarishia mazingira ya kazi vijana wetu hawa wa Polisi pamoja na Uhamiaji, basi ni sawa na kuweka usalama wetu rehani. Niwapongeze sana vijana wetu wa Polisi pamoja na vijana wa Uhamiaji Wilaya ya Micheweni, kwa jinsi wanavyojitolea kufanya kazi yao kwa umakini pamoja na mazingira magumu wanayofanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie kumwomba Mheshimiwa Waziri, awasiliane na Wizara ya Uhamiaji Wilaya ya Micheweni, ili wapunguziwe masharti na wapunguziwe bei ya kupata *Passport* ili wananchi wangu wa Jimbo la Micheweni, walio wanyonge ambao wengi wao hawana uwezo wa kuweza kumiliki *Passport* hizi ili wakajitafutie ajira kule nchini Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nampongeza Waziri kwa Hotuba yake nzuri. Napongeza Hotuba ya Kamati ya Ulinzi na vilevile naipongeza Hotuba ya Kambi ya Upinzani. Naomba tu yale yaliyoelezwa kwenye Hotuba ya Kambi ya Upinzani, yafanyiwe kazi. Yale ni maoni, ni Watanzania wametoa maoni yao kadri wanavyoona na maoni ya mtu yeyote ile, ni maoni na imekuwa ni vizuri tumesikia maoni ya watu fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu wote umuhimu wa Jeshi la Polisi. Ni watu ambao wanalinda usalama wa raia na mali zao. Tunajua wanafanya kazi katika mazingira magumu na ndio maana tumekuwa tukipiga kelele tukiiomba Serikali iwaongezee maslahi, iwapatie nyumba nzuri za kuishi pamoja na vifaa bora vya kufanyia kazi. Hilo tunalitambua na tunaiomba Serikali ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo nitatembelea Wilaya ya Temeke. Wilaya ya Temeke kuna matukio ambayo yalifanywa na Askari Polisi, pengine ni kwa bahati mbaya walikuwa kwenye shughuli zao za kikazi, walikuwa kwenye doria lakini nitaomba niyazungumze.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtoto mmoja anaitwa Juma Hamza. Mtoto huyo alikuwa ni mwanafunzi hapa Dodoma katika shule ya Msingi Makole, alikwenda Dar-es-Salaam kwa wazazi wake wanaoishi Keko Magurumbasi. Kwa bahati mbaya, amekumbana na Polisi wakiwa kwenye doria wakamjeruhi na risasi. Mtoto huyu ameishi kwa mateso makubwa sana katika Hospitali ya Muhimbili, Polisi hawakumhudumia huyu mtoto, amefanyiwa *operation* ya kwanza, amefanyiwa *operation* ya pili, ambayo ilisababisha kidonda kikubwa sana. Katika matibabu hayo, mtoto huyu ambaye ametoka katika familia ambayo ni maskini ilifikia mahali muda wake wa kutoka ukawa umefika akanyimwa Hati ya Kuruhusiwa na muda wa kuendelea kuishi Hospitali, ulikuwa umeisha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoto huyu licha ya kujieleza kwamba yeye ni maskini na wazazi wake hawana uwezo, kwanza kabisa, naomba niwajulishe kwamba, mtoto huyu ana miaka 12 na kwa bahati nzuri katika gazeti hili la Mwananchi, ameoneshwa, lilikuwa ni gazeti la tarehe 2 Julai, picha yake ipo inaonekana hapa, mtoto ameoneshwa.

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge alionyesha Gazeti la Mwananchi analolizungumzia)*

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Ni mtoto mdogo mwenye miaka 12, wazazi wake ni maskini. Alipoondolewa kwenye ile Hospitali ya Muhimbili, zilikosekana shilingi 50,000/= ili aweze kupewa Hati ya Kuruhusiwa ambayo ilikuwa inaonesha kwamba anatakiwa aendelee na matibabu ya aina gani na ama atumie dawa zipi na anatakiwa arudi lini hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoto huyo aliishi kwa mateso makubwa sana kwa ajili ya kukosekana hizo shilingi 50,000/=. Baada ya watu kufahamu kwamba zinatakiwa shilingi 50,000/= ili hiyo Hati ipatikane akiwa na hali mbaya, wakajitokeza wasamaria, mmoja akatoa shilingi 50,000/= ile Hati ikawa imepatikana. Mpaka tarehe 2 Juni, mtoto yule alikuwa hajapata dawa yoyote ile! Ilipofika tarehe 5 Juni, ndipo zikapatikana shilingi 13,000/= ambazo zilitakiwa zinunue dawa ili yule mtoto aweze kuendelea kutumia. Mtoto huyu ameathirika sana, kidonda hiki ni kikubwa, kinatoa usaha mwingi ambao umechanganyika na maji na kwa kweli, mtoto huyu ana hali mbaya sana! Hata ukimuona hana matumaini ya kuishi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamoja na kwamba Polisi walikuwa kwenye kazi yao, kazi ya doria, nzuri ya kutulinda dhidi ya majambazi, dhidi ya lolote linaloweza kutokea. Baada ya kugundua kwamba huyu mtoto ni wao, wamemjeruhi, walikuwa ni Polisi wa Kituo cha Chang'ombe, ni kwa nini basi mtoto huyu asihudumiwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namtaka Waziri wa Mambo ya Ndani, atueleze hatma ya mtoto huyu na mambo haya ndiyo yanayofanya kunakuwepo na haya mambo yanayoitwa maandamano, malalamiko! Katika hili ni kwa nini tusiandamane? Kwa kweli, mimi kama Waziri hataweza kunipatia majibu mazuri kwa huyu mtoto na mimi kama mzazi ambaye nimelala leba, najua shughuli ya kumtoa mtoto tumboni, nimeumia, kwa kweli sitakubali! Nitawaongoza wananchi wa Temeke, tutaandamana mpaka Ofisini kwa Waziri, tumpitie Waziri atuongoze tuandamane mpaka kwa Mheshimiwa Rais, kwa kuwa Mheshimiwa Rais ndiye anayekusanya kodi zetu labda atatoa fungu mtoto huyu akatibiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile inawezekana taarifa hizi hazikumfikia Mheshimiwa Waziri na pengine hata *IGP* hafahamu! Maana wakati mwingine huku chini kuna mambo yanafanyika Viongozi wao hawafahamu! Basi kwa taarifa hii kama Mheshimiwa *IGP* alikuwa hafahamu au Mheshimiwa Waziri alikuwa hafahamu, naomba utaratibu wa haraka sana ufanyike ili kuokoa maisha ya huyu mtoto ambaye alikuwa ni mwanafunzi wa shule ya msingi na ameshapoteza matumaini ya kuendelea na shule. Pamoja na kwamba yuko hai, ukikaona kanacheka tu lakini si hakajui lolote! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hilo tu. Kuna kijana mwingine, Ahmed Abdalah wa Temeke. Polisi hawa wa Chang'ombe wakiwa kwenye doria, ilikuwa ni mchana, kwa bahati mbaya walimpiga risasi kiunoni! Hiyo risasi bado iko mpaka leo kiunoni! Walipomwona Polisi wale walisimama, wakaenda wakampa pole, tunashukuru hata kwa ule uungawa wa kusimama na kwenda kumpa pole lakini iliishia palepale! Kijana yule ndugu zake walimchukua, wakampeleka

Hospitali ya Muhimbili. Huyo baba, maana ana umri wa kati ya miaka 34 mpaka 36, hivi navyozungumza yuko nyumbani kwake, risasi bado iko kiunoni, anajihudumia mwenyewe!

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Jeshi la Polisi ndio waliosababisha hiki kitu na ilitokea bahati mbaya, kunakuwa na kigugumizi gani cha hawa watu kuhudumiwa? Kwani ni binadamu gani ambaye hafahamu bahati mbaya? Kila mtu bahati mbaya anaifahamu na kama ni bahati mbaya vitu hivi ni kwa nini hawa watu hawahudumiwi? Namwomba Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa *IGP* ananisikia, Serikali hii sikivu inanisikia sana na hata Mheshimiwa Rais, ananisikia kabisa ninaamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wawili ambao pengine inawezekana wakawa vilema, Serikali naomba iwahudumie, naomba iwahudumie na naomba Waziri kwenye majumuisho aniambie hawa watu wanahudumiwa vipi, ambaye hata tumbo lake sasa hivi linaonekana liko kama mkeka kwa ajili ya mishono, ikibidi apelekwe hata nje afanyiwe matibabu ya hali ya juu huyu mtoto tuokoe maisha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Madaktari pale Muhimbili walikataa wakasema hatukutambui, hatuwezi kukopokea kwa sababu huna Hati na hatuwezi kuwalaumu ndiyo haohao wamechanganyikiwa mishahara yao mibovu, maisha yao ndivyo hovyo sasa watafanya nini? Naomba Mheshimiwa Waziri hilo aliangalie na anipatie jibu zuri vinginevyo ndiyo yale maandamano hamtayakwepa, tutaandamana na yeye Waziri atatusaidia tuandamane twende mpaka kwa Rais, tukatafute pesa ya kumpeleka huyu mtoto hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pale ninapoishi ninaishi karibu na Kituo cha Kilwa Road Polisi, ni jirani sana. Kuna mtaa mmoja unaitwa Keko Machungwa, kumekuwa na usumbufu mkubwa sana nyakati za usiku. Wanasheria kuna kitu wanaita *Tort*, kuna watu huwa wanaamua kufanya shughuli zao kwa maana kwamba wamepata sijui vibali Polisi, wanapiga muziki, wanatundika spika kwenye madirisha ya nyumba za watu, wanapiga muziki kuanzia saa nne usiku mpaka saa 11 alfajiri, mtu hulali, nyumba hizo zina wanafunzi, hao wanafunzi wata-*concentrate* vipi kwenye masomo yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napaki gari langu pale Kilwa Road Polisi, niliwahi kuzungumza na Mkuu wa Kituo akasema ni kweli mama hili tunalifanyia kazi na tunawaeleza lakini sasa hawa watu wengine wakati mwingine ndiyo hivyo lakini tunajitahidi. Mheshimiwa Waziri hili nimeliongea tena kwa uchungu kwa sababu tunapata shida, unashinda ni mzima, unalala ni mzima unaamka ni mgonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia mtaa huo una vijana wengi sana ambao wanatumia madawa ya kulevya, bangi, sijui wanazitoa wapi? Vijana wanasumbua sana mpaka wenyewe wameuita kwamba ni mtaa wa wasumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifika mitaa hiyo muda wa saa nne, tano, sita mchana kama huna mwenyeji unaweza ukakimbia, ukasema kuna msiba wa nani au kuna tukio gani, vijana wamejipanga zaidi ya 100 hata walipotokea haijulikani, wanavuta hayo madawa, wanayapata wapi? Yanapita wapi? Hao vijana ukiwaangalia hakuna hata mwenye uwezo wa shilingi 5000, ukiwaambia ni wakali kwelikweli tena ukikaa vibaya mkoba wanaukwapua. Naiomba Wizara ya Mambo ya Ndani iliangalie hilo, Mheshimiwa *IGP* anasikia, Mkoa wa Temeke, Keko Machungwa Mheshimiwa *IGP* unanisikia watu hatulali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumaliza nizungumzie suala la Askari Magereza, kwa kweli kama kuna Askari ambao wanaishi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Ya kwanza?

**NAIBU SPIKA:** Ya pili, ahsante.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Siungi mkono hoja mpaka Waziri aniambie hatma ya mtoto huyu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwamba umenipatia fursa hii ili nami niweze kuchangia hoja hii ambayo ina mambo yanayonigusa katika utendaji wangu wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa hatua ya awali kabisa, napenda kwa nafasi na kwa niaba ya ofisi yangu, kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwa hotuba yake. Pia napenda kuwashukuru sana Wabunge wenzangu wote waliosema kabla yangu, pamoja na wale ambao wamesema mambo ambayo hata mimi sikubaliani nayo, lakini ndiyo demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natangulia kwa kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia zote na nampongeza Waziri lakini nawashukuru sana Maafisa na Watumishi wa ngazi zote wa Wizara hii kwa jinsi ambavyo tunashirikiana bila kushikana mikono. Tunashirikiana kwa mujibu wa Sheria, lakini wanapokosea tunasema umekosea na wenyewe wanakubali. Sisi pia tunakosea wakati fulani wanatuambia na ninyi mmekosea hapa tunafanya maamuzi mengine, hivi ndivyo tunavyoshirikiana na wenzetu. Najua wanafanya kazi nzito lakini lawama lazima ziwe ni sehemu ya utendaji wa kazi za umma na nashukuru sana kwa ushirikiano huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi na Wizara hii ya Mambo ya Ndani ni mhimili mkubwa sana katika utawala wa Sheria kitu ambacho ni moja ya nguzo za dira ya Taifa ya kufikia 2025. Nampongeza sana Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali Said Mwema na Maafisa wengine hasa kwa kusimamia vizuri Programu ya Kuboresha Jeshi la Polisi. Hatua ya manufaa ya Programu hiyo zinaanza kuonekana kwamba wanafanya kazi kama Polisi wataalamu, naomba mwendelee*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba yetu, Ibara ya 3, mwanzo kabisa inasema nchi hii sasa ni ya kidemokrasia na ya kijamaa, isiyokuwa na dini, yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa. Mtazamo huo wa Katiba upo ndani ya Bunge hili. Wanachama wote wa Vyama vya Siasa wapo hapa isipokuwa mimi na kiti hiki siku zote kitaendelea kukaliwa na mtu ambaye hana Chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi kama Mtanzania na kama Mshauri wa Mambo ya Sheria wa Serikali, kitu kimoja tu ambacho lazima tukielewe ni kwamba Vyama vya Siasa vinasukuma itikadi zake na hili linaonekana hapa Bungeni, kwa hiyo, mnahitaji uvumilivu wa hali ya juu sana. Hii miongozo, kuhusu utaratibu, ni jambo jema lakini peaneni nafasi ya kuvumiliana, kama vile mkono wako wa kushoto na mkono wako wa kulia vinavyoshirikiana na vidole vyote ulivyonavyo, wale wenye vitano, wale wenye sita iwe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa ajili ya kufafanua baadhi ya mambo ambayo naona yanahitaji ufafanuzi ambayo yako matano. Nimeisoma hotuba ya Mheshimiwa Godbless Jonathan, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Mambo ya Ndani. Mambo mengi ameyasema kwa lugha kali kidogo na kama alivyosema Mnadhimu Mkuu na namshukuru sana Mheshimiwa Lukuvi kwamba alisikia nilipomwambia kwamba amwaachie Mheshimiwa Mbunge aseme, amalize na kama atakuwa na Mwongozo aseme baada ya yeye kuwa amemaliza. Kwa sababu naamini kama alivyokuwa ameamini Jaji Blandes, katika kesi moja huko Marekani, kwamba unapokuwa na mawazo ya mtu mwingine unapata nafasi nzuri zaidi ya kutafakari. Mimi naamini kwamba katika hotuba ile yapo mambo ambayo yanahitaji kusemewa na kama alivyosema Mbunge yule wa Shinyanga, mimi hapa siondoki naingia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni dhana kwa kweli kwa Kanuni za Bunge haturuhusiwi kuzungumzia mambo ambayo yako Mahakamani na matukio ya Arusha yale ambayo ameyazungumzia yapo Mahakamani na mimi naona si sahihi kuyarejea. Itafurahisha kuyarejea lakini ninajizuia kuyarejea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni la uchaguzi, Waheshimiwa Wabunge, katika ustaarabu wa kawaida, Bunge hili liliona ni muhimu kwamba tunapokuwa tunashindana katika siasa katika uchaguzi, njia moja ya kupinga matokeo ya uchaguzi ni kufungua kesi Mahakamani siyo kuandamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naomba mpunguze makofi kwa sababu nafikiri kwamba tukianza hivi hatutafika, ni lazima tuheshimu Sheria. Njia ya kupinga matokeo ya uchaguzi ni *petition* na Ibara ya 83 ya Katiba inasema hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, la Chama kuandikishwa. Chama cha Siasa, sharti moja la Chama cha Siasa kuandikishwa, ukisoma Ibara ya 20, ni kwamba Chama hicho hakitumii au hakipiganii matumizi ya nguvu au mapambano kama njia ya kufikia malengo yake kisiasa. Nimesikia lugha kali hapa kwamba tutaandamana mpaka kieleweke toka Mwanza mpaka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandamano ni haki yenu kwa mujibu wa Sheria na yazingatie Sheria lakini pengine tunahitaji kufanya mabadiliko katika Sheria kwa ajili ya ku-*regulate* maandamano kwenye maeneo ambayo watu wengine ambao hawataki kuandamana wanafanya kazi. Nafikiri ipo sababu ya kufanya hivyo. Nchi nyingine kama Ujerumani wamefanya hivyo. Nimemsikiliza Mheshimiwa Kiwia akizungumza maneno makali, hisia ni hisia lakini rudi sasa umekuwa mtu mzima, mtu mzima dawa, tuvumiliane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni suala kwamba Serikali hii ambayo mimi ni Mwanasheria Mkuu wake, inaua watu na inaonekana kama ni Sera ya Kuua Watu. Sitaki kusema mengi, mimi ni Mkatoliki na nafahamu uzuri na utakatifu wa maisha ya mtu jambo ambalo liko kwenye Katiba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshalitolea maelezo jambo hili na amesema Serikali haitakaa kimya. Mimi nikubali kwamba kuna wakati tumelegea kufanya uchunguzi kwa mauaji yanayotokea na ambayo sababu zake hazijulikani na kufuatia agizo lile la Waziri Mkuu sasa shughuli hiyo itaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kwenye Gazeti la Serikali, Na.252 la tarehe 16 Julai, 2004, Jaji Kiongozi baada ya kushauriana na Jaji Mkuu waliteua Mahakimu Wakazi Wafawadhi wa Wilaya zote kuwa *Coroner*. Kwa hiyo, wapo watu wa kufanya kazi hiyo, tutakwenda taratibu na tumesoma pia ripoti za taasisi zingine zinazofanya uchunguzi kuhusu utawala bora na vitu vingi ambavyo tunafikiri kwamba ni vizuri kuamshwa na tutavifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo ambao wanalaumu Polisi, kwamba wanawakamata au wanawapiga watu wanaoandamana, kwa mfano kesi ya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa ambao tumekuwa nao kwa siku ya leo na mimi naamini siku nyingine zingefanana na leo, heshima yetu kama Wabunge na Bunge hili mbele ya macho ya wananchi ingeweza kupanda zaidi. *(Makofi)*

Ni kweli pamesemwa maneno mengi sana yanayohusu uhamasishaji wa maandamano kwa wananchi na mimi ni Mbunge, nchi hii ina uhuru lakini tafsiri ya Ubunge ambayo mimi ni kipindi cha tatu ni kwamba wananchi wa Kongwa wamenituma kuwa mwakilishi wao, kuiambia hii Serikali ambayo iko hapa shida zao. Iwe hapa Dodoma, iwe kwenye Wizara mojamoja, iwe kwa

Waziri Mkuu, iwe Ikulu, kama kuna shida inayohusu kupeleka ujumbe huo huko na hivyo ndivyo ilivyo kwa kila Mbunge. Kitu cha mwisho wanachokitarajia watu wa Kongwa ni kuona mimi naenda kuwahamasisha waandamane, maana yake ni kwamba mimi kazi yangu ya kufikisha ujumbe kule nimeshindwa, ndiyo tafsiri yangu mimi. Ila wao wananchi wakiandamana, hilo ni suala lingine maana wanaweza wakawa wanaandamana wananipinga mimi au wana jambo lao wanataka kufikisha wao wenyewe wameona kwamba ule mdomo wao wa kuwafikishia hautoshi, sasa wafikishe wenyewe, hilo ni suala lingine lakini mimi siwezi kuwahamasisha wao tena, kwa mambo ambayo ningefikisha mimi na wamenichagua, kidogo inakuwa tabu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba Wabunge tufanye kazi yetu ya Ubunge, pale ambapo Mbunge unapaswa kufikisha ujumbe, fikisha ujumbe, sasa ukiwa Dodoma tena unafikiria kuwachukua watu Mwanza uwalete Dodoma, maana yake sasa wewe hapa Dodoma hakuna haja ya kuwepo.

La pili kabla sijafikia lile la Mwongozo wa Pauline Gekul, nianze na Kanuni zetu katika kukumbushana kwetu kwa kawaida, ukurasa 49, Kanuni ya 72, kuhusu amani na utulivu Bungeni ambayo ndiyo kazi ya Mwenyekiti anayekuwa hapa awe ni Spika, Naibu Spika au Wenyeviti, kazi yao kubwa ni kuweka utulivu na amani Bungeni, kuhakikisha kwamba kila Mbunge anapata nafasi yake ya kuwakilisha wananchi wake ipasavyo.

Kanuni ya 72(1) inasema Spika atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa utaratibu bora unafuatwa Bungeni, na uamuzi wa Spika kuhusu jambo lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho. Ndiyo maana nilipowaona baadhi ya Wabunge waaanza kujadili kuhusu maamuzi nikawa nawaambia unakaribia kuvuka mstari na wangevuka basi tungekuwa tunaongea mengine. Bahati nzuri walizingatia, mimi naamini kipindi cha kujifunza Wabunge wote kimepita, sasa ni kipindi cha kuwa Wabunge na kufanya kazi yetu ya Ubunge, vile vikao vilivyopita vya kujifunza tulivumilia sana, sasa wote ni Wabunge, kwa hiyo, tufanye kazi yetu ya Ubunge na tutambue mamlaka ya Kiti.

Sasa ikifika mahali mtu umetolewa nje kama nilivyosema jana, basi unatoka kwa staha, nisisitize kwa sababu ndiyo utaratibu kote. Unaweza ukajikuta una jazba fulani umesema maneno ambayo labda hata wewe mwenyewe hukutarajia, Kiti kikakuomba hebu kidogo kapunguze jazba nje basi unatoka taratibu, usipotoka taratibu ni utaratibu wa Mabunge vilevile ndiyo maana wapo Maaskari hapa watakubana tu na kukutupa nje. Huu ni ukweli ambao wala hauna haja ya mjadala lakini ukitoka kwa utaratibu wala haina shida na ukitoka, unatoka nje ya geti, kwa Kiingereza katika Kanuni zile wanasema *out of the premise of Parliament* kwa sisi hapa kwetu ni kwenye ukuta wetu, kule kwenye machungwa kule, kwa sababu mliona juzi baadhi walitoka nje, mliona magazeti ya jana Wabunge wananyoosheana vidole, wanataka kupigana nje hapa kwa sababu walitoka na baadhi ikaleta tatizo. Kwa hiyo, anayekuwa na jazba tunamsindikiza aende akapoe kesho yake anarudi tunaendelea na shughuli kama kawaida.

Kwa hiyo, nirudi kwenye *rulling* yangu kuhusu Mheshimiwa Pauline, yeye amesema kwamba imetumika lugha ya kuudhi kwa Mheshimiwa Lusinde, kwamba baadhi ya watu aliyewaona yeye kwamba ni wanafiki, lugha hii imemtatiza akaomba ushauri wa Kiti. Sasa ushauri ambao naomba niutoe unaendana na ushauri ambao Mwanasheria ametoka kuutoa hapa muda si mrefu sana kwamba iko haja kubwa sana ya kuwa na uvumilivu mkubwa sana hapa ndani. Kwa nini nasema hivyo? Katika mjadala huuhuu wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Felix Mkosamali, alirudia kwa kusema Serikali hii ni legelege na hakuna aliyesimama kumkatiza, mara nne, maana yake ni kwamba walichukua hivyo kwa kuwa na ngozi ngumu kidogo. Mheshimiwa Wenje leo amesimama akasema Mawaziri hawa wa Tanzania wakiteuliwa wanasheherekea kwa sababu watakuwa na nafasi ya kutia sahihi mikataba ya rushwa, ni kauli ambayo si ya Kibunge lakini hakuna mtu aliyesimama hapa, kwa maneno mengine watu wamepuuza au siyo jamani? *(Makofi)*

Haya, Mheshimiwa Chiku jana amesema maneno mengi, lakini baadhi aliyosema amesema Mheshimiwa Mrema na Mheshimiwa Cheyo ni vibaraka. Kanuni inakataa kabisa kumsema Mbunge mwingine kwa jina na kumtaja katika *that negative right* kwamba wewe unatumia kipimo gani kusema kwamba huyu yuko hivi. Kama Mbunge fulani wa Chama fulani anaamua kufanya *alliances* hiyo ni kawaida ya Mabunge duniani, Uingereza *Liberal Democratic* wanafanya kazi na *Conservative*, kwa hiyo wale *Liberal Democratic* ni vibaraka? Haipo hivyo!

Kwa hiyo, neno unafiki linaashiria tabia, tabia ya mtu kusema neno moja na kutenda tendo lingine kabisa, yaani maneo na matendo yanakuwa ni tofauti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa ujumla ni kwamba tujitahidi kuwa na lugha ambayo ni nzuri ya Kibunge, sote, pande zote, hii itatusaidia sana katika kufikisha ujumbe na wananchi wetu kwa kweli hawapendi maneno ya kuudhi hasa wakati huu wa Siasa ya Vyama Vingi, tuvumiliane kidogo, vinginevyo itakuwa vigumu kwa Kiti kuendesha taratibu zake na ndiyo maana ni kazi yangu mtu anataka kuvuka kidogo namkumbushakumbusha aweze kurudi kwenye mstari vinginevyo tunatenda haki.

Mwisho kabisa nilipata ushauri kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge mmoja, kwa Mheshimiwa Philipa Mturano, kwamba kwa wale ambao tunachangia kuhusu wagonjwa, iko taratibu na sheria zinazolinda haki za wagonjwa, hairuhusu kuwataja majina yao na magonjwa wanayoumwa, ni ushauri tu kwamba ni vizuri tuwe tunaangalie vilevile kwa ajili ya kulinda haki zao ikizingatiwa kwamba huyo ni mtoto.

Baada ya maelezo hayo, naomba sasa kusitisha shughuli za Bunge hadi saa 11 leo jioni ahsanteni.

Waheshimiwa Wabunge, jambo moja dogo tu, kesho hakutakuwa na semina ya kilimo na chakula, ahsante.

*(Saa 7.05 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ili kupitisha makadirio na matumizi ya Wizara yake kwa mwaka 2011/2012. Sasa naomba nimwite moja kwa moja Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Balozi Kagasheki, yeye atatumia muda wa nusu saa. Mheshimiwa Naibu Waziri, karibu!

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba yake iliyokusanya mambo mengi kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kupitia Wizara hii, kwa kukamilisha ujenzi wa nyumba za Askari Polisi pale Kilwa Road Dar es Salaam, Unguja Ziwani na kule Pemba Limbari Wete. Japokuwa kwa sasa nyumba hizo hazitoshelezi kulingana na mahitaji ya nyumba kuwa makubwa kwa Askari wetu lakini Serikali imewasaidia kwa kiwango cha kuridhisha. Kwani nyumba hizo ni bora na kuwa na viwango vinavyolingana na kazi zao. Naishukuru sana Serikali kwa kuingia mkataba na *NSSF* ili kuboresha makazi ya Askari wetu. Pia naomba Serikali isiishie hapo iendeleze ubora huo katika maeneo mengine ili kuboresha makazi katika sehemu zilizobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niungane na Serikali kwa kuamua kuweka mkakati wa kujenga Vituo vya Polisi kila Tarafa. Ni kweli kwamba utaratibu huo utasaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza matatizo yanayojitokeza kutokana na kutokuwepo Askari Polisi katika maeneo mengi na kusababisha uhalifu, fujo, wizi na mengineyo. Hii ni hatua mojawapo itakayoendelea kusaidia kuendeleza amani na utulivu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kikosi cha Zimamoto nchini, naiomba Serikali kuongeza fedha za kutosha kupitia fungu husika ili Askari hao waweze kumudu kazi zao. Mara nyingi hulalamikia mafuta, ubovu wa magari na mengineyo. Pia kuweka mazingira mazuri ya ufuatiliaji kwa kitengo hiki ni vyema Serikali kujikita na hilo. Inawezekana matatizo yanajitokeza kutokana na kukosa ufuatiliaji wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakumbuka kwamba idadi kubwa ya Askari nchini wanaishi katika mazingira magumu, kutokana na hali ya makazi yao waliyopangiwa na kusababisha familia kubwa kukutana katika kota moja kinyume na maadili yetu. Wakati mwingine familia hizo hubahatika mke na mume kuwa wafanyakazi wa Jeshi la Polisi na Serikali huwatengea kota moja hiyohiyo kuwa makazi yao na kusababisha mlundikano wa familia. Serikali ifikirie namna ya kuwatengea kila mtumishi hata kama ni mke na mume wake waweze kupata kila mmoja kota yake ili kuondoa usumbufu unaoendelea kujitokeza kifamilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo chakavu yaliyopo Polisi Line Wete, yana nyufa na mengine hayakaliki kabisa. Naiomba Serikali katika harakati zake za kuboresha majengo iangalie na majengo hayo. Wengi wa Askari wanaoishi katika maeneo hayo wamehama, kwa vile eneo tayari limezoeleka kuwa ni makazi ya Askari tokea tupate uhuru na ili kuepuka aibu ya kuonekana kushindwa kwa Serikali kumudu matengenezo ya nyumba hizo, naiomba Serikali kuliweka katika matengenezo ili kufufua kwanza majengo hayo. Kupitia bajeti hii, naiomba Serikali kuboresha ofisi za Askari Polisi kwa kupatiwa nyenzo mbalimbali ili kuondoa aibu zinazojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuta ya kutosha, zana zinazohusiana na ofisi hizo. Mara nyingi Askari wanashindwa kutekeleza majukumu yao kutokana na ukosefu wa nyezo kama hizo. Naiomba Serikali kuboresha Fungu hili linalohusiana na mafuta, silaha, vyumba vya kuhifadhi na silaha zenyewe, *redio call*, fanicha zenye ubora, *uniform*, gari za kutosha, pikipiki za kutosha, posho za pango, posho za uhamisho na posho baada ya saa za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo mfupi, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi ni chombo muhimu sana hapa nchini na jukumu lake la kwanza ni kulinda raia na mali zake. Nitambue na kupongeza kazi kubwa sana linalofanya Jeshi la Polisi maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya Polisi bado ni duni sana, mishahara yao ni midogo sana haiendani na hali ya maisha ya sasa. Shilingi 200,000 kwa Askari atawezaje kuishi kwa mwezi yeye na familia yake? Hawapandishwi vyeo kwa wakati na hili linapelekea mishahara yao kutopanda zaidi ya miaka 10. Hawalipwi fedha zao wakati wa uhamisho, wanateseka wao na familia zao. Tunaitaka Serikali ihakikishe uhamisho unaambatana na cheki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Askari Polisi wanaokiuka maadili ya kazi zao na hivyo kusababisha Jeshi lote la Polisi kuonekana halifai/limeoza. Ni Sheria gani inayoruhusu Polisi kumpiga mwananchi/mtumhumiwa pale anapomkamata? Polisi kazi yake ni kumkamata raia na kumpeleka kwenye chombo husika, mamlaka ya kumpiga anayapata wapi? Polisi wamebadilika wao ni wakamataji na wao wanakuwa Mahakimu, wanawahukumu kwa kipigo hadi watu wasio na hatia wanapoteza maisha na wengine kupata ulemavu wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wanatumia nguvu sana/zaidi wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao. Hata kwenye suala ambalo halihitaji nguvu wao wanatumia nguvu. Matumizi makubwa sana ya nguvu yanalidhalilisha Jeshi la Polisi na tena ni ukatili kwa raia na zaidi linawajeruhi wananchi wasio na hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji yanayofanywa na Polisi maeneo mbalimbali hapa nchini ni aibu kwa Jeshi la Polisi na ni aibu kwa Taifa linalotegemea Polisi walinde amani ya raia. Polisi wanafyatua risasi za moto kiholela sana, hawatumii akili hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanafunzi wa Sekondari ya Mbezi aliyepigwa risasi ya kooni (yuko hospitali) alikuwa anapiga ngoma na kuimba walipoandamana kutaka matuta eneo ambalo mwenzao aligongwa na kufa. Kwa nini apigwe risasi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wamekuwa wanawatesa sana watuhumiwa wanaowakamata na kuwalazimisha kukubali tuhuma ambazo Polisi wamewabebesha.

Wanawanig'iniza watuhumiwa kama kuku, kichwa chini miguu juu, wanawaminya bumbu zao kwa plaisi, wanawapiga matako kwa butu zao maeneo mbalimbali ya miili yao, wanawavunja miguu kwa kipigo, wanawapofua macho kwa ngumi na madhara mengine mengi. Kwa mateso haya ili kuokoa maisha yake analazimika kukubaliana na matakwa yao na hivyo kubambikizwa kesi asiyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushahidi tosha, mwananchi kapigwa sana na Polisi kipigo hicho kimesababisha kukatwa mguuu wake, wamemhasi kwa lazima (wameponda *scrotum*) kwa plaisi na sasa hawezi kutoa huduma kwa mke wake. Mtuhumiwa huyu amepelekwa Mahakamani na Mahakama imemwachia huru kwa sababu Polisi wamekosa ushahidi wa tuhuma zake. Mwananchi huyu amekuwa kilema tayari na ni maskini na familia yake imeathirika na inaendelea kutaabika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali/Waziri aeleze Bunge matukio kama haya yanayotokea sehemu mbalimbali yanashughulikiwa vipi? Nini hatma ya raia huyu ambaye yuko hapa Dodoma kudai haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza yetu hapa nchini yamekuwa na mlundikano wa Watuhumiwa na Wafungwa hali inayopelekea wakose huduma stahili. Sio wafungwa wote walioko Gerezani wanastahili kuwepo pale. Yapo makosa madogomadogo ambayo zingetolewa adhabu za nje kwa muda fulani na baadaye aachiwe huru, aende kuzalisha huko mitaani. Mfano mtu anafungwa kwa kosa la kuiba godoro moja au kuiba Shilingi 10,000/= au kugombana na mwenzie!

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye Magereza yetu wapo Mahabusu ambao wamekaa muda mrefu zaidi ya miaka 9, 8, 7 bila kesi zao kusikilizwa. Kuchelewesha kusikiliza kesi za Watuhumiwa, nalo ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Kilimo la Urambo lina Mahabusu wanawake wamekaa miaka mingi bila kufika Mahakamani, wapo waliokaa miaka 9-6. Wengine wamechanganyikiwa/vichwa vimeharibika kwa sababu ya kutojua hatma ya maisha yao pale walipo. Hata familia/ndugu walishawasahau. Naomba Serikali isaidie Watuhumiwa hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza hili liko kilometa 12 tu kutoka Mjini Urambo. Ni Gereza la Kilimo na Ufugaji na wanalima sana hadi wanalisha Magereza mengine. Cha ajabu, Gereza hili hawana umeme wala gari lolote la kufanyia kazi. Serikali ieleze kuna mipango gani ya kupeleka gari na umeme?

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, ukurasa wa 3, aya ya 7, amekiri kwamba Jeshi la Polisi katika kipindi cha Julai 2010 hadi Aprili, 2011, jumla ya Watuhumiwa 507 walikamatwa na kilo 17,000 za bangi na kilo 5,316 za mirungi pia Jeshi liliteketeza ekari 309 za mashamba ya bangi. Naomba kuishauri Serikali kwamba viwango hivyo ni vikubwa mno kwa hiyo lazima Serikali ifanye utafiti kwa nini wananchi wanashiriki kwenye biashara haramu kama hizo? Pia naishauri iwasaidie wananchi wanaoishi maeneo hayo kwa kuwapatia miradi ya maendeleo ambayo itawasaidia kujiongezea vipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri, naomba sana lifanye utafiti wa kina juu ya vigogo wanaojihusisha na biashara haramu ya madawa ya kulevya ambao huwatuma vijana kuingiza dawa hizo haramu hapa nchini hivyo kuweza kuvunja mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Magereza, napenda kutoa ushauri wangu kwamba Idara hiyo muhimu ipatiwe wataalam wa *sociology* ambao watasaidia kutoa elimu ya ushauri nasaha kwa wanafunzi (wafungwa) ili baada ya kutumikia adhabu zao wabadilike na kuwa raia wema. Magereza yote yafanye kazi za kurekebisha tabia za wanafunzi (wafungwa), *all prisons should be operating as rehabilitation centre.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kupitia Programu ya Ulinzi Shirikishi ambayo imesaidia kupunguza uhalifu hapa nchini. Naomba programu hii ipanuliwe hasa kwa kuwapatia

mafunzo ya Kiaskari wananchi. Hii ni kwa sababu, wananchi wanapata maadui wakati wanapotekeleza jukumu hili la ulinzi shirikishi. Mafunzo ya Kiaskari yatawasaidia kujilinda na kujihami dhidi ya maadui wanaojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu la Polisi lina vitendea kazi duni na ambayo havikidhi haja ya kuwalinda Watanzania na mali zao. Naishauri Serikali katika kuliimarisha Jeshi la Polisi, Jeshi letu lipatiwe zana za kisasa na pia lipatiwe mafunzo ili waweze kutenda kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na azma ya Serikali kujenga Vituo vya Polisi katika kila Tarafa, naomba Serikali ikarabati Kituo cha Polisi Mwera na kukipanua kituo kidogo cha Polisi Mwembemchomeke katika Jimbo la Dole.

Mheshmiwa Spika, napenda pia kuzungumzia juu ya Vitambulisho vya Taifa. Suala hili ni muhimu lakini ni aibu kwamba limechukua muda mrefu kutekelezwa, hadi sasa bado utekelezaji wake haujaanza licha ya ahadi za Serikali. Vitambulisho vitasaidia kuwatambua watu ambayo sio raia wa Tanzania kwa urahisi. Pia vitasaidia kudhibitui uhalifu. Vilevile mipango yetu ya maendeleo itaweza kuwa ya uhakika kwani kwa sasa hatujui idadi halisi ya Watanzania mbali ya sensa zilizofanywa. Nashauri Serikali yetu ilitekeleze suala hili la Vitambulisho vya Taifa kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara yetu ya Uhamiaji iangaliwe na Maafisa wote wanaouza *Passport* za Tanzania kwa watu ambao sio Watanzania waadhibiwe vikali ili kukomesha tabia hiyo mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba sana maslahi ya Askari wetu yaangaliwe kwa haraka na waboreshewe maslahi yao. Naomba Askari wapewe haki zao ili kuwatia moyo vinginevyo tusipowatunza Askari wetu watashindwa kutimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia mchango wangu kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *IGP*, Kamishna wa Magereza, Mkurugenzi wa Upelelezi na Watendaji wote wa ngazi zote na Askari wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Polisi Jamii, Jimbo la Vunjo lina uhalifu mkubwa unaotokana na ujambazi, wavutaji bangi, unywaji gongo, ni dhahiri Polisi peke yao hawawezi kuthibiti uhalifu huo. Kutokana na hali hiyo, inabidi Jeshi la Polisi lihamasishe wananchi kujiundia vikundi vya ulinzi wa jamii. Wananchi wako tayari kushirikiana na Jeshi la Polisi kuimarisha na kuendeleza vikundi hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni fidia kwa nyumba ya Mwenyekiti wa kijiji cha Kiraracha, Marangu na ndugu yake waliounguziwa nyumba zao na kusababisha vifo vya mke na mtoto. Waliosababisha maafa hayo ni dhahiri ni wananchi ambao ni maadui wa Sungusungu. *RPC* Kilimanjaro ametuma maombi kwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Inspekta Jenerali wa Polisi kuomba msaada ili Serikali itoe mchango wake kuunga mkono jitihada zilizofanywa na wananchi kukamilisha ujenzi wa nyumba ya Mwenyekiti wa Kijiji na ndugu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kituo cha Polisi, Kata ya Kilema Kati, kuna wahisani waliojenga Kituo cha Polisi Kilema Kati, kituo hicho kimekamilika. Kina nyumba ya Polisi ya kuishi na jengo la kutunza silaha. Ombi la wananchi ni kutaka Wizara ya Mambo ya Ndani ipeleke Polisi katika kituo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kuhusu ujenzi wa Kituo cha Polisi, Samanga Marangu. Mwaka jana wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete anafungua Benki ya *CRDB* Marangu, Mkurugenzi Mtendaji wa *CRDB* alimuahidi Rais kwamba Benki yake itajenga nyumba za Polisi na Kituo cha Polisi pale Marangu Samanga. Naomba Wizara ya Mambo ya Ndani ifuatilie ahadi hiyo ili nyumba hizo za Polisi na hicho kituo cha Polisi ziweze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, operesheni maalum ya kupambana na uhalifu. Miaka minne iliyopita, wananchi walipiga kura kuwatambua watu wanaotumia silaha, wanaokunywa gogo na kuvuta bangi na kwa kuwa orodha ya majina hayo ipo kwa *OCD* na Afisa Usalama wa Taifa wa Wilaya, ingefaa Polisi iendeshe operesheni maalum ili kuwatia mbaroni wahalifu hao.

**MHE. ASHA MOHAMED OMARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, uimarishaji wa Vituo vya Polisi na nyumba za Polisi. Kuhusu Vituo vya Polisi vimekuwa haviridhishi, haviko katika hali nzuri vinapaswa kujengwa upya na vijengwe vituo vya kisasa hasa kule Pemba vituo vingi ni vibovu pamoja na nyumba za Polisi wanahitaji kujengewa ingawa Wizara imejenga kituo kipya cha Polisi cha Mkoa pale Chakechake lakini na Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mkoani ni kibovu kinahitaji kujengwa upya hivyo naiomba Serikali pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani kuliangalia suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri kwa Askari, mara nyingi Askari wanakabiliwa na matatizo ya usafiri wa gari, inapotokea vitendo vya uhalifu baadhi ya sehemu Askari huchelewa kufika eneo la tukio kwa sababu ya ukosefu wa magari ya Polisi hayakidhi haja. Hivyo, namwomba Waziri wa Mambo ya Ndani kulipa uzito tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Idara inayoshughulikia malalamiko ya wananchi kwa Jeshi la Polisi likiwemo Magereza, Kikosi cha Zimamoto na Uwokozi na Uhamiaji, iboreshe utendaji wa vyombo hivyo ili kuondokana na malalamiko hayo hususan Polisi. Hivyo namwomba Waziri kulichukulia hatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho za Askari zimekuwa ni tatizo sugu ambapo Askari wengi wanalalamikia posho zao hawapatiwi na hasa pale wanapopewa uhamisho. Usafiri na mishahara yao iboreshwe kwani Askari hawa wanafanya kazi kubwa ndani ya nchi ya kulinda usalama wa nchi, raia na mali zao. Hivyo, naiomba Wizara hii ya Mambo ya Ndani kulifikiria tatizo hili ili malalamiko haya yasitokee tena.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi, ni kituo muhimu ukilinganisha wingi wa watu na shughuli za uchumi wa kijamii unaofanyika. Katika maeneo yetu kutokana na ukosefu wa Kituo cha Polisi, wananchi walihamasika na kuamua kuchangia nguvu zao na kujenga Kituo cha Polisi Motwisa, jengo likafikishwa usawa la lenta toka mwaka 2002 Serikali haijaona umuhimu wa kuwasaidia wananchi hao kumalizia jengo hilo. Pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa ahadi hiyo haijatekelezwa. Naomba Serikali inipe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ipeleke pikipiki katika vituo vya Polisi vya Milepa kilichojengwa na wananchi asilimia mia moja, Kituo cha Polisi Mtowisa, Kituo cha Polisi Laela na Kituo cha Polisi Kipeta.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, posho za Askari zinalipwa katikati ya mwezi, hulipwa kiasi cha shilingi 100,000 (laki moja) tofauti na Majeshi mengine ambayo hulipwa kiwango kikubwa kuliko Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa majengo. Majengo mengi ni ya enzi ya ukoloni, Serikali inatakiwa kutenga fungu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Askari Polisi/Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira, kutokana na mwingiliano wa jamii na hali ya kutofautiana kwa maendeleo ya elimu baina ya maeneo, ajira zinazoainishwa kwa ajili ya Wilaya fulani, basi ni bora wazawa au watu wenye asili ya maeneo hayo wapewe fursa (kipaumbele) ili Idara ya Polisi, Magereza au Idara nyingine yoyote ya Serikali iwe na sura ya Kitaifa. Kwa mfano watu wa Arusha inawezekana akaomba kazi katika Mkoa/Wilaya nyingine na kuchukua nafasi ya mtu wa Mkoa/Wilaya husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kamati ya kuchuja waombaji wa nafasi ya kazi kwa Majeshi yetu, Wenyeviti wa Mitaa hupokea maombi na kuyapeleka kwa Mtendaji wa Kata kabla ya kufikishwa mbele ya Kamati inayoitwa ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya/Mkoa. Kushiriki kwa wajumbe hao ambao ni Mkuu wa Wilaya/Mkoa ambao ni wanasiasa huathiri mchakato mzima wa kuwapata watu wenye sifa *(compentence).* Maoni yangu ni kuwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu

wa Wilaya wasishiriki katika mchakato wa kuchuja waombaji badala yake Kamati hiyo iwe ya wataalam kwa kuangalia sifa/vigezo vilivyoainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho ya uhamisho kwa ajili ya Polisi/Magereza pale wanapohama kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine hucheleweshwa na kusababisha usumbufu kwa Askari wetu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Kuzuia Polisi kuoa/kuolewa kwa muda wa miaka mitatu, imepitwa na wakati. Kwa sababu waombaji wengi wanakuwa wameshafikia umri wa kuoa/kuolewa (*marriageble age*) hivyo kuwazuia kuoa/kuolewa ni kwenda kinyume na Haki za Binadamu. Kutokana na ukweli wa mahitaji ya kimwili *(biologically*), kuwataka waajiriwa hao wakae muda wa miaka mitatu ni kurudisha nyuma juhudi za kupambana na janga la Ukimwi. Kutokana na halisi ya kupungua kwa kipindi cha kuishi *(life expectancy*) hasa kwa nchi maskini ambapo ni miaka 45, huwafanya Askari wengi kutofanya kazi kwa ari au ufanisi unaotarajiwa na wananchi. Maoni yangu ni kuwa umri huo upunguzwe na walau kufikia mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mateso kwa watuhumiwa. Jeshi la Polisi/Magereza huwatesa Watuhumiwa wanapokuwa chini ya ulinzi wao, kwa kuwapiga, vitendo ambavyo husababisha vifo na vilema vya maisha. Polisi siyo wanaotoa hukumu kwa Watuhumiwa hivyo vipigo wanavyowatembezea Watuhumiwa ni uvunjifu wa Haki za Binadamu. Watuhumiwa wanaouawa, Polisi haitoi taarifa na Serikali kwa ujumla hukaa kimya. Watuhumiwa wanaotiwa vilema vya kudumu na hatimaye kuonekana hawana hatia, hawana msaada wowote wanaopatiwa na Polisi wala viongozi wa Serikali (wanatekelezwa).

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kuwa Jeshi la Polisi/Magereza waheshimu Haki za Binadamu. Askari wetu wapatiwe elimu ya Haki za Binadamu na Haki ya Raia na kusisitizwa kufuata ili kukomesha mateso kwa Watuhumiwa. Askari watumie mafunzo wanayopatiwa ya kufanya upelelezi kitaalam badala ya kupiga hata pasipohitajika kipigo.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Taarifa iliyowasilishwa na Wizara ya Mambo ya Ndani, ni nzuri na ya uwazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi, changamoto zipo nyingi. Serikali iangalie kwa makini suala zima la uboreshaji wa makazi na huduma bora kwa Askari wetu. Makazi ya Askari yaboreshwe kuanzia nyumba mbovu za makambi na zile za kikoloni zilizokuwepo kwenye baadhi ya Mikoa. Sambamba na suala la kumtaka Askari akae uraiani si ufanisi mzuri wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jeshi letu la Polisi upande wa Zanzibar kumekuwa na malalamiko mengi kwa Askari hao. Kumekuwa na malalamiko zaidi ya makato yanayokatwa ya Shilingi 5,000/= kila mwezi kwa madai ya kwamba ni pesa za kufiwa na pesa hizo hata mtu akifiwa hapewi na akipewa anakawia sana, kwa nini zikawie na zinakuwa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuchelewa kupanda mishahara baada ya mfanyakazi kuongeza elimu yake iwe Kidato cha Sita au Diploma na kadhalika, kumekuwa na ucheleweshaji wa makusudi kutopandisha mishahara yao kwani sheria na utaratibu upo wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira ya Polisi upande wa Zanzibar halipo wazi. Nalisema hili kwa masikitiko kwani dhana iliyopo kwa vijana wa Unguja sio nzuri kwa upande wa Jeshi hili. Imani yao huwezi kupata ajira ya Polisi mpaka uwe kabila fulani ndio uweze kuajiriwa Polisi au uwe na mkubwa. Zana hii inaondosha mapenzi ya vijana kwa Serikali yao, utafutwe mfumo wa wazi ili kupunguza malalamiko na kuwapa imani na mapenzi vijana wa Unguja kwa viongozi wao na Serikali yao kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la rushwa kwa Askari imekuwa ni kawaida kwao na imekuwa ndio mila na desturi ya Jeshi hilo zaidi Kitengo cha Trafiki, ni aibu isioelezeka. Ombi langu kwa Waziri suala hili alifanyie kazi kwa nguvu zake zote ili kulipa heshima Jeshi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kasoro nilizozieleza pia napongeza Askari wetu kwa kazi nzuri wanazozifanya. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa jitihada zake za muda mfupi. Ni imani na matumaini yangu kuona mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. AMINA N. MAKILLAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niunge mkono hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kisha nitoe mchango wangu wa mawazo, katika maeneo machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Vuai Nahodha, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kuandaa hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kipindi cha 2011 – 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Jeshi la Polisi na Magereza. Naipongeza Serikali kwa kuimarisha na kuendelea kuimaisha Jeshi letu ili liendelee kuwa imara kwa ustawi na usalama wa raia na mali zao. Pamoja na pongezi, naomba kuishauri Serikali iboreshe masuala kadhaa ili kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ni ujenzi wa nyumba za Askari wa Jeshi la Polisi na Magereza. Nyumba za Polisi na Magereza zikarabatiwe, vilevile Serikali itafute fedha za kutosha na kujenga nyumba za Askari Polisi na Magereza walau kwa kuanzia Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya na baadaye maeneo ya Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, vitendea kazi, Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kuwawezesha Askari kupata vitendea kazi kama vile magari, pikipiki na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, maslahi ya Askari Polisi na Magereza yaboreshwe hasa posho zao za kufanya kazi masaa ya ziada na maeneo yenye mazingira magumu na hasa Mikoa ya pembezoni kama vile Mkoa wa Mara, Kigoma, Rukwa, Pemba na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, kuongezewa madaraka Askari Polisi na Magereza. Utaratibu wa kupandisha vyeo Askari Polisi na Magereza pia utazamwe upya kwa sababu Askari Polisi na Magereza wanapanda vyeo baada ya kufanya kazi kwa muda mrefu kiasi cha baadhi ya Askari kustaafu bila kuwapa madaraka zaidi tofauti na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, ujenzi wa Vituo vya Polisi katika Vijiji. Serikali iandae mpango wa kujenga Vituo vya Polisi kila Kijiji ili kuimarisha usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, mpngo wa utii bila shuruti. Naipongeza Serikali kupitia Jeshi la Polisi kwa kuandaa mpango wa kuhamasisha wananchi kutii sheria bila shuruti. Naomba Serikali izielekeze Wizara zote kuiga mfano huo na kuandaa mpango utakaowawezesha wananchi kupenda kufanya kazi pasipo shuruti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja hii. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara hii. Mimi nina mambo machache tu ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba itafutwe namna ya kubadilisha utaratibu wa Askari wa barabarani kusimamisha gari kwa mtindo wa kusimama barabarani tena katikati na kunyoosha mkono. Kwani kwa mtazamo wangu, huwa naona Askari hawa wanahatarisha maisha yao kwa Madereva wakorofi, anaweza kumgonga na akakimbia. Hivyo kwa usalama wao, ni kheri kubadilisha pengine tuangalie nchi za wenzetu zina utaratibu gani hasa zilizoendelea ili tuige.

Mheshimiwa Spia, pili kuhusu kumaliza au kutatua tatizo la nyumba za Askari kwa nchi nzima, nashauri kutumia mtindo wa kupitia makampuni yaliyo chini ya mkataba na Benki, itarahisisha ujenzi huo kwenda pamoja nchi nzima. Naongea hivi nikiwa na maana kwamba, Wizara iingie mkataba na makampuni husika kwa maana hiyo nyumba zibaki kuwa mali ya Wizara, mimi naona itaharakisha. Jamani ni aibu sana kuona Askari wetu wanaishi kwenye nyumba za ajabu, nawaomba sana tuwaonee huruma. Kuna haja Mashirika au Taasisi za Mifuko ya Hifadhi, Serikali itumie Taasisi hizi kama ambavyo wamefanya katika ujenzi wa *UDOM*. Pamoja na hayo, naomba muanzie Singida kwani hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, katika Wilaya ya Iramba, kuna Magereza yaliyoanzishwa eneo la Ushora ambako wananchi walitoa maeneo yao ya mashamba bila kudai fidia yoyote kwa kujua kuwa Gereza lile lingekuwa darasa na msaada kwao kwa kuwa lilikuwa ni Gereza la Kilimo na kweli walipoanza mimi nilikuwa bado mdogo sana nikiwa *primary,* walilima ikawa ni somo kwa wananchi wa eneo jirani. Cha kushangaza miaka hii ya karibuni, hakuna cha kilimo wala nini, matokeo yake wameingia kwenye uharibifu wa mazingira kwa kukata miti na kuchoma mkaa hata kuna wakati walichoma matofali. Kinachoniuma sasa mimi ni kwamba wametupotezea ule uoto wa asili kwani hata mvua zimepungua eneo lile. Mimi nalijua kwa kuwa ni kwetu. Kwani miti au msitu ule ulikuwa na wanyama kama chui, simba, tembo na wengine, lakini sasa hivi wamekata miti inayotumia miaka mingi kukua na miti mingine ni matunda ya asili ambayo mimi binafsi nayapenda sana matunda hayo yanaitwa Mapama, kwa kweli naumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna eneo la miembe mingi sana ambalo Magereza walichukua wakajimilikisha bila kulipa fidia kwa wenye miembe ile, wananchi hawakulalamika, tulikuwa tunachuma *free* tukiwa wadogo, lakini walipoingia walianza kuilinda na tukazuiliwa labda uombe kana kwamba sio yako, sasa hayo yalipita swali langu, je, kwa nini Kilimo cha Magereza kimesimama? Kama hawana mpango wa kuendelea na kilimo, wako tayari sasa kurudisha eneo lile kwa wahusika? Kwani na mimi ni mdau, eneo la Babu yangu ni kubwa sana, ili mimi mjukuu nikaendelee na Kilimo Kwanza? Naomba majibu na wananchi walionituma wasikie. Je, Waziri atakuwa tayari kuongozana nami twende kule kwenye eneo nalozumgumzia ili akajionee, huenda atakuwa na maamuzi mazuri zaidi? Je, Waziri yuko tayari kuwaambia Magereza Ushora, kama walivyotumia Wafungwa kukata miti, wawatumie Wafungwa haohao kupanda miti mingine ili kurudisha hali ya uoto na kuleta mvua?

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, naomba nipongeze Jeshi la Polisi kwa kazi kubwa wanayoifanya hasa ya kulinda usalama wa raia na mali zao. Ukweli hali ya ujambazi imekuwa shwari kuliko ilivyokuwa mwanzo. Nawapongeza na kuwatakia kheri sana. Mungu aendelee kuwapa uwezo zaidi. Ila Serikali iongeze bajeti iwe na fedha za kutosha ili waweze kupanua wigo wa miundombinu ya kimazingira ya kazi yao, waweze kufanya kazi vizuri. Pia Magereza wapewe fedha za kutosha ili waweze kuboresha maisha ya Wafungwa. Pia waweze kumudu kulipa madeni ya chakula cha Wafungwa kwa wazabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, napenda nimpongeze Waziri juu ya suala la Vitambulisho vya Taifa. Ni hatua kubwa sana, kwani mimi naona vitambulisho hivi vitakuwa ni kichocheo kikubwa katika kukuza uchumi wa Taifa letu. Naamini itarahisisha mambo mengi, hata wananchi wenzangu, hasa wajasiriamali sasa watatambulika kwenye asasi mbalimbali zinazotoa mikopo na kadhalika. Mambo ya kutakiwa barau za Wenyeviti wa Vijiji au Watendaji na kadhalika yataisha. Wakwepaji wa kodi watapatikana, wanafunzi wa Vyuo Vikuu, wataweza kupata mikopo kwa kutambulka vema lakini Bodi ya Mikopo wataweza kuwapata wadeni wao kwa urahisi na kadhalika, hivyo kweli nampongeza. Ninachoomba hatua iliyofikiwa isirudi nyuma, Mheshimiwa Waziri funga mkanda, kaza buti tupate *National ID.* lakini mchakato huu usikimbizwekimbizwe, fanyeni kazi kwa ufanisi kwa awamu kama mlivyoanisha kwenye hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe kwa kuendesha Bunge vizuri na kwa busara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Kiongozi Mstaafu na Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Vuai Nahodha, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Hamis Kagasheki (Balozi) kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza wote *IGP* Mwema na Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Kukuza na Kuhamasisha Utalii wa Ndani, Ndugu Suleman Kova, kwa kutuimarishia ulinzi. Mwenyezi Mungu ameniwezesha mchango wangu ni kama ufuatao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, wananchi wa Kata ya Tegeta CCM, wazazi walipendekeza ngazi ya Mabalozi irudi kama ilivyokuwa mwanzo, yaani itambulike Kiserikali ili kuimarisha ulinzi na kuongeza uwezo wa kufahamu wageni na hivyo kupunguza hali ya ujambazi kutoka nje ya eneo husika kutambuliwa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, hongera kwa Vitambulisho vya Uraia, tunavisubiri kwa hamu na ni muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, jana nilikuwa kwenye *Council* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam moja ya mambo yaliyojitokeza ni kuongezeka kwa matukio ya uhalifu katika eneo la vyuo hususan *UDSM* kutokana na kuwatumia walinzi kutoka sekta binafsi ambao wengi wao si waaminifu na hawana ujuzi wa kazi yao vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi kutoka kituo cha jirani hawaonekani kuwa *serious* na kazi ya doria na ulinzi, mara nyingi wamekuwa na doria ya mbali, nadhani kwa vile wanajua kuwa kuna ulinzi huo wa *private*. Hivyo ni hatari hasa katika kipindi hiki ambapo watu mbalimbali wakiwemo wanasiasa kupenyeza mambo yao katika vyuo. Pakitokea fujo na usalama kwa ujumla umepungua. Ni vema vyuo vitumie ulinzi wa Polisi hata kama ni kwa kulipia gharama husika, ili kuwa na usalama katika maeneo ya vyuo kama ilivyo kwenye mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limeingia makubaliano na Makampuni kadhaa ya Madini yenye leseni za utafiti au chimbaji wa madini ambapo Jeshi la Polisi linalipwa fedha na makampuni hayo ili kuyapa ulinzi katika migodi au maeneo wanayofanyia utafiti wa madini. Kwa mfano, Jeshi la Polisi lina *Memorandum of Understanding (MoU)* na Kampuni ya Uchimbaji ya *African Barrick Gold* ambayo kwayo Jeshi la Polisi linatoa ulinzi katika Mgodi wa Dhahabu wa North Mara Wilayani Tarime. Aidha, Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Singida lina makubaliano na Kampuni ya *Shanta Mining Company Limited* ambayo kwayo Jeshi la Polisi linatoa ulinzi kwa kampuni hiyo katika mradi wake wa utafiti wa madini ya dhahabu katika maeneo ya Samberu na Mang'onyi katika Jimbo la Singida Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, makubaliano ya aina hii yameligeuza Jeshi la Polisi na Askari wetu kuwa Jeshi la mamluki au Askari wa kukodiwa wa Makapuni ya Madini ya kigeni katika vita zao na wanavijiji ambao wamenyang'anywa ardhi zao na Makampuni hayo. Ripoti mbalimbali ambazo zimetajwa katika hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani zimeonyesha matokeo ya ndoa hii kati ya Jeshi la Polisi na Makapuni ya Madini ya kigeni, mauaji ya raia wasio na hatia yanayofanywa na Jeshi la Polisi kwa niaba ya Makampuni ya Madini. Kwa upande wa *Shanta Mining*, ndoa ya Kampuni hiyo na Jeshi la Polisi imesababisha Wanavijiji wengi wa Vijiji vya Samberu na Mang'onyi kukamatwa na kuwekwa Mahabusu ya Singida Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka Serikali itoe kauli rasmi Bungeni kama ni halali kwa Jeshi la Polisi kugeuzwa mamluki wa Makampuni ya Madini ya kigeni, Serikali iseme kama Jeshi linalolipwa posho na Makampuni ya kigeni kwa ajili ya kulinda maslahi ya makampuni hayo linaweza kuwatendea haki wananchi ambao wana ugomvi na Makampuni hayo? Serikali itoe kauli Bungeni kama ni sahihi kwa Serikali kuacha kutimiza wajibu wake wa kuwalipa Askari Polisi mishahara na posho stahiki pamoja na vitendea kazi na badala yake kuyaachia Makampuni ya Madini ya kigeni kufanya kazi hiyo? Vitendo vya ukiukwaji wa Haki za Binadamu ambayo vimeelezwa kwa kirefu katika hotuba ya Kambi Ramsi ya Upinzani vinaonyesha wazi haja kubwa

ya kufanya mageuzi katika mfumo mzima wa Kipolisi (*policing reforms*). Maeneo yanayohitaji mageuzi ni haya yafuatayo:-

(i) Mabadiliko katika Sheria ya Uchunguzi wa Vifo *(Inquests Act)*, Sura ya 24 ya Sheria ili kuwezesha mambo yafuatayo:-

(a) Uchunguzi wa Kidaktari *(antopsy)*, uwe wa lazima katika matukio yote ya vifo vinavyotokana na matumizi ya nguvu za dola na waliokufa katika mazingira hayo wasizikwe kabla ya uchunguzi huo.

(b) Uchunguzi wa Kimahakama (*Inquent*) kwa kutumia Mahakama ya Korona uwe ni lazima na ufuatie uchunguzi wa Kidaktari.

(c) Pale ambapo Mahakama ya Korona inathibitisha kwamba kifo cha raia kimetokea katika mazingira ya kijinai basi Askari waliohusika wasimamishwe kazi mara moja ili kupisha hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yao. Aidha, Makamanda wa Wilaya au Mikoa wanaowasimamia Askari hao nao walazimishwe kujiuzulu ili wawajibike kutokana na makosa ya Askari wa chini yao.

(ii) Sheria ya Mwenendo wa Jinai, Sura ya 20 ya Sheria zetu ifanyiwe marekebisho ili kuwezesha mambo yafuatayo:-

(a) Kufanya makosa yote ya jinai yawe na haki ya dhamana mara baada ya siku thelathini kupita tangu mtuhumiwa kukamatwa na Polisi.

(b) Kufuta mashtaka ya jinai dhidi ya mtuhumiwa endapo upelelezi wa Polisi utakuwa haujakamilika ndani ya siku sitini tangu mtuhumiwa aliposomewa mashtaka.

(c) Kulazimisha Jeshi la Polisi na upande wa Mashtaka kuwalipa fidia na gharama za kesi wananchi ambao wanaachiliwa huru baada ya kufutiwa hatia na au mashtaka na Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko mengi ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani imeyapendekeza yatasaidia kwa kiasi kikubwa katika kusafisha Jeshi la Polisi kutokana na uchafu huu wa kuwa Jeshi mamluki linaloua au kutesa au kubambikizia raia kesi za uongo ili kuwakamua fedha za rushwa.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu bila ya kumsahau *IGP* na Jeshi lote la Polisi na Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuishukuru Wizara na Jeshi la Polisi kwa kuipatia Wilaya gari jipya la Polisi. Nitashukuru zaidi kama pikipiki mpya nazo zitapatikana kwani ni moja ya Wilaya zinazokabiliwa na migogoro kati ya wafugaji na wakulima pamoja na wizi wa ng'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi sasa nimeomba Kituo cha Polisi kujengwa katika Tarafa yetu ya mpakani ya Simbay hasa katika Kata ya Gisambalang. Eneo hili lipo mpakani mwa Hanang na Kondoa na usalama wa raia kila wakati umekuwa wa mashaka. Tafadhali naomba Wizara pamoja na Jeshi waone umuhimu wa kujenga kituo mara moja muda mrefu umepita toka nilipoomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani zangu na naunga mkono hoja ya Waziri.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo ya kero zifuatazo:-

Kwanza, Wilaya ya Mvomero, ni mpya, hakuna ofisi ya *OCD* wa Wilaya, kwa sasa Kituo cha Polisi ndio ofisi ya Polisi Wilaya, nataka kujua ni lini ofisi ya Wilaya itajengwa.

Pili, Tarafa ya Mgeta ina kata saba (7) ambazo ni Mgeta, Langali, Bunduki, Kikeo, Wale, Nyanelira na Tchenzema. Kata hizi hazina Vituo vya Polisi kwa kudumisha usalama wa raia, lini ujenzi huu utafanyika?

Tatu, Kata hizi zipo umbali wa Km.34 toka Makao Makuu ya Wilaya, kwa nini Kata hizi zisijengewe hata Kituo kimoja tu, mpango wa Serikali ukoje katika kujenga vituo hivi?

Nne, Kata za Pemba, Kabati na Kanga. Hizi ni Kata za pembezoni lakini hazina Kituo cha Polisi, ni Kata za mpakani kati ya Wilaya ya Handeni na Kilindi, mpango ukoje wa ujenzi huo?

Tano, Mji wa Madizini, mji huu unakua sana na uwepo wa Kiwanda cha Mtibwa, kuna umuhimu sasa wa kujengwa Kituo cha Polisi. Naomba Waziri atembelee eneo hili na ajionee mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara kwa kuandaa mpango mzuri na kuuwasilisha. Nimefurahia hasa ukubwa wa andiko la bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mawaziri hasa kwa uendeshaji wa Wizara hii nyeti na muhimu. Kazi ya Wizara hii ni ngumu lakini pia uendeshaji unahitaji umakini, mmeendesha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za Maaskari. Maaskari wanaendelea kuishi katika makazi ya ajabu. Tujitahidi kujenga na kukarabati *'Police Lines'* ili Maaskari waishi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera, tunashukuru kwa jitihada zote ambazo zimefanywa kuhusiana na ujambazi Mkoa mzima hasa Kimisi lakini bado huko Kagera tunahitaji nguvu za ziada hasa huko Ngara na Biharamulo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya Maaskari. Kwa nini Serikali haitoi malipo ya Maaskari kwa muda muafaka? Jana Waziri alijibu swali kuwa Askari elfu ishirini na mbili hawajalipwa mafao yao. Waziri atuambie kwa nini wanatumia *loyality* ya Maaskari kutokuwalipa maslahi yao, naishauri awamu nyingine Serikali itenge fedha za kutosha kwenye bajeti ya Wizara hii kwa ajili ya suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahabusu, naomba majengo ya mahabusu yaboreshwe, miaka 50 ya Uhuru Watanzania wanaadhibiwa kwa kulala na vinyesi, kunguni, sio wote wanaopelekwa jela wana hatia. Waziri atuambie ni lini watasisitiza usafi katika Mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji ya raia, Waziri atuambie ni lini Polisi wataacha kuwapiga wananchi wasiokuwa na hatia na kuwaua? Mauaji yanaongezeka kila siku, Waziri atuambie ni lini mauaji ya Askari kwa nchi hii yatakoma? Ushahidi upo mwingi tu mfano Selu Tarime, Babati, Manyara, Dar es Salaam na kwingineko haya yalishajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa, Waziri atuambie ni lini rushwa barabarani itaisha? Kwa kweli tupe jibu la kutosheleza kuhusu rushwa hii inayoongoza kwa nchi nzima, Wizara ina mkakati gani juu ya kumaliza tatizo hili linalowakera sana wananchi?

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni mwaka wa kumi sasa naomba magari katika Kituo cha Polisi Peramiho na Madaba. Madaba sasa ni Mji Mdogo lakini Peramiho sasa ni Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya. Ni lini magari yataletwa katika vituo hivyo? Naomba majibu ya kiutekelezaji.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha (Mb), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Mheshimiwa Balozi Khamis Juma Sued Kagasheki (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Pongezi nyingine nazitoa kwa Watendaji Wakuu wa Wizara hii kwa kuandaa bajeti ambayo imewasilishwa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuichangia bajeti hii, binafsi mchango wangu utaegemea katika changamoto zifuatazo kwa njia ya maswali.

Mheshimiwa Naibu Spika, shutuma dhidi ya Polisi. Kwa kiasi kikubwa Jeshi letu la Polisi linaandamwa na shutuma nyingi sana kama vile rushwa, kudanganya, kunyang'anya, kutowajibika na hata upendeleo kwenye ajira. Je, shutuma hizo ni za kweli? Kwa nini Polisi wapokee rushwa? Suala la uadilifu liko wapi? Je, Polisi hawa walikula kiapo cha utii? Je, Polisi hawa wanaijua Sheria? Kwa nini kwa kiasi kikubwa watumishi wa Jeshi la Polisi hawasemi ukweli? Kwa nini Polisi hudanganya? Kwa nini Polisi husingizia kesi ya uongo kwa raia? Kwa nini Jeshi la Polisi huandamwa na kashfa ya ubakaji na hata unyang'anyi? Je, ni kweli kuwa Polisi wetu hawajui wajibu wao kwa jamii? Je, ni kweli kuwa ajira katika Jeshi la Polisi hutolewa kwa ukanda au ukabila?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usalama Wilayani Tarime. Suala hili linatia shaka kwani tangu enzi za utawala wa Awamu ya Kwanza wa Mwalimu J. K. Nyerere, utawala wa Awamu ya Pili wa Mzee Ali Hassan Mwinyi (Ruksa), utawala wa Awamu ya Tatu (Mzee Benjamin William Mkapa) na huu wa Awamu ya Nne (Mzee J. M. Kikwete), bado suala la amani Wilayani Tarime halijatulia hata kidogo. Ina maana Serikali imeshindwa kudhibiti amani Wilayani Tarime? Kama ni ndiyo, kwa nini? Kama ni hapana, kwa nini? Kwa nini mauaji ya mara kwa mara hutokea Wilayani Tarime? Je, Polisi imesaidiaje kutatua mapigano ya koo na koo Wilayani Tarime? Je, Polisi ina taarifa gani juu ya baadhi ya Viongozi na Watumishi wa Serikali wanaovuruga amani Tarime? Je, Polisi inadhibiti vipi Viongozi wa Vyama vya Siasa wanaovuruga amani Tarime? Serikali inatoa kauli gani ya uhakika juu ya mauaji ya mara kwa mara yanayotokea katika Mgodi wa Dhahabu wa *North Mara* maarufu kama Mgodi wa Dhahabu wa Nyamongo? Serikali inasema nini juu ya silaha zilizozagaa Wilayani Tarime?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda Maalumu ya Kipolisi ya Tarime – Rorya. Lengo la kuanzishwa kwa Kanda hii lililenga kurejesha amani Wilayani Tarime – Rorya. Je, Serikali inafikiri lengo hilo limetimia? Kwa nini Polisi wa Kanda Maalum hawajajengewa ofisi? Kwa nini Polisi wa Kanda Maalum hawana makazi? Kwa nini Polisi wa Kanda Maalum wanajihusisha na rushwa Wilayani Tarime? Kwa nini kuna machafuko ya mara kwa mara Wilayani Tarime huku kuna Kanda Maalum ya Kipolisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la rushwa katika Jeshi la Polisi. Kuna tetesi kuwa Jeshi la Polisi ndilo linaloongoza kwa kupokea rushwa hapa nchini. Hii ni kwa sababu haki haiwezi kutendeka Mahakamani pasipokuhusisha upelelezi wa Polisi. Serikali haioni kuwa kitendo cha Polisi kujihusisha na rushwa husababisha haki kutotendeka? Je, mbele ya rushwa Polisi hupeleleza nini? Kwa nini Trafiki wa Barabarani huomba rushwa hadharani? Je, Serikali hailioni hilo? Kama inaliona kwa nini inaendelea kulifumbia macho? Nini kifanyie ili kudhibiti hali hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi duni ya Polisi. Makazi duni ya Polisi hususani Kanda Maalum ya Kipolisi Tarime – Rorya nayo hupelekea Polisi wetu kuwa na tamaa ya kutaka rushwa na hata kusababisha haki kutotendeka. Serikali inatoa kauli gani juu ya hilo? Ni lini makazi ya Polisi wetu yataboreshwa? Ni lini makazi ya Polisi Kanda Maalum ya Kipolisi Tarime – Rorya yatajengwa na yatakamilika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo kwa Wazabuni. Ni ukweli usiopingika kuwa kumekuwa na kilio cha Wazabuni wengi kutolipwa kwa muda malipo yao pindi wanapotoa huduma ya uzabuni katika Jeshi la Polisi. Pia kuna malalamiko kuwa Jeshi la Polisi lina tabia ya kubadilishabadilisha Wazabuni hasa pale linapodaiwa na mbaya zaidi ubadilishaji huo unapotokea, baadhi ya Wazabuni ndio huanza kilio cha kusaga meno kwani malipo yao huwa ni ombi na si wajibu! Serikali inashauri nini juu ya hilo? Je, huo ni utapeli juu ya Jeshi la Polisi? Ni lini Wizara itahakikisha kuwa

inalipa madai ya Wazabuni bila usumbufu? Je, ni lini Kanda Maalum ya Tarime – Rorya itamlipa Bwana Mairo Wanzaku, mmiliki wa *Wansaken Filling Station* madai yake takribani milioni 23 kwa kuwa ni muda mrefu sasa tangu atoe huduma hiyo kwa Askari wetu? Je, kama huo si unyanyasaji ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara/posho na ruzuku. Ifahamike wazi kuwa kuna tatizo kubwa la mishahara, posho na ruzuku kwa watumishi wa Wizara hii. Je, Serikali inalionaje suala hilo? Serikali haijui kuwa kitendo cha kutoa mishahara kidogo katika Jeshi la Polisi huchochea rushwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa wito kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ahakikishe analiondoa Jeshi la Polisi katika Mgodi wa Nyamongo kama nilivyokwishasisitiza. Naomba majibu ya uhakika kuhusu hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ya kusimamia na kuhakikisha usalama wa wananchi pamoja na mali zao. Majukumu haya ni mazito na yanahitaji wafanyakazi waaminifu na waadilifu wenye wito wa kazi yao. Inasikitisha sana kuona kwamba watu ambao tumewakabidhi dhamana ya usalama wetu na mali zetu wanaishi katika makazi duni pamoja na mishahara na mikataba ya kazi isiyowapa tija. Vitendea kazi navyo ni matatizo makubwa. Hii inachangia kuzorotesha utendaji kazi wao na kupelekea kuwepo na malalamiko mengi sana toka kwa wananchi ambao hawaridhishwa na utendaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa bajeti yake inayolenga kuondoa matatizo yanayoathiri utoaji huduma kwa watendaji wake. Ikiwa ni kutoa mafunzo kwa Askari Polisi, Magereza na Maofisa wa Uhamiaji, pamoja na kuimarisha ulinzi shirikishi. Bajeti hii pia imelenga kuimarisha vitendea kazi kama usafiri, majengo ya ofisi na makazi pamoja kuboresha huduma nyingine mbalimbali kama usimamizi wa usalama barabarani kubadilisha leseni, kupunguza msongamano wa Wafungwa Magerezani, kutoa vifungo vya nje, kuharakisha mchakato wa Vitambulisho vya Uraia na pia kuendelea kutoa elimu ya usalama wa raia. Utekelezaji wa mipango iliyoko katika bajeti hii inayozingatia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inasisitiza usalama na amani kwa raia pamoja na mali zao, hali bora ya kazi, upatikanaji wa vitendea kazi kwa Majeshi ya Polisi na Magereza, kuwarahisishia katika kutekeleza kazi zao na kutoa huduma bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo, kuna malalamiko mengi sana kutoka kwa Watendaji wa Majeshi haya. Ni jambo la kawaida kabisa kukuta Askari Polisi au Magereza wakilalamikia maslahi duni na mishahara midogo na mazingira duni na ya dhiki, ni rahisi kushawishika na kurubuniwa katika kushiriki au kufanya uhalifu. Askari mwenye shida na njaa, akikabiliwa na mtu aliyefanya uhalifu akampa fedha kidogo ya kuweza kutatua tatizo lake, je, Askari huyu hatashawishika kushiriki katika kuficha maovu? Hali hiyo pia iko kwa Askari Magereza pamoja na Maofisa wa Uhamiaji. Nashauri ni wakati sasa Serikali ifanye tathmini ya kazi za Maofisa na Askari wa Majeshi haya kuona jinsi watakavyoweza kupatiwa mishahara wanayostahili kufuatana na hali ya maisha ya sasa, mafunzo, vitendea kazi, usafiri wa uhakika pamoja na kuwajengea nyumba bora za kutosha na mazingira mazuri ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linalalamikiwa sana kwa kutokuwa na vitendea kazi vya kutosha na hasa usafiri. Mara kwa mara wananchi wanapokabiliwa na tatizo linalohitaji msaada wa Askari Polisi wakipiga simu au kwenda Kituo cha Polisi kutoa taarifa ya uhalifu aliotendewa, hujibiwa hakuna usafiri wa kufuatilia tukio na kama kituo kina gari ataelezwa kwamba gari haina mafuta hivyo atoe pesa ya mafuta. Baada ya kutoa pesa ya mafuta ataambiwa pia atoe na pesa ya posho kwa ajili ya Askari watakaofuatilia tatizo lake. Kinachofuata hakuna lolote linalofanyika. Mwananchi huyu atasubiri kuona mafanikio ya ama

kupata mali zake au kupatikana kwa mhalifu na haki itendeke lakini hapewi hata taarifa ya kinachoendelea na kila anapofuatilia anapewa matatizo yaleyale ya ukosefu wa usafiri, pesa ya mafuta na posho ya Askari, mwananchi huyu akitoa pesa yake mara mbili tatu na baadaye akionyesha kutoridhishwa na utendaji wa aina hii anaambiwa yeye ni mtata, kweli hiyo haki? Huo usalama wa raia na mali una mashaka na raia wengi wanapata matatizo mengi kama ya kuibiwa, kutishiwa usalama wa maisha yao, kutapeliwa na kadhalika lakini wananyamaza kimya wakichelea wakitoa taarifa watadaiwa usafiri na posho. Serikali ichunguze tabia hii kwani hili ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba raia anaibiwa kisha chombo kinachotakiwa kulinda usalama wake kumtaka atoe pesa na hatimaye hakuna lolote linalofanyika. Je, huu sio wizi mara mbili? Kwa maana raia kapoteza mali zake kakimbilia kwa mwenye jukumu na dhamana ya kulinda usalama na mali zake nako huko bila huruma kaambiwa atoe hela na sio kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanafarijika sana kuona juhudi zinazofanywa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana kwa karibu zaidi katika kukabiliana na vitendo vya uhalifu kwa kuanzisha Ulinzi Shirikishi. Hili ni jambo jema kama kutakuwa na usiri kati ya watoa taarifa za uhalifu na Askari Polisi. Mara nyingi imetokea wananchi wakilalamikia Jeshi la Polisi kutoa siri na majina ya wanaotoa taarifa za wahalifu kama wezi, majambazi, wauza madawa ya kulevya na vitendo vingine vingi. Taarifa hizo zinapovuja unakuta wale wahalifu ama wanawatishia maisha waliotoa taarifa au wanaumizwa bila kujua nani katenda jambo hilo. Dhana hii ya Ulinzi Shirikishi itafanikiwa endapo Askari watakumbuka kiapo cha kazi zao ili raia wema waweze kuwa huru kushirikiana nao katika kukabiliana na vitendo viovu katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kitengo cha Usalama Barabarani ndiko kunakolalamikiwa sana kwamba Askari wa Usalama Barabarani hawako makini kuangalia mwendo wa magari au uendeshaji wa madereva, ubovu wa barabara na kutoa taarifa sehemu husika, uegeshaji kiholela wa magari na hasa sehemu za milima au kona katika barabara mambo ambayo yanasababisha ajali nyingi zinazopoteza maisha ya watu na kuzalisha walemavu wengi. Hii pengine si uzembe hasa wa Askari wa Usalama Barabarani bali hutokana na kutokuwa na vitendea kazi vya kutosha kama magari ya kufanya (*patrol*) na kadhalika. Serikali katika bajeti hii ihakikishe inawapa Askari hawa magari pamoja na vidhibiti mwendo. Napenda kusifu Jeshi la Polisi kwa kuona umuhimu wa kutumia TEHAMA kudhibiti mwendo wa magari, hii inaashiria kwamba tunatoka katika utendaji wa mazoea na kufuata mbinu za kisasa na za kitaalamu zaidi katika kufanya kazi. Natumaini vifaa vitakavyonunuliwa vitafanya kazi, wataalamu wa kuvitumia watapewa mafunzo na motisha *(incentives)* ya kuwawezesha kutumia vifaa hivi kwa umakini ili isijekuwa mradi *(elephant projects)* ambao hauleti tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda sana kutoa kilio cha wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini la kujengewe Vituo vya Polisi. Jimbo la Kibaha Vijijini ni Jimbo ambalo limegawanyika kutoka Jimbo la Kibaha. Kwa maana hiyo kuna huduma nyingi ambazo zinahitajika ambazo ni pamoja na Vituo vya Polisi. Kata ambazo zinaweza kujengwa Vituo vya Polisi, ni Kata ya Ruvu na Magindu. Kata ya Ruvu, ina wananchi wakulima, wafugaji na wafanyabiashara. Kata hii imewezeshwa kukua kwa sababu pana stesheni kubwa ya Reli yetu ya Kati *(Ruvu junction)*. Stesheni hii ndipo mabehewa ya treni za mizigo na abiria zinazokwenda na kutoka Bara kwa maana ya Morogoro hadi Tabora, Mwanza, Kigoma, Mpanda na ile iendayo Kilosa hadi Kilombero na ile ya Tanga hadi Arusha zinabadilisha mizigo. Kwa hali hii na kwa umuhimu wake ni mahali ambapo maeneo ya ardhi bado ni makubwa na yanapatikana kwa urahisi hivyo Jeshi la Polisi linaweza kujenga kituo pamoja na nyumba za Askari bila kubanwa na msongamano wa wananchi. Pia naamini katika bajeti hii, Kituo cha Polisi Mlandizi kitaimarishwa kwa kukipatia vitendea kazi ikiwa ni magari na vifaa vya ofisi kwani Kituo hiki kinatoa huduma kubwa za kulinda usalama wa wananchi wa Jimbo zima, Majimbo ya jirani pamoja na mizigo na wasafiri wanaotumia barabara kubwa ya Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama. Kazi ya Askari Polisi ni kulinda usalama wa wananchi wake bila kuvuruga amani ya wananchi na nchi kwa ujumla lakini siku za karibuni

kumekuwa ni mtindo wa kawaida kwa Askari Polisi kuwapiga wananchi kwa virungu, mabomu ya machozi hata kutumia silaha za moto na kupelekea kuua raia wasio na hatia. Mpaka sasa Serikali imefumbia macho uhalifu huu unaofanywa na Askari wetu. Maandamano ni kitu cha kawaida haswa pale yanapokuwa ni ya amani unakuta wananchi wale hawana hata kizibo (kifuniko) cha soda cha kumpiga Askari halafu Askari anakiuka haki za binadamu na kumpiga raia yule kwa risasi za moto. Je, huu ndio utaratibu mpya wa Askari Polisi kutumia silaha za moto kuua raia wasio na hatia na hata kama wana hatia Askari anatakiwa kumkamata mhalifu na kumfunga pingu na kumpeleka mahabusu ili kosa lile lishughulikiwe kisheria ikiwa ni pamoja na kuwapeleka Mahakamani. Je, katika Jeshi la Polisi ni kiasi gani cha bajeti kilichotengwa kwa ajili ya kununulia pingu ili kila Askari aweze kuwa nayo ili kupunguza mauaji yanayofanywa na Askari kwa kutumia silaha za moto? Ni kiasi gani cha fedha kilichotumika kwa kipindi cha miaka mitatu 2007-2011, kwa Jeshi la Polisi kulipa Askari (FFU) wanaoenda kupiga wananchi (Arusha, Mwanza, Dodoma, Dar es Salaam) ikiwa ni pamoja na mabomu na risasi zilizotumika, magari, *petrol* na *diesel*. Hizi ni fedha za walipa kodi wa Tanzania, tuna wajibu kujua zinatumikaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi ya Askari Polisi Dodoma. Dodoma ndio Makao Makuu ya Nchi lakini nyumba wanazoishi Askari Polisi hapa Dodoma zile za *(Full suit)* zinazoanza na bati juu mpaka chini, ni ndogo ukizingatia mabadiliko ya hali ya hewa duniani ni joto sana. Hivyo ni vigumu sana kwa Askari hawa na familia zao hawawezi kulala ndani na joto kali. Hii inawalazimisha kulala nje matokeo ya kulala nje ni kuanza kuumwa na mbu na kupata malaria. Wakiugua nguvu kazi inapungua. Hawa Askari ni wanadamu kama wananchi wengine, nyumba zaidi ya tatu (3) zinatumia choo kimoja na bafu moja, je, huu ni ubinadamu? Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nafuu kwa Askari Polisi hapa Dodoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, ajali za barabarani haswa za pikipiki zijulikanazo kama bodaboda. Ajali zitokanazo na bodaboda hapa Tanzania nazichukulia kama janga la Taifa. Ukitembelea kwa mfano wodi ya Sewahaji Muhimbili Hospitali na Ghorofa ya Kwanza katika Hospitali ya *KCMC* utashtuka kuona wagonjwa karibia asilimia 80 ni waliogongwa na pikipiki, waliovunjika miguu/mikono na kadhalika. Hii ni hatari kwa Taifa letu. Je, waendesha pikipiki huwa wanapatiwa mafunzo wapi? Je, Serikali imejiandaa vipi kwa kipindi cha miaka 10 ijayo kuwatunza watu watakaopata ulemavu kutokana na ajali hizi? Je, Serikali haioni ni wakati muafaka kuzisitisha kabisa pikipiki hizi kufanya biashara ya kubeba abiria mpaka ihakikishe Dereva wote wanafanya mafunzo na kuelewa Sheria zote za barabarani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili nimekuwa nikiliuliza tangu mwaka 2005 – 2010 kuhusu kijana aitwae Swai aliyeuawa kikatili kwa kuchomwa na *petrol* hadi kufa na raia wa Moshi aitwaye Jafari, napenda kujua limefikia wapi. Serikali ilijibu ndani ya Bunge lako Tukufu bado wanamtafuta Jafari ili afikishwe kwenye vyombo vya sheria. Je, Serikali imefikia wapi katika kumtafuta Jafari?

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wasimamao barabarani na tochi za kuangalia mwendo. Ni jambo la hatari Askari Polisi wanapojificha kichakani ili kukamata gari linaloenda kwa mwendo wa kasi. Ni hatari ikiwa gari hilo limefeli *brake.* Tochi ile haionyeshi namba ya gari hivyo kupelekea hisia za rushwa. Nchi nyingine duniani huwa zinaweka *warning* kwamba kuna *Police Camera Ahead* hivyo Madereva *automatically* wanapunguza *speed* na wanajijengea utamaduni wa kupunguza *speed* badala ya hapa kwetu Askari kuvizia magari na kupiga picha. Ni kiasi gani kwa kipindi cha mwaka mmoja tu 2009 – 2010 kilichopatikana (kukusanywa kwa kosa la kuendesha kasi nchini Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, *TGS* ya Polisi, tunaomba malipo yazingatie pia muda wa Askari alivyolitumikia Jeshi siyo mishahara inapandishwa pale tu atakapopandishwa cheo. Hii inawavunja moyo waliotumikia Jeshi hili kwa uaminifu, anakuja mgeni wanapata kipato sawa.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ufinyu wa bajeti lakini kitendo cha mgawo huu mdogo kwa Wizara hii ndiyo kinachosababisha watumishi wa Idara hii kujiingiza katika upokeaji au uombaji wa rushwa, watumishi kukosa nyumba nzuri za kuishi, watumishi kukosa huduma ya usafiri, watumishi kutokupata huduma muhimu kama maji safi na salama, umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, umbali kutoka Makao Makuu ya Polisi na vituo vidogo vya Polisi kunahitajika magari ya vituo hivyo au pikipiki za ofisi. Kutokana na ukosefu wa Vituo vya Polisi wananchi walio mbali na vituo hukosa huduma na uhalifu kuwepo mkubwa. Basotu ina umbali wa Km.55 toka Makao Makuu ya Wilaya ya Hanang. Hivyo kituo cha Polisi Basotu kinatakiwa kuwa na gari au pikipiki ili kituo hicho kiweze kufanya kazi yake kwa ufanisi hasa panapotokea uhalifu. Kituo cha Basotu kinahudumia Kata zaidi ya tano (5) toka kituo cha Basotu kwenda kwenye Kata nyingine ni zaidi ya Km.10-20. Hivyo ni muhimu wakapata pikipiki au gari ili ifanye misako na kufuatilia huduma kwa jamii bila kuchelewa mpaka uhalifu unapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Basotu kinahangaika kupata nyumba, kwa hivi sasa wameazimwa na Kanisa Katoliki nyumba na wameambiwa wahame ili Kanisa liendelee na matumizi ya jengo lao. Je, Wizara ni lini mtatoa fedha kwa ajili ya kujenga jengo la Kituo cha Polisi Basotu ili Kituo hicho kifanye kazi kwa ufanisi? Inafahamika kuwa mwaka 1998 tulipata mvua za Elnino zilizosababisha kubomolewa kwa Kituo hicho. Kwa nini Serikali imefumba macho kwa maafa hayo yaliyotokea? Tafuteni fedha za haraka ili kujenga Kituo hicho cha Basotu, Wilaya Hanang.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana Jeshi la Polisi kwa kufanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwenye Wilaya ya Korogwe, Polisi kila majengo wanayotumia wameazima. Jengo la Afisa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ni la Mkuu wa Wilaya, jengo la Mgombezi – Mamlaka ya Mkonge, jengo la Polisi Makuyuni ni la Mahakama ya Mwanzo, jengo la Mombo – Mamlaka ya Mkonge. Je, Serikali watawajengea majengo yao kwa ajili ya Polisi tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba zilizoko katika Makao Makuu ya Polisi zipo nyumba 40, wakati Polisi Wilaya wapo 155 watakaa wapi? Mkuu wa Polisi wa Wilaya anakaa kambini na Askari wa kawaida, ni kwa nini Serikali imeuza nyumba hadi za viongozi wakubwa? Huu sio uungwana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo kikubwa cha Polisi kama Korogwe, gari ni moja na kila wakati kuna matatizo kwenye barabara kuu. Msiangalie Miji mikubwa angalieni na Wilayani ambako huwa uhalifu unatokea mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na shida ya Askari kukaa sehemu moja bila kuhama na kupandishwa vyeo wakati kawaida ya Askari akikaa miaka mitatu (3) bila makosa yoyote anastahili kupanda cheo. Pili, Polisi ikitokea bahati mbaya ameua, anaundiwa Tume za kuchunguza mauaji, je, Polisi anapouawa kwa nini isiunde Tume ya kuchunguza kifo chake? Mkuki kwa nguruwe binadamu mchungu. Hivi kweli uwape waandamanaji bunduki kisha Polisi apewe kirungu, waandamanaji wakipigwa virungu hawatafyatua risasi? Tuache uonevu kwao, mnyonge mnyongeni haki yake apewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi analipwa mshahara Shs.240,000/= akikatwa mshahara anabakiwa na shs.170,000/= au 150,000/= na bado anaishi uraiani pesa hii inatosha nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi anapokuwa safarini analipwa Shs.40,000/= hivyo pesa hiyo atakuwa amejilipia nauli, kurudishiwa pesa yake ya safari inafika miaka mine (4), mtoto anazaliwa hadi anatembea pesa hajarudishiwa. Hii ni shida kwelikweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mfuko wa Kuzikana kwenye Jeshi la Polisi, kila Polisi anakatwa Shs.5,000/=, hizi pesa zinaenda wapi mbona Polisi wanafiwa hawapewi pesa hiyo? Toka wameanza kukatwa ni shilingi ngapi zipo na ni kwa nini zinakatwa, ni mradi wa nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wana *SACCOS* yao ambayo inaitwa Yura SACCOS. Hii *SACCOS* inamsaidia nani wakati Polisi wa kawaida wanakatwa bila sababu yoyote na hawapewi hiyo mikopo, hakuna haja ya kukatwa Polisi pesa wakati hawana faida nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na shida ya Askari wanaokwenda kusoma, wakirudi na digrii kupandishwa kwake mshahara pamoja na kusoma kwake ni shida hadi kwa kutumia rushwa kinyume cha hapo faili linaachwa tu Wizarani. Huu si uonevu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi akihamishwa huwa halipwi na kama atalipwa inachukua muda mrefu bila kujali kuwa ni binadamu anastahili kupewa haki zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Askari amefanya kazi Mwanza, WP 4355, huyu aliendа kwenye Uchaguzi Mdogo wa Tarime baada ya kifo cha Chacha Wangwe, kushika tu fulana yenye nembo ya CCM amefukuzwa kazi, je, kweli inatenda haki kwa Askari hata kama hawana Vyama vya Siasa? Wakati wa uchaguzi tunawapenda sana kwa ajili ya kulinda masanduku, ukishapita hawana thamani, wapewe heshima na wapewe haki, kama na wao waseme waandamane tutafika? Athari zake ni kuingia kudai rushwa kwa nguvu na kukamata baiskeli, pikipiki na bajaji kuwasumbua bila sababu yoyote na wengine kukimbilia barabarani na kuanza kukamata magari na kutaka rushwa, hebu waongezwe mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamiaji, hii Idara ina matatizo makubwa sana, baadhi ya watumishi wanafanya kazi kwa majina ya watu, wakati wa uchaguzi wa Tanzania wengi wamewapachika majina ya nchi za nje eti mtu katoka Malawi, Kenya, Uganda, Somalia na Burundi. Je, siku zote hawakujua kuwa watu hao sio raia hadi ikifika wakati wa uchaguzi tu, hawatendi haki kabisa. Pili, kila Msomali akiwa kwenye basi anasumbuliwa kwa nini?

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kuniwezesha kuamka salama siku ya leo na nikiwa na afya njema

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi wa wananchi na mali zao ni jambo la msingi sana ili kuwapatia fursa wananchi wetu kujishughulisha na mambo mbalimbali ya maisha pamoja na kuishi kwa usalama bila ya wasiwasi pamoja na kuwa sisi raia wengine tuna wajibu mkubwa kuwasaidia vijana wetu hawa katika kutekeleza wajibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina masikitiko makubwa sana kwa vijana wetu hawa Askari Polisi wa wilaya ya Micheweni kwa jinsi wanavyopata tabu kutokana na kukosekana kwa makazi kwa Askari hawa. Baadhi ya Askari hawa wanalazimika kutoka kituo chao cha kazi Micheweni na kurudi makwao kila siku, ikizingatiwa wengi wao hawana usafiri binafsi wa kurudia majumbani kwao, wanapata shida sana. Vilevile Mheshimiwa Waziri anafahamu vyema kwamba Micheweni hakuna usafiri wa uhakika wa kurudi Wete na maeneo mengine, hivyo tunawasumbua ndugu zetu hawa na hii si haki. Kituo cha Polisi Wilaya ya Micheweni kilifunguliwa mwaka 1979, hadi sasa ni miaka 32. Miaka 32 ni mingi sana na niseme miaka 32 ni sawa na maisha ya mtu mzima. Kinachoonekana hapa ni kuitelekeza Micheweni na kuwatelekeza Askari Polisi Micheweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwa machungu kabisa, ubaguzi huu au urasimu huu mpaka lini? Serikali ifikie mahali ione haya. Wilaya ya Micheweni ni Wilaya sawa na Wilaya nyingine Tanzania, hivi ni kwa nini? Wilaya karibu zote Askari Polisi wamejengewa makazi lakini Wilaya kongwe kama hii Micheweni Askari Polisi hadi sasa hawajajengewa makazi na hatujasikia angalau kuna mpango wa kujengewa makazi ili wajisikie huru katika kutekeleza majukumu yao na waone si wenye kutelekezwa na Serikali yao. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hoja aniambie ni kwa nini na ni lini Askari Polisi Wilaya ya Micheweni watajengewa makazi yao ili Askari waondokane na kadhia ya kwenda na kurudi kila siku?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru yapo magari ya kazi kwa ajili ya Askari Polisi, lakini jambo la kusikitisha mara nyingi kunapotokea tukio lolote Askari hawa wanakosa ufuatiliaji wa mara moja na wa kina kutokana na uhaba wa mafuta kwa ajili ya magari haya na ikumbukwe kuwa Micheweni ni eneo ambalo lina bandari ndogondogo nyingi ambapo kuna uwezekano mkubwa kwa wengine kujipenyeza na kuweza kufanya lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kuona uwezekano mkubwa wa kuwapatia makazi Askari wetu lakini pamoja na Maofisa wa Uhamiaji wa Wilaya ya Micheweni kwani na hata wao wana matatizo makubwa yanayofanana na hayo ya Askari Polisi jambo ambalo kwa Maofisa wa Uhamiaji hawana hata usafiri wa aina yoyote. Ikiwa

Maofisa wa Uhamiaji wa Wilaya ya Micheweni hawana hata usafiri wa aina yoyote vipi watafanya kazi yao kwa ufanisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ifahamike kwamba kutowaimarishia mazingira ya kazi vijana wetu hawa maana yake ni sawa na kuweka usalama wetu rehani. Mimi niwapongeze sana kwa juhudi zao wanazozifanya pamoja na mazingira magumu wanayofanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa au kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi, naamini itafahamika.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Waziri kwa hotuba yake nzuri. Pamoja na hotuba nzuri ya Waziri, naomba kupata ufafanuzi kuhusu ujenzi wa Makao Makuu na Kituo cha Kati cha Polisi Wilayani Misungwi. Wilaya hii ni ya zamani lakini hadi sasa bado haijapewa au kujengewa Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya na imeendelea kutumia Kituo cha Polisi Misungwi kama Makao Makuu yake. Kituo hiki ni kidogo na huduma zimekuwa si za kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nashauri Wizara ione umuhimu wa kuanzisha Gereza la Wafungwa Wilayani Misungwi ili kupunguza msongamano wa Wafungwa katika Gereza la Butimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naipongeza Wizara kwa kufanya kazi nzuri licha ya mazingira magumu yanayokabili utendaji kazi hususani wa vikosi vyetu vya Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za wananchi za kujenga kwa kujitolea Kituo cha Polisi Mkata, Handeni bado kazi iliyobaki si kubwa sana. Kituo hiki kisaidiwe kikamilike hasa ikizingatiwa kuwa eneo la Mkata sasa ni kituo kikubwa na Mji Mdogo unaokua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za kuomba kupata mradi wa ujenzi wa nyumba za Polisi pale Chanika, Handeni bado hatujapata mwelekeo wa mradi huu kutekelezeka. Nyumba za kuishi Polisi ni duni. Eneo hili lipatiwe maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wa wakimbizi wa Chogo, niliomba Serikali ikamilishe taratibu za watu wale Wazigua kutoka Somalia, kupatiwa uraia. Hadi hivi sasa zoezi hili halijafanyika kwa tija na ukamilifu, bila ya kujua sababu. Inaweza kuashiria labda ni tatizo la urasimu au ucheleweshaji wa kutoa maamuzi. Naiomba Serikali kulikamilisha zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, napenda kutoa mchango wangu katika bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya Askari wanapopata uhamisho. Kumekuwa na malalamiko, masikitiko na manung'uniko mengi kutoka kwa Askari wetu kwamba kumekuwa na ucheleweshwaji mkubwa kwa Askari hao kulipwa. Wakati wanapopata uhamisho, kitu ambacho kwa kweli kinawapa ugumu mkubwa wa maisha wakati wanapofika katika maeneo mapya ya kazi zao. Kwa kweli hili jambo ni zito na naiomba Wizara husika iongeze juhudi katika kulishughulikia kwa nguvu na ari zaidi ili vijana wetu wasivunjike moyo na kujiona kwamba si watu muhimu katika Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahamiaji haramu. Kumekuwa na ongezeko kubwa la wahamiaji haramu, hili linajulikana linatokana na sababu nyingi zikiwemo migogoro na vita katika nchi jirani. Hili ni jambo ambalo linaleta tatizo na hasa pale mara nyingi wahamiaji hao wanapoingia na silaha jambo ambalo ni la hatari kwa Taifa letu. Pamoja na hali na wimbi hilo la

wahamiaji haramu wanaoingia hapa nchini, hivi karibuni limejitokeza tatizo ambapo wahamiaji haramu wanaokamatwa katika nchi ya Msumbiji wanaletwa katika nchi yetu na kupokelewa na hali inajulikana kwamba si Watanzania wala hawakutokea Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa zenye uthibitisho kwamba kuna mamia ya wahamiaji haramu katika Gereza la Mtwara ambao ni raia wa Ethiopia na Somalia. Je, kwa nini Serikali inakubali kubeba mzigo ambao hakuna Sheria zozote za Kitaifa wa Kimataifa zinazotulazimisha kupokea wahamiaji hao? Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni kwa nini tunabeba mzigo wa gharama kubwa kuwahudumia watu hawa kuanzia pale wanapoletwa mpaka wanapofikishwa kwenye vyombo vya sheria na hatimaye kufungwa Gerezani? Ahsante.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na uwasilishaji makini. Pia nichukue fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa uandaaji mzuri wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya usafiri, pamoja na kuipongeza Wizara kwa juhudi kubwa ya kuvipatia Vituo vya Polisi vitendea kazi, naomba kutaja changamoto tunazoendelea kupambana nazo katika Jimbo la Bagamoyo na Wilaya nzima ya Bagamoyo. Vyombo vya usafiri ni moja ya changamoto kubwa. Kituo cha Polisi Bagamoyo ambacho ndio Kituo Kikuu cha Wilaya Bagamoyo kina gari moja tu na kuukuu. Kwa kuzingatia ukubwa wa Wilaya na pia wingi wa shughuli za *OCD* na Askari wake, ufanisi katika Wilaya umeathirika sana. Ukiacha Kituo Kikuu cha Polisi cha Wilaya, karibu vituo vyote vidogo havina vyombo vya usafiri. Naomba Wizara iiangalie Bagamoyo kwa jicho la huruma, tupatiwe lau gari moja kwa ajili ya Makao Makuu Bagamoyo na lau usafiri wa pikipiki kwa vituo vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uadilifu wa Utumishi wa Jeshi la Polisi. Katika mwaka 2009, Bagamoyo ilitikiswa sana na vitendo vya ujambazi vilivyosababisha wananchi kupoteza maisha na mali zao. Ili kupunguza matukio haya nchini na kuongeza uadilifu wa kazi ya Polisi, naomba Wizara ihakikishe kuwa Polisi hawachanganyiki na wananchi, kwa kuwa na makazi yao wenyewe. Polisi wasikae katika kituo kimoja kwa muda mrefu sana kiasi cha kuzoeleka na kuwa na mahusiano ya karibu na wananchi na wakati mwingine mahusiano na watu wasio na maadili mema. Polisi wahamishwe vituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuvipongeza vyombo vya dola vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambavyo ni Jeshi la Polisi, Magereza na Uhamiaji pamoja na Vitambulisho vya Taifa na Zimamoto kwa kazi nzuri ya kuhakikisha ulinzi wa raia wa nchi hii na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nichukue pia fursa hii kuiomba Serikali ihakikishe kwamba mafao mbalimbali ya Askari waliopo chini ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili madeni mbalimbali na stahili za watumishi walio chini yake waweze kupata kwa wakati muafaka kwa mfano malipo ya madai mbalimbali. Vilevile uwepo ufuatiliaji na chombo maalum ndani ya Wizara kusimamia na kuratibu upatikanaji wa haraka na mirathi kwa familia za Askari pindi wanapofariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri linayofanya ya kukabiliana na matukio ya uhalifu hapa nchini hasa ujambazi wa kutumia silaha. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola limeweza kwa kiwango kikubwa kudhibiti uhalifu huu ambao kwa kiasi kikubwa ulitishia usalama, amani na utulivu wa Taifa letu kwa vile maisha ya raia wasio na hatia na mali zilipotea katika matukio ya kinyama ya ujambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze juhudi za Jeshi la Polisi katika juhudi zake za kukamata silaha kwa maana ya bunduki, mabomu na risasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipongeze Jeshi la Polisi kwa kuja na Sera ya Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi. Mkakati huu umewezesha wananchi kuwa karibu na Jeshi la Polisi na hivyo kufanikiwa kupata kwa urahisi taarifa mbalimbali muhimu kuhusu wahalifu. Hali hii ilisababisha katika nyakati tofautitofauti wahalifu kukamatwa kabla ya kutekeleza uhalifu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi pia ziende kwa Jeshi la Polisi kwa jinsi linavyokabiliana na vitendo vya uhalifu wa biashara ya madawa ya kulevya. Sote ni mashahidi jinsi wahalifu wanaojihusisha na biashara hii na madawa yenyewe wanavyokamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Aidha, pamoja na pongezi tajwa hapo juu bado zipo changamoto muhimu ili kuweza kuhakikisha kunakuwepo na utaratibu mzuri wa kuharakisha upelelezi ili kuzisukuma kesi zinazowakabili watuhumiwa mbalimbali ambao ni mahabusu wanaosababisha msongamano mkubwa Magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipongeze Jeshi la Magereza kwa kazi ngumu ya kulinda wahalifu licha ya kuwepo na changamoto ya msongamano mkubwa wa mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika changamoto tulilonalo la ajali za barabarani, hapa panahitajika jitihada za kukabiliana na jinamizi hili linaloangamiza maisha ya Watanzania wasio na hatia. Katika hili, mafunzo kwa Madereva liwekewe umuhimu wa pekee ili kunusuru pia uchumi wa Taifa letu ambao unaathiriwa na matukio ya uhalifu wa ajali barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya tuhuma ya rushwa ndani ya chombo hiki inapaswa kuchukuliwa hatua za dharura ili kulifanya Jeshi letu liendelee kuaminiwa na wananchi wa nchi hii. Jeshi la Polisi ambalo ni chombo chenye dhamana ya kulinda raia na nchi hii na mali zao, ni vema kikawa chombo makini chenye kuwa na haiba machoni pa raia wa nchi hii. Hatua kama hii ya kuziondoa tuhuma na vitendo vya rushwa kutaifanya Sera ya Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi iweze kupokelewa kwa ukamilifu na jamii husika ambayo ndiyo hasa inaishi na wahalifu katika makazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vitambulisho vya Taifa ni chombo madhubuti cha kuwatambua raia wa nchi hii. Vitambulisho hivi vitasaidia katika kurahisisha kuwepo na kumbukumbu muhimu za raia. Zoezi hili lifanyiwe kazi kwa haraka na vitambulisho hivyo vigawiwe kwa raia halali wa nchi hii. Vilevile vitambulisho hivi vitasaidia kuwabaini wahamiaji haramu na wale wanaoingia nchini kinyume cha sheria pindi zoezi hili litakapokamilika utakuwa ni mwanzo wa kuwatambua Watanzania halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Jeshi la Zima Moto, ni vema Jeshi hili lijengewe uwezo kwa kupewa vitendea kazi vya kisasa vya zima moto na kuanzisha ofisi zake katika Wilaya zote na Miji mikubwa nchini mwetu ili kukabiliana kwa wakati na matukio ya majanga ya moto ambayo huleta hasara kwa maisha ya wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi ni chombo muhimu kwa ulinzi wa Taifa pamoja na mali zao. Amani haiwezi kulindwa kama Jeshi la Polisi siyo imara. Majukumu ya kupambana na uhalifu wa kila aina ni kazi kubwa sana. Majukumu hayo ya kupambana na wahalifu, wauaji, wenye kuuza madawa ya kulevya, wananchi wanapaswa kuheshimu chombo hiki kwamba ni muhimu kukisaidia katika majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hapo juu, napenda kuzungumzia ulinzi wa maeneo ya mipaka nchini kwetu. Wilaya ya Longido ni miongoni mwa Wilaya zilizoko mipakani. Kutokana na mwingiliano wa wananchi wa pande zote, hata wahalifu wa pande zote huingia na kutoka haraka baada ya kufanya uhalifu wao. Ndio maana majangili wa Kisomali walivyoingia

Tanzania sehemu ya Longido na Ngorongoro hufanya uhalifu wa kila aina. Nashukuru Jeshi letu la Polisi kwa kazi kubwa ambayo ilifanya kwa kupambana nao mpaka wakawaondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo umeonekana kwamba ni muhimu kuwa na Kituo cha Polisi huko mpakani. Wananchi wamejitoa kujenga kituo cha Polisi Gilay Lumbwa na Serikali kusaidia kutoa fedha kiasi cha zaidi ya Sh.20 milioni. Jengo hilo limekamilika lakini halitumiki mpaka sasa. *RPC* Mkoa wa Arusha anafahamu kituo hiki kwani ni wao ndio walikuja kumalizia ujenzi wa kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kwa kuwa eneo hilo ni mbali na Kituo cha Polisi Longido na Namanga ni muhimu kufungua kituo hicho ili wananchi wa Tarafa ya Ketumbeine na maeneo ya Lake Natron waweze kupata ulinzi. Mahitaji yanayotakiwa ili kituo kifunguliwe ni nyumba ya Polisi na kuwepeleka Askari kwenye kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Longido ni miongoni mwa Wilaya mpya. Kituo cha Polisi ni cha zamani sana, kilijengwa wakati wa ukoloni. Ombi langu la muda mrefu ni kujengewa Kituo cha Polisi cha Wilaya kwa ajili ya umuhimu wa eneo la mpakani. Halmashauri ya Wilaya wametenga eneo la kutosha kwa ajili ya kujenga kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu wananchi washiriki kutoa ushirikiano kwa Polisi ili ulinzi wao uweze kuimarika kwa kusaidia kutoa taarifa ya uhalifu endapo Polisi hawakuona uhalifu au wahalifu waliko. Naomba Polisi wa Longido wawe na ushirikiano na wananchi kwani bila ushirikiano huo Polisi hawawezi kulinda mpaka huo kwani ni mrefu kwao kutoa ulinzi, kila wakati ushiriki wao na wananchi siyo mkubwa, kuna kutoelewana. Jambo la ushiriki ni muhimu sana. Magendo ya wahalifu kutoka na kuingia zinapitia mpaka huo wa Longido ambao ni mrefu sana. Kutoka Rombo mpaka Lake Natron ni eneo kubwa sana kwa Polisi wenyewe kufanya kazi bila msaada wa wananchi. Naomba ushirikiano huo kati ya Polisi na wananchi wa Longido, ahsante.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na vurugu katika chaguzi zetu zilizopita huko Zanzibar na vurugu hizo kwa asilimia kubwa zilikuwa zinachangiwa na Polisi. Polisi walikuwa wakitumiwa na Chama fulani na kupiga watu bila sababu na kuwabambikia kesi ambazo hazina msingi lakini kwa mwaka 2010, napenda kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kuonyesha kujali kazi yao na kusimamia uchaguzi kwa haki bila kujali Chama au Mgombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikumbushe kuwa kule kwetu Zanzibar baada ya uchaguzi kabla ya matokeo watu wengi walijazana Hoteli ya Bwawani ambapo yanatolewa matokeo ya Rais, umati wa watu walijaa Bwawani Hoteli, walishinda kutwa lakini kwa busara waliyotumia Polisi, wale watu walitawanyika na hakuna hata mtu mmoja aliyepigwa. Kwa hili napenda kwa dhati kabisa kumpongeza *OCD* wa Wilaya ya Mjini kwa kuweza kumudu hali hiyo bila madhara yoyote kutokea. Kwa kuwa maelezo yangu ni kwa maandishi, namwomba Waziri katika majumuisho, hizi pongezi zangu azieleze ili wahusika wote wazisikie. Naishauri Wizara kupitia Jeshi la Polisi kuendeleza mambo kama haya katika Wilaya zote za Tanzania 39 nchi nzima katika uchaguzi ujao 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na uhalifu wa kutosha sasa hivi Zanzibar, tulizoea hapo zamani kurudisha mlango tu na sio kuufunga lakini sasa hivi tunatia mageti lakini tunavunjiwa na silaha mkononi. Kwa hiyo, naiomba Wizara kujipanga upya kukabiliana na jambo hili kwani hali ya mauaji na wizi umekuwa wa kutisha na kuleta wasiwasi katika jamii yetu. Pamoja na kwamba tumeanzisha Polisi Jamii na kuondosha neno *Polisi Force,* naishauri Serikali kuweka mkakati juu ya wahalifu kwani wamekuwa wakihatarisha maisha ya raia na wageni huko Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Uhamiaji, naishauri Serikali kukabiliana na wimbi la wageni wanaoingia nchini bila kufuata taratibu na sheria za nchi. Kumekuwa na ajenda hapa juu ya namna ya wageni haramu, inaonesha rushwa inatumika. Kwa hiyo, Serikali isifanye mchezo juu ya suala la uhamiaji haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na usumbufu mkubwa wa kupata *passport* kwa vijana wetu na wamekuwa wanakata tamaa ya kupata huduma hiyo japokuwa ni haki yao.

Naishauri Serikali iwe wazi juu ya watu wenye sifa za kupata *passport* pale wanapokamilisha masharti kwani huduma hii wanaipata zaidi waliopungukiwa na sifa lakini wana uwezo wa kifedha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hii naomba mchango wangu ulenge katika Mkoa wa Dar es Salaam na pia Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite katika Jeshi la Ulinzi – Polisi. Katika Vituo vya Polisi vidogovidogo havina silaha na havina hata mawasiliano ya *redio call* ya mawasiliano wakati matukio yanatokea, naomba Serikali tulione hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza Jeshi la Polisi chini ya Kamanda Kova, kwa kazi kubwa wanayofanya ya kupambana na ujambazi Dar es Salaam. Mheshimiwa Kova endelea hivyo kumbe Polisi wanaweza. Pia napenda nitoe pongezi kwa Kikosi cha Usalama Barabarani. Wanafanya kazi kubwa sana ya kuongoza magari na kupunguza msongamano, hongereni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Maaskari wetu, naomba sasa Serikali iangalie jinsi ya kuwawezesha kwa kuwapa "posho", wanafanya kazi masaa mengi kama Madaktari na mazingira yao ni hatarishi. Pia pale wanapookoa kitu au tukio wapewe motisha kubwa na kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja 100%. Ahsante sana.

**MHE. DKT. SEIF SELEMAN RASHID:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kushukuru kupata nafasi hii na niipongeze Serikali yangu kwa kujitahidi kuiendesha Wizara hii kwa mafanikio ya kupunguza wastani wa uhalifu kwa asilimia nne (4%).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi, nichangie katika maeneo yafuatayo ili hali ya usalama iweze kuendelea. Kwanza, hali ya kuwa na watuhumiwa 19,000 na wafungwa 18,000 ni hali inayodhihirisha kwamba Watanzania wengi wananyimwa haki yao ya Kikatiba ya kutendewa haki kwa wakati maana haki iliyocheleweshwa ni kunyimwa haki. Naitaka Serikali kuweka mikakati ya kupunguza hali hii kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Vitambulisho vya Uraia. Napata taabu sana kukubali kwamba kwa teknolojia ya leo tunahitaji miaka mitatu hadi mitano kukamilisha zoezi la kutoa Vitambulisho. Huu ni moja ya mwelekeo wa makusudi kusingizia teknolojia na ukubwa wa nchi kuchelewesha zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa kuwa ni muhimu kujenga mfumo wenye uwezo mkubwa wa kiusalama na udhibiti wa uwezekano wa matumizi mabaya ya ama mfumo au vitambulisho husika. Naishauri Serikali kwanza Idara hii ya Vitambulisho kutoa maelezo ya kazi zao kwa Wabunge ili tuelewe zaidi na kuwasilisha mapendekezo yetu. Pamoja na maelezo hayo, sijaona ni kwa nini kitambulisho kitolewe baada ya umri wa miaka 18 na kwa nini mfumo usiunganishwe na mfumo wa RITA ili wale wanaozaliwa nchini waeleweke moja kwa moja na mfumo na wakati ukifika mtu huyo anapatiwa kitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Jeshi la Polisi lianzishe mfumo wa kupima utendaji kazi wa Askari wake Vijijini na kuwaondoa mara moja katika ajira wafanyakazi wazembe ambao wanadhalilisha Serikali mbele ya wananchi. Kwa mfano, Jeshi la Polisi wamekuwa wakihusishwa na mambo mengi kule Rufiji, wanatuhumiwa kuwasaidia wafugaji kushusha ng'o mbe wao usiku kinyume na sheria huku wakijua kuwa eneo hilo haliruhusiwi kushushwa ng'ombe. Wamekuwa wakiwabeba wenye nacho na kuwanyima haki wasiokuwa nacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji wa wananchi kwenye mipaka ya hifadhi na ndani ya hifadhi ya wanyamapori huko Rufiji ni mazito na tuhuma za uvunjaji wa sheria kwa Askari

kujichukulia hatua wenyewe unazidi kukua. Tunaitaka Serikali kuunda Tume itakayoaminiwa na wananchi ili iweze kuchunguza hali hii kwa nia safi sana ya kufahamu Askari Wanyamapori waliojichukulia madaraka na kupiga risasi raia walioingia kwenye hifadhi kwa nia ama ya kuvua samaki katika mabwawa au hata wale ambao wameingia hifadhi kwa madhumuni ya kuua wanyamapori na wengine walioadhibiwa au kuteswa wakiwa katika maeneo hayo. Nazungumzia Wilaya ya Rufiji na maeneo ya hifadhi katika Kata ya Mwaseni, Ngorongo, Kipugira na Ngarambe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Askari katika Vituo vya Tarafa vya Mkongo na Vijiji ambavyo havina Watendaji hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wetu wanafanya kazi nzuri lakini katika mazingira magumu kwa maana ya mishahara midogo na maslahi duni. Kwa Dar es Salaam nimeona juhudi za kuboresha makazi zimeanza. Hivyo, naomba makazi ya Askari pale Mbinga yaboreshwe ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba angalau moja ya ghorofa itakayochukua Askari wengi, inawezekana, kwani ujenzi Mbinga ni rahisi kwa kutumia matofali ya kuchoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Uhamiaji, Mbinga inatia aibu, inahitaji ukarabati na kuimaliza vizuri pia kuwapatia samani na kompyuta pamoja na gari moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vitambulisho vya Taifa, mradi huu umechukua muda mrefu na gharama kubwa. Nafahamu kwamba ni pamoja na kujenga ofisi kila Wilaya lakini kwa maendeleo ya teknolojia, sasa ni kweli gharama hizi au *"justificable"* naomba Wizara ijiridhishe kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ada za wageni wanaoingia nchini. Nimepata malalamiko toka kwa Wamisionari kadhaa kwamba ada za kuingia nchini imepanda maradufu. Naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili na kama ni kweli basi ada hizi zipunguzwe maana pamoja na kazi zao za kiroho wanazotoa lakini Wamisionari hutusaidia katika masuala ya kiuchumi na kijamii pia kuna Madaktari, Walimu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Kitai Mbinga pamoja na lile la Mkwaya yanafanya kazi nzuri ya kilimo. Naomba sasa wapewe vifaa vya kisasa zaidi vya kilimo ili kuongeza uzalishaji lakini pia mafunzo kwa wananchi katika Vijiji vinavyozunguka maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Shamsi Nahodha, Naibu Waziri Mheshimiwa Balozi Khamis S. Kagasheki, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Mambo ya Ndani kwa utendaji wao mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu uharamia unaofanyika katika Ziwa Tanganyika. Wananchi wa Mkoa wa Kigoma ambao ni wavuvi wamekuwa wakitekwa wanapokuwa Ziwani na vyombo vyao kuchukuliwa zikiwemo boti na kadhalika. Naomba Serikali iweze kutusaidia ili wavamizi hao wanaotokea nchi za jirani *DRC* na Burundi waweze kudhibitiwa na Jeshi la Polisi. Naomba Serikali iongeze silaha zinazoweza kukabiliana na wahalifu hao na zana hizi ziwe za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma mara nyingi sana unakumbwa na matatizo ya ujambazi hasa katika njia ya kutoka Nyakanazi, Kibondo na Kibondo Kasulu na maeneo hayo yana pori kubwa sana. Wananchi wamekuwa wakipoteza maisha kwa kuuawa na majambazi, naomba Serikali iweze kutusaidia Kanda ya Kipolisi katika maeneo hayo ambayo ni ya hatari zaidi ili kunusuru maisha ya wananchi wanaosafiri kupitia njia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iwajengee nyumba bora Polisi ili waweze kuishi sehemu nzuri. Katika Kituo cha Polisi Kakonko, nyumba zimechakaa zaidi na hazitoshi. Vituo vyote vya Polisi Mkoa wa Kigoma nyumba za Polisi zimechakaa, naomba Serikali iweze kutenga fedha ili Mapolisi wetu wajengewe nyumba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wanafanya kazi kubwa ya kulinda raia na mali zao, lakini pia wanakumbana na mambo mengi sana na wakati mwingine kuhatarisha maisha yao, naomba Serikali iweze kuwaongezea posho ili waweze kuendana na hali halisi iliyopo kwa sasa. Pia Polisi wapewe vyombo ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri upande wa magari yanayosafirisha abiria, gari linapoondoka liondoke na Askari wa Usalama Barabarani, likifika kituo kingine Askari wa Usalama ashuke na Askari mwingine apande kuendelea na safari. Angalau kila mara Askari awemo kwenye basi, hii inaweza kusaidia Madereva kuwa na nidhamu wanapoendesha magari yaliyobeba abiria ili kuweza kunusuru maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima, naomba kutoa pongezi kwa Waziri pamoja na Wizara yake kwa kazi nzuri ya utayarishaji wa bajeti hii ambayo inaleta sura nzima ya utendaji wa kazi pamoja na utekelezaji wake, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo ya Vituo vya Polisi – Zanzibar. Katika ukurasa 18 na 19 (Ibara 33 na 34) imeelezea ujenzi na majengo ya makazi na vituo vya kazi. Kwa upande wa Zanzibar (Unguja) majengo yote ya Polisi yapo katika hali mbaya, kwani mengi yao ni ya kizamani tokea wakati wa ukoloni yamekaa kama Ngome Kongwe. Majengo yote yanahitaji ukarabati wa kuzipa uhai nyumba hizo au hata kuzipaka rangi ili nyumba za umma zithaminiwe. Hasa ukiangalia Vituo vya Fuoni, Bububu, *Ngambo Police Station* (Kibiriti Ngoma) na hata ukiangalia Makao Makuu ya Polisi kilichopo Kilimani – Zanzibar, jengo hilo kubwa, zuri lakini tayari limechakaa. Hata ukiangalia majengo ya Ziwani hapo ndio vurugu tupu, majengo machakavu, uzio wa waya umeng'olewa na raia wamefanya ndio njia ya mkato kwa safari yao ya kwenda mitaa mingine iliyopo karibu na kituo hicho. Ili heshima ya kituo hicho iendelee walau kuwekwe uzio kuhifadhi heshima ya Jeshi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uajiri wa Polisi – Zanzibar. Nakubaliana na masharti yote yaliyowekwa na Serikali kwa ajili ya uajiri Zanzibar, lakini vijana hao wanapopata nafasi ya kuelekea mafunzoni na kuanza mafunzo kunatokea pingamizi mbalimbali na wakati wa kufikia hatua ya mwisho ya mafunzo vijana hao huambiwa wameshindwa na kuondoshwa katika nafasi hizo. Kijana kama hawezi, tokea mwanzoni utamuona, siyo kishafanya kazi kwa vitendo tena kazi ngumu ndiyo mwisho unamtoa. Je, nafasi yake anapewa nani au ndiyo itakuwa imepotea? Je, idadi ya nafasi hizo Kitaifa si itapungua au itajazwa kinyemela.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastaafu wa Jeshi la Polisi, utakuta baadhi ya wastaafu wa Jeshi la Polisi wanahangaika katika maofisi ya viongozi wa juu kuomba msaada kwa sababu haki zao baada ya kustaafu bado hawajazipata, huo ni usumbufu. Wengi wao wakati wa kustaafu mafao yao hukwama, inabidi afuatilie, anaanza kufuatilia Zanzibar hapati jibu wala mafanikio. Ndio anakwenda Tanzania Bara, Makao Makuu huko yeye ni mgeni na alikuwa kwa cheo mdogo na unapostaafu tayari ofisini unakuwa huna hadhi na hakuna wa kukujali, ingawa unafuatilia haki yako utajibiwa lugha mbaya na hata mtu anadiriki kukuambia "usimfundishe kazi", hataki kukusaidia wakati unachodai ni haki yako. Naomba Wizara kuwaangalia wastaafu na kuwalipa ili kuwaondoshea usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwiano wa upandishwaji wa vyeo. Afisa kupanda vyeo kunategemea elimu au uwezo wa kazi wa Afisa husika lakini ukiangalia kwa Zanzibar wengi wa Maofisa wanastaafu wakiwa bado wapo katika nyadhifa za chini na hasa katika uwiano wa jinsia,

upandaji wa vyeo unakuwa mgumu. Naomba Wizara kusomesha Maofisa kutoka Zanzibar ili nao wawe miongoni wa Maafisa wa Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatiliaji kazi baada ya maamuzi ya Mahakama. Ufuatiliaji huo bado huwa unasuasua, hii inatokana na kwamba Jeshi la Polisi linaangalia sura ya mtu au uwezo wa mtu. Zanzibar kuna kesi nyingi tayari Mahakama zimeshatoa hukumu na kutakiwa Jeshi la Polisi litekeleze lakini hakuna hatua inayochukuliwa. Naliomba Jeshi la Polisi kuwasaidia raia ambao tegemeo lao ni Jeshi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LAMECK O. AIRO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Wilaya ya Rorya kuna eneo lilitengwa kwa ajili ya kujengea Ofisi za Uhamiaji, *TRA* pamoja na Kituo cha Polisi, sehemu hiyo inaitwa Boda ya Kirongwe, Tarafa ya Nyancha. Wananchi walitakiwa kuhama katika maeneo hayo na tayari wananchi wameacha maeneo hayo wazi. Je, Serikali itawafidia lini hao wananchi na je, Serikali itajenga hayo majengo ya Uhamiaji, *TRA* na Polisi? Wenzetu nchi jirani (Kenya) tayari wameshajenga za kwao na kujenga barabara hadi mpakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza sana Serikali kwa kutupatia Polisi Kanda Maalum, imepunguza sana wizi wa mifugo kwa kutumia nguvu (silaha), tunapongeza sana Serikali. Sasa tunaomba Serikali kutujengea vituo vya Polisi vya kisasa, kwani vituo vilivyopo sasa ni vibovu, kuna hatari watu wabaya ambao ni majambazi kuvamia vituo vyetu na kuwanyang'anya Maaskari wetu silaha. Tunaomba sana Serikali yetu Tukufu kutujengea vituo vya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu inaonyesha toka tarehe 1/1/2007 hadi 17/5/2009, mifugo (ng'ombe) zaidi ya 3000 ziliibiwa katika Wilaya ya Rorya. Hawa wananchi ni Watanzania wamebaki maskini, tunaomba Serikali iwafidie kwani hawana ng'ombe wa kulimia au Serikali iwape hawa wafugaji ng'ombe au matrekta ya kulimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia ya maandishi nachangia bajeti ya Wizara hii ambayo ni muhimu kwa usalama na ulinzi wa Taifa letu. Natanguliza kuipongeza Wizara hii kwa kazi wanayofanya na rasilimali zinazotengwa kwa ajili ya majukumu waliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kushauri ni nidhamu ya watendaji wa sekta hii hasa Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi ni kioo cha jamii na Watanzania wote. Ipo haja ya kuimarisha nidhamu ya Watendaji wetu hasa katika eneo la rushwa. Tuzuie tabia hii ya kudai/kuomba na kupokea rushwa hasa utaratibu wa Askari kujipanga barabarani wakifanya vitendo hivyo viovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni huu mfumuko wa wimbi la wahamiaji haramu toka nchi za Somalia na Ethiopia. Kila mtu anafahamu kuwa eneo la nchi hizi linakaliwa na maharamia au na vikundi vya kigaidi. Masikitiko yangu ni jinsi vyombo vya usalama vinavyoshindwa kudhibiti watu hawa kabla ya kuingia nchini. Vitendo vya watu hawa kumudu kuingia nchini kunaonyesha upungufu na utabiri wa janga kubwa iwapo maharamia /magaidi watalenga kutudhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, ni uwepo wa wahamiaji haramu toka nchi za Burundi na Rwanda wanaoishi na kuendesha shughuli zao katika misitu na hifadhi za Taifa wakifuga na kuendesha shughuli haramu. Watu hawa wanaharibu mazingira, wanatishia na kuua wanyama na baya zaidi hatuna taarifa ya uwepo wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa Mikoa ya Ziwa na Magharibi ya nchi huwezi kusafiri usiku na hofu inatokana na uhalifu unaofanywa pamoja na watu wengine hawa

jamaa wanaoendesha shughuli zao kwenye hifadhi. Naomba na kushauri Serikali kwa kutumia vyombo vyake vya ulinzi na usalama waendeshe oparesheni ya kufagia uhalifu huu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wote huu yanatuvua nguo. Tujiulize hawa wahalifu wanaendesha shughuli zao Watendaji wetu wakiwa wapi? Nakiri kuwa hatuna rasilimali za kutosha lakini ni wazi kuwa Watendaji wanao mgawo wao wa lawama. Jeshi letu na vyombo vyote vya usalama vinapaswa kuwa makini na kufanya kazi kwa kuziba mapengo/madhaifu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nielezee matatizo ya usalama katika Mkoa wa Kagera. Raia wa Rwanda na Uganda wameingia kinyume cha sheria Mkoani Kagera. Wimbi kubwa la wahamiaji hawa wakiwa na mifugo yao si watu wastaarabu, wananyanyasa wananchi kwa kulisha kwenye mashamba yao, wanawapiga na wana lugha chafu. Kutokana na nguvu yao ya kuongea, wanadiriki kudai hadharani kuwa nchi hii wameinunua. Tatizo hapa ni kuwa watu hawa wanaingia bila kujulikana, lakini watu hawa wanatoka katika maeneo ambayo yametawaliwa na migogoro ya vita vya wao kwa wao. Katika makundi haya, matendo yao yanadhihirisha uwemo wa wahalifu wa kivita – Interahamwe. Nimehoji hili kwenye mkutano wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na Afisa Uhamiaji alithibitisha hili. Ni hatari kukaa na watu usiowajua na ambao ni wahalifu wa kivita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali Mkoani Kagera si salama, wageni wanawaswaga wananchi kama kuku katika maeneo yote yenye wafugaji hawa. Wameingilia hifadhi na kuwasumbua wanyama tabia iliyopelekea Ndovu kuvamia mashamba ya wananchi kutokana na maeneo yao kuingiliwa. Yote haya yamekuwa yakifanyika ilihali vyombo vya usalama vikiwepo. Wananchi usalama wao uko hatarini, Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Ngara wahamiaji hawa wamefanya uhalifu ikiwemo kuua watu. Hali ni hiyo Muleba katika Kata ya Rutoro na Wilaya za Karagwe na Misenyi. Tunaomba watu hawa waondoke nchini kwetu. Tunashauri mipaka yetu idhibitiwe kila anayekuja na aje kwa utaratibu uliowekwa. Utaratibu uliowekwa ni pamoja na mgeni kuishi kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria za nchi.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakazi wa Kasuli wamekuwa katika wakati mgumu kutoka kwa baadhi ya Askari Polisi ambao wengi wao ni wale walioko Wilayani Kasulu kwa muda mrefu sana. Askari hawa huwatisha wananchi ikiwa ni pamoja na kuwasabishia usumbufu wa kila aina licha ya kwamba wao ndio wenye jukumu la kuwalinda wasipate usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitaka Serikali iliangalie suala hili kwa mapana zaidi ili kupata ufumbuzi ikiwa ni pamoja na kuwaondoa Askari wote waliodumu Kasulu kwa muda mrefu kwani wao ni chanzo cha tatizo kwa kiasi kikubwa. Aidha, namwomba Waziri afanye uchunguzi kwa kushirikiana na wananchi ili kubaini Askari wote wanaokiuka maadili yao ya kazi na hatimaye sheria ichukue mkondo wake na mwisho wa siku adha na usumbufu wanaoupata wananchi visiwepo tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Uhamiaji Wilayani Kasulu imekuwa kero na kama mzigo mzito kwa wananchi wa Kasulu, huwakamata na kuwaambia wananchi kwamba siyo raia wa Tanzania. Mbaya zaidi hufanya hivyo kipindi cha uchaguzi kwa wafuasi wa Vyama vya Upinzani hasa wagombea hali inayowafanya wananchi wa Kasulu waone kwamba Idara hii inaendekeza ukada wa Chama fulani cha Siasa na hivyo kuathiri ufanisi katika kuwatumikia wananchi na hata kuvuruga uchaguzi. Hivyo basi nashauri Serikali ifanye mikakati ya kuiboresha kwa kuwa na watendaji wazalendo na waadilifu mapema iwezekanavyo ili kuepusha vurugu zinazoweza kutokea pindi wananchi watakapokata tamaa juu ya Idara hii ya Uhamiaji Kasulu hasa ukizingatia kwamba ni heri kuziba ufa kuliko kujenga ukuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Polisi Jamii, ni suala muhimu na zuri sana kwa usalama wa raia na mali zao lakini suala hili hufeli pale panapokuwa na mahusiano mabaya na kutoaminiana kati ya Askari Polisi na wananchi. Naomba Serikali ihakikishe kwamba inakuwa ni amri kwa Jeshi la Polisi pindi ifikapo wiki ya Polisi Jamii ili wananchi wapate nafasi ya kuchangia mawazo yao na kutoa taarifa juu ya Askari ambao pengine ni waonevu na wanakiuka maadili

yao ya kazi. Hili litarahisisha kuimarisha imani na mahusiano mazuri kwa Askari Polisi na wananchi na zifanyiwe kazi ili kuimaraisha nidhamu kwa kila Askari katika kutekeleza majukumu yake bila uonevu wa aina yoyote. Aidha, ninaamua kutoa hoja hii kwa kuzingatia kwamba suala hili ni nyeti na sijawahi kuona likifanyika katika Wilaya yangu ya Kasulu licha ya kwamba kuna malalamiko mengi kwa wananchi Polisi kwenda Vijijini usiku bila taarifa, ni tatizo kubwa.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kijengwe Kituo cha Polisi imara katika eneo la Mtambaswala Mkoani Mtwara ili kudhibiti uhalifu unaoweza kusababishwa na wananchi wa Msumbiji na Afrika ya Kusini. Zipo dalili kubwa za madawa ya kulevya kuvuka kutoka Msumbiji na kuingia Masasi. Pia magari na pikipiki ya wizi kuingizwa Mtwara. Vilevile Wasomali inasemekana huvushwa kwenda Msumbiji kupitia Mtambaswala. Hii inahatarisha usalama wa wakazi wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maaskari Polisi wastaafu wapo baadhi ambao hawapatiwi pensheni kwa sababu tu walipoteza cheki namba. Je, ina maana Wizara haina utaratibu wa kutunza kumbukumbu za wastaafu wake? Hawa wanaohusika wanazo *force* namba, tarehe ya kuajiriwa na kustaafu pamoja na mahali walipoanzia kazi na kustaafia pia na kile cheti cha kustaafu. Je, Wizara haioni kwamba iko haja ya kuwasimamia Askari hawa Hazina ili waweze kupata haki zao za pensheni. Inashangaza kusikia kwamba Wizara inachoma moto mafaili kila baada ya miaka mitano wakati ambapo nchi nyingine hutunza kumbukumbu za miaka mia nne iliyopita. Je, nini sababu za kuchoma moto kumbukumbu? Ni vipi tutaendeleza historia ya Wizara bila kuwa na kumbukumbu. Katika suala hili Wizara haiwatendei haki wastaafu wake.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia ya maandishi naomba nichangie bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri na ngumu ambayo wamekuwa wakikabiliana nayo katika utendaji kazi wa kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuanza kujenga nyumba za kuishi Askari Polisi kwani nyumba wanazoishi Askari na familia zao zinasikitisha hasa ikizingatiwa tunasherehekea miaka 50 ya Uhuru. Askari hawa wanateseka kwa kukaa Kota yenye chumba kimoja na sebule akiwa na watoto wa kike na wa kiume na hata kuwepo na wajukuu. Tunazungumzia maadili ya vijana yameporomoka hivi kwa utaratibu kama huo kwa nini watoto wanakomazwa kwa nguvu kwa kusikia au kuona matendo mabaya ambayo hayaepukiki kwa wazazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, leseni mpya za magari. Zoezi hili limeanza vizuri, lakini wananchi wameanza kulalamika kutokana na utaratibu wa kuwataka wenye *Leseni Class C* wakasome na rushwa ndio imepamba moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, madai ya Askari/Malimbikizo. Naiomba Serikali iangalie na kulipa madeni/malimbikizo ya Askari hususani wale wa chini kwani kwa kufanya hivyo kutaendelea kuwatia moyo na kupunguza hata kuomba rushwa. Hii iende sambamba na kuwapatia vitendea kazi kama vile pikipiki/ magari hata kwa kuwakopesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira za Polisi/Magereza ziwe zinatokana na vijana ambao wanajitolea JKT, hii itawavuta vijana wengi kujiunga na JKT na ndipo vijana hao itakuwa rahisi kuwapata kwa mafunzo ya kuipenda nchi yao na huku wakiwa na matumaini ya ajira ambazo zimekuwa hazipo kwa sasa na hata zikipatikana ni chache sana. Niombe kuishauri Serikali, ni vema uwepo utaratibu wa kuwatambua Askari wenye familia kubwa, zikatazamwa tofauti kwa kuwaruhusu kupanga nje eneo tofauti kwa ili heshima ya Askari wetu iwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la Askari wa Usalama Barabarani wamekuwa wakifanya kazi kama sehemu nyingine ya ajira ya kujipatia ujira. Kwani rushwa huombwa au hutakiwa zitolewe bila hata ya aibu hasa wanapowakamata Madereva. Askari hawa wa chini upatikanaji wa nafasi hiyo ya *Traffic* ni ya mizengwe na wanaobahatika kupata ni lazima afanye kazi kwa bidii ya kukusanya mapato yasiyo halali kwa ajili ya Viongozi Wakuu. Suala la rushwa barabarani lina *chain,* siyo ya Askari wadogo tu. Hivyo rushwa ya barabarani sio rahisi kumalizika, lakini kama Viongozi Wakuu wakiamua kuacha kupokea basi inaweza kupunguza tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Askari Magereza nayo hairidhishi hasa pale wanapowapeleka Wafungwa maeneo ambayo wamepangiwa kufanya kazi. Mfano hai, Gereza la Iringa Mjini wanawatoa wafungwa na Askari kwa mguu umbali wa kilomita 5x2 kwenye kufanya kazi (Igumbiro) hapo anayeumia na kutumikia adhabu ni pamoja na Askari anayewapeleka. Naomba uwepo usafiri ili Askari huyu asiadhibike.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika ni pamoja na nyumba za kuishi Askari hawa hazina hadhi, wapo Wafungwa ambao wana ujuzi wa ujenzi, hawa wangetumika kujenga nyumba za kuishi Askari Magereza/Polisi na Serikali imalizie kwa kutoa vifaa kama vile mabati na kadhalika. Hii itasaidia kupunguza upungufu wa nyumba za kuishi Askari na zitakuwa zenye hadhi.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kupata muda wa kuweza kuchangia hotuba hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri kabisa aliyoitoa hapa kwetu leo. Aidha, naomba pia nipongeze Watendaji wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa ushirikiano na umahiri wao katika kuendeleza majukumu yote ya Wizara, tunawapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Askari wetu hawa wa Jeshi la Polisi kwa kweli kazi yao ni ngumu sana, lakini cha kushangaza Askari hawa, wanaishi maisha ya chini sana ukilinganisha na kazi wanazozifanya. Niiombe Serikali iweze kuboresha maisha ya Askari wetu hawa kwa kuwajengea nyumba za kuishi ili waweze kuthaminiwa. Kwani Askari hawa wanapochanganyika na raia huko uswahili tunawapunguzia sana hadhi yao. Wapewe hata mikopo ya ujenzi wa nyumba kama wanavyopewa wafanyakazi wengine. Aidha, naiomba Serikali iboreshe pia mishahara yao ili iweze kukidhi mahitaji yao ya kimwili na tukifanya hivyo, sidhani kama tutaona Askari wanaojihusisha na vitendo vya uhalifu kama ujambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimwombe Waziri wa Mambo ya Ndani aweze kusimamia vizuri zoezi la Vituo vya Polisi katika maeneo mbalimbali, bado ni tatizo, vituo ni vichache sana, havitoshi ukilinganisha na mahitaji ya watu waliopo. Katika Mikoa ya Mwanza, Geita vituo ni vichache sana kwa mfano katika Wilaya mpya ya Nyang'hwale, kituo kimoja tu ambacho ni kituo cha Karumwa. Tunaomba tupate angalau vituo vitatu (3) kwani maeneo haya yanazungukwa na machimbo kwa hiyo uhalifu ni mwingi.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kuunga mkono hoja iliyowasilishwa kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja naomba nichangie kwa kuipongeza Serikali kwa kuamua kutengeneza vitambulisho vya Taifa. Naiomba Serikali kuhakikisha fursa hii ya vitambulisho vya Kitaifa kwamba yanakidhi haja zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile kila kitambulisho kitakuwa na picha na taarifa zote muhimu basi ni vizuri Serikali ikahakikisha kwamba kama Taifa tunakuwa na *database*.
Mheshimiwa Naibu Spika, *database* hii isambaze taarifa na picha sehemu zifuatazo:-

(i) Polisi
(ii) Uhamiaji
(iii) Mamlaka ya Mapato
(iv) Taasisi za kibenki na sehemu zote ili taarifa na picha isiwe tena, ni suala la mwananchi kuendelea kuulizwa anapokuwa na shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, *database* kama hii haitakuwa ya kwanza kwani nchini Singapore taarifa unaulizwa mara moja tu na kila sehemu unazokwenda kupata huduma unakuwa huna sababu tena kuanza kujieleza, hivyo hata sisi tukijipanga vizuri tunaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Jeshi letu la Polisi kuna baadhi ya Askari Polisi wamekuwa wakilipaka matope Jeshi hili kwa kushiriki vitendo vya ujambazi na kuwabambikia kesi watuhumiwa ili kuficha uovu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina taarifa ya kijana mmoja ambaye alikuwa anasafiri kwenda China kibiashara akitokea Mbeya kwa kupitia uwanja wa Mwalimu Nyerere Dar es Salaam. kosa alilofanya mfanyabiashara huyu ni kitendo cha kuaga na kusikika na mtu ambaye inaonekana anashirikiana na askari wa Kituo cha Polisi cha Chalinze. Mfanyabiashara huyu alisafiri na gari dogo yeye na dereva wake akiwa amechukua kiasi cha pesa Sh. 100,000,000/=, alivyofika maeneo ya Chalinze alikamatwa yeye na dereva wake na kupigwa sana kwa kutuhumiwa kwamba ni jambazi amekuwa akiteka magari na kuiba *Copper*. Aliwekwa ndani na huku akiwa amenyang'anywa simu yake hivyo kutokuwa na mawasiliano na ndugu zake huku wao wakiamini kwamba ndugu yao amesafiri kwenda China kama alivyoaga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano ya mwisho aliyofanya mfanyabiashara huyu ilikuwa baina yake na mfanyakazi wa *Airport* akitoa taarifa juu ya uwezekano wa yeye kuchelewa kufika *Airport*. Baada ya kuwekwa ndani na baadaye kupelekwa gereza la Kibaha amekuja kutolewa kwa dhamana na kukuta pesa zake kwenye gari hazipo na askari polisi kukana katakata kwamba hawakuziona.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo kama hivi ni vingi na vinalipaka matope Jeshi letu la Polisi. Nashauri uchunguzi wa kina ufanyike ili kubaini askari wote wanaolipaka matope jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri jeshi hili likawa na utaratibu wa kuboresha maslahi na hasa kwa wale wanaofanya vizuri kwa kupewa motisha na pia wakakopeshwa ili wajenge nyumba zao ili pindi wanapostaafu wasikose mahali pa kujisitiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na timu nzima ya Wizara kwa maandalizi na uwasilishaji mzuri wa Bajeti ya Wizara. Naomba kuchangia maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa jambo la kusikitisha sana kuona Watanzania wengi wanapoteza maisha na ama wanapata ulemavu, kutokana na ajali nyingi za barabarani. Nyingi za ajali hizi zinasababishwa na uzembe wa Madereva, Askari Trafiki na kadhalika. Naiomba Serikali sasa iseme *enough is enough,* vifo hivi vinavyokumba watu wetu, vinaweza kuzuilika. Naomba Serikali ijaribu kuzuia vifo hivi visivyo vya lazima kwa kufanya yafuatayo:-

Nashauri tuweke upya (ama tutazame upya kama ipo) sheria ya mtu kuwa dereva. Vibuniwe vipengele vya kudhibiti ajira ya madereva wazembe. Vile vile hii sheria ijumuishe na umri wa dereva (hasa anayepaswa kuendesha mabasi na magari makubwa.

Trafiki wanaokuwa zamu kwa tarehe husika na barabara husika wachukuliwe hatua kali, kwa sababu wanapaswa kuwajibika kukagua magari na leseni za madereva kabla na baada ya safari kuanza. Pia wapewe elimu ya kuelewa gari bovu ili ikibidi ikaguliwe kabla ya safari.

Uanzishwe utaratibu wa kutoa nishani au *recognition* kwa madereva wazuri kama motisha na hamasa ya dereva kujitahidi sana asisababishe ajali ili apate hiyo zawadi kubwa inayovutia.

Magari makubwa au mabasi yawekewe utaratibu wa huduma ya kwanza (ikiwepo vifaa), iwe ni sheria kufanya hivi.

Rushwa iliyokithiri ni sababu ya uovu kuendelea kuwepo, kwa sababu kila mara askari wa barabarani wanaomba rushwa na hivyo kumaliza matatizo yaliyokuwa kwenye gari lililokamatwa. Rushwa ipigwe marufuku. Itakapobainika askari (Trafiki) amepokea rushwa apewe adhabu

ambayo itakuwa fundisho kwa wenzake. Hii pengine itapunguza au kuondoa rushwa na halafu matatizo yanayosabisha ajali kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa nini wahanga wa ajali ya gari la *Buffalo* lililotokea tangu 2007 hawajalipwa fidia hadi leo kulingana na ahadi ya Serikali na sheria zilizopo. Hili naomba sana sana nimetumwa na wahanga hao, Mheshimiwa Waziri alitolee ufafanuzi wakati anahitimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Waziri wa Mambo ya Ndani kwa hotuba yake nzuri na ambayo ina uchambuzi wa kina iliyotolewa asubuhi hii. Naunga mkono hoja hii. Nampongeza pia Mheshimiwa Balozi Khamis Suedi Kagasheki, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani kwa msaada mkubwa anaoutoa kwa Mheshimiwa Waziri na hivyo kuleta ufanisi wa hali ya juu katika Wizara, Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wananchi tutatoa kila aina ya ushirikiano kwa Jeshi la Polisi, Wilayani Siha ili kuweza kukabiliana na aina yoyote ya uhalifu ambayo itajitokeza katika eneo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukumbushia maombi ya muda mrefu ya kusaidiwa kupata Makao ya Polisi ya Wilaya kwani kwa sasa tunatumia Kituo cha Polisi kilichopo katika mji wa Sanya Juu. Itakumbukwa kuwa kwa sasa Wilaya zetu ni Wilaya kamili, jambo ambalo limeshuhudia ukuaji wa kiuchumi na wa kimaendeleo. Hali hii imeshuhudia pia ukuaji wa matukio ya uhalifu katika eneo letu.

Mara nyingi nimewasiliana na uongozi wa Wizara husika umuhimu wa kuanzisha *(a Central Police Station)* katika Wilaya ya Siha bila ya mafanikio yoyote yale. Naomba kwa mara nyingine nikumbushie kuhusu ombi hili la muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kusema naunga mkono hoja.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba za makazi kwa Askari Polisi, Kituo cha Polisi Chwaka, Wilaya ya Kati Unguja, nyumba ziko katika hali mbali zinahitaji matengenezo au kujengwa upya. Jengo la ghorofa ambalo litakuwa na nafasi kubwa na kuweza kukaa askari wengi na familia zao badala ya baadhi yao kuishi uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni kwa Askari Polisi yalipwe kwa wakati ili Askari wetu wasiwe ombaomba na kushindwa kufanya majukumu yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tabia ya wananchi kujichukulia sheria mikononi mwao tayari imeanza kuzoeleka kwa visingizio vya kudai haki, miongoni mwa mambo yanayowachukiza wananchi ni kwa nini Serikali kupitia Wizara tumekuwa wapole sana na hata pale viashirio vya uvunjifu wa amani vinapojitokeza tunakawia kuzuia badala yake tunahangaika sana kuwabembeleza wahalifu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya *Traffic* imegubikwa na wingu la rushwa. Malalamiko haya ni ya muda mrefu. Bado hadi leo hatua madhubuti za kuzidhibiti hali hii hazijachukuliwa. Moja katika hatua itakayosaidia ni kubadilishwa askari idara kila baada ya miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kutolewa kwa adhabu kali kwa wale wote watakaokamatwa wakifanya dhambi hii. Vilevile mitego iwekwe ili wale wote wanaojihusisha na rushwa wakamatwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko mengi kuwa Zanzibar haipati idadi ya ajira ile iliyopangiwa. Wengi wa wanaochaguliwa kujiunga na Polisi hurejeshwa baada ya muda mfupi kwa visingizio vilivyokuwa si vya msingi. Hivyo nafasi zao kuchukuliwa na vijana kutoka Tanzania Bara. Naiomba Wizara ichukue hatua madhubuti kuhakikisha vijana wa Zanzibar wanapata nafasi waliyopangiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna nafasi tupu katika Jeshi la Polisi hasa katika nafasi ya Maofisa. Mfano, nafasi ya Naibu Kamishna Zanzibar imeendelea kuwa tupu kwa zaidi ya miaka sita sasa. Maofisa wenye vyeo vya chini wameendelea kufanya kazi za Naibu Kamishna huyo kwa muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri achukue hatua za haraka kurekebisha suala hili Zanzibar na Tanzania nzima.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la nyumba za kukaa kwa Askari wetu ni kubwa katika nchi yetu japo Wizara kwa kujenga maghorofa 30 katika awamu ya pili naipongeza Wizara kwa hili, lakini katika mwaka huu wa fedha sijaona ujenzi huu kufanyika katika sehemu ya pili ya Muungano ya Zanzibar, ambako kuna tatizo kubwa la makazi kwa askari wetu. Pamoja na uchakavu wa majengo, maoni yangu iwapo hakutakuwa na uwezekano wa kupatiwa nyumba mpya basi mwakani ipewe kipaumbele kupunguza tatizo la makazi kwa askari wanaoishi Zanzibar. Kwa hiyo, naona wangefanyiwa matengenezo nyumba zilizopo hivi sasa, ili kuwawekea mazingira mazuri ya makazi kwa askari waliokuwemo kwenye nyumba za Polisi Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo na mfumo wa kuwapatia elimu zaidi kwa wale waliokuwa *form four*, ambayo ni lazima kwa hivi sasa wakati wa kujiunga na Jeshi hilo. Askari wasichukue muda mrefu bila ya kupatiwa mafunzo katika vyuo vya Bara na kilichopo Visiwani Zanzibar. Motisha ya kupandishwa vyeo, ni jambo muhimu kwa askari wetu ili kusaidia kupunguza uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ifikirie kwa raia wema, kuwawezesha namna ya kumiliki silaha kwa visiwa vyetu vya Zanzibar, maana sasa ulimwengu umebadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAULIDAH A. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kwenye hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Hii ni Wizara muhimu sana kwa ajili ya kuwalinda raia na mali zao na pia kuhusu madawa ya kulevya na wageni wanaoingia nchini na kutoka na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madawa ya kulevya kwa kweli inabidi kuongeza juhudi zaidi na kuwashukuru wale wote wanaosaidia vita hii hasa ndugu zetu wa Balozi ya Marekani. Madawa ya kulevya ni janga kubwa sana kwa vijana wetu kwani hata gonjwa la UKIMWI hupata nafasi kubwa kwa maambukizi. Ushauri wangu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali iwape majukumu Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji kuwa wa kwanza kutoa taarifa waonapo watu wanaingia na kutoka kwenye nyumba fulani (na hapo hapo Serikali kuwa waangalifu kutokutoa majina ya hawa ambao hutoa taarifa hizo) kwani usalama wao huwa mashakani.

Pili, kijana anapoonekana afya yake inadhoofika wazazi wajitahidi kutoa taarifa kwa Wenyeviti wao ambao watasaidia kumpeleka kijana huyo kwenye kituo ambacho atasailiwa (wazazi wapewe elimu hiyo haraka).

Tatu, Serikali isione tabu kutoa hadharani jina la yeyote aliyehusika pindi wakiwa na uthibitisho wa kutosha kwani wahusika ni vigogo wakubwa ndani ya nchi.

Nne, Serikali ijitahidi kuwapa elimu Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji kwani hawa ndio wako karibu na wananchi na kujitahidi kuwa nao karibu wakati wote hawa huwa wanajua mambo mengi kwenye maeneo yako tusiwatenge kwenye usalama wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu msongamano ndani ya Magereza. Bila ya Serikali kukaa chini na kufikiria tatizo la vijana ambao hawana kazi ya kufanya na wamezagaa mijini, wanataka kuishi kwa kupata chakula na mahitaji muhimu. Hili ni bomu, lazima tukae chini na kuangalia tatizo hili, kwani elimu imeshuka, maadili hayapo kwa vijana, ndoa za utotoni na mimba zisizo na mipangilio vinachangia kuzaa watoto wasiokuwa na malezi mema na hawa ndio wamejaa magerezani kwa makosa tofauti. Kwa hiyo nashauri:-

(a) Naishauri Serikali irudishe utaratibu wa kuendeleza elimu kwenye kliniki zetu za wajawazito.

(b) Kujitahidi kufikiria kuondoa umaskini uliokithiri sio bla bla za kipuuzi.

(c) Mahakama kujitahidi kuendeleza kesi kwa haki bila upendeleo na kuhakikisha kupiga vita rushwa.

(d) Mahakama kujitahidi kutunza nyaraka kwa uangalifu na kupewa fedha za kutosha.

(e) Huduma kwa jamii iimarishwe ili vifungo vya nje vitumike kihalali.

(f) Askari wa upelelezi watoe haki kwa kutoa taarifa ya upelelezi iliyo kweli na kujitahidi kutopokea rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Wizara hii ni Wizara ambayo ina njia kukusanya fedha basi Serikali ingekaa na kuangalia njia ya kuwaongezea mishahara watendaji wake wote wa Wizara hii kwani ni Wizara nyeti na ndio inayolalamikiwa sana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu zimamoto. Nimeshangazwa sana na bajeti hii kuona kwamba Fungu la 14 la Jeshi la Zimamoto na uokoaji halijawekewa fedha za maendeleo. Je, Jeshi hili limejitosheleza kimaendeleo? Ni ajabu kubwa kwani moto na majanga mengine ni jambo la hatari na ninavyoelewa wanahitaji kujiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi ni muhimu sana kwani kazi yake ni kumlinda raia na mali zake lakini ndio chombo ambacho kwa hivi sasa kila siku unasikia vituko vya kujihusisha na mauaji ya raia na kila mwisho wawili kupita kukamata vijana kuwapeleka kwenye vituo vya Polisi na baadaye kutaka walipe kiasi cha Sh. 10,000/= ili watolewe, wahalifu ambao hukamatwa na raia kwa wizi, wakipelekwa vituoni huachiwa na baadaye raia huwaona mitaani hapa ndipo raia wanakosa imani na jeshi lao na kuchukua sheria mikononi mbele ya vijana wadogo ambao huwa wanashuhudia tendo hilo la kinyama likitendeka. Hii inajenga watu wa ajabu baadaye na raia hawataki kusikia lolote. Natoa ushauri ufuatao:-

(a) Narudia kuomba kwa Serikali kuangalia upya mishahara ya wote kwenye Wizara hii pamoja na vitendea kazi.

(b) Kuvipitia vituo vya polisi hususan wakati wa mwisho wa wiki kwa siri kubwa ili kubaini unyanyasaji huo wa vijana.

(c) Askari wa usalama barabarani bado hawafanyi kazi zao kwa utaratibu mzuri, uaminifu na ukweli. Hii inasababisha ajali za barabarani kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujitahidi kuwapa raia elimu na namba za simu ili wakiona dereva anaendesha vibaya watoe taarifa au kila basi la abiria liwe na namba za simu za kutoa ripoti.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamiaji ni chombo muhimu sana kwanza nawapongeza kwa kuweza kukamata wahamiaji haramu ambao wanaingia nchini kila siku. Nashauri:-

(a) Wao pia wawashirikishe Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Vijiji ili kubaini wageni wanaoingia na kutoka.

(b) Kurudisha utaratibu wa zamani kwa wenyeviti wa mitaa na vijiji kuwa na daftari la kujua wageni wanaoingia mitaani mwao au vijijini mwao na uhamiaji kupata taarifa hizo kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Serikali imeona ni muhimu kutunga sheria kuwa wahamiaji iwe ndani ya Wizara hii. Wafanyakazi wa uhamiaji wapatiwe maslahi ya kusaidia wafanye kazi zao vizuri. Kupatiwa *uniform* iliyokamilika kila wanapokuwa kazini. Hii itasaidia vijana wanaojifanya uhamiaji kupita majumbani wanamokuwepo wageni na kudai *permit* au *passport* na hapo kudai rushwa na kulitia doa Jeshi hili la Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa waangalifu na Maafisa wa uhamiaji waliopo barabarani ambao wamefukuzwa kazi na kuendelea kufanya kazi hizo nje na uangalifu zaidi inasemekana wana mihuri yote ya Uhamiaji (fanyeni uchunguzi wa kina juu ya hili).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuwatakia kheri Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii. Hekima, busara, moyo wa kukataa rushwa, utendaji makini na kutoa haki. Hii ni Wizara ambayo ina neno la Mwenyezi Mungu. Toa haki na wewe upate haki kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Waziri kwa kazi yenu nzuri mnayofanya katika Wizara. Baada ya pongezi hizi naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuimarisha Vituo vya Polisi. Vituo vingi vya Polisi hasa katika Kata mbalimbali nchini havina kabisa mahitaji muhimu ili kuwawezesha askari kutekeleza vizuri majukumu yao. Kwa mfano, vituo vingi wanatumia nyumba za kuazima ambazo watu wamejitolea na kibaya zaidi, hawana usafiri wowote kuwawezesha wafike haraka kwenye maeneo ya matukio. Mfano wa jirani ni kituo cha Ifunda, pale wako kwenye nyumba ya mtu na hawana usafiri wowote. Naomba Wizara itatue tatizo hili. Kituo cha Ifunda kinahudumia Kata za Ifunda, Lumuli, Maboga na Wasa haiwezekani Polisi wafike maeneo hayo bila usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pilil, kuboresha maslahi ya askari. Kuna malalamiko mengi kutoka kwa raia kwamba wanapopeleka malalamiko yao kwenye Vituo vya Polisi huambiwa vikwazo lukuki vikiashiria kwamba askari wakati mwingine huwa wanadai kitu chochote ndipo jambo linalolalamikiwa lishughulikiwe na askari. Hayo ni madai ya wengi wa wananchi lakini siamini kwamba kila askari hudai chochote ila ni ishara ya kueleza kwamba kuna tatizo na Serikali ichukue hatua. Pendekezo langu ni pamoja na kuwaongezea maslahi ili askari wasiingie katika vishawishi hivyo.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linafanya kazi katika mazingira magumu hasa katika suala la miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi za Polisi. Jambo hili ni tatizo kubwa katika ufanisi wa utekelezaji wa kazi za kipolisi ndani ya ofisi zao hata raia anaporipoti tatizo, pia hutakiwa anunue karatasi kwa ajili ya kuchukuliwa maelezo. Ofisi za Polisi ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja

majengo yote ukitoa lile la Madema ni chakavu sana. Silingi katika vyumba vya ofisi zimeoza na hupelekea mvua zinaponyesha askari kutumia ndoo (makopo) kukinga maji yanayotoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu magari. Katika mkoa huu magari yaliyopo ambayo hutumika wakati wa kukabiliana na kazi za kila siku za kawaida hazitoshi kwani kuna gari moja katika Wilaya ya Magharibi na moja katika Wilaya ya Mjini ambalo halifanyi kazi. Tatizo la mafuta ya magari katika Mkoa huu ni kubwa sana kwani kwa siku moja gari hupewa lita tano za mafuta, jambo ambalo hudhoofisha utendaji wa kazi za Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ajira ndani ya Polisi ni tatizo kubwa kwa upande wa Zanzibar, kwani hadi leo hili jambo limekuwa ni siri sana mbali na matangazo yanayotolewa lakini utaratibu na uhalisia katika hili haueleweki. Ni vema Zanzibar kama mshirika wa Muungano huu ikaelezwa kwa uwazi, ni asilimia ngapi ya nafasi za ajira kwa upande wa Zanzibar hasa ikizingatiwa hii ni haki yetu na sio suala la kufikiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa sasa wa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kuwa ni miongoni mwa wale wanaoshiriki katika zoezi la kupitisha majina ya waombaji nafasi hii si haki hasa ukizingatia kwamba hawa ni Makada wa CCM, dhana iliyopo ni kwamba (watapitisha vijana wao wa CCM) na wengine kukosa nafasi pamoja na sifa walizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya siasa ndani ya Polisi, katika miaka ya 1992 – 2010, Zanzibar iligubikwa na utofauti wa kisiasa baina ya Vyama vya Siasa hasa Zanzibar. Jambo hili liliathiri pia utendaji kazi wa Polisi kwani kwa kiwango kikubwa Polisi walitumiwa ipasavyo na Chama cha Mapinduzi kwa maslahi ya chama hicho. Baadhi ya watumishi wa Polisi walisakiziwa tuhuma za makosa kwa dhana za hisia na mitazamo ya kisiasa. Walifukuzwa kazi na kunyimwa haki zao za kimsingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvunjaji wa Sheria. Polisi kwa mshangao mkubwa bila kujali kwamba wao wanaongozwa na nidhamu na kufuata sheria wamekuwa wavunjifu wa sheria. Polisi walikataa kutii amri ya Mahakama ya Zanzibar ya kuwarejesha kazini na kuwalipa haki zao zote askari waliowafukuza na Mahakama kuamuru warudishwe kazini. Naiomba Serikali itoe kauli juu ya watu hawa walioamuliwa na Mahakama warejeshwe kazini na kulipwa haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maslahi ya Polisi. Jeshi la Wananchi na taasisi nyingine za ulinzi hapa Tanzania ni taasisi ambazo tumezikabidhi usalama wa nchi yetu. Hivyo ni vyema, Serikali ikaangalia maslahi yao ya mishahara na posho mbalimbali ili zifanane lakini pia ziendane na hali ya maisha. Posho za kujikimu *(ration allowance)* kwa Polisi ni Sh. 100,000/= lakini JWTZ ni Sh. 150,000/= zilingane. Askari jeshi mwenye cheo cha Sajenti ana uwezo wa kumwajiri Afisa Polisi mwenye cheo cha nyota moja. Mshahara wa Sajenti wa JWTZ unafanana na kwa karibu sana na mshahara wa Polisi mwenye nyota tatu, jambo hili linatia wivu wa kiutendaji kwa watendaji wa vyombo hivi muhimu sana ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Balozi Ali Kagasheki, Katibu Mkuu, *IGP* Ndugu Said Mwema pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madai mbalimbali ya Askari Polisi. Pamoja na juhudi za Serikali za kulipa madeni ya Askari Polisi bado kuna madai ya fedha nyingi za Askari Polisi wakiwemo askari wa Mkoa wa Singida. Ni ukweli usiofichika kuwa tabia ya Askari Polisi wanapopewa amri yoyote husema ndiyo afande hata kama atatekeleza amri kwa mazingira magumu. Tabia hiyo ya Askari Polisi isiwe kigezo cha kutokulipwa stahili zao mapema. Napenda kupata maelezo, je, kupitia bajeti hii madai mbalimbali ya Askari Polisi yatalipwa yote?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majengo ya Kituo cha Polisi, Itigi. Napenda kuiarifu Serikali kuwa Kituo cha Polisi, Itigi kinatumia majengo ya *TRC* yaani Mamlaka ya Reli. Tena ofisi ina jengo lenye chumba kimoja na sebule. Naomba Serikali itambue ukubwa wa Tarafa ya Itigi yenye

Kata kumi na tisa. Naomba maelezo ya Serikali kituo hiki kikubwa kitajengwa lini ili kiweze kupata askari wa kutosha pamoja na silaha ukizingatia Tarafa huwa ina matukio mengi ya ujambazi wa kuteka magari, kuvamia maduka na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vituo vya Polisi vya Shelui na Itigi kupewa magari. Ni ukweli usiofichika, Kituo cha Polisi, Shelui na Itigi vina maeneo makubwa na matukio ni mengi ya uhalifu mfano, magari kutekwa, wizi wa mifugo, uvamizi wa maduka na kadhalika. Hivyo askari hufanya kazi kwa mazingira magumu sana. Naomba Serikali inieleze lini vituo hivi vitapatiwa usafiri wa gari ili askari waweze kufanya kazi zao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Manyoni. Naishukuru Serikali kwani ilisikia ombi au kilio cha wana Manyoni cha kutaka kujenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ili kuachana na majengo ya Halmashauri ambayo nayo yamechakaa sana. Jambo la kusikitisha ni kuwa sasa ni miaka mitatu tangu kiwanja kiliponunuliwa. Napenda Serikali inieleze ni fedha kiasi gani zimetengwa za kuanza ujenzi wa kituo hiki pamoja na kukarabati majengo kituo hiki pamoja na kukarabati majengo kituo kilipo, sasa kwani wamepewa na kwa kusogeza huduma kwa wananchi kituo hicho kitakuwa cha ukweli majengo yamechakaa sana na bati zinavuja sana suala ambalo linajulikana siku nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ahadi ya *IGP* ya kuchangia ujenzi wa Kituo cha Polisi Shelui. Napenda kumpongeza sana *IGP* kwa uwezo wake mkubwa wa kazi ndani ya Jeshi la Polisi kupitia mikakati yake kwa nyanja mbalimbali pia kwa imani yake kwa wananchi wa Tarafa ya Shelui alipotembelea kituo hicho aliahidi kuchangia shilingi milioni tano. Hivyo, naomba Mheshimiwa Waziri atamke fedha hizi zitapatikana lini ili kusaidia kukamilisha ujenzi wa ofisi na chumba cha amari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gari la antirobari *patrol* ya Mkoa. Napenda kuitaarifu Serikali kuwa pamoja na mikakati mizuri ya Polisi Mkoa wa kufuatilia hali ya ulinzi hasa kwenye *highway* na kikosi kipo kwa kazi hiyo bali hakuna Gari la Antirobari *Patrol* ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matukio ya magari kutekwa, kuanguka au wafanyabiashara kuvamia kupungua sana Mkoani Singida chini ya Uongozi kabambe wa Kamanda Mwanamama Selina Kaluba bado pana haja ya kupewa gari la Antirobari *Patrol* ili kuendelea kudhibiti uhalifu mkoani hasa kwenye *highway* ya Manyoni–Singida, Singida–Babati na Singida–Shelui. Naomba Serikali inipatie majibu yenye kuonyesha ushirikiano wa kuunga mkono juhudi za *RPC* Selina Kaluba (Mama).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa jengo la ghorofa la makazi ya askari wa *FFU*. Ni ukweli usiojificha *RPC* Selina Kaluba anafanya kazi kubwa ukiwemo ujenzi wa nyumba ya ghorofa ya makazi ya askari wa *FFU* bali anakwamishwa na bajeti anayopata, naomba Serikali itusaidie hata kwa kutuombea kwenye Mfuko Maalum Hazina ili jengo hili likamilike askari wapate pa kukaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchakavu wa nyumba za *line Police* Singida Mjini na Manyoni. Naomba Serikali irejee maombi ya Wabunge ya kila mwaka ya kujenga upya nyumba za askari polisi zikiwemo za Singida Mjini na za Manyoni kwani nyumba hizi ni chumba na sebule tofauti na matumizi ya familia za askari zenye watoto wa jinsia tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri nyumba hizi kubomolewa ili kujenga zingine hasa majengo ya ghorofa ili familia nyingi kupatiwa nyumba. Naomba Serikali inipe maelezo hasa nyumba za Mjini Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu wa kupandisha askari vyeo. Huwa napata faraja sana askari wanapopelekwa kozi ili kupata mafunzo ya kupandishwa cheo. Kinachosikitisha sana ni pale askari wanapokwenda kozi wenye elimu ya kufanana na umri kazini unafanana lakini unakuta wanachukua kozi tofauti. Hali hii inawavunja moyo askari wetu, naomba Serikali kulisahihisha suala hili ili kuwapa haki sawa askari wetu. Nasubiri maelezo ya Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madawa ya kulevya. Napenda kuieleza Serikali kuwa bado madawa ya kulevya yanaendelea kuwaumiza vijana wa Tanzania. Naiomba Serikali kuwafuatilia wale wanaojihusisha na uuzaji wa madawa ya kulevya mfano, Magomeni Mikumi, Mtaa wa Muhuto. Naweza kuwasaidia endapo mtahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja nikiamini mchango wangu utatolewa maelezo wakati wa Waziri kujibu hoja.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *IGP*, Kamishna Mkuu wa Magereza na watendaji wote kwa kuleta hotuba nzuri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie matatizo yanayowapata wananchi wanaoishi na kufanya biashara katika maeneo au masoko yaliyoko mipakani. Nimepata fursa kutembelea vituo viwili vya Kabanga (Ngara) na Mabamba (Kibondo). Tatizo kubwa lililopo ni kuwepo kwa vituo vya ukaguzi hususan wa mazao unaofanywa na watendaji wetu wa Serikali wakiwemo wakaguzi wa mazao na Askari Polisi ambao vituo vyao havikai ndani ya mpaka. Katika vituo hivyo viwili, wananchi na wageni (Warundi) hukaguliwa wakiwa katika vituo vya Tanzania wakati wanakwenda ama nyumbani kwao (Watanzania wanaoishi katika vijiji vinavyopakana mpaka) au wageni (wanaopita katika vijiji vinavyopakana na mpaka wakati wanaporejea makwao).

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kero hasa kwa Watanzania suluhisho la kero hii ni kusogeza vituo vya ukaguzi kutoka ndani ya nchi kwenda mipakani kama vile, tuwe na *one stop border post* katika kila mpaka. Nashauri Wizara zinazohusika na ulinzi na usalama wa raia mipakani ziweke katika mipango yao ujenzi wa vituo mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ABDULLA JUMA ABDULLA SAADALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wafugaji wavamizi kutoka nchi jirani. Natoa pongezi kwa jitihada za Jeshi la Polisi na vitendo vyake vyote katika kudhibiti uhamiaji haramu na uvamizi wa Wafugaji kutoka nchi jirani. Napendelea hatua zaidi zichukuliwe kwa kupitia Sekretarieti ya Afrika Mashariki *Council* ya *Peace, Security and Internal Affairs* katika *Level* ya Afrika Mashariki ili udhibiti uwe katika pande zote mbili. Ukosefu wa hili ni viashiria vya vita vya nchi Tanzania – Burundi, Tanzania- Rwanda kwani itafika wakati Watanzania watashindwa kustahamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kesi za Mahakamani kudorora. Imebainika kuwa kuna kesi nyingi ambazo zimerundikana hasa zile za jinai na mauaji ambazo ni nyeti. Uamuzi wa kusikiliza kesi hizo unategemea upatikanaji wa pesa ili kuwawezesha majaji wasafiri kuzihukumu kesi hizo. Kwa kweli ni dhuluma kumweka mtuhumiwa kwa zaidi ya miaka mitatu, halafu kesi yake kuhukumiwa kuwa iwe batili au hana hatia. Napendekeza hatua maalum zichukuliwe ili kuharakisha kusikilizwa kwa kesi za mauaji. Majaji/Makarani/*Counsellors* (Washauri nasaha) ni wa muhimu katika kufanikisha hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhalifu wa mtandao wa kompyuta. Napenda kutoa tahadhari kwa Jeshi la Polisi na Serikali juu ya matumizi mabaya ya elimu ya kompyuta juu ya wizi wa fedha mabenki. Kutumia mtandao wa *Twitters*, *Facebook* au hata *Blogs* katika kuhatarisha amani hapa nchini. Ni maoni yangu kuwa, jambo hili lisidharauliwe kwani limeshaanza kutoa athari mbaya ya kuhatarisha amani ulimwenguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za jitihada za Wizara hasa Jeshi la Polisi kwa jitihada zake za kuondoa silaha hizo pamoja na kuzisajili na kwa kutumia uwezo wa nguvu za umoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pia napongeza jitihada za Wizara kuanza mchakati wa kuanzisha vitambulisho vya Mtanzania. Pongezi za Wizara juu ya ulinzi shirikishi na nyumba za askari polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa angalizo rasmi juu ya wana usalama kutotumia silaha nzito pasipo na usalama na ikibidi hata wasiende na silaha hizo kwenye tukio. Kwanza

wapime nguvu za tukio halafu watumie nguvu zenye uwiano kukabili nguvu hizo. Mfano, wanafunzi wa Sinza waliokaa barabarani kutumiwa silaha nzito za risasi kutimua fujo hiyo. Hili ni jambo linaloashiria ukosefu wa taaluma na *ethics* za askari katika matokeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu rushwa. Ni jambo la kusikitisha kuona watendaji wa Polisi (Maafisa) wamekuwa ombaomba na pengine walaji rushwa wakubwa. Jambo hili limekithiri kwa polisi wa kaunta kituoni na *Traffic* na *CID*. Napendekeza askari kanzu kutoka vikosi vya TAKUKURU, usalama wa Taifa na hata Jeshi (JWTZ) wawe ni miongoni mwa vikosi vya doria zote za Jeshi la Polisi ili kuondoa kujuana, uzoefu na upokeaji wa rushwa unaoongezeka kila kukicha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MUHAMMADI IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ile ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ndani ya Bunge hili iheshimiwe na itekelezwe. Kwa kuwa ahadi hiyo ni ya kulipa madeni yote yanayodaiwa na askari polisi yakiwemo ya uhamisho, likizo na madai ya Wazabuni. Nashauri vilevile kwamba baada ya kumaliza madeni hayo kuanzia sasa uhamisho usitolewe hadi pale fedha za uhamisho huo ziwepo, yaani uhamisho uambatane na cheki yake askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile askari anapopandishwa cheo iwe ni vema watengenezewe haki zao za nyongeza ya mishahara ambayo inakwenda sambamba na vyeo vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendea kazi vya askari wetu viwepo vya kutosha hasa ukizingatia kwamba kazi zao ni nzito na zenye kuhitaji ustahimilivu wa kutosha. Leo hii utamkuta askari akiongoza magari katika barabara nyingi tu za nchi hii, lakini husimama hapo ama iwe nyakati za mvua au majira ya joto bila hata chupa ya maji. Kumsafirisha askari polisi na kumpeleka katika kituo au lindo alilopangiwa kazi hiyo ni vema wakatafutiwa gari iliyokuwa inahimili joto au mvua yaani *bus* badala ya malori yaliyo wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango wanayokatwa askari juu ya pale anapofiliwa ni kadhia nzuri ila tu inasemekana kwamba askari wa Zanzibar wanapofiliwa hupewa kiasi cha sh. 500,000/= tu wakati wenzao upande wa pili wa Muungano hupata Sh. 1,000,000/=. Hii sio haki iwapo kuna ukweli wa habari hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho za askari polisi bado ni kidogo ni vyema wakaongezewe toka Sh. 100,000/= angalau hadi Sh. 200,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wa Magereza wakopeshwe matrekta toka SUMA – JKT kuwe na Co-*ordination* baina ya Wizara hizi ili yale maeneo yanayomilikiwa na magereza waweze kuzalisha kwa ajili ya chakula chao na cha ziada kuweza kuuza. Uwezo huu upo iwapo usimamizi mzuri utakuwepo kwa kutumia mbegu bora na zenye kuzalisha mazao mengi na yaliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *ID's*, zoezi hili lianzishwe haraka ili kuleta ufanisi bora wa kujua nani ni Mtanzania na itaweza hata kudhibiti mapato kutokana na ukusanyaji wa mapato kuwa mzuri na kutokuepuka ulipaji kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimamoto wawe na gari za kutosha na zenye viwango vitakavyokwenda sambamba na ukuaji wa miji yetu ambayo tunaona jinsi maghorofa yanavyozidi kujengwa katika miji yetu. Ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Idara za Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto kwa kazi nzuri na hotuba nzuri ya bajeti 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuomba ushauri na kutoa maombi katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kuboresha vitendea kazi. Wizara ifahamu mabadiliko ya teknolojia duniani na athari zake kwa usimamizi kuwa mgumu kwa majeshi yetu ya Ulinzi, Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto. Hivyo, vifaa vya utendaji vya kisasa vitafutwe na kutumika kwa watendaji wa taasisi zetu. Magari ya Polisi ya kisasa yenye zana bora, mtandao mzuri wa mawasiliano ya kisasa, magari ya kisasa ya zimamoto na kuboresha usafiri wa watendaji kwenda na kutoka kazini ni muhimu kwa jeshi la kisasa. Polisi wa barabarani wanafanya kazi katika hali ya jua na mvua ili kusaidia kupunguza ajali na hata misongamano. Watendewe haki na kupewa zana bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vya zimamoto Jiji la Dar es Salaam vilivyopo *Airport*, Bandari na Makao Makuu Kariakoo/ Morogoro *Road* havitoshi hasa ukizingatia ukubwa wa jiji, Wilaya za Ilala, Temeke na Kinondoni na foleni za Jiji la Dar es Salaam. Ipo haja kuwa na vituo Temeke na Kinondoni licha kuendelea kutegemea kampuni binafsi katika baadhi ya maeneo kama magari ya ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za Maofisa Magereza, Muheza. Mwaka 2003/2004 aliyekuwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Capt. John Chiligati alitembelea Muheza na kuona hali mbaya ya nyumba za tope au makuti na zinazovuja za Maofisa Magereza, Gereza dogo la Muheza. Pamoja na masikitiko aliyoonyesha hadi sasa hakuna lolote lililofanyika! Huku ni kuwadhalilisha watumishi wa Serikali na familia zao! Je, ni lini hali hii ya aibu itarekebishwa pale Muheza? Nini mkakati wa ujenzi wa Magereza ya kisasa pale Muheza badala ya jengo dogo na bovu lililopo na kuendelea kutegemea Gereza la Maweni, Tanga?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo kubwa la ardhi limehodhiwa karibu sana na eneo la Mji Mdogo wa Muheza unaokua kwa kasi kubwa. Ni wazi kwamba bila kuendelezwa malalamiko toka kwa wananchi yataendelea kukua. Tunapenda kupata mwelekeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za Jeshi la Polisi, Muheza. Pamoja na maelezo niliyokwishatoa kwamba eneo la Kituo cha Polisi cha zamani na nyumba za polisi zilipo ni mali ya Shirika la Reli tangu ukoloni! Nilishauri Serikali ibadilishe hati ili eneo limilikiwe na Jeshi la Polisi na kujenga nyumba mpya za polisi eneo kilipojengwa kituo kipya cha polisi Muheza. Hivyo, napenda kujua utekelezaji umefikia wapi na ujenzi wa nyumba mpya utaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuboresha kituo kidogo cha Polisi Amani, Muheza. Kumekuwa na matukio mengi ya uhalifu katika Mji wa Muheza na barabara ya Muheza–Amani kiasi kwamba magari ya abiria kusindikizwa kwa ulinzi wa polisi. Kwa kuwa eneo la Amani ni kubwa na lina wawekezaji wakubwa wa chai (zaidi ya Kampuni mbili) hifadhi ya msitu wa amani na eneo kubwa la utalii na watalii wengi toka nje ya nchi naendelea kushauri kuboresha Kituo cha Polisi, Amani kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kukarabati na kuongeza nyumba za polisi eneo la Amani.

(b) Kuongeza vifaa (vitendea kazi) vya kisasa kama vile *Radio call*, simu, gari, chumba cha kuhifadhi silaha.

(c) Kuongeza idadi ya polisi katika kituo.

(d) Kufungua vituo vidogo katika Kata zilizopo katika maeneo yafuatayo.

| **Kata** | **Kijiji/Kituo kidogo** |
|---|---|
| Zirai | Zirai au Antakae |
| Misalai | Mgambo |
| Kisiwani | Mashewa |

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongeza Kituo cha Polisi, Wilaya ya Muheza. Wilaya ina Kituo cha Makao Makuu, Kituo cha Amani na Kituo cha Kigombe

(i) Kituo cha Kigombe kinahitaji kuboreshwa hasa ikizingatiwa kuwa eneo lina shamba kubwa la Mkonge, watu wengi, hoteli nyingi za utalii na wavuvi wengi wanaoingia kutoka Pemba na Zanzibar.

(ii) Kijengwe kituo kidogo Kwa Fungo, Kwa Fungo ipo katikati ya Kata za Songa, Mtindiro, Kwa Fungo, Potwe, Bwembwera.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutulinda sisi na kudumisha amani na utulivu walionao wanajeshi wetu, ni jambo la kumshukuru Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari polisi na Magereza wakiwa chini ya Jeshi walishiriki katika vita vya Kagera 1978/1979 ya Nduli Idd Amini Dada mwanzo mpaka mwisho. Askari wengine waliopigana vita vya Kagera 1978/1979 walibaki Uganda kwa kazi maalum, baada ya vita kumalizika, kwa hiyo, askari polisi na magereza walishiriki bega kwa bega na jeshi husika katika vita hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la wananchi Tanzania hawakupigana peke yao kutetea nchi hii, wastaafu wa Jeshi la Wananchi Tanzania waliopigana vita vya Kagera vya Nduli Idd Amini Dada mwaka 1978/1979 waliorodheshwa. Je, Askari Polisi na Magereza walioshiriki vita hivyo hawahusiki na utaratibu huo? Je, kama hawahusiki ni nani wanaohusika na atakayetambua kama walikuwa tayari kuifia nchi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Askari Polisi na Magereza walioshiriki katika vita hiyo utaratibu upi kwa wastaafu hao waliopigana vita hivyo kuandikwa na kutambuliwa? Kama kuna chochote kilichotolewa na Serikali kwa Jeshi la Wananchi Tanzania au wanategemea kupewa kwani ndio walioorodheshwa hawa wengine wafanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi na Magereza hawajaorodheshwa mpaka sasa, je, kama Serikali inataka kuwapa kifutia machozi, watakipataje kama hawajatambuliwa rasmi kwa kuorodheshwa? Jeshi la Wananchi Tanzania hawakupigana peke yao kutetea nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara hii iwaorodheshe Askari Polisi na Magereza walioshiriki katika vita hiyo ili waweze kukumbukwa kwa uzalendo wao waliouonyesha na wengine pia hata kupoteza maisha yao. Kwa kuwa minong'ono hii inasikika kwa baadhi ya watu waliofanya kazi hiyo Serikali iwapatie kifuta machozi hata kidogo. Njaa kali waliyonayo inawapelekea kuilaumu Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani kwa Naibu Waziri na watumishi kwa kuandaa hotuba ambayo imebainisha baadhi ya mambo muhimu ambayo Polisi lazima iyashughulikie (Ukurasa wa 3 -10, Hotuba).

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambaye hotuba yake imesisitiza misingi ya haki na utawala bora ambayo lazima izingatiwe na Jeshi la kisasa la Polisi katika kutekeleza majukumu yake.

Mchango wangu utajielekeza katika mambo yafuatayo:-

- Masuala yahusuyo Polisi Bukombe.

- Masuala ya kijumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala yahusuyo Polisi Bukombe. Kituo cha Polisi cha Runzewe (Kata ya Uyovu, Bukombe) kiimarishwe kwa kupatiwa gari litakalosaidia askari katika majukumu yao ya kupambana na uhalifu na kuhakikisha usalama wa raia na mali zao. Hili ni ombi la wananchi wa eneo hilo. Eneo hili liko karibu na mpaka na kuna changamoto nyingi za uhalifu.

Yapo malalamiko ya wananchi kuwa baadhi ya askari polisi Bukombe wanashiriki vitendo vya ukatili kwa mahabusu, rushwa na kesi za kubambikiza. Malalamiko haya yasipuuzwe, yafanyiwe kazi. Askari wanaobainika ni wakosaji waadhibiwe kwa mujibu wa sheria. Askari Polisi wote wakati wote wasisitiziwe kuzingatia na kuheshimu haki za binadamu na utawala wa sheria. Pia maslahi ya Polisi yaboreshwe ili waweze kuondokana na ushawishi wa rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake, ukurasa 11 analalamikia maandamano yanayofanywa na Vyama vya Siasa. Naona ni haki yake kutoa maoni yake kuhusu jambo hili na mengine yote. Lakini ni jukumu lake kama Waziri kuwaelekeza Polisi watende haki kwa kufuata sheria kuyaruhusu na kuyalinda maandamano na mikutano. Katu wasijiingize katika Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya bajeti, ukurasa wa 16, Waziri analalamikia tabia ya kujichukulia sheria mikononi ya baadhi ya wananchi. Akumbukwe kuwa watu hufanya hivyo baada ya kuona au kuhisi kuwa polisi hawafanyi kazi yao kwa misingi ya utawala wa sheria. Tatizo hasa ni rushwa inayowafanya baadhi ya askari kutozingatia sheria. Polisi wakizingatia na kuheshimu sheria kwa vitendo vya wazi hata vitendo vya kujichukulia sheria mikononi vitapungua sana.

**MHE. JUMA OTHMAN ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kusisitiza jengo la Kituo cha Polisi cha Mkokotoni, kwa kuwa kituo hiki kinatumika Wilaya nzima na tokea kiungue bado ujenzi huu haujaanza, naiomba sana Wizara yako ifikirie kituo hiki kwa ujenzi ili askari wafanye kazi zao kwa utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iwafikirie wafanyakazi wanaovuka kwenda Kijiji cha Tumbatu wafikiriwe, wapatiwe usafiri wa boti kwa sababu wakati likitokea tatizo wanapata tabu sana, kwa kuwa hakuna usafiri wa boti wa uhakika. Askari wanafanya kazi katika mazingira magumu sana hasa pale panapotokea mhalifu na anataka kusafirishwa kuja kituoni, hii inasababisha pia kukimbia kwa mhalifu kwa njia ya bahari kwa kuwa ana uhakika hakuna boti ya kumfuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za askari ziko chakavu sana, naomba Serikali ishughulikie haraka nyumba za askari hao ili wawe wanaishi katika mazingira mazuri angalau wajenge imani nao wanajaliwa katika kazi yao ya ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa vitambulisho vya uraia umechelewa sana, hata hivyo, nazipongeza juhudi za Serikali kwa kuteua kampuni imara ya kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali itimize haraka makubaliano na mkandarasi hasa ya kumlipa fedha ya awali ili aweze kuanza kazi. Kwa kuwa mradi huu ni mtambuka, Serikali ikae na taasisi za Mifuko ya Jamii ili kuona namna watakavyofaidika na matumizi ya teknolojia hii, ili waanze kuchangia gharama za mradi huu. Aidha, mradi wa sensa, ungesimamishwa kwanza na fedha zake zipelekwe kwenye mradi huu ili matumizi mazuri ya rasilimali fedha na watu ipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu teknolojia ya kupunguza shida ya makazi na kujitosheleza kwa kilimo. Naishauri Wizara iwasiliane na kampuni inayotengeneza vitambulisho ili waelezee teknolojia ya ujenzi wa nyumba ambapo nyumba ya vyumba vitatu inajengwa kwa siku saba tu. Aidha, kampuni hii ya *IRIS* ina utaalam wa kuzalisha nafaka, matunda bila ya kutumia udongo wala kemikali. Kwa mfano, chembe moja ya mpunga hutoa shuka la kilo zaidi ya moja.

Magereza wanaweza kupata teknolojia hii ambayo ni *organic* na rasilimali kujitegemea kwa chakula na matunda pamoja na ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Case Management System*. Utaratibu ulioanza miaka ya nyuma wa kuangalia ushughulikiaji wa mashtaka mbalimbali, ni vema ukapanuliwa kwa kuunda Kamati hizi kila mikoa. Kamati hizi zifanye yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Polisi. Upelelezi wachambue kesi ambazo wamekamilisha upelelezi lakini *DPP* hajawafikisha wahusika Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkuu wa Jeshi aanzishe program ya kuwatunuku zawadi wale watakaokuwa na rekodi nzuri ya kuharakisha upelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *DPP*. Kwa kupitia waendesha mashtaka waeleze sababu za kuchelewa kuwafikisha Mahakamani ili ajulikane mwenye kucheleweshа badala ya lawama kutupiwa Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mahakama. Waeleze sababu za kuchelewesha kuendesha kesi. Haya yakifanyika kwa njia ya kushirikiana, msongamano na ucheleweshaji wa mashauri utapungua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwa na uraia wan chi mbili. Wizara ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi ili kuona ni namna gani utekelezaji wa kuwapa raia wetu kuwa na uraia wa nchi mbili. Jambo hili ni jema hasa tukitilia maanani ushirikiano wetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *private investigation*. Kwa kuwa Serikali imemudu kuratibu makampuni binafsi ya ulinzi na kwa kuwa imekuwa vigumu kwa wapelelezi wanaostaafu kupata ajira, ni vema Serikali ikaruhusu kuanzishwa kwa kampuni za kufanya upelelezi binafsi ili kujenga uwezo wa upelelezi, kuharakisha upelelezi na kujenga imani kwa wale wanaohitaji huduma hii muhimu. Nchi nyingi duniani zina utaratibu huu na umesaidia sana katika kupata ufumbuzi wa masuala ya upelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kila la heri.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kupongeza hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri na maelezo yote yaliyoelezwa katika hotuba hii ni ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ningependa kuelezea baadhi ya kasoro ninazoziona.

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo hiki kimejaa rushwa sana na kinalalamikiwa sana na wananchi japokuwa si Askari wote walio na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Jeshi la Polisi, Trafiki. Jeshi halifanyi kazi ya kupunguza ajali za barabarani bali wanafanya biashara, nasema kila *Traffic* anaposimamisha gari haangalii makosa bali husimamisha ili achukue fedha, inahifadhiwa ndani ya kadi ya Gari au ndani ya Gazeti. Vitendo hivyo Serikali inaona na mara nyingine hutumwa na viongozi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwananchi anapopata tatizo la kufikisha Polisi, bila kuwa na fedha, hapati haki, haki ni fedha. Ukitoa fedha Polisi watakusaidia hata kukufundisha vyovyote hata kama una hatia watakuponyesha. Rushwa imekithiri mno na ndio maana wananchi wamekosa kuwa na imani na Jeshi la Polisi, wamekata tamaa na ndio maana wameanza kuchukua sheria mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gharama za mahabusu katika vituo vya Polisi vilivyopo Katani na Tarafani. Serikali iwajibike kutunza watuhumiwa waliopo (mahabusu) katika huduma zote, kuwalisha, kuwasafirisha ili walalamikaji wasibebe mzigo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Polisi wakae katika vituo walivyopangiwa. Kumekuwa na tabia ya Polisi kutokukaa katika kituo kilichojengwa kwa nguvu za wananchi kwa michango yao, kwa nguvu zao na kituo kufunguliwa na Polisi kupelekwa. Cha ajabu Polisi pamoja na majengo mazuri hawakai kituoni wanafukuzia rushwa katika maeneo mengine na mfano huo ni Kituo cha Polisi, Milepa, Jimbo la Kwela, Wilaya ya Sumbawanga. Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi waboreshewe maslahi yao, waongezewe mishahara, walipwe posho na wapewe vyombo vya usafiri. Pia naomba Kituo cha Polisi Mji Mdogo wa Laela wapatiwe gari au pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, *IGP*, Katibu Mkuu, Makamanda na watendaji wote wa Wizara hii, napenda kuchukua nafasi hii kutamka kuwa siungi mkono hoja hii hadi pale Waziri atakaponieleza ni kwa nini na lini nyumba za kuishi Askari katika Vituo vya Magomeni, Polisi Kijitonyama (Mabatini) na Oysterbay zitajengwa? Askari katika vituo hivyo hasa Magomeni wanaishi katika mabanda ya mabati yaliyochakaa, vyumba vimegawanywa kwa maboksi, hii ni hatari kwa afya zao, askari anaishi kama mhalifu, familia yake inaishi kwenye mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeongelea jambo hili tangu niingie hapa Bungeni 2005, lakini hadi leo nyumba hizo hazijajengwa. Hata nilipomwomba Waziri wa Wizara hii mwaka 2009 afanye ziara kutembelea Kituo cha Polisi Magomeni ili aone askari wake wanavyoishi kwenye majengo hayo machakavu lakini ziara hiyo haijafanyika hadi leo. Namwomba tena Mheshimiwa Waziri afanye ziara katika Kituo cha Polisi Magomeni ili ajionee hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tatizo la uhalifu linaendelea katika Jiji la Dar es Salaam na majambazi wanatumia pikipiki kufanya uhalifu, ni vema kukawa na ukaguzi wa kushtukiza ili kuwakamata hawa waendesha pikipiki wanaotumia silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Kamanda Kova kuhamasisha ulinzi shirikishi bado naliomba Jeshi la Polisi kuongeza kasi ya kuhamasisha na kuanzisha vikundi vingi vya ulinzi shirikishi ili kukabiliana na uhalifu katika Jiji la Dar es Salaam hususan Kinondoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vitendea kazi kama vile magari, pikipiki, kompyuta ni muhimu sana na naomba vifaa vya kutosha katika vituo vya Magomeni na Mabatini, vituo hivi vinahudumia eneo kubwa na lenye watu wengi. Upanuzi wa Kituo cha Polisi Magomeni ni vyema ukafanyika kwa kuwa jengo la Kituo hiki ni dogo sana lililojengwa miaka zaidi ya 35 iliyopita na wakati huo wakazi wa Dar es Salaam walikuwa wachache sana ukilinganisha na sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, stahili za Askari wapewe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, tutakutana kwenye vifungu. Nawasilisha.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Nahodha kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri sana. Nawapongeza pia Naibu wake Balozi Kagasheki na Mkuu wa Jeshi la Polisi Said Mwema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hotuba ya Waziri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wa usalama barabarani wanawanyanyasa sana madereva na wamiliki wa malori ya mizigo. Inatia aibu kiasi sasa gari hata kama haina chenji ya

elfu mbili mbili hatafika safari yake kwa wakati kutokana na kusimamishwa na *Traffic Police* wote waliopo barabarani atakakopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, leseni mpya za kuendeshea magari zimetengenezwa vibaya na zinasababisha usumbufu mkubwa zinapotumika nje ya nchi yetu. Mpangilio wa masharti yake hauendi kwa mtiririko wa namba *(Numerical disorder)*. Kama makosa haya ni ya bahati mbaya basi asahihishe kwa kutoa leseni mpya na kurudishiwa zote ambazo amezitoa tayari. Kama ni kosa la makusudi basi hafai kuendelea kutoa leseni hizi na nashauri zabuni yake isitishwe na itangazwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi na hapa nasisitiza baadhi ya askari polisi, bado hawajaachana na tabia ya kusingizia watu makosa ili baadaye wapate kuwaomba rushwa. Iko mifano yenye ushahidi wa jambo hili na endapo suala la kumkamata mtu halikuanzishwa na Polisi bali limeanzishwa na raia, basi Polisi wasikurupuke kumkamata mwananchi huyo hadi wawe wamejiridhisha kwamba kweli mtuhumiwa anayo hatia na kesi ya kujibu na kwamba asipokamatwa basi usalama wa raia utakuwa hatarini. Vinginevyo kukamata watu ovyo ovyo kunawafanya wananchi wapoteze imani kabisa kwa Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mdogo, ni ule uliotokea Jimboni kwangu, Kijiji cha Kanyala, Kata ya Bulyahehe Sengerema. Jambazi kauawa na wananchi na baadaye wanatajwa wananchi wengine kinyemela kwamba eti yule jambazi aliwataja kabla hajauawa, kumbe ni hila tu za kuwanyamazisha wasiendelee kupiga kelele juu ya ubadhirifu wa fedha kwenye ujenzi wa shule ya msingi.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja zifuatazo katika Wizara hii:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni hali ya Jeshi la Polisi nchini. Askari wanaishi mitaani, hawana nyumba na pia wengine wanaishi katika mazingira magumu, mishahara midogo, nyumba ndogo ambazo nyingi zilijengwa awamu ya kwanza. Siungi mkono hoja mpaka nipewe majibu sahihi ni jinsi gani Serikali itatatua matatizo hayo?

Pili, Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji yanayofanywa na Jeshi la Polisi, ripoti ya *LHRC* imeonesha jinsi gani Polisi wanavyofanya mauaji ya Raia, siungi mkono hoja mpaka nipatiwe majibu kwa nini na hatua gani zinachukuliwa dhidi ya askari waliofanya mauaji ya raia wema wa Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa katika Jeshi la Polisi, Uhamiaji takwimu za *LHRC* 2010 na Ripoti ya *Transparent International* 2010 kuwa Jeshi la Polisi ndio taasisi inayoongoza kwa rushwa, ikifuatiwa na Magereza ambayo inashika nafasi ya nne, huku *Immigration* (Uhamiaji) ikiwa taasisi ya saba? Siungi mkono hoja mpaka nipatiwe majibu, Serikali inakabiliana vipi na hali hii ya rushwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni Uhamiaji, katika Wilaya ya Kibondo hasa kwenye Jimbo la Muhambwe Watanzania wamekuwa wakibambikiziwa kesi kuwa ni wakimbizi, hivyo, Maafisa uhamiaji wakiomba rushwa na hili nitaleta kama nilivyozungumza na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne ni kuhusu Kituo cha Uhamiaji kilichopo Wilayani Kibondo katika Kijiji cha Mukarazi katika Kata ya Mabamba. Kituo hiki kipo katikati ya vijiji hivyo Watanzania wanaopita hapo wanakaguliwa kama wakimbizi ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja mpaka nipate majibu ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki kilichopo katikati ya vijiji na kuwafanya Watanzania kila wanapopita kukaguliwa? Utadhani wanavuka nchi, kumbe wako ndani ya nchi yao. Toeni kituo hiki kiwe mwisho na mpakani ili wananchi wasisumbuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ya ujambazi, Kibondo haipiti mwezi au wiki bila matukio mazito ya ujambazi. Naomba iundwe Tume maalum kuchunguza na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uchakavu wa Kituo cha Polisi Vwawa (Mbozi) pamoja na nyumba za askari. Mwaka 2007/2008 na mwaka 2008/2009 nimekuwa nikiiuliza Serikali kuhusu kukarabati au kujenga kituo cha Polisi Vwawa ambacho ni kichakavu sana, kimejengwa mwanzoni mwa miaka ya 1960, majengo yaliyoachwa na Mkoloni! Aidha, nyumba chache za askari zilizopo ni chakavu sana na kwa kweli hazifai kuendelea kutumika kwa makazi ya binadamu! Majibu ya Serikali kupitia Wizara hii yamekuwa kwamba kituo hicho pamoja na nyumba za askari zingejengwa au kukarabatiwa. Wizara iliahidi kwamba kazi hizo zingefanywa katika kipindi cha miaka minne, tangu Serikali itoe ahadi hiyo hakuna hata dalili ya kazi hiyo kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kufahamu je, Serikali kupitia Wizara hii itatekeleza ahadi yake lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tabia ya kutowalipa askari posho zao. Posho hizo ni kama vile malipo ya safari, gharama za matibabu, malipo ya kustaafu na kadhalika. Napenda kujua hivi, tatizo ni nini la kutowalipa askari hao haki zao, hasa ukizingatia kwamba tunatumia *Cash* bajeti? Kwa nini matatizo hayo yawe kwa askari wa vyeo vya chini tu? Hivi askari anapotumwa kwenda kufanya kazi nje ya kituo na nje ya wilaya au mkoa wake halafu halipwi, Serikali inategemea kwamba huyo askari anaishije huko anakokwenda? Nashauri askari wote walipwe stahili zao kama ilivyo kwa watumishi wengine wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa hatua iliyofikiwa kwa ajili ya vitambulisho vya Taifa. Hatua iliyofikiwa hata hivyo, vitambulisho vitagharimu Serikali yetu pesa nyingi sana, kinachonishangaza au ambacho ningetaka kujua ni hiki, kwa nini vitambulisho vya Taifa vitolewe kwa watu wasio na Utaifa wa nchi yetu? Je, hatuoni kwamba kama uingiaji wa watu wasio Watanzania utakuwa mkubwa, Serikali itakuwa inatumia pesa nyingi bila sababu za msingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa na kwa muda mrefu kidogo gari za mizigo/abiria zimekuwa hazifanyi safari usiku. Sababu zinazotolewa ni za kiusalama zaidi, kwamba gari hizo zikitembea usiku zinaweza kuvutia ujambazi! Kwa maoni yangu, nadhani kwa kufanya hivyo tunapunguza sana kasi ya kukua kwa uchumi wetu. Hivi nyingine jirani zetu kama vile Kenya, Uganda, Zambia nakadhalika ambazo gari za mizigo na abiria zinafanya safari za usiku wanatumia miujiza gani? Nashauri sheria inayozuia gari za mizigo na abiria itazamwe upya ili turuhusu safari za usiku na hivyo kuchochea shughuli mbalimbali zikiwepo za kiuchumi zikiendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza sana Jeshi la Magereza kwa kazi nzuri za kiuchumi wanazofanya kupitia Shirika lao la Uchumi. Hata hivyo, bado maisha ya wafungwa gerezani hayajaboreshwa vya kutosha. Zipo taarifa kwamba bado wafungwa wanatumia ndoo kama chombo cha kujisaidia. Hivi jambo hili lina ukweli. Naomba Serikali itoe maelezo kuhusu jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Makazi ya Askari wetu hayafanani na kazi nzuri na muhimu wanayofanya nchini kwa ajili ya usalama wa nchi yetu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa makazi bora askari wetu?

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja. Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara hii kwa hotuba nzuri yenye mipango au mikakati ya kuimarisha hali ya usalama wa raia na mali zao nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa maoni katika maeneo mawili:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kuhusu kifungu cha *11 cha Tanzania Citizenship Act No. 6 of* 1995 kinabagua wanawake, tunahitaji marekebisho. Tanzania ina wajibu wa kuhakikisha kuwa wanawake hawabaguliwi. Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (*Convention on the Elimination of All forms of Discrimination Against Women-CEDAW*) wa 1979, *African Protocol on Women's Rights (2005)* na pia *SADC Protocol on Gender and Development (2008)* yote ambayo Tanzania imeridhia, inatoa wajibu kwa Serikali kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake katika nyanja za kisiasa, kisheria, kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara) inatamka kuwa: "Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria". Ibara ya 13(2) na 13(5) ya Katiba zinakataza sheria na mamlaka yoyote kuweka sharti lolote la ubaguzi ukiwemo ubaguzi kwa misingi ya jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kuwa miaka 50 baada ya Uhuru bado tuna sheria ya uraia (The Citizenship Act No.6 ya 1995) yenye kifungu 11(1) kinachotamka kuwa:

*"Subject to the provisions of subsection (2) and of section 6, a woman who is married to a citizen of the United Republic shall at any time during the life time of the husband be entitled, upon making an application in the prescribed form, to be naturalized as a citizen of the United Republic."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki hakitoi haki hiyo kwa wanawake wa Kitanzania walioolewa na wanaume wasio Watanzania. Je, Wizara haioni kuwa sheria hii au kifungu hiki kinakinzana na Katiba ya nchi na majukumu ya Kimataifa *(International obligations)* ambayo Tanzania imeyakubali chini ya Mikataba ya Haki za Wanawake?

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yangu ni kwamba, wakati umefika kwa Wizara kuleta Bungeni marekebisho ya sheria ya uraia ya mwaka 1995 (kifungu cha 11) ili kuwawezesha wanawake wa Kitanzania kufaidi *(to enjoy)* haki yao ya msingi kama wanaume.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukatili wa kijinsia. Nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kuanzisha na kuendeleza mikakati mbalimbali ya kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia hapa nchini. Uanzishwaji wa madawati ya jinsia katika baadhi ya vituo vya Polisi katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Mara, ni jitihada ambazo zinabidi kupongezwa. Pia nimefarijika kuona kuwa, kwa mujibu wa Taarifa ya hali ya uhalifu Januari hadi Desemba 2010 makosa ya ukatili wa kijinsia ukiwemo ubakaji na ulawiti yamepungua. Hata hivyo, udhitibi wa vitendo vya ukeketaji hasa Mkoani Mara bado si wa kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara iendelee kushirikiana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuhakikisha madawati ya jinsia yanaanzishwa katika vituo vyote vya Polisi nchini. Jeshi la Polisi liongeze juhudi katika kudhibiti vitendo vya ukeketaji wa wasichana hasa katika Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichangie kwa maandishi katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hoja hii nianze na haya madawa ya kulevya. Katika Ukurasa wa tatu, Kifungu cha saba (7), jukumu la kuendeleza mapambano dhidi ya madawa ya kulevya na ukasema katika kipindi cha Julai hadi Aprili, 2011, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vya dola lilikamata watuhumiwa 557 wenye kilo 529 za dawa za kulevya za viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, watuhumiwa hao wamechukuliwa hatua gani na hizo kilo 529 za dawa zimepelekwa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kubaini mtandao unaoingiza dawa ndani na nje. Kwa kweli Serikali bado haijakuwa tayari kuzuia na kupamba na uhalifu huu wa madawa ya kulevya. Kwa nini nasema hivyo, dawa zinapitishwa uwanja wa ndege wa Kimataifa kuna waangalizi wa kila aina pia kuna vyombo vya usalama pale, pia bandarini kuna usalama pia, hali kadhalika mipakani kuna vikosi vya usalama. Pia cha kushangaza dawa bado zinaingizwa nchini, hapa kuna tatizo, kuna baadhi ya watu wanaendesha maisha yao kwa ajili ya kazi hii ya madawa ya kulevya. Kwa nini hamna huruma na watoto wetu ambao ndio Taifa la kesho. Hapa tukitaka kuondoa hili ni lazima Serikali ichukue maamuzi magumu la sivyo Taifa litaangamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza yetu sio mazuri kwa hali ya sasa, wafungwa wengi magereza kidogo, hali ambayo inawafanya wafungwa kuishi kwa kubanana sana. Katika hali ya sasa sio nzuri kwani kuna maradhi mengi na wale ni binadamu. Naomba tuboreshe magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitika kuona wafungwa kidogo ila mahabusu ndio wengi inakuwaje hali hii? Kwa nini 19,544 nao pia kesi zao zisihukumiwe mapema na kwanini zinachukua muda mrefu kabla ya kifungo. Hawa ni binadamu.

Nikija kwa hao wafungwa wenyewe basi inasikitisha, baadhi ya Magereza kwa mfano, hapa Dodoma nimeona kwa macho yangu mfungwa anafanywa kama hana haki, kuna haki za kibinadamu jamani. Wanapakiwa katika kigari kidogo sana kama makumbi. Ikipinduka si ushaua? Kosa litakuwa sio uzembe wa dereva, ni uzembe wa Wizara kutokupeleka gari kubwa la kutosha. Naomba wafungwa nao wapewe haki ya kibinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika nyumba za kuishi: naishukuru Wizara kwa jitihada za kuboresha makazi ya askari lakini bado nyumba hizo hazitoshi na wengi wao bado wanaishi katika makazi ya raia na kwa misingi hiyo basi huwa hawafanyi kazi kwa ufanisi, pia hali hii ndio inapelekea kuvuja siri nyingi za askari polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maslahi. Inashangaza askari anaposafiri kikazi kwenda Mkoa mwingine hata nauli hapewi, achilia mbali pesa za kujikimu. Je, tunategemea askari huyu atafanya kazi yake kwa ufanisi au tunamtengenezea mazingira ya kuomba na kupokea rushwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie mishahara. Kwa kweli mishahara ya Polisi bado ni midogo kulingana na wakati na majukumu yao. Ndio maana rushwa haiondoki nchi hii, jamani kwa nini tusiwatengenezee mazingira mazuri ya mishahara yao ili nao basi wapate kufanya kazi zao kwa imani zaidi? Posho zao tunazowapa laki moja kwa mwezi mzima hazitoshi. Kulingana na wakati waongezewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendea kazi havitoshi kulingana na jiografia ya Tanzania. Utakuta matukio mengi na gari kwenye Wilaya ni moja, gari hilo moja na hata mafuta halina, je, tunategemea hapa usalama kwa wananchi utakuwepo kweli? Katika Wilaya kuna vituo mbalimbali na gari moja kwa kweli halitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kozi za askari. Kuna malalamiko ya Askari ambao walienda Depo kwa tatu hivi:-

- *Depot* ya sh. 70,000/=
- *Depot* ya sh. 60,000/=
- *Depot* ya sh. 40,000/=

Askari hawa ni wa Mikoa ya Zanzibar. Katika kupeleka malalamiko hayo wakaambiwa waende Makao Makuu. Walipofika tu wakaambiwa wasaini tu na kuondoka lakini pesa zao hadi leo hii hawajapewa. Nataka kujua askari hawa watapewa lini malimbikizo hayo? Pia wakirudi *depot* hawapewi pesa za kuanzia maisha na pia wana malimbikizo ya uhamisho hadi leo hawajapata. Naomba unifahamishe hawa Askari watalipwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maandamano ya Vyama vya Siasa. Kila Chama kina haki ya kufanya maandamano kwa mujibu wa sheria ya nchi ila kisivunje amani tu. Maandamano hayafanyi nchi hii kuwa maskini kwani maandamano ni uamsho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wako wa 11 kifungu 20, umesema maandamano yanatia umaskini kwani wananchi hawashiriki katika shughuli za maendeleo kwa sababu ya maandamano. Sio kweli kwani kilimo ni asubuhi na kazi nyingine wanafanya na Tanzania haitiwi umaskini kwa maandamano ila ni kwa ufisadi wa viongozi wa nchi ambao hawawapendi wananchi wao na mipango mibovu ya kila siku lakini haitoi matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na hongera kwa Watendaji wote wa Wizara hii. *In particular* Jeshi la Polisi ambalo linafanya kazi nzuri ya kulinda raia na mali zao. Polisi hawana nyumba nzuri na vitendea kazi. Serikali ilione hili kwa kuwapatia Polisi makazi na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizopo kwa wakati huu hasa *problems* za uhalifu wa *TEHAMA – Cyber crime* ni lazima Polisi wapatiwe fedha, mafunzo ili kukabiliana na uhalifu huu. Aidha, Polisi wa Majini wapewe fedha za kutosha na Boti ili kulinda bahari yetu, maziwa na kadhalika. Aidha, *Highways patrol* ziimarishwe ili kuzuia ujambazi na ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wanalalamika juu ya upandishwaji cheo hili nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhamiaji. Nchi yetu ina mipaka mingi, sasa kinachotakiwa ni kuimarisha mtandao wa *Clearance* ya kuingia nchini–*entry points* ili kuhakikisha kwamba wahalifu hawajiingizi nchini mwetu kinyemela. Pasi ni haki ya kila raia. Hivyo hilo nalo pia linatakiwa kufanyiwa kazi ili kila mwenye haki ya kupata pasi anapata baada ya kutimiza masharti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi, Wilayani Pangani kiko katika hali mbaya. Nyumba zao ni za zamani sana. Vyote hivi vinahitaji ukarabati na kuwajengea Polisi nyumba nzuri ili kuwapatia motisha na ni haki yao ili kufanya kazi kwenye mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitambulisho vya Taifa. Naipongeza Serikali kwa suala hili na hatua iliyofikiwa katika kutoa vitambulisho vya Taifa. Kazi hii iharakishwe ili wale walengwa kwa awamu ya kwanza wanapata vitambulisho hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa Bajeti 2011/2012.

**MHE. MUSSA HASSAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Naibu Waziri wake, aidha, Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa uwezo wao mkubwa kiutendaji aidha, uelewa wao kiutawala, hayo yanathibitishwa na uwasilishaji wa hotuba hii ya bajeti Bungeni hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi naomba nijielekeze katika maeneo matatu ambayo ningependelea kupata maelezo na msimamo wa Wizara kuhusiana na maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina utaratibu gani kumaliza madai ya pesa za kuanzia maisha ambazo kwa kawaida huwa wanapewa baada ya kumaliza mafunzo ya awali. Fedha hii inayodaiwa ni kwa waliomaliza miaka 2001, 2003 na wengine 2005 na baya zaidi askari wanadai kuwa walitilishwa saini hewa mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokana na sera nzuri za Wizara ya Mambo ya Ndani ya kuhakikisha kujenga vituo vya Polisi kwa kila Kata. Ningeomba Wizara iwe na mawasiliano ya karibu na Wizara ya Ardhi ili kuwa na utaratibu maalum wa kuelimisha jamii na wafanyakazi wa Wizara, sifa na maeneo ambayo yanaweza kujengwa vituo vya Polisi ikielewa kuwa vituo

vinaweza kuwa na milipuko mbali na athari hiyo pia kuwe na utaratibu maalum wa kueleza umuhimu wa kujenga vituo katika maeneo yanayoonekana kuwa kuna umuhimu wa kujengwa vituo hivyo mfano:-

- Maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa watu.

- Maeneo ambayo kuna taarifa za wahalifu na watu ambao wana sifa mbaya.

- Sehemu ambazo zina mali nyingi zikiwa za Serikali au za watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ichukue hatua za makusudi kuelimisha watu juu ya umuhimu wa vitambulisho vya Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirejee tena nawapongeza na naunga mkono hoja.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na malalamiko toka kwa Wabunge wa Mkoa wa Kagera kuhusu uvamizi wa wafugaji ambao ni wahamiaji haramu wanaoingia Mkoani humo wakiwa na makundi makubwa ya mifugo. Wahamiaji hawa hunyanyasa raia kwa kuwapiga na hata kuwaua. Kupitia vyombo vya habari Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alishakwenda kujionea hali ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kauli ya Waziri kuhusu adha hii, kwa kuwatamkia wananchi wa Wilaya ya Ngara, Biharamulo, Missenyi, Muleba na Karagwe hatima yao, uhai wao na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ameshatoa maelezo ya wahamiaji wafugaji kuondolewa na kunyang'anywa vibali vilivyotolewa na viongozi wa vijiji operasheni imeshaanza.

**MHE. PEREIRA AME SILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima. Pili, nikushukuru wewe kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii. Napenda kuupongeza uongozi wa Wizara kwa jitihada kubwa wanazofanya kutuhakikishia utulivu wetu na usalama wa mali zetu licha ya changamoto nyingi. Baada ya utangulizi huo, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kuhusu Vitambulisho vya Taifa. Wimbo wa vitambulisho vya Taifa umeshakuwa wa zamani na bila mafanikio. Pamoja na umuhimu wake, jambo hili limekuwa ni hadithi ya kila siku, ni lazima tutambue kwamba kuwa na vitambulisho katika karne hii, si jambo la kiulinzi bali ni jambo la kimaendeleo kutokana na umuhimu wake katika ukusanyaji wa kodi, elimu, afya na kadhalika na wakati umefika Watanzania au Wizara kuongeza kasi katika kutimiza azma hii ya kiulinzi, kiuchumi na kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kuhusu Rushwa. Kwa mara ya pili Jeshi la Polisi limetajwa miongoni mwa taasisi vinara katika kuomba na kupokea Rushwa. Ukweli huu si jambo zuri kwani athari zake ni kubwa kwa Taifa. Wahalifu sugu na wengine ambao wana nia mbaya hutumia udhaifu huu katika kutimiza malengo yao batili. Ni ukweli usiopingika kwamba kazi ya kugundua kuwa askari na hata makamanda wa Jeshi hili kuomba na kupokea rushwa katika maeneo mengi. Hata hivyo, bado haionekani kwamba jitihada ya kukomesha jambo hili zimefanikiwa. Kwa mfano, pamoja na mambo mengine, kuongezeka kwa ajali za barabarani ni matokeo dhahiri ya uozo wa Jeshi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe tahadhari kwamba kama jitihada za makusudi hazitochukuliwa tena, hivi sasa nchi yetu itakumbwa na balaa la njaa. Mbali na Serikali kupiga marufuku usafirishaji wa chakula umezidi kushika hali na hili linasababishwa na si kingine ila rushwa iliyotukuka na kukithiri. Pamoja kuwa rushwa ipo kila sekta, rushwa kwenye vyombo vya ulinzi na usalama athari zake huathiri sekta zilizosalia. Ni lazima tubadilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu mlundikano wa wafungwa Magerezani. Hali ya Magereza yetu inatisha. Magereza haya yamejaa mahabusu na wafungwa na ni tishio kubwa

katika kutimiza haki za binadamu. Moja ya chanzo cha mlundikano huu ni kuongezeka kwa idadi ya watu na kutumia miundombinu michache na ya zamani, kuongezeka kwa wahalifu kunakosababishwa, pamoja na mambo mengine, matumizi ya madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria ya wafungwa kutumika katika kazi za jamii. Kwa fikra yangu matumizi ya sheria hii ni jibu tosha na la haraka ili kutoa taswira nzuri kwa nchi na pia kuharakisha upatikanaji wa huduma za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujambazi Jimboni Igalula. Tunaomba Kituo cha Polisi Kata ya Goweko, Goweko stesheni. Goweko *Center*, Kijiji cha Goweko ndiyo Makao Makuu ya Biashara Jimboni Igalula. Mazao ya mahindi, mpunga, karanga, tumbaku na misitu, mbao, asali, nta yanapatikana kwa wingi. Mafundi Seremala pia ni wengi, hivyo fenicha hutengenezwa kwa wingi. Maduka, nyumba za wageni zimekuwa zikivamiwa na majambazi wenye silaha. Hawa majambazi huja kwa baiskeli wanapora na kuondoka mara kadhaa. Yamekuwepo matukio pia ya mauaji kwa kuteka mabasi mawili kutoka Goweko, Igalula, Tabora. Watu wawili walipoteza maisha, tunaomba kituo cha Polisi Goweko. Kituo cha jirani ni kilometa 30, mzunguko wa fedha ni mkubwa pale Goweko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujambazi jimboni Igagula. Majambazi huteka magari kati ya Tura na Manispaa ya Tabora. Barabara ya Itigi (Singida)-Tura-Tabora ina matukio mengi ya utekaji nyara wa magari ya aina zote. Tunaomba Kituo cha Polisi Tura ili *patrol* zifanyike. Pia kushirikiana na kituo cha Kigwa na Manispaa Tabora kuukabili ujambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kupongeza Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya Mambo ya Ndani. Askari Polisi wetu wanafanya kazi ngumu sana ya kuwalinda raia na mali zao. Japo yapo mapungufu kwa baadhi yao lakini ni rahisi kuwabaini na wachukuliwe hatua ili kulinda heshima ya Jeshi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makazi ya Askari Polisi. Makazi ya Askari wetu siyo mazuri sana hasa kwa Askari wadogo (wenye vyeo vya chini) waliobahatika kupata nyumba. Askari wengi wa nchi hii hawana nyumba za kuishi na hivyo kupanga nyumba za mitaani ambako huchanganyika na raia. Wameniomba Askari wa Mbarali kwa nyakati tofauti wakizungumza nami kwamba, wanaomba wajengewe nyumba ili wapate makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maslahi ya Jeshi la Polisi. Askari wa Jeshi la Polisi wanafanya kazi masaa ishirini na nne. Kutokana na hali hiyo, naomba wapewe posho maalum au waongezwe mishahara, kutokana na mazingira ya kazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mauaji ya raia wawili, Wilayani Mbarali yaliyofanywa na vyombo vya Dola. Itakumbukwa Wilayani Mbarali askari Polisi waliua mwananchi mmoja na mwingine kumtia ulemavu wa kudumu. Raia aliyekuwa alipigwa risasi kichwani jambo ambalo linaonesha wazi kuwa haikuwa bahati mbaya, ingekuwa bahati mbaya kwa maana kujihami nilitegemea angepigwa risasi mguuni angalau ingeleta maana. Familia ya marehemu leo inaishi kwa kuchangiwa tu na wananchi wanaoihurumia. Naomba kujua ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali kwa Askari aliyehusika na mauaji hayo? Je, Serikali haiwezi hata kutoa mkono wa pole kwa familia ya marehemu. Je, yule mwananchi aliyepata kilema cha kudumu Serikali inamsaidiaje ili aweze kumudu maisha yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio haya yote mawili yalitokea Kata ya Ubaruku, Kijiji cha Ubaruku katika tukio la kufungwa kwa barabara ya Igawa-Ubaruku Wilayani Mbarali, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani anajua. Naomba kupewa majibu ya kuridhisha wananchi wa Ubaruku (Mbarali) wamenituma, naomba nijulishwe ili niwe na majibu ya kuwajibu ndugu na jamaa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwananchi mwingine aliuawa na Askari wa Wanyama Pori (*TANAPA*), Kijiji cha Yala, Kata ya Ruhanga Wilayani Mbarali. Marehemu kabla ya mauti alikutwa nyumbani kwake na Askari wa *TANAPA* wakaunganisha mifugo yake na mifugo ambayo wanadai ilikuwa imeingia kwenye eneo la hifadhi, katika kukataa mifugo yake isichukuliwe, alipigwa risasi ya tumboni akafa akiwa anakimbizwa hospitali. Nilipewa taarifa na wananchi nikatoa taarifa Kituo cha Polisi Rujewa. Askari Polisi wakatoa taarifa yenye kuwalinda Askari wa Wanyama Pori, nikatoa taarifa kwa *RPC* Mbeya, walikamatwa wale Askari walioua wakawa chini ya Ulinzi, lakini baadaye waliachiwa. Nataka kujua kwa nini askari hawa hawajachukuliwa hatua na jamii ikajua kuwa Serikali yetu inawajali raia wake?

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali namna ya kukabiliana na madawa ya kulevya. Jeshi la Polisi kama inavyofanya kwa kuwashirikisha wananchi katika ulinzi shirikishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kupita Wizara hii idhibiti uingizaji wa madawa kwa kuwasaka waagizaji, wauzaji pia watumiaji kwa kuwa na vikundi rafiki shirikishi kwa watumiaji ambao wamezagaa kila mitaa, vituo vya daladala, vijiwe, kuwa na mpango maalum shirikishi kuendesha mikutano na watumiaji hao na itakuwa mbinu mbadala ya jeshi kuwabana wauzaji kupitia watumiaji hao, pia kubaini wasafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa katika Jeshi la Polisi, rushwa kubwa na ndogo ni kilio kikubwa kwa wananchi ambapo, mwananchi yeyote wa kipato cha chini anapokamatwa na Polisi ni lazima atoe pesa ndipo aachiwe huru, hadi kuna msemo unasema: "Kuingia bure kutoka na hela." Ndivyo ilivyozoeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa ni kero, hivyo Serikali iweke mazingira mazuri ya kazi kwa askari hao kwa kuboresha kipato chao, vitendea kazi, kama karatasi, peni, wino, mafaili, usafiri, ofisi na makazi yao. Pia upandishwaji wa madaraja kwa maaskari hao, kumwacha askari anatumikia Jeshi la Polisi miaka kumi na kuendelea bila kupandishwa daraja, inapelekea askari hao kukata tamaa na kujihusisha na vitendo viovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha miundombinu ni jambo muhimu sana. Mfano, katika Wilaya ya Kilombero katika vituo vingi vya Polisi havina vitendea kazi, ofisi, nyumba za kuishi na viko gizani bila umeme. Mfano halisi, ni Kituo cha Polisi Mbingu ambacho kinahudumia Kata ya Mofu, Idete na Mbingu yenyewe. Pamoja na kuwa na miundombinu mibovu sana ya barabara na eneo kubwa la kazi, lakini hakina ofisi, maaskari hawana nyumba za kuishi, wako kwenye godauni, hawana usafiri hata wa baiskeli, matokeo yake huazima pikipiki kwa raia ili wafuatilie matukio ni mwezi Mei 2011, walikamata bunduki na risasi kadhaa kwa kutumia usafiri wa kuomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatari kwa usalama wa raia na mali zao na usalama wa askari hao. Wanateswa na Serikali yao na wao hawawezi kugoma kutokana na maadili yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, umaskini wa Watanzania haujaletwa na maandamano ya amani, bali umeletwa na unaendelezwa na ufisadi na uongozi usiowajibika. Haki itendeke ili kudumisha amani.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Kamanda wa Polisi *IGP* Said Mwema ambapo pamoja na mapungufu mbalimbali bado nimejitahidi kuonesha tofauti ukilinganisha na watangulizi wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchungu mkubwa napenda kufikisha kwako kilio chetu wakazi wa Mkoa wa Kigoma. Huu ndio Mkoa unaoongoza kwa kusumbuliwa na Idara ya uhamiaji kwa hoja za uraia. Askari wa Uhamiaji wanaendesha zoezi la kusumbua wakazi hasa wa maeneo ya ukanda wa Kusini wa Ziwa Tanganyika, Kata za Simbo, Ilagala, Kalya, Sunuka, Sigunga na Buhingu. Huku kinachofanywa na askari hawa ni manyanyaso na hasa kwa raia wasio na fedha za kuhonga askari hawa. Hili ni tatizo sugu sana. Najiuliza hivi sisi Kigoma sio Tanzania? Kuna mikoa mingi ipo mpakani, kwa nini usumbufu wote utukabili Kigoma tu? Kwa nini hatusikii watu Kagera, Kilimanjaro, Mbeya, Arusha, Mara ambao pamoja na kuwa mpakani hawasumbuliwi kiasi hiki?

Nchi hii katika eneo la uhamiaji linatekeleza majukumu yake kibaguzi na watu wa Kigoma tunabaguliwa na tunadhalilishwa utadhani sio raia wa nchi hii. Naomba Mheshimiwa Waziri ulipe uzito jambo hili, tembelea ukanda huu, Maofisa wa Uhamiaji Kigoma ni mafisadi wasiotekeleza majukumu yao, sina imani nao hata chembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kanda Maalum. Napenda Wizara itambue kuwa Mkoa wa Kigoma ndio Mkoa unaopakana na nchi ambazo usalama wake ni mdogo kama Burundi, Rwanda na Congo. Mkoa huu una mpaka mrefu kuliko mpaka wowote wa Tanzania. Nimewahi kuzungumza na Waziri Mkuu kuhusu kuipata uzito wa kipekee Mkoa wa Kigoma. Tangu Februari, 2011 tulipozungumza na Waziri Mkuu na akatoa ahadi ya kulipa uzito suala hilo mpaka leo na hata Bajeti hii sioni tofauti ya Mkoa wa Kigoma na mingine. Naomba Mheshimiwa Waziri atazame jambo hili katika uhalisia. Huu ni Mkoa wenye kila sababu ya kuwa na hadhi ya Kanda Maalum. Kama hilo haliwezekana basi Wizara ihakikishe ukanda wote wa Kata za Kusini, unakuwa na Vituo vya Polisi kwa maana ya Kata za Sunuka, Sigunga, Buhingu, Kalya na Igalula. Hili ni eneo muhimu sana kwani ni mpaka wa wazi na kuna matukio mengi ya ujambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Nguruka. Napenda kukujulisha kuwa Kituo cha Polisi cha Tarafa kubwa kuliko zote ndani ya Wilaya ya Kigoma, Tarafa ya Nguruka. Kituo chake ni kibovu na jengo lililopo ni kama nyumba ya mganga wa kienyeji. Naomba Wizara ione aibu. Hiki sio kituo cha Polisi kabisa, ni jengo duni sana, mahabusu wanawekwa chumba kidogo ndani ya jengo duni utadhani kuku. Naomba sana jengo la Polisi, katika eneo hili kwani ni eneo muhimu, hiki ni kituo kinachosimamia Kata za Nguruka, Itebula, Mganza na Mtego. Naomba sana kituo hiki kijengwe kwani pale hakuna jengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa Gereza la Ilagala na wananchi. Naomba Mheshimiwa Waziri aongeze msukumo katika jambo hili. Natambua jitihada zako katika kufikia muafaka lakini bado nasisitiza ili tufikie hitimisho. Tatizo hapa ni kwamba gereza lilijengwa wakati sensa ya watu ikiwa ndogo sana. Leo eneo la wananchi halitoshi, tufike mahali tupunguze eneo la mashamba ya gereza hili ili kiasi liweze kupewa wanakijiji. Naomba sana hili kama njia ya kujenga mahusiano baina ya jeshi na raia. Mkuu wa Gereza hili ni mwelewa na anaweza kusaidia sana mchakato mzima wa kukaa salama katika eneo hili. Naomba tuzidi kushirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la upandishwaji wa vyeo. Naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili, kuna tuhuma za Jeshi la Polisi kutokuwa na utaratibu mzuri wa kupandishwa vyeo. Kuna polisi wanashiriki matukio makubwa ya kimapambano lakini Jeshi la Polisi halioni umuhimu wa kuwaongeza vyeo, hii inakatisha tamaa. Nashauri fuatilieni kwa karibu, nimepata malalamiko toka Polisi Kituo cha Nguruka walioshiriki zaidi ya matukio matatu ya kukabiliana na majambazi wenye silaha lakini bado hawapandishwi cheo. Nashauri mambo haya yatazamwe ili kujenga moyo kwa wapiganaji hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nahitimisha kwa kurejea hoja mama ya sisi watu wa Kigoma, tumechoka na maofisa Uhamiaji wanaoendesha unyanyasaji kwa raia wa Kigoma. Kigoma ni Tanzania.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la maslahi ya Askari Polisi, kwa kipindi kirefu Askari Polisi wamekuwa wakidai malipo yao mbalimbali katika Jeshi la Polisi. Aidha, maslahi hayo ni ya uhamisho, safari za masomoni pamoja na malipo ya viinua mgongo na kadhalika. Hivyo, naishauri Wizara kuunda *task force* maalum ya kupita kila Kituo cha Polisi kuorodhesha askari ambao wanadai haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwenda kozi kwa askari hao, nimebaini kuwa kuna upendeleo wa kuwapeleka *course* (mafunzoni) kwa Askari Polisi, kwa kila mwaka, kuna baadhi ya Askari tena vijana wa siku nyingi wako vituoni hawajapelekwa mafunzoni wala hakuna sababu za msingi, labda kuna ubaguzi na wenye wakubwa zao ndio wanaopewa kipaumbele. Hivyo naishauri Wizara itoe ufafanuzi wa suala hili na lisimamie ili kuona haki inatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la makazi nyumba za askari, katika Kituo cha Bububu kuna jengo ambalo limeanza kujengwa tokea zamani lakini hadi hii leo jengo hilo

halijamalizwa kujengwa, hivyo kuwapa tabu askari wa kituo hicho kwenda na kurudi mjini kwa nauli zao binafsi. Hivyo, katika kutatua suala hilo naiomba Wizara kuharakisha ujenzi wa majengo hayo. Vile vile Kituo cha Bububu kimeshakuwa chakavu yaani hata kupakwa rangi huwa ngumu. Hivyo, nashauri Wizara kutekeleza masuala haya madogo madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mavazi kwa askari. Hapo zamani Jeshi la Polisi, lilikuwa na utaratibu maalum wa kukagua mavazi yote ya askari ikiwemo suruali, shati, viatu na vifaa vingine. Aidha, kutokuwepo au kuondolewa kwa utaratibu huo, Askari wetu wamekuwa wachafu na sare mara nyingine zinakuwa mbovu, hususan viatu na hasa Askari wa Trafiki kwani nguo zao ni nyeupe na ndio mwanzo wa mgogoro huo. Hivyo, naishauri Wizara kurejesha utaratibu huo angalau mwezi mara moja kila Kituo inapigwa foleni kwa ajili ya ukaguzi. Nahisi askari akiwa nadhifu anaheshimika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la vifaa vya kufanyia kazi katika Jeshi la Polisi la Zanzibar. Nimebaini kuwa utendaji wa Polisi, Zanzibar umekuwa mgumu kwa kukosa nyenzo za kufanyia kazi. Nyenzo hizo ninazoziomba ni magari ya vituoni, pikipiki hasa kwa trafiki, magari ya *Patrol* hasa kwa nyakati za usiku. Hivyo, nashauri Wizara kutoa msukumo maalum wa kuwapatia vifaa hivyo kwa Jeshi la Polisi, Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la utendaji kazi katika Jeshi hili la Ulinzi na Usalama wa raia. Hivyo, ili kweli kazi hii ifanyike ni lazima Polisi atimize wajibu wake, sasa utaratibu wa kumweka askari katika kituo kwa zaidi ya miaka mitano, basi, utendaji wa askari huyo unashuka tu, kwani tayari anakuwa mwenyeji. Hivyo, naishauri Wizara kuandaa utaratibu maalum wa *Rotation* kwa askari wote wahamishiwe huku na kule, ili kuboresha utendaji kazi.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya ya kutosha na naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa kuandaa bajeti yao na hatimaye leo tunaweza kujadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo naomba sana Wizara hii iwaangalie kwa huruma sana Askari Polisi, iwajali kwa usafiri, nyumba na walipwe posho zao kwa wakati muafaka. Nasema hivyo kwa sababu haipendezi kabisa kuona askari wanaishi uraiani nyumba za kupanga. Askari hawa inawalazimu kupanga nyuma ambazo kodi yake ni ndogo ili mradi wapate sehemu za kujihifadhi. Hii inapunguza heshima kwa askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usafiri katika Vituo vya Polisi. Vituo vyetu vingi havina usafiri, hili linafanya kuwa na utendaji mbovu kwani tukio linapotokea sehemu mbali askari hawa hawawezi kufika kwa muda muafaka na kama watafika mara nyingi ni kwa kutafuta usafiri kwa raia na mafuta ya kuomba. Pia kwa hali hii tunategemea nini kwa askari wetu kama siyo kuomba rushwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kuhusu suala la wakimbizi, ni kwa nini nchi yetu tumekuwa na huruma sana. Sioni sababu ya hawa watu kuwapa uraia wa Tanzania hata kama wameomba ni vyema warudi makwao. Mbona sisi Watanzania tunahangaika kupata uraia katika nchi zingine? Naiomba Serikali ilitafakari kwa kina suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kusema naunga mkono hoja lakini Serikali iangalie haya kwa makini. Ahsante kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuchangia Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa kuwa Zanzibar ni Jamhuri ya Muungano na Wizara hii ipo katika mambo ya Muungano. Kinachonikera ni kucheleweshwa kutatuliwa kero za Muungano na hizi zinasababisha Wazanzibari wengi kuuchukia Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Polisi Ziwani kimesahaulika. Kimekuwa hakina hadhi kutokana na majengo yake kuwa chakavu na majengo yale yalikuwa yakitumiwa na makamishna wa mwanzo waliopindua Zanzibar na mpaka sasa hivi majengo yale yameharibika na

hayajafanyiwa ukarabati wa kutosha mpaka leo na ukiangalia humo ndani ya Chuo cha Polisi Ziwani majengo wanayoishi mapolisi na familia zao hayana hadhi, yanavuja na huduma za jamii pia hazitoshelezi, na ukiangalia pia Hospitali iliyopo kwenye chuo hicho cha mafunzo haijatengewa fungu la kutosha. Hospitali hii haitibu mapolisi peke yao. Wananchi wa Jimbo la Jang'ombe na Majimbo mengine yaliyopo jirani na chuo hicho cha Polisi Ziwani wamekuwa wakifika katika hospitali hiyo kupatiwa huduma za afya. Je, Serikali na Wizara haioni sasa kuna umuhimu wa kutenga fungu la kutosha la bajeti kushughulikia matatizo ya muda mrefu ya chuo hicho cha Polisi Ziwani Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la uchakavu wa majengo si kwa Chuo cha Polisi, Ziwani tu bali hata majengo mengi ya Zanzibar na vituo vingi vya Polisi, Zanzibar ni chakavu, havina vitendea kazi kwa mfano, Kituo cha Polisi Mahonda, hakina vitendea kazi na majengo yake pia ni chakavu sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali na Wizara ihakikishe inatenga Bajeti ya kutosha kuhusu kurekebisha majengo ya vituo hivi kwa sababu ndiyo kero zenyewe za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ajira za Polisi zinazotolewa kwa upande wa Zanzibar. Hii imekuwa kero kwa visiwa vyote viwili vya Zanzibar yaani Unguja na Pemba. Nafasi hizi hazitolewi kwa uwiano, nafasi hizi zimekuwa zikitolewa kwa umaarufu wa kujuana na umaarufu wa itikadi za kisiasa. Vijana wengi wa Zanzibar wamekuwa wakilalamikia jambo hili kwa kuwa limekuwa ni kero. Na hata vijana wengine wanaobahatika kupata nafasi hizi Zanzibar wamekuwa wakipimwa afya Zanzibar na wakishafika Tanzania Bara pia wanapimwa afya na wakishapimwa wanarudishwa Zanzibar na nafasi hizo hawazipati tena. Nafasi hizo zinachukuliwa na wengine hatujui ni akina nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atakapokuja kutoa majumuisho ya Wizara hii anipe majibu ya kunitosheleza kama siyo hivyo, sitaunga mkono hoja. Pia nilikuwa naiomba Serikali na Wizara kuchunguza kwa makini nafasi hizi za ajira ya polisi zinazotolewa kwa upande wa Zanzibar zinazopitia kwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Nafasi hizi zimekuwa zikitolewa kwa upendeleo kwa kuwapa jamaa zao, marafiki zao, watoto wao na hata kuingiza itikadi ya vyama vya siasa, na vijana wengi wa vijijini ambao hawana umaarufu Serikalini wamekuwa hawazipati nafasi hizi na hata vijana wanaopenda Vyama vya Upinzani imekuwa pia kupata ajira hizi ni ndoto. Kwa hiyo, naiomba Serikali na Wizara imekubali mfumo wa vyama vingi na ajira za Serikali pia zitolewe bila upendeleo wa itikadi za siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la wastaafu wa Zanzibar. Wastaafu hawa wamekuwa wakisumbuliwa kuhusu mafao yao ya ustaafu. Suala hili naomba Serikali na Wizara iangalie kwa makini, wastaafu hawa mapolisi wengi wanastaafu wamekuwa wakisumbuliwa kufuata mafao yao Tanzania Bara. Naiomba Serikali na Wizara ianzishe utaratibu wa kuwapelekea mapolisi hawa wanaostaafu pensheni zao kwenye mikoa yao wanayotoka ili kuepusha usumbufu na hii itasaidia kumpunguzia gharama za usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la maaskari kufanya kazi katika mazingira magumu. Maaskari hawa wanapofanya kazi katika mazingira magumu na mishahara kuwa midogo ndiyo maana wanajiingiza katika vitendo vya kupokea rushwa na kutotenda haki kwa wananchi wetu wanapokamatwa na makosa mbalimbali. Kwa hiyo, naishauri Serikali na Wizara kuhakikisha maaskari hawa wanapewa mishahara ya kutosha na makazi yao kuwa mazuri na kupata huduma nzuri za kijamii. Hii itasaidia maaskari hawa kufanya kazi ipasavyo na wataipenda kazi yao na kutojiingiza katika vitendo vya kupokea rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la wafungwa magerezani. Wafungwa waliofungwa kifungo cha muda mrefu wamekuwa wakiteseka sana, hususan akinamama wanaokuwa magerezani. Akinamama wengi wamekuwa hawapati huduma za kijamii katika magereza, mavazi yao hayakidhi mahitaji yao, wanapokuwa katika siku zao za hedhi hawapatiwi hata pedi za kuweza kujihifadhi. Naiomba Serikali na Wizara iangalie suala hili kwa makini nao waweze kuwa kama binadamu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali na Wizara kuhusu wafungwa wa muda mrefu akinababa na akinamama ambao wapo kwenye ndoa. Ili wapate kukutana kama wanandoa ili

kuepusha maradhi kama UKIMWI na kama sheria hii ya wanandoa kukutana haipo basi Serikali na Wizara iangalie kwa makini ili kama binadamu wengine ambao sio wafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja hii, endapo haya yote niliyoyachangia hapo juu kama nitapatiwa majibu ya kujitosheleza.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanywa na Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote. Pia naipongeza Wizara kwa uendelezaji wa Ulinzi Shirikishi. Wizara iongeze vitendea kazi kwa Idara ya usalama wa raia, barabarani, zimamoto na Magereza. Pamoja na vitendea kazi hali ya makazi ya askari hawa ni mbaya kwa asilimia kubwa sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri anipe jibu wamepanga vipi kwa kuongeza nyumba (mradi) zinazojengwa na pia ni Wilaya zipi zitakazofuata kwa ujenzi huo, kwani askari hao na wao wana haki ya kuishi mahali pazuri na Ofisi, hii itapunguza mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Pwani ni kiungo cha Mikoa yote ya Tanzania Bara. Hivyo basi, ni vyema wakapatiwa magari kwa ajili ya Doria, *Radio Calls* na hata pikipiki, kwani zitawawezesha kupata mawasiliano ya karibu sana. Naomba nielezwe watatupatia gari ngapi kwa Wilaya za Bagamoyo, Kibaha Mjini na Vijijini, Kisarawe, Mkuranga, Mafia na Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mafia ni kisiwa na usafiri wake ni ama ndege au bahari na hata sehemu ya ajira za wananchi wa kule ni uvuvi. Hivi sasa kumezuka wizi au ujambazi kwenye maboti, wanatega na kuwaibia. Tunaomba ulinzi (doria) kwa boti zinazosafiri toka Nyamisati-Mafia, Kilwa-Mafia, taarifa hizi zilitolewa kwa Polisi, Wilaya ya Mafia. Naomba jibu ni vipi au lini tutapatiwa Askari wa kusindikiza abiria kama inavyokuwa kwenye mabasi yanayopita njia ambazo zina ujambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika tunaomba ujenzi wa vituo vya Polisi, Wilaya kwa Wilaya zote za Mkoa wa Pwani ambazo hazina ofisi rasmi. Ni lini ujenzi utaanza?

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuendelea kulinda raia wa Tanzania na mali zao kwa kupitia Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kujali maslahi ya Polisi hasa ujenzi wa makazi kwa ajili ya polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Jeshi la Polisi liendelee na uhamasishaji wa polisi jamii. Zoezi hili ni zuri linafundisha raia wa Tanzania mambo mengi wasiyoyajua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi nchini kote, Serikali iandae utaratibu jeshi likishirikiana na Halmashauri za Wilaya wawe na *breakdown standby* kuondoa magari yote yaliyosimama barabarani (*Highways)* ili kuondoa ajali zinazoweza kutokea na wenye magari watozwe gharama za kuondoa magari hayo. Hili litasaidia sana kupunguza ajali zinazotokea barabarani hasa magari yaliyosimama ambayo hayana *parking lights* nyakati za usiku. Nashauri Serikali waendesha pikipiki wote nchini wapewe mafunzo na kila mwendeshaji aende *VETA* apate cheti kabla hajaruhusiwa kuendesha pikipiki, na wavae fulana za *reflectors* ili watambuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, magereza mengi nchini ni madogo kulingana na idadi ya wafungwa na mahabusu. Nashauri Serikali iandae mpango wa kuhamisha wafungwa kutoka magereza yenye msongamano wahamishiwe magereza ya kilimo kama Urambo – Tabora na Kwitanga – Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali, magereza ya watoto, yawe na mitaala ya shule za msingi na sekondari, vema watoto hawa wakitoka gerezani wawe wana elimu ya msingi, sekondari au chuo kikuu, wakitoka bila elimu itawa-*frustrate* sana na itachochea kuendelea kuwa mhalifu. Akitoka akiwa na elimu atatamani kuendelea kuwa raia mwema. Kwa waliomaliza kidato cha sita, waelekezwe kujiunga na masomo ya chuo kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vema pia magerezani viongozi wa dini waruhusiwe kutoa mafunzo ya dini kwa njia yoyote ile isiyoingilia taratibu za gereza, mfano, anaweza kuwa ofisini kwa kamishna lakini akafundisha kwa *loudspeakers.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya dini yanajenga maadili na hofu ya Mungu kwa mwanadamu. Inawezekana kabisa malezi ya mfungwa huyu, mafunzo ya dini hayakupata nafasi maishani mwake na hivyo kujiingiza katika tabia ya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda muafaka wakimbizi 37,000 wa Burundi walioko katika kambi ya Mtabila warudi kwao. Burundi hakuna vita, waliorudi kwao kwa hiari hawajarudi kuashiria amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilifunga shule za msingi na sekondari. Wakimbizi walipeleka watoto wao kusoma Burundi lakini wazazi wao bado wanang'ang'ania kuishi Tanzania. Kuna haya Serikali itoe kauli (watake warudi kwao).

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kusitisha zoezi la kuwatawanya wakimbizi 164 waliopewa uraia. Nashauri Serikali iwatake Umoja wa Mataifa (*UNHCR*) watoe hela ya kuwatawanya, lakini pia kule watakapokwenda kuishi wananchi waulizwe wakubali ujio wa wakimbizi hao. Nashauri Serikali ilifanye hili kwa makini hasa kwa sababu raia wa Tanzania wanaogopa tabia na desturi za Warundi za kikabila.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Zimamoto linafaa Serikali iliongezee fungu ili liende na wakati. Yapo matukio mengi ya moto yametokea mahali kama Dar es Salaam na jeshi hili limeshindwa kudhibiti kwa kukosa vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko haja utaratibu ufanywe na Serikali ili Zimamoto iweze kupita katika nyumba za wakazi mijini kuhakikisha wakazi wanajua jinsi ya kutumia vizima moto kama *fire extinguishers* na mchanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa jitihada inazozifanya kuandaa vitambulisho vya Taifa. Hakika ni wakati wa kuwajua wakwepa kodi. Nashauri Serikali kuwa makini wakati wa kuandikisha raia ili wasijepewa vitambulisho watu wabaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikoa ya mipakani mwa Tanzania hasa mikoa ya magharibi mfano Kigoma, Tabora na Kagera ina watu wengi wanaoingia kutoka nchi ya jirani ya Burundi na Kongo na wageni wana wenyeji ambao ni wa mikoa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashauri Serikali ijenge Kituo cha Polisi eneo la njia panda Himo ,Mkoani Kilimanjaro katika Wilaya ya Moshi Vijijini. Eneo hili lina mizani na magari ni mengi sana masaa 24 kwa sababu magari mengine yanakwenda Arusha, Nairobi, Holili na kadhalika, yumkini mizani inakuwa na fedha nyingi kila siku. Ni hali ya hatari kama kutakuwa hakuna Kituo cha Polisi na hata idadi ya watu pale ni zaidi ya wakazi laki tatu (300,000).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha pamoja na Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongoza Wizara kwa nafasi ya Waziri na Naibu Waziri. Nimeridhika sana na ushirikiano unaotupa na usikivu wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa dhati Inspekta Jenerali wa Polisi (*IGP*) Said Mwema, Makamishna na Makamanda na askari wote kwa ubunifu wao wa mipango na mikakati inayoendelea kutekelezwa na hivyo kuboresha hali ya usalama wa raia na mali zao nchini. Nashauri kuwa ubunifu wa namna ya kuongeza motisha ya askari ufanyike ili watekeleze majukumu yao kwa uaminifu na uadilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upelelezi wa tuhuma au kesi, mwaka 2009 ulitokea wizi kwenye *SACCOS* ya wanawake Wilayani Arumeru. Wizi huo uliripotiwa Polisi Wilaya, Kituo cha Usa. Mwaka

2010 wananchi walitaka kukiadhibu Chama cha Mapinduzi kupitia uchaguzi mkuu kwa madai kuwa walioiba fedha hizo kiasi cha Sh. 250,000,000/= ni viongozi wa UWT ambao ndio waliokuwa wajumbe wa Bodi ya *SACCOS* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Januari, 2011 nilikuteua na *OCD* wa Arumeru ofisini kwangu na kumshauri kuwa watuhumiwa wa wizi huo wafikishwe Mahakamani ili haki itendeke na kuondoa lawama kwa Serikali kuwa inalinda wahalifu dhidi ya wananchi. Hadi leo hakuna aliyeletwa Mahakamani kuhusiana na tuhuma hizo. Nashauri kuwa uongozi wa Polisi Makao Makuu (*DCI*) achukue jukumu la kukamilisha upelelezi wa tuhuma hizo na kukabidhi kwa *DPP* ili wahusika wafikishwe Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya Polisi, Wilaya ya Arumeru. Malalamiko dhidi ya askari na maafisa wa Polisi Wilayani Arumeru kuwa sehemu ya uhalifu yameongezeka sana. Nashauri kuwa askari na maafisa hao akiwemo *OCD* wahamishwe. Askari wa Vituo vya Namanga, Longido, Oldonyosambu na Ngaramtoni ambavyo ndio milango ya kupitishia wahamiaji haramu, dawa za kulevya na magendo wasikae zaidi ya miaka miwili. Aidha *OCS* wa Ngaramtoni alihusika kusimamia ubomoaji wa shule eneo la Lengijave na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa dhidi yake ingawa taarifa ilitolewa kwa uongozi wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusogeza huduma za karibu na wananchi. Wilaya ya Arumeru ni kubwa sana na ina wakazi wengi. Makao Makuu ya Polisi, Wilaya yako Usa ambapo ni pembeni sana kwani iko Mashariki na hivyo kufanya wananchi wanaoishi upande wa Magharibi mfano Kisongo, Oljoro, Ihemi ya Simba na nyingine zilizo pembezoni kuingia gharama kubwa sana kupata huduma za polisi. Hii imekuwa kero kwani yule asiye na uwezo kusafiri hadi Usa hapati huduma. Ili kusogeza huduma karibu na wananchi nashauri na kuisihi Serikali igawe Wilaya hiyo kipolisi kwa kufuata mipaka ya Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza, nawapongeza maafisa na askari wa Jeshi la Magereza nchini chini ya uongozi wa Kamishna Mkuu, Ndugu Augustino Nanyalo kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuboresha mazingira na huduma za magereza. Sijaridhika na kiasi cha fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mfano, mwaka 2011/2012 wametengewa Sh. 200,000,000/=, kiasi ambacho kitatosha magari mawili tu. Hali ya mabweni ya wafungwa hairidhishi. Msongamano ni mkubwa sana. Nashauri kuwa Serikali iandae mpango kamambe wa kupanua na kuboresha magereza yetu ili wanaoishi huko wasione kuwa wametupwa. Utaratibu wa kutumia mabasi na magari mengine ya abiria kupeleka watuhumiwa Mahakamani kwenye mikoa mingine kama ilivyo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uhamiaji. Kwa muda mrefu yamekuwepo maombi ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi kuwa uraia wa nchi mbili uruhusiwe. Naunga mkono maombi haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitambulisho vya Kitaifa. Nawapongeza viongozi wa *NIDA* kwa kazi nzuri wanayofanya kukamilisha zoezi la kuanzisha vitambulisho vya Kitaifa. Nashauri kuwa utaratibu ufanyike kuhusisha wadau hususan *TCRA* kukamilisha taratibu za kuwa na anwani ya makazi kabla ya kutoa vitambulisho hivyo. Pia mambo yatakayojumuishwa kwenye vitambulisho yatangazwe ili wananchi wachangie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata maelezo, kwa nini Serikali inapeleka nje kutengeneza vitambulisho nchini Malasya, badala ya kutengeneza hapa nchini? *TRA* wamefanikiwa kutengeneza leseni za madereva kwa mfumo wa kisasa *(electronic)* hapa hapa nchini. Ni kwanini Serikali haikutaka kutumia mfumo huu uliopo hapa nchini? Tayari vile vile wenzetu wa Zanzibar wamefanikiwa kutengeneza vitambulisho vya Taifa, ni kwa nini Serikali haikutaka kutumia uzoefu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na badala yake inapeleka nchi za nje na kuliingizia Taifa gharama kubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, *dependant pass* sasa hivi imepandishwa sana bei kutoka dola 270 hadi 500. Ieleweke kwamba wanaolipa fedha hii ni Watanzania wenzetu, kwa mfano, wako vijana wanaotoka masomoni Ulaya na wanakuja na familia zao za wanawake wa nchi hizo ambazo wamesoma. Huyu kijana hata kazi anakuwa hajapata, hivi atapata wapi hizi dola 500? Hii bei kupanda inawanyanyasa Watanzania wenzetu na wengine ndoa zao zinavunjika kutokana na kukosa fedha hizo na hivyo kulazimika kuishi nchi tofauti. Tunaomba Serikali ipunguze bei hii, ni kubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali ianze kutoa *Permanent Resident Permit* kwa wageni hasa wale walioolewa au kuolewa na Watanzania badala ya kupewa *Dependent Pass Resident Permit* itamwezesha mhusika kupata kazi na hivyo kuchangia katika familia badala ya mmoja wao tu kuhangaikia familia. Serikali inaweza kuweka utaratibu ili wasipate kazi kwenye maeneo nyeti ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupata fursa ya kuchangia jana, kulikuwa na mambo mengine ya msingi ambayo kwa ufinyu wa muda sikuweza kupata nafasi ya kuyazungumza. Kuna malalamiko ambayo askari wetu wamekuwa wakilalamika, pamoja na wingi wa malalamiko na mengi pia Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameyaelezea, mimi nimeona hili moja niliongezee kwa maandishi. Kwa kweli namwomba sana Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ya kina ili askari wetu wapate kuridhika, vinginevyo nitashika kifungu cha mshahara wake na shilingi nitaondoka nayo moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hilo ni kwamba Jeshi la Polisi wamekuwa wakikatwa Sh. 5,000/= kila mwezi kwa kuambiwa wanachangia pesa hizo kwa ajili ya mfuko wa maafa, ambazo zinahifadhiwa ili kusaidiana katika shida anapotokea askari akafiwa na baba yake, mama yake ama mtoto, atapewa Sh.1,000,000/=. Mwanzoni Mfuko huu ulipoanzishwa ulikuwa na msaada mkubwa sana. Lakini baadaye wanapunguziwa, badala yake, wanaopata maafa wanaanza kupewa Sh. 500,000/= na sasa imekuwa hata hizo Sh. 500,000/= kupatikana ni tatizo wakati makato ya Sh. 5000/= kila mwezi yanaendelea kukatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo ya kina, kumetokea nini katika mfuko huu? Kwa kuwa makato yanaendelea hadi sasa, kuna Shilingi ngapi katika mfuko huu? Kama malengo ya Mfuko huu yalikuwa mazuri: Je, Serikali itasaidia vipi? Serikali inasaidiaje askari wanapopata maafa haya ya kufiwa na wazazi wao na watoto? Kwa kuwa kuanzishwa kwa mfuko huu, kumeashiria wazi kabisa kwamba kuna tatizo kubwa ndiyo maana pamoja kuwa na mishahara midogo sana wakaona ni bora wakubali kujinyima, wachangie mfuko huo ili wasije kuadhirika wakipatwa na maafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali sana, naomba nipata maelezo ya kina.

**MHE. AHMED J. NGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha zaidi utendaji wa Jeshi letu la Polisi, napendekeza kuwa utaratibu wa sasa wa Polisi, ngazi za cnihi ambao hukatwa Sh. 5,000/= kila mwezi ambapo hata katika hutoba ya upinzani imelionyesha hili, utaratibu huo uondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limelegeza msimamo wake katika kuendeleza ushirikiano wa Jeshi la *Interpol*, Shirikisho la Polisi la nchi za Afrika Mashariki na pembe za Afrika kinyume na ilivyoelezwa na hotuba ya bajeti ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika ukurasa wa 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Jeshi la Polisi haliwezi kumaliza vitendo vya uhalifu na pia linahitaji wananchi waliunge mkono, inapaswa kwa Jeshi la Polisi lenyewe lijisogezwe karibu na wananchi na kuwafanya wananchi kuwa marafiki badala ya kutumia vitisho na ubabe kwa wananchi ambao ni sehemu kubwa katika kuhakikisha usalama wa Taifa letu. Sidhani kwamba Jeshi la Polisi pekee kama linaweza kumaliza suala la uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, limekuwa jambo la kawaida kwa Ajira za Jeshi la Polisi kuangalia kwa mtazamo mdogo, sehemu ya pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yaani Zanzibar na kutoa fursa hafifu kwa Wanzanzibar. Hii inapelekea tofauti kati ya Zanzibar na Tanzania Bara iongezeke na mwisho kutapelekea hili liingie katika kero za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Jeshi la Polisi linakusudia kufanya kazi zake kwa uangalifu zaidi na ufanisi, ni lazima jeshi hili likabiliane na mabadiliko ya sayansi na teknolojia ya dunia ya sasa, mitambo ya kisasa, utaalamu yakinifu na taaluma endelevu inaweza kusaidia kufanya kazi zake kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa na wimbi kubwa la vyombo takriban 3,795 ambavyo vimesajiliwa na hii inapelekea kupoteza takwimu sahihi za mapato na mazao ya uvuvi na vyombo hivi kuendelea ku–*operate,* vinasababisha utoroshaji wa mazao ya uvuvi na hata uharamia. Unaoendelea katika mwambao wa Ziwa Tanganyika ambapo wavuvi wanauawa na vyombo vyao kuchukuliwa: Je, ni lini vyombo hivi vitadhibitiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa na Makampuni mengi ya Ulinzi ambayo ni *Private:* Je, ni Sheria zipi zinaruhusu uanzishwaji huo? Je, wanakula kiapo? Wakitaka kuacha kazi au kuanza kazi, kuna udahili wowote unaofanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa na wimbi kubwa la makosa dhidi ya maadili ya jamii katika ukahaba, usagaji, na ushoga, vitendo hivi vinaendelea na mashoga tunawaona: Je, Serikali imechukua jitihada gani kudhibiti hali hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa na wimbi kubwa la makosa ya/au kesi za dhuluma za viwanja na nyumba feki: Je, Serikali sasa haioni kuwa kuna haja ya kutunga sheria ili mauziano yote yafanyike kupitia mawakili ambao wana uwezo na wana upeo wa kutambua nyaraka feki na halali ili kupunguza makosa haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tumekuwa tukikabiliana na athari nyingi za wakimbizi hususan wakazi wa Kigoma ikiwemo ujambazi, maambuzi ya Ukimwi na hata ufinyu wa huduma za jamii: Je, Serikali haioni kwa kutoa uraia kwa watu takriban 160,000 na hali hatarishi kwa maendeleo ya nchi yetu hususan tuki-*refer* matatizo yaliyokumba Mkoa wa Kigoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi ni muhimu katika usalama wa nchi. Kila mwananchi huwa makini wakati anapoona jeshi lake linafanya kazi kwa vizuri bila ubaguzi, siyo kwa sasa hivi tu, bali hata wakati wa uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa za kulevya ni moja kati ya janga kubwa linaloathiri nchi na vijana katika kuleta maendeleo endelevu. Kuna baadhi ya sehemu ambazo zinauzwa dawa/unga, na Polisi hupewa taarifa na kuonyeshwa nyumba, lakini badala ya kwenda kumkamata mhusika, huenda kumpa taarifa na kupewa chake, ili wakati wanapokwenda kumsachi huwa hakuna kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba hizi zinajulikana na zipo hadi hii leo. Wanaoleta dawa za kulevya wanajulikana, lakini Serikali ina kigugumizi kuwakamata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Vituo vya Polisi vya Mijini vinakosa umeme wakati wa kukatika na huwasha mishumaa, kandili au kibatari. Hii ni picha mbaya kwa jeshi kama hili, na hasa wakati wa sasa hivi ambapo kuna wahalifu wengi katika Mitaa. Ni vyema Serikali ikajitahidi kuwawekea *generators* ili ionekane tofauti ya Jeshi la Polisi na raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mahabusu watu wazima na watoto. Ni vyema watoto wakawa na sehemu yao ya kuishi ili waondokane na tabia mbaya ya watu wazima hao ambao wanaweza kuwadhuru kimaadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya wafungwa na mahabusu ni haya yafuatayo:-

(1) Mahabusu kutofikishwa Mahakamani kwa wakati;

(2) Kuna utaratibu mbovu wa kusikiliza malalamiko ya wafungwa na mahabusu, Askari wa Magereza hawawapi nafasi ya kutoa malalamiko yao;

(3) Kwa kuweka wanawake, wanaume na watoto pamoja na watu wazima. Nashauri kwamba wanawake walio na watoto wawekwe sehemu nzuri ili mtoto asiwe na mazingira mabaya na kuathirika kisaikolojia;

(4) Watoto waliofungwa kukosa haki yake ya kielimu. Ni vyema kuwekewa sehemu maalum na wakati muafaka wa kupewa elimu utengwe, ili watakapotolewa waweze kujiendeleza kielimu na maisha; na

(5) Vyumba vya wafungwa vina mwangaza hafifu/mdogo ambao unaweza kuwaathri maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya ajali nyingi zinazotokea wanaosababisha ni Polisi wa Usalama Barabarani. Polisi hawa hufanya urafiki na madereva, wanajuana vyema tabia zao, nani ukimpa nini anakuachia, hawaendi kituoni. Polishi hupokea rushwa wakati dereva kafanya kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kuwa Polisi waongezewe mshahara ili waondokane na kadhia hii. Mara kwa mara wawe wanabadilishwa vituo ili wasiwe marafiki wa madereva. Polisi wapewe elimu mara kwa mara juu ya maadili yao. Serikali ipange mikakati mizuri katika madawa ya kulevya. Kuwe na vituo/*sober house* kwa hawa vijana wanaovuta dawa za kulevya. Watoto wanaofungwa wapewe haki yao ya kielimu. Wanawake wafungwa wapate mazingira mazuri hasa wale wenye watoto ili wasije kuathirika kisaikolojia.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa juhudi kubwa wanazofanya katika kuhakikisha usalama wa raia na mali zao nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize, kwa nini Askari Polisi wasiajiriwe kwa mkataba kama wanavyoajiriwa wafanyakazi wengine na badala yake wanafanyakazi miaka (12) ndipo wajaze mkataba? Hatuoni kwamba tunawanyima haki yao ya *Pension* kwa kiwango kikubwa? Naomba basi Serikali iliangalie tatizo hilo kwa umakini na pia kufanya utaratibu wa kubadili sheria hiyo, kwani ikiwa Askari amefanya kazi miaka 20, basi *pension* yake ni miaka minane tu. Hatuoni askari wetu jinsi wanavyodhalilika baada ya kustaafu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mahabusu 19,544 ni wengi mno, lakini inaonyesha wazi kwamba ukienda katika Magereza yetu, utawakuta mahabusu ambao pengine kesi zao ni za kuiba nazi, machungwa, kuku na vitu kama hivyo, kesi ambazo zinawezekana kupewa dhamana. Lakini lingine ni kwamba wanaadhibiwa watu kabla ya kutiwa hatiani jambo ambalo ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Inaonekana kwamba Jeshi la Polisi limeshindwa kufanya uchunguzi na kuhakikisha kwamba kabla ya mtuhumiwa kushikwa na kupelekwa Kituo cha Polisi na kupelekwa mahabusu, na hili huchangia mlundikano wa mahabusu katika Magereza yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya watuhumiwa wa madawa ya kulevya ya viwandani aliyoitoa Mheshimiwa Waziri ambayo inaonyesha kwamba ni watuhumiwa 557 waliokamatwa kwa

mwaka 2010/2011 wenye kilo 529; lakini Mheshimiwa Waziri hakutuambia wangapi wamefikishwa Mahakamani na wangapi wametiwa hatiani na hatua zilizochukuliwa (adhabu gani).

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa uhamisho wa Askari utolewe kila baada ya muda maalum kwani kumwacha askari katika kituo kimoja muda mrefu kunaleta utendaji mbovu na wa kimazoea. Naomba wahamishwe japo ndani kama hakuna fedha za kuwalipa za uhamisho (yaani wabadilishiwe japo Wilaya na Wilaya).

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wanapostaafu wanacheleweshewa malipo yao hasa askari wa chini *(rank* and file) zaidi wale wanaotoka Zanzibar wanakuja wanasota *Polisi Marine* zaidi ya miezi miwili hadi minne na hawaambulii kitu, wanarudi kwao kwa kuomba hata nauli ya kuwafikisha nyumbani na baadaye wanarudi tena hivyo hivyo.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu usalama. Kumekuwa na matukio ya uvamizi wa mara kwa mara katika maeneo ya Kata ya Iguguno Kando Kando ya barabara kuu iendayo Mwanza, ikitokea Singida mjini, katika kijiji cha Kilade. Pindi tukio linapotokea, askari wanachukua hatua ya kuwakamata wananchi, kuwapiga bila kuwa na uhakika kuwa wao ndio watekaji wa magari. Watakaokutwa hapo kwenye miji yao, basi hatua inayofuata wanakamatwa wake zao, wanawekwa ndani, bila kujali wana watoto wanaonyonya. Askari hawa wa Kituo kidogo cha Polisi Kata ya Iguguno wamekuwa wanawanyanyasa sana wananchi. Pamoja na malalamiko kwenda ngazi ya Mkoa na Wilaya, askari hawa wamejenga kiburi kwa vyombo husika, huwa hawachukuliwi hatua kwa kuwapiga na kuwanyanyasa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari hawa wamekaa muda mrefu, wamekuwa wazoefu na kujichanganya na wananchi kiasi cha kusahau majukumu yao ya kiaskari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maaskari kote nchini waongezwe mishahara na kujengewa nyumba na kupatia vyombo vya usafiri ili watoe ushirikiano kwa wananchi, hapo tutapunguza uhalifu au kuuondoa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pale wananchi wanapojenga kwa nguvu zao kituo cha Polisi, basi Serikali itoe maaskari wa kuhudumia vituo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, Kituo cha Polisi cha Iguguno kishughulikiwe, askari hao walishapoteza maadili ya kazi.

**MHE. MAJALIWA K. MAJALIWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba upokee matatizo makubwa yanayolikabili Jeshi la Polisi Wilaya ya Ruangwa ambako kuna Kituo cha Polisi kilicho kwenye jengo dogo la kurithi, pia chakavu kwa kuwa lilijengwa mwaka 1952 wakati wa ukoloni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ruangwa, kipolisi imepata hadhi ya kuwa Kituo cha Wilaya, bado kuna idadi ndogo ya watumishi ili kuwasambaza kwenye vituo vidogo vya Polisi vya Mbekanyera na Mandawa. Vituo h ivyo havina nyumba za askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sasa Wilaya ikapata nyumba za watumishi (maaskari) na jengo rasmi la kituo chenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ruangwa inayo gari, lakini Jeshi lina hali mbaya sana ya namna ya kuendesha gari walilonalo ili kutekeleza wajibu wao kwa kukosa mafuta na matengenezo mengine *(service).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa Jeshi la Polisi kufikisha fedha za mafuta na samani ni ngumu na zikiletwa hazitoshi. Ni vyema sasa Jeshi likapata huduma sahihi ili watende kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata nafasi ya kuongea na Makamanda wote wa Jeshi la Polisi, malalamiko makubwa ya askari ni kukosekana kwa stahili zao. Wanaidai Serikali madeni makubwa ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu. Ni wakati sasa Wizara kupitia bajeti yake ianze kulipa madeni yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu tatizo lililoanza kushika kasi la ukosefu wa maadili wa baadhi ya Askari Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko mengi sana kutoka kwa wananchi wa maeneo ya Jimbo la Bukene, Kituo cha Polisi cha Mambali, Kituo cha Polisi cha Mangoye katika Wilaya ya Nzega. Kuna malalamiko mengi sana kutoka kwa wananchi kuwa baadhi ya askari Polisi wanatumia vibaya dhamana waliyonayo kwa kubambikiza wananchi kesi za uongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko mengi hasa sehemu za vijijini ambazo zina wafugaji wa ng'ombe kuwa wafugaji ndio walengwa na hawa Askari Polisi walio na ukosefu wa maadili. Jambo wanalolalamika wananchi ni kuwa iweje ni wafugaji tu ndiyo watuhumiwa wa mauaji, bangi na makosa mengine na baadaye kuwaomba fedha ili kesi zifutwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba tatizo la ukosefu wa maadili kwa baadhi ya Askari Polisi lifanyiwe kazi. Askari Polisi vijana wanaojiunga na Jeshi la Polisi wapewe *councelling* ya kutosha na wafanyiwe *vetting* ya kutosha ili tuingize jeshini vijana waadilifu. Jambo lingine ninaloshauri ni kuwa Jeshi la Polisi liwe lina *respond* kwa haraka kuchukua hatua pale ambapo wananchi wana-*report* kuhusu upungufu wa maadili kwa baadhi ya askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara itoe maelekezo kwa *OCD* wa Nzega ili afuatilie malalamiko ya wafugaji wa maeneo ya Jimbo la Bukene kubambikiwa kesi za mauaji, bangi na kadhalika ili washinikizwe kuuza ng'ombe na kutoa pesa ili kesi zifutwe. Vituo vya Polisi vinavyolalamikiwa sana ni Kituo cha Polisi Mambali, Kituo cha Polisi Mwangoye na Kituo cha Polisi Bukene.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuendeleza mchango wangu au maoni yangu kwenye Wizara hii inayohusika na Jeshi la Polisi la Tanzania ambalo katika kitabu cha taarifa, hali ya uhalifu kuanzia Januari hadi Desemba, 2010 imeainisha bayana kuwa, naomba kunukuu: "Dira ya Jeshi la Polisi la Tanzania ni kuwa na Jeshi linalozingatia weledi, usasa na ushirikiano na wananchi lisaidialo utunzaji na ulinzi wa amani nchini." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kueleza masikitiko ya manyanyaso na udhalilishaji anaopata mwananchi/wananchi wa Tanzania hususan wananchi wa Mkoa wa Mara. Hii inawezekana ni kutojali maadili ya kazi zao au kujua na kudharau *ethics* za kazi, kwani weledi wa Askari wa Jeshi la Polisi unatia walakini. Sasa hapa kuna mawili, aidha hawa askari ambao hukiuka maadili ya utendaji kazi zao ni kwa kupata amri toka ngazi ya juu au ni kwa utashi wao wenyewe unaotokana na chuki binafsi au maslahi yao wenyewe kitu kinachojenga chuki na jamii husika na kupelekea ugumu hata katika programu ya ulinzi shirikishi kwa maana ya kujumuisha jamii husika kwenye harakati za kutokomeza uhalifu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamekuwa wakinyanyaswa na kukosa uhuru ndani ya nchi yao na baadhi ya hayo manyanyaso ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 14 Julai, 2011 askari wanaolinda Mgodi wa *North Mara* unaomilikiwa na *Barrick African Gold Mine* waliwapiga risasi na kuwajeruhi wananchi wa Kijiji cha Keganga na Nyangoto kwa tuhuma za kuokota kifusi/mchanga uliotupwa wakidhani kuwa kuna dhahabu kwenye kifusi hicho ambacho kilitupwa kwenye makazi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi hawa waliwapiga risasi na kuwatelekeza hapo hawa wanaodhaniwa kuwa ni wahalifu, ningetarajia basi hadi wanawapiga risasi, basi lengo ni kuwakamata na kuweza kuwafikisha kwenye nguvu ya sheria na labda walikaidi kitu ambacho

sicho maana hamna ukaidi wowote ule uliotokea na kwa nini wapigwe risasi? Huu ni uvunjifu wa haki za binadamu na Wizara/Serikali lazima ikomeshe hili. Cha ajabu na cha kusikitisha, Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Vuai Nahodha alisitisha Polisi kulinda mgodi ule na kwamba mgodi ulipewa muda kutafuta walinzi wake. Sasa nashangaa ukiukwaji wa kauli ya Waziri na je, hatua gani zimechukuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, waliojeruhiwa ni Mwita Masaita aliyejeruhiwa mguuni, Mwita Marembora alipigwa risasi kwenye kiganja cha mkono, hawa wote wa kijiji cha Kafanja Kata ya Kamambo na mwingine ni Kikoma Mageko aliyepigwa risasi pajani wa kijiji cha Nyangoto. Baada ya kutelekezwa na Polisi, ndugu zao ndiyo walilazimika kuwapeleka Hospitali ya Wilaya ya Tarime. Napenda kupata majibu juu ya hatua iliyochukuliwa na ni lini hawa Polisi wataondoka na kuacha ulinzi wa Mgodi wasiulinde. Cha ajabu, *RPC* wa kanda maalum hakuwa na taarifa ya hao watu waliopigwa risasi na wenye mgodi wenyewe nao hawakujua. Sasa uhalifu utokee na risasi zitumike *then* kusiwepo na taarifa wakati risasi zimetumika na kupigwa watu. *RPC* hajui? Jamani jamani, hii inaleta fedheha sana au hamna Polisi wenye *private bullets* zao?

Mheshimiwa Nabu Spika, tatizo lingine ni la tarehe 25 Mei, 2011 ambapo askari waliwakamata wananchi waliozunguka mgodi ule na hata wengine kupigwa risasi na kujeruhiwa, na cha ajabu sana kati ya watu waliokamatwa alikuwepo mzee mmoja ambaye ni kilema hawezi hata kukimbia, anaitwa Magaigwa na hata leo yupo Gerezani akihusishwa na uvamizi wa tarehe 16 Mei, 2011 ambapo watu zaidi ya watano walifariki kwa kupigwa risasi. Naomba Waziri na ngazi nyingine husika wamwone huyo mzee Mgaigwa, kwanini kama alikuwa kwenye *scene* na ulemavu wake, Polisi walishindwa nini kumkamata? Maana sasa vijana, akina mama na wazee wamekimbia Miji yao na wanaishi porini.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio mengine ambayo yanadhihirisha uvunjaji wa haki za binadamu ni dereva wa gari *(private saloon)* Mjini Tarime alipigwa risasi pegani na Polisi kisa amesimamishwa na kusimama baada ya hatua chache na sasa Polisi wale wanataka kumlipa fidia nje ya Mahakama. Sasa mnyonge huyu alikosa nini? Nini adhabu kwa Polisi wanaotumia silaha ovyoovyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 16 Novemba, 2010 Polisi Mugumu walimpiga na kumuua Mchota James, tena mwanafunzi aliyekuwa anahitimu *Form Four* akisubiri matokeo eti kwa tuhuma ya kuiba kuku na kulikuwa hakuna taarifa ya kupotea kwa kuku. Cha ajabu, Polisi aliyeongoza mauaji hayo alihamishiwa Manyara, kama sijui zawadi ya kuua au ni nini? Nilidhani angewajibika aidha kwa kufungwa kwa kuua na kumkatiza kijana yule asiye na hatia maisha. Naomba Wizara inipe majibu kwenye hili, kwani hata kwenye swali langu la nyongeza la tarehe 11 Julai, 2011 niliuliza hili swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 20 Desemba, 2010 Polisi walimuua Hamis Ngasagara (27) wa Kijiji cha Kegonga Matare, ambapo Polisi hawa walikwenda nyumbani kwa Marehemu asubuhi na kumkuta Bwana Hamisi amelala na kumpiga risasi wakidhani ni jambazi ilhali wamemkuta nyumbani kalala na hakuwa na ukaidi ambapo *RPC* Mara alidai uchunguzi unafanywa, lakini hadi leo hajatoa taarifa juu ya uchunguzi huo, na inasadikika Marehemu alikuwa siyo jambazi. Nataka Wizara itoe majibu katika hili suala. Hiki Kitongoji kipo Mugumu mjini, na huu ni mwendelezo wa Polisi wa Mugumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tena kwa mwaka huo huo na mwisho tarehe 2 Januari, 2011 Polisi walimpiga Chacha Marwa (33) wa Kijiji cha Bondugu na kufia kituoni wakimlazimisha kukiri kuua faru. Sasa kweli mtuhumiwa ameshakamatwa, na anatakiwa apelekwe kwenye sheria, lakini Polisi wanamuua. Ina maana faru katika nchi yetu ana thamani kuliko uhai wa Mtanzania? Hii inasikitisha sana. Napenda kujua ripoti au taarifa juu ya hili, kwani kamanda walidai wangetoa taarifa juu ya mauaji haya, lakini hadi leo imekua kimya, hana ripoti yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni masikitiko makubwa juu ya mauaji ya wananchi na matumizi makubwa au mabaya ya silaha kwa Jeshi la Polisi la Tanzania. Mnamo tarehe 16 Mei, 2011 ni mauaji ya Nyamongo na wamepigwa sehemu za kichwani, mgongoni, tumboni, kiunoni na kadhalika. Sasa kweli hata kama uchunguzi unaendelea, mbona hii ipo wazi kabisa, kwani

kumdhoofisha mhalifu siyo kumpiga risasi katika sehemu tajwa. Hii ni dhahiri kuwa walidhamiria kuwaua wale wananchi na siyo kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria ili sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa Serikali kwamba ifanye juhudi za hali na mali kuzuia hii hali ya Polisi kuua binadamu kama wanyama, maana hata kuku tunawaonea huruma tukipata wageni kuwachinja. Hivyo haki na amani itumike. Polisi wakumbushwe au wafundishwe matumizi ya silaha ni nini wafanye mara wamkamatapo mhalifu. Pia Polisi wasitumie vyeo vyao kulipiza visasi na kwa maslahi binafsi. Hii itajenga taswira nzuri kwa Jeshi la Polisi na kurudisha imani kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba kumekuwepo na matukio mengi ya Polisi kutumia nguvu nyingi, hata mahali ambapo hapahitajiki na matokeo yake kusababisha madhara makubwa kwa raia wasio na hatia. Mfano, Polisi kutumia silaha kuua watu kwenye mkusanyiko kama ilivyotokea Mbeya, Arusha na katika Mgodi wa dhahabu wa *North Mara*. Napenda kujua Je, kazi ya Polisi ni kulinda raia au kuua raia wasiokuwa na hata fimbo? Kwanini Polisi wetu wamekuwa wepesi kufyatua risasi zinazonunuliwa na kodi za wananchi na matokeo yake kodi zao hizo hizo ndizo ziwaue?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua mpaka sasa ni Polisi wangapi wamefikishwa katika vyombo vya sheria ili kujibu mashtaka ya mauaji na wangapi wameshapewa adhabu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matukio pia ya kuwaletea vilema vya kudumu raia wasio na hatia yanayofanywa na Polisi wakati wanapokuwa wanapambana na majambazi. Inatokea kwa bahati mbaya wanaweza kuwapiga risasi raia kwa bahati mbaya kama ilivyotokea kwa mtoto mmoja wa miaka 12 aliyeitwa Jaji wa Temeke, alipigwa risasi na kutumbua utumbo na kuachwa bila matibabu yoyote na Polisi mpaka sasa mtoto huyo wa kiume anaishi kwa kuhangaika na hapewi matibabu kwa kukosa pesa na tumesikia anaomba msaada kwa wasamaria wema. Je, Jeshi la Polisi ni kwanini lisiwajibike kumpatia mtoto huyo matibabu wakati Polisi ndiyo walimsababishia madhara hayo? Naomba kupata majibu kwa suala la mtoto huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na tafsiri potofu kuhusu ufanywaji wa Mkutano na maandamano kwa Vyama vya Siasa. Sheria ya Vyama vya Siasa No. 5/1992 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya *National Assembly Administration Act* 4 of 2008 zinaeleza bayana kwamba Vyama vya Siasa au kiongozi yeyote wa kisiasa anapotaka kufanya Mkutano wa hadhara au maandamano ni lazima atoe taarifa masaa 48 kabla ya Mkutano wa hadhara au maandamano husika. Kwa nini Jeshi la Polisi limebadilisha sheria hizi na kuzifanya kwamba ni kuomba kibali cha Mikutano au maandamano? Siyo kutoa taarifa kama inavyoelekeza kwenye sheria. Kauli za kwamba habari za kiintelijensia zinaonyesha kuna uvunjifu wa amani utatokea, huwa ni za nini kama siyo kuwanyima watu haki yao ya kufanya Mikutano na kueleza sera zao? Habari za kiintelijensia kwanini zisiwakamate waleta fujo na kuwafungulia mashtaka na matokeo yake kuwakatisha watu kufanya Mikutano wakati maandalizi ya muda pamoja na fedha yanakuwa yamefanyika? Jeshi la Polisi halioni lenyewe ndiyo chanzo cha uvunjifu wa amani nchini badala ya kulinda amani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufafanuzi kuhusu sheria hizi kama zilishabadilishwa au la, na kwenye kikao kipi cha Bunge kilichokaa kubadili sheria hizi mbovu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mgambo wamekuwa ni askari ambao ni wanyanyasaji wakubwa hasa Vijijini na Mijini. Askari hawa wamekuwa wakizagaa katika majiji hasa Dar es Salaam na kuwanyang'anya wafanyabiashara wadogo wadogo mali zao bila ustaarabu hasa pale wanaponyimwa kitu kidogo (rushwa). Ni kwanini mgambo hawa wanapewa uhuru mkubwa wa kuvamia wananchi na kuwapora mali zao bila kuwachukulia hatua zozote za kisheria? Badala

ya mgambo hawa kufanya kazi za kuwasaidia Polisi sasa wamekuwa ni karaha, hivyo naomba Serikali ifanyie kazi jambo hili la ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kiijijini, mgambo hawa wamekuwa wakitumia nguvu nyingi kwa kuwakamata wananchi ambao hawana hatia. Mfano, mwananchi anaposhindwa kuchangia mchango wa Sekondari, mgambo hufika na kukamata mali kama kuku, mbuzi na hata ng'ombe na wakati mwingine vyombo vya nyumbani, kama mtu hana kitu, basi yeye mwenyewe anakamatwa kwa nguvu na kupewa mateso makubwa. Kwa nini mgambo hawa wamekuwa wakijipatia mali za wanachi kwa nguvu kwa visingizio visivyo na tija? Naomba majibu kwa hilo.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hotuba ya bajeti ya Wizara. Hata hivyo, nina yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa kwa watumishi wa Wizara hii umekidhiri na sasa hakuna hata mdogo wala mkubwa hasa katika Wilaya zetu. Mtu akipatikana na tatizo, unakuwa ni mradi wa wenzetu. Hawana kosa kubwa, au mtu maarufu mwenye pesa akipatikana na tatizo atashughulikiwa na wakubwa wenzake kujua hapa kuna fedha za kutosha labda tuwaongezee posho kisha tuanze kuwachunguza, tukishahakikisha kuwa maslahi yao yamekaa sawa. Rushwa ni kubwa kuliko tunavyodhani. Polisi, uhamiaji, Magereza, hakuna shughuli au tatizo la kukutatulia bila rushwa, tena nafuu Magereza kidogo, na hakuna hatua zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi wanajitahidi sana katika kufanya kazi. Pamoja na tatizo la rushwa, lakini wapo kazini na wanafanya kazi kabisa. Bila Polisi hali ingekuwa mbaya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongea kuhusu Polisi na Mikutano ya Kisiasa. Hapa nina ushauri kwamba Polisi wawe wanavuta subira, inapotokea uwezekano huo upo na baadaye wanawapata hawa wasio na hatia wanaosukumizwa, wapate viongozi wanaolazimisha na kuwahamasisha. Wale viongozi wanaochochea fujo waadhibiwe vikali. Ningependa tuanze na kesi iliyotokea Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Vituo vya Polisi viboreshwe, maeneo mbalimbali yenye watu wengi Polisi waongezeke, wasaidie kulinda raia wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Polisi waongezwe posho, waongezewe mshahara, wapewe huduma ya nyumba na katika eneo langu Jimbo la Nkasi Kusini wajengewe vituo kila Kata. Kata ya Kala, Kata ya Nkasindasi, Kata ya Isale, Kata ya Sintali, zote hazina Polisi. Tunaomba vituo vijengwe na naomba pia Polisi wagatuliwe katika huduma fulani Fulani, au basi Halmashauri ya Mji na Manispaa waruhusiwe kuajiri Polisi, watatusaidia katika suala zima la usalama pamoja na kuwahudumia itasaidia katika udhibiti wa masuala ya usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanyika Wilayani Nkasi, bado nyumba za Polisi Wilayani ni duni na zimeshindikana kuendelezwa. Naiomba Wizara itenge fedha ya kumalizia nyumba za Polisi Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wa usalama barabarani Dar es Salaam watafanya ile kazi ya kuongoza magari yale mpaka lini? Ni kwamba tumeshindwa kufufua ule utaratibu wa taa zinazoongoza barabarani? Endapo uwezekano huo ni mgumu, basi tutatue suala la wingi wa magari Dar es Salaam, ile sio kazi, ni mateso makubwa na nashauri kazi ile iwe na posho kubwa zaidi tena ilipwe kwa masaa, na awekewe Bima ya maisha askari ambaye anafanya ile kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, machafuko yaliyoenea ya migogoro katika jamii, sehemu nyingi nchini, ikiwemo uhamiaji holela ndani ya nchi na maeneo mengine pamoja na kutapakaa kwa silaha haramu za moto zikiwemo za kivita na kutengenezwa kienyeji, hali hii inasababisha kuendelea kushuka kwa utulivu na amani ndani ya nchi yetu. Mfano, ni askari Upendo wa Serengeti aliyeuawa na majambazi waliompiga risasi shingoni na kufariki akiwa kwenye operasheni ya kukamata majambazi waliokuwa na silaha haramu. Tukio hili lilitokea Nyamongo huko Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii idhibitiwe haraka iwezekanavyo, kwa sababu hali hii ya uchochezi inayoendelea kufanywa na Vyama vya Upinzani inaweza ikasababisha machafuko ambayo yataweza kutoa kabisa amani iliyoko nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mambo yafuatayo yafanyike:-

- Operesheni ya kudhibiti uhamiaji holela na uhamiaji haramu ifanyike;

- Operesheni ya ukamataji silaha haramu ifanyike na iwe endelevu, ikiwezekana kiundwe kikosi maalum cha kushirikisha majeshi yote nchini;

- Makazi ya Polisi yaendelee kuboreshwa;

- Vitendea kazi viongozwe;

- Ulinzi shirikishi na Polisi, jamaii uboreshwe;

- Wakuu wa Wilaya wasimamie na kufuatilia ulinzi na usalama katika ngazi zote kwa ukaribu zaidi ikiwemo kufanya vikao katika ngazi ya jamii. Wasikae maofisini tu kwa kutoa amri na kusubiri taarifa toka kwa Maafisa Tarafa. Hiyo siyo sahihi;

- Mafunzo ya Polisi yaangaliwe upya kulingana na ngazi na cheo ili mafunzo hayo yaendane na mazingira tuliyonayo nchini ya kisiasa, kijamii na mpito wa utandawazi uliopo; na

- Kero za malimbikizo ya madai ya posho za uhamisho na safari zitatuliwe bila ucheleweshо.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wilaya ya Serengeti, mauaji yaliyotokea mwaka 2009 katika mapigano ya kikabila na jamii iliyokuwa inaishi Kijiji cha Massongo, ufuatiliaji wa kina ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, *passport* zinazotolewa Tanzania zinatumika vibaya kwa watu wengine wanaozipata kwa kuwaibia Watanzania na kuzibadilisha kwa kompyuta na kuzitumia vibaya kwa sababu tu za binafsi. Hiyo ni kutokana na Tanzania kuwa na heshima kubwa duniani. Hivyo, wanaghushi *passport* hizo kwa manufaa yao. Hili siyo suala la kuacha liendelee, ufuatiliaji wa karibu ufanyike ili hali hii idhibitiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, askari wetu wanaishi katika makazi mabaya sana yasiyo na staha. Suala hili limezungumzwa kwa muda mrefu sana. Ifike wakati sasa Serikali iamue kufanya mkakati maalum wa ujenzi wa nyumba katika Wilaya zote na maeneo yote ambapo kuna Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vingi vya Polisi ni vichakavu sana, vifaa vya kufanyika kazi ni duni sana, hawana karatasi za kuandikia, mara nyingi anayekwenda kushitaki anatakiwa kununua katarasi na hata kulipia mafuta ya gari ili aliyeshitaki pamoja na Polisi wafike eneo lenye tukio au kumkamata mtuhumiwa. Hii siyo sahihi, haki haitatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wetu wanadai pesa nyingi sana za uhamisho, mafao na baadhi yao wanadai posho zao mbalimbali wanazotakiwa kulipwa kwa kazi maalum. Serikali iwalipe askari madai yao ili wakidhi mahitaji yao kwani mishahara yao ni kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza yetu yanajaa sana kwa kutoitumia ipasavyo Sheria ya *Parole*. Ifike wakati utaratibu ufanyike, sheria hii itumike ipasavyo ili mlundikano upungue katika Magereza zetu. Sheria hii ilitungwa makusudi ili kupunguza mlundikano hasa kwa wale wenye makosa madogo madogo, wafungwe kifungo cha nje kwa kufanya kazi za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukirejea repoti ya *Human Rights,* Askari wamekuwa na tabia mbaya ya kuua raia. Ripoti imeonyesha Polisi katika mwaka 2010 wameua watu 52, watu 10 waliuawa na Jeshi la Polisi katika maeneo ya mgodi wa dhahabu wa *North Mara* Nyamongo Wilayani Tarime peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatoa haki ya kuishi kwa kila mtu na inaitaka Serikali kumpatia kila mtu hifadhi ya maisha yake. Vile vile vifungu vya 195 na 196 vya kanuni ya adhabu, sura ya 16 ya Sheria za Tanzania vinakataa vitendo vya mauaji vilivyo kinyume na sheria kwa mujibu wa Ibara ya 30 (2) (c) ya Katiba, mauaji yanaweza kuwa halali endapo yamefanywa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa kwa ajili ya kuhakikisha (utekelezaji wa hukumu au amri ya Mahakama iliyotolewa katika shauri lolote la kosa la jinai).

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee kuhusu mateso na udhalilishaji katika Magereza yetu. Katika Gereza la Bangwe Kigoma upande wa Gereza la Wanawake, anapofikishwa mwanamke mtuhumiwa ambaye ni mahabusu, au mfungwa anaamrishwa kuvua nguo zote kila kujali umri wala hali ya mama huyo na kuamrishwa kuruka kichurachura akiwa mtupu. Serikali ikemee makosa hayo yanayofanywa makusudi na askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kigoma ni Mkoa ulio pembezoni, hivyo umepakana na nchi ya Rwanda, Burundi, *DRC* na Zambia. Askari wa Uhamiaji wamekuwa na tabia mbaya ya kusumbua raia, kwani upo mtindo wa askari hao kutumika vibaya. Ikitokea watu wamegombana wanawashitaki kwa Afisa Uhamiaji na kuwapa rushwa ili wawakamate waliokosana nao kama wakimbizi hata kama wamethibitishwa na wanajulikana siyo wakimbizi ni raia halali, na wamekuwa wakisumbua wananchi kuwa siyo raia ili wapewe rushwa. Hili likomeshwe! Lakini vile vile vituo wanavyofanyia kazi Maafisa Uhamiaji ni duni, viboreshwe.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wa Jeshi la Polisi, Magereza, *Traffic* pamoja na Uhamiaji waboreshewe mishahara pamoja na stahili zao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba zao nyingi ni chakavu sana, zinatia aibu kwa kweli. Vituo vingi vingi vya Polisi vina hali mbaya sana, ni vichakavu sana, ni aibu kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilombero ina Kituo cha Polisi cha Wilaya ambacho ni chakavu kupita kiasi. Naiomba Serikali kuboresha kituo hiki, tena kituo chenyewe wakati wa mvua hakifikiki. Kituo hiki cha Polisi kipelekewe fedha za kutosha kwa ajili ya kujiendesha kwani kina hali mbaya sana kiutendaji. Kituo hiki kinahitaji kupelekewa nyenzo za kutosha kama vile gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu mpaka leo kuwa na vituo vya polisi vyenye mabati *(full suit).*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kkwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri Katibu Mkuu Mkuu, Mkuu wa Jeshi la Polisi, Maafisa wote na Watendaji wa Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wetu wanaishi katika mazingira magumu, nyumba zao ni ndogo na chakavu. Maisha haya yanafanya watoto wa Polisi wanakuwa waathirika wakubwa katika malezi. Hakuna *privacy.* Kwa hiyo, nashauri askari wajengewe nyumba nzuri za kuishi. Nyumba hizo ni pamoja na askari wa Wilaya ya Njombe na Makao Makuu Iringa Mjini. Ni vizuri nyumba hizi zikawa za ghorofa ili kuchukua familia nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafungwa waendelee kutumia fani zao wawapo Magerezani ili ujuzi wao uendelee kutumika. Wafungwa pia waendelee kupewa ujuzi mbalimbali ili wakitoka pamoja na kuacha uhalifu waweze kufanya kazi za kujitegemea na kuweza kuwa raia wema.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Idara ya Uhamiaji kwa kuwa mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya Ukimwi. Idara hii imeonyesha mfano mzuri, nina uhakika Idara zote zinaweza kuiga mfano wa Idara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wa Askari washirikishwe katika kuainisha vikundi vya kiuchumi hasa kwa wale wanaokaa *Line Police*.

Mheshimwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia napenda kuchukua fursa hii kuchangia bajeti ya Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya jamii iliyobora na yenye uadilifu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii pia inalo jukumu zito katika kuhakikisha usalama wa raia unalindwa pamoja na mali zao. Aidha, Wizara hii ndiyo inabeba dhamana ya kuhakikisha wafungwa wanarekebishwa, pamoja na udhibiti wa uingiaji na utoaji wa wageni katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Polisi wote kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiendelea kuifanya. Hata hivyo, Serikali itafute misaada mbalimbali ya fedha ili fedha hizo ziweze kutumika katika ujenzi wa nyumba za makazi kwa ajili ya Polisi wetu, kwani hivi sasa nyumba zilizopo ni chache sana na hazitoshelezi kulingana na idadi iliyopo ya Polisi wetu. Vile vile, nyumba zilizopo ziko katika hali mbaya na hazifai kwa matumizi ya binadamu, na ni kinyume na matakwa ya mikataba mbalimbali ya kulinda na kuhifadhi utu wa mtu na haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba wafungwa wanatakiwa kurekebishwa tabia kupitia programu mbalimbali za mafunzo kwa vitendo, lengo ni kuwafanya wawe raia wema pindi wanapotoka Magerezani au katika programu nyingine za mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa kwamba Sheria ya *Community Sentence* ipo na inapaswa kufanya kazi. Inashangaza kuona Magereza yamejaa kwa mlundikano wa wafungwa. Wakati mwingine, unakuta wafungwa wako Magerezani wala hapakuwa na umuhimu wa wao kuwepo huko. Makosa mengine ni ya kutozwa faini tu na wafungwa wengine walishindwa kulipa faini na wamepelekwa Magerezani. Siyo sawa, ni uonevu kabisa! Kwa nini wafungwa hawa hawakupewa adhabu nyingine za jamii au kifungo cha nje? Vile vile kwa wafungwa waliopo Magerezani, basi watumiwe kuzalisha chakula kwa ajili yao na kinachobakia, kwa ajili ya kuuzwa, pamoja na kuzalisha bidhaa mbalimbali nyingine. Hii itasaidia kupunguza gharama za fedha katika kuendesha Magereza hayo. Pia hela za ziada itakayopatikana, inaweza kugawanywa kwa kila mfungwa ili pindi wanapomaliza vifungo vyao, waweze kupata hela kidogo ya kuanzia maisha. Tumeshashuhudia wafungwa wengi wamekuwa wakiachiwa au wanapomaliza vifungo wamekuwa hawana nauli za kuwarudisha makwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na uhamiaji wa uraia, Idara hii ina maovu mengi. Ni vyema ikajipanga upya. Rushwa imekithiri hususan katika vibali vya kuishi *(Resident Permits)* na ya kufanya kazi *(working permits).* Ningependa Waziri afafanue takwimu za vibali vya kufanya kazi, ni vingapi vimetolewa kwa kila mwaka, kwa miaka mitano? Je, vikao vya kujadili maombi ya vibali hivyo, yanafanyika mara ngapi kwa mwaka? Vile vile, yapo malalamiko wawekezaji wanapewa vibali vya kufanya kazi kwa nafasi/taaluma ambao Watanzania wengi tu wanazo mfano *Vodacom*, wapo Wazungu wengi tu ambao vibali vyao unakuta wao ni *gardening experts;* kweli kampuni ya simu tunahitaji *expertiate* wa *gardening?* Siyo sahihi, ni vyema Tume Maalum ikaundwa ili kupitia sifa za waombaji wa vibali vyote ambavyo vimekwishatolewa. Baadaye, wahusika wa uhamiaji wakapatiwa onyo, ili tuweze kwenda vizuri na matatizo na kasono za utendaji zisijitokeze tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema pia hotuba ingeainisha ni fedha kiasi gani zimepatikana kutokana na uzalishaji mali unaofanywa na Shirika la Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ndiyo pekee ambayo tunatoa uraia baada ya mgeni kuishi katika kipindi kifupi sana, mara nyingine mwaka mmoja. Tena cha kushangaza, tunawapa

watu uraia bila ya kuwapa mafunzo waifahamu nchi yetu, hususan kihistoria, siasa na jiografia ya nchi yetu na baadaye watahiniwe kwa kufanya mtihani. Sisi, tunawapa tu uraia. Inasikitisha! Ni vyema tubadili mfumo wetu wa utoaji wa uraia kwani una matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri, na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani kwa hotuba yake nzuri ya bajeti aliyoitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana, inashangaza sana jinsi uhamiaji wanavyotoa *passport* (hati ya kusafiri) kwa watu ambao sio raia wa nchi hii. Mara ya mwisho nilikuwa natoka Instanbul (Uturuki) nakuja Dar es Salaam nikamwona mtu mmoja akiwa na *passport* ya Tanzania, nikakimbilia kumsalimia kwa Kiswahili. Nilishangazwa sana na yule jamaa alikuwa hajui Kiswahili hata chembe, alipoona namfuatafuata akakimbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni aibu kubwa sana kwa Serikali yetu. Rushwa imetawala sana katika eneo hili, watu wanafanya uhalifu mkubwa nchi za nje ambao sio Watanzania lakini kwa sababu tumeshindwa kudhibiti hati zetu, tunaonekana Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atoe maelezo, Serikali itachukua hatua gani kwa hilo? Kama itashindikana, tunataka Watendaji Wakuu wa Uhamiaji waachie ngazi ili iwe funzo kwa Idara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la Msingi ni kuhusu vitambulisho. Naomba sana Serikali yetu na hasa Waziri aliangalie hilo kwa upana wake, tusijikute watu wanaopata hivi vitambulisho sio raia wa nchi hii sababu ya rushwa zilizoko kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali bado inakurupuka na haiko tayari kutuambia imejipanga vipi kudhibiti ajali zinazotokea kila siku katika nchi yetu? Hii ni aibu kubwa sana kwa Serikali, ajali nyingi ni za uzembe mkubwa, magari mengi mabovu yanatembea na *traffic* wanaziangalia sababu ya rushwa. Rushwa imekuwa kubwa sana katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi haioni aibu kuomba rushwa. Naomba sana Serikali ijipange kwa kuboresha maisha ya askari, pamoja na kuwajengea nyumba za maana. Inasikitisha sana kuona askari wakiwa wanaishi katika vijumba vya ovyo ovyo ambavyo havilingani kabisa na dhamana za kazi tunazowapa, ndio maana rushwa kwenye hii Wizara inakuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia iangalie sana huu usafiri wa boda boda, badala ya kuwa msaada kwetu, ndiyo umekuwa chanzo kikubwa cha vifo vya ndugu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine muhimu ni masomo kwa askari. Kumekuwa na malalamiko makubwa sana ya jinsi askari wanavyopewa nafasi ya kwenda kusoma. Askari wengi wa Mufindi wamenilalamikia kuwa wanabaguliwa katika suala zima la elimu. Tafadhali, naomba maelezo juu ya jambo hili la kubaguliwa kwa askari wa Wilaya ya Mufindi wanaotaka kwenda kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iongeze idadi ya askari katika Wilaya ya Mufindi, na nilikuwa nataka kujua, kwanini Serikali isifungue vituo kwa kuanzia kila Tarafa, na baadaye kila Kata, uhalifu mwingi unaojitokeza katika Jimbo langu la Mufindi Kaskazini halishughulikiwi kwa wakati muafaka. Naomba maelezo juu ya hili.

Mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. JADDY S. JADDY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kabisa kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yake. Lakini pia

napenda kuwapongeza wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri katika kufanikisha kazi zake za kila siku za Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza mchango wangu kwa kuigusia Idara ya Uhamiaji Zanzibar. Idara ya Uhamiaji Zanzibar ilinunua majengo yaliyokuwa yakimilikiwa na Benki ya watu wa Zanzibar *(PBZ)* yaliyopo katika kijiji cha Kivunge ndani ya Jimbo la Mkwajuni Wilaya ya Kaskazini 'A' Mkoa wa Kaskazini Unguja, lakini tangu kununuliwa kwa majengo haya, bado wananchi hawajaelewa ni makusudio yapi hasa yaliyopelekea kununuliwa kwa majengo hayo, kwa sababu hadi sasa bado huduma zitolewazo na Ofisi ya Uhamiaji, wananchi wanalazimika kuzifuatia Makao Makuu (mjini). Hivyo, namwomba Waziri kutoa agizo kwamba ofisi hiyo itumike kutoa huduma angalau kwa hatua za mwanzo hasa zile za utoaji wa "*passport*" kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalotaka kulizungumzia hapa ni lile la haki za warithi wa askari wanaofariki wakiwa bado ni waajiriwa wa Jeshi hili linavyocheleweshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu, yapo malalamiko toka kwa warithi wa Marehemu Nyange Mohammed Kombo, askari ambaye amefariki akiwa kazini tokea mwaka 2004 kwamba hadi sasa warithi hao bado hawajapatiwa haki ya Marehemu ndugu yao. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kufanya uchunguzi wa suala hilo na kulipatia ufumbuzi unaostahili ili na warithi wa Marehemu huyo na wao wapate kupumzika na utoaji wa gharama za kila siku katika kufuatilia kadhia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kujiendeleza kazini nalo linapaswa kuangaliwa kwa namna ya kipekee. Nalisema hili kutokana na baadhi ya matokeo yaliyowahi kutokea kuhusiana na askari kujiendeleza kielimu na kisha Jeshi la Polisi lisichukulie kitendo hicho kama ni hatua mojawapo ya kufanya askari aliyejiendeleza kupandishwa cheo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana inapotokea askari aliyeko kazini ambaye amechukua juhudi za kujiendeleza kielimu hadi kufikia kiwango cha elimu ya juu kutopewa kipaumbele cha kupandishwa cheo kutokana na elimu yake na badala yake anatokea mtu mwingine ambaye ndio kwanza apatiwe ajira ambaye ana elimu sawa na askari aliyepo katika kazi na ambaye amejiendeleza na wakati mwingine kwa kutumia gharama zake mwenyewe, lakini inapotokea kupandishwa vyeo, basi askari mpya aliyeajiriwa kwa mara ya kwanza ndiye anapewa kipaumbele cha kupandishwa cheo na akaachwa askari aliyekwishalitumikia jeshi hilo kwa muda mrefu. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie sana suala hili kwa umakini mkubwa ili kuweza kuondoa nidhamu ya jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa uhai unaoniwezesha kuendelea kutimiza majukumu yangu ya kibunge yanayohusiana na kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Pia nawapongeza Mkuu wa Jeshi la Polisi, Mkuu wa Jeshi la Magereza, Mkurugenzi Mkuu wa Uhamiaji na Mkurgenzi Mkuu wa Kikosi cha Zimamoto kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ya kuhakikisha raia na mali zao zinalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajielekeza katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi kubwa inayoifanya ya kulinda usalama wa raia na mali zake pamoja na changamoto kubwa inayoikabili Jeshi hili. Nalipongeza sana Jeshi la Polisi kwa kupunguza wimbi la ujambazi ambalo lilikuwepo kabla ya mwaka 2005. Sambamba na hilo, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kupambana na biashara ya dawa za kulevya ndani na nje ya nchi ambayo imeshika sana kasi siku za karibuni. Biashara hii imechangia sana kuharibu vijana wetu ambao ni nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kutekeleza vizuri jukumu lake la kuwapatia wananchi mafunzo ya ulinzi shirikishi ili wananchi hao wawe tayari kujilinda katika maeneo yao. Mafunzo haya kwa kiasi kikubwa yameamsha ari ya wananchi kujilinda na mali zao. Dhamana ya Polisi jamii imesaidia sana kupunguza uhalifu katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa mikakati yake ya kukabiliana na changamoto inayozikabili Jeshi hilo, mfano uboreshaji wa makazi ya Polisi, ulipaji wa malimbikizo ya madeni yao na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa sita, Serikali imekamilisha ujenzi wa nyumba za makazi katika Kambi ya Polisi, barabara ya Kilwa. Aidha, nyumba 82 za askari zimeanzwa kujengwa katika maeneo yanayotajwa. Hata hivyo, maeneo yaliyotajwa, hakuna kabisa nyumba zozote zitakazojengwa Mkoa wa Pwani ambako kuna shida kubwa sana ya makazi ya Askari wa Jeshi la Polisi. Matatizo ya nyumba za askari yapo katika maeneo ya Kibaha ambako hali ni mbaya sana (nyumba ni za *full suit*) Wilaya ya Rufiji, Mkuranga, Kisarawe, Mafia. Naiomba Serikali itupie jicho Mkoa huu wa Pwani, ni lini nasi katika bajeti zinazofuata tutengewe pesa za ujenzi wa nyumba za Polisi katika Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi inayofanywa ya kuwarekebisha kitabia wafungwa na mahabusu, lakini hata hivyo Magereza yetu yanakabiliwa na tatizo kubwa la msongamano. Hali ya Magereza yetu ni mbaya sana hasa miundombinu. Jeshi la Magereza, linakabiliwa na tatizo la upungufu mkubwa wa nyumba za Askari Magereza na zilizopo ni chakavu sana katika Mkoa wetu wa Pwani, kuna uhaba mkubwa wa nyumba za Askari Magereza hasa katika Gereza la Utete, Bagamoyo na Kibaha. Naiomba Wizara iliangalie suala hili na kulipatia ufumbuzi awamu kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Uhamiaji pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Idara hii hasa katika zoezi la kudhibiti wageni haramu nchini, bado hawajafanikiwa sana kutokana na kushuhudia ongezeko la wageni haramu toka 2,212 mpaka 3,339. Miongoni mwa wahamiaji haramu waliokamatwa 1,371 walitokea Somalia. Wahamiaji hawa haramu toka Somalia njia yao kuu ni kupitia baharini maeneo ya Winde, Kitame na Saadani Wilayani Bagamoyo Mkoa wa Pwani. Naomba Jeshi hili la Uhamiaji kuongeza Doria kwa maeneo hayo, kwani tatizo ni kubwa sana na kuna ongezeko la uhalifu linalochangiwa na wahamiaji hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuwepo kwa wingi wa watu kutoka nje kuingia nchini kinyemela bila kuwa na kibali na kuanza kuifanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hao inadaiwa kushirikiana na Maofisa wa Uhamiaji na kupata hati ya kibali cha kuishi bila kufuata taratibu. Je, Wizara inajua jambo hilo na imejipanga vipi kimkakati ili kukomesha wahamiaji haramu?

Mheshimiwa Naibu Spika, inasemekana tatizo hilo lipo katika Makampuni ya Simu hasa *Zantel*, pamoja na kujenga mahoteli.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kumekuwa na raia wa nchi nyingine ambao wamekuwa wakifanya uhalifu na wanapokamatwa wanakutwa na *passport* za Tanzania na kwamba wamekuwa wakipata *passport* kwa kushirikiana na Maafisa wa uhamiaji. Wahalifu hao wamekuwa wakifanya matukio ya kiuhalifu nje ya nchi na kupaka matope Tanzania. Pia kuwawekea mazingira magumu wafanyabiashara wa hapa nchini, ikiwepo kunyimwa hati ya kusafiria kwa baadhi ya nchi kwa kuwa Tanzania tunaonekana siyo waaminifu.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ichukue hatua thabiti kulikabili suala la wananchi kuvunja sheria kwa kujichukulia sheria mkononi mwao hasa wanapoamua kuwaua kwa mateso ya hata kuwachoma moto watu wanaoshukiwa kuwa ni wezi tena wezi wa vitu ambayo havilinganishwi kabisa na thamani ya uhai kama vile kioo cha pembeni cha gari au simu ya mkononi. Naomba tabia hii ambayo inachukuliwa kama kawaida, ikomeshwe. Mauaji ya raia wanaodhaniwa ni wachawi na kadhalika pia ikomeshwe na sheria ifuatwe kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la kusimamia sheria lifuatwe katika mambo mengi, naomba litiliwe mkazo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapanda pikipiki wengi bado hawavai kofia za kukinga kichwa na abiria wote wa bodaboda hawavai kofia hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajali za magari linahitaji kuwekewa mikakati ya ziada ya usalama barabarani ili ajali hizi zisiongezeke kama ilivyo sasa. Kuna haja ya kuweka adhabu nzito ya kukomesha tabia za baadhi ya madereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri na yenye busara kubwa inayolenga kuleta na kudumisha amani na utulivu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa katika mstari wa mbele kwa kupigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika kama vile Afrika Kusini, Mozambique, Zimbambwe, Namibia, Angola na kadhalika. Katika kufanya hivyo, Kambi za Wapigania Uhuru zilifunguliwa katika sehemu nyingi za Tanzania kama vile Kongwa, Mazimbu, Wami – Dakawa, Bagamoyo, Nachingwea na Kihesa – Mgagao katika Wilaya ya Kilolo – Iringa. Baada ya nchi hizo kufanikiwa kupata uhuru makambi hayo yalikabidhiwa Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Kihesa – Mgagao iliyoko Kilolo ilikabidhiwa Magereza licha ya ukweli kwamba Kijiji kilijitolea ardhi hiyo yenye hekta 2,600. Wananchi waliomba kutumia Kambi hiyo kwa ajili ya kuanzisha Shule ya Sekondari ya Wasichana Kidato cha I hadi cha VI, jambo ambalo liliungwa mkono na *RCC*. Tarehe 5 Agosi, 2008 wananchi wa Kilolo walifikisha ombi lao kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa ziara yake Wilayani Kilolo. Rais alikubali ombi hilo na akaagiza Magereza wapewe eneo lingine na wahamie huko. Pamoja na agizo hilo la Rais la tarehe 5 Agosti, 2008 hadi leo hii agizo hilo halijatekelezwa licha ya wahisani wa *New Forest Company* kuwa tayari kusaidia ujenzi wa shule hiyo. Je, kuna tatizo gani kwa Kambi la Kihesa – Mgagao kukabidhi kwa wananchi wa Kilolo ili kuendeleza elimu kama ilivyo kwa Kambi za Mazimbu (sasa Chuo Kikuu), Wami - Dakawa *(High School)*, Kongwa *(Secondary School),* Bagamoyo (*Secondary School*) na Nachingwea (*Secondary School*)? Naomba jambo hili litekelezwe haraka kabla sijalipeleka mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilolo hadi leo hii haina Makao Makuu ya Wilaya. Naomba ifikiriwe kujengewa Makao Makuu ya Polisi Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilolo ina vituo vidogo vya Polisi vinne (Mbigili, Ilolo, Ruaha – Mbuyuni na Mtitu). Lakini askari wake wamekaa katika vituo hivi kwa muda mrefu sana na wengine kujihusisha na uhalifu. Tunaomba mabadiliko.

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa asilimia mia moja. Lakini napenda kuzungumzia hasa kuhusiana na Polisi na Magereza hususan katika Jimbo langu la Kilombero. Kilombero kuna matatizo, kwanza ni majengo ya Ofisi ya Polisi ya Wilaya hiyo. Majengo hayo yamechakaa sana. Pili, Polisi wa Wilaya hiyo wengi wao hawajalipwa posho zao kwa miaka mingi. Naomba Serikali iwalipe posho hizo. Tatu, ofisi hiyo ya Wilaya ya Polisi inasumbuliwa sana na *TANESCO* bili inakuwa kubwa kiasi kwamba kila siku *TANESCO* inataka kuwakatia umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza ya Jimbo la Kilombero wanalima sana mazao ya biashara na chakula kama Gereza la Kiberege na Idete. Nilipenda kujua, hao wafungwa wanalipwa chochote baada ya kumaliza kifungo chao? Maana wanalima miwa hasa Gereza la Kiberege na wanalima mpunga, machungwa na alizeti hasa katika Gereza la Idete.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na msongamano mkubwa sana na hii ni hatari kwa afya za mahabusu na wafungwa waliopo Magereza hayo. Hata kwenye hotuba ya Waziri ukurasa wa tano, Waziri ameonyesha suala hilo. Nimebahatika kutembelea Magereza, hali ni mbaya, inatisha, huduma kwa wagonjwa ni sawa na hakuna, hawapati mpaka hali inapokuwa mbaya ndiyo wanapelekwa hospitali. Hii ni hatari na wala haipendezi hata kama ni wahalifu, nao wana haki ya kupata huduma muhimu kama Watanzania wengine. Namwomba Waziri afuatilie hili suala kwa ukaribu. Tukiweza kutimiza wajibu wetu, naamini tunaweza kukuza uchumi wetu kupitia mahabusu na wafungwa kwa sababu wataweza kufanya kazi kwa kuwa watakuwa na afya njema, hasa kwa wafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la matumizi ya vituo hivyo ambavyo vilijengwa enzi za Mheshimiwa Mrema akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, vingi vimekuwa havitumiki na matokeo yake vimekuwa vikitumika kufanyia uhalifu. Mfano vibaka wamekuwa wakijihifadhi wakati wa usiku, wakisubiri kwenda kuvamia kwenye makazi ya wananchi na hata wengine wamevifanya vituo hivyo kuwa nyumba za kulala wageni, wanakwenda kufanya mambo ambayo siyo kusudio la Vituo hivyo vya Polisi. Tunaitaka Wizara ifuatilie suala hili ili Vituo hivyo viweze kufanya kazi iliyokusudiwa kwa manufaa ya Taifa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo malalamiko toka kwa wapiga kura wetu kuwa wamekuwa wakidaiwa rushwa na Polisi wanapofika kwenye Vituo vya Polisi kwenda kupata msaada wao. Wanaposhindwa kutoa rushwa hupata vitisho na kutishiwa kufunguliwa kesi za uongo, na matokeo yake wananchi wanaacha kwenda kwenye Vituo vyetu vya Polisi na kuamua kuchukua hatua mkononi mwao. Namwomba Waziri na viongozi wa Jeshi la Polisi kufuatilia suala hili ili tuweze kurejesha heshima ya Jeshi letu la Polisi. Najua siyo askari wote wanaofanya hivyo, lakini Waswahili wanasema samaki mmoja akioza, wote wameoza. Naomba sana huyu samaki mmoja tusimpe nafasi ya kuharibu Jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, hivyo basi, ni muhimu baada ya kazi apate mahali pazuri pa kupumzikia nikiwa na maana ya nyumba. Askari wetu wameoa na wengine wameolewa, leo hii askari hawa wanapewa chumba kimoja. Hivi kweli tunawatendea haki kweli! Sisi ni Waafrika, tena Watanzania, mila na desturi zetu zinaturuhusu kukaa chumba kimoja na watoto wetu wa kike na wakiume?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Wizara hii iongeze kasi katika ujenzi wa nyumba za askari wetu. Tunajua yako maeneo ambayo Wizara imeanza kujenga ila mengi bado ujenzi huo haujaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika upandishwaji wa vyeo kwa mujibu wa *PGO* inasema kama askari hajashitakiwa, anatakiwa apande cheo kimoja baada ya miaka mitatu. Lakini hayo yamekuwa hayafanyiki. Utakuta askari anakaa na cheo kimoja zaidi ya miaka na kuendelea, mtu anakaa na cheo cha *Constable* miaka kumi na ukiangalia kwenye *file* lake hana mashtaka. Ni kwanini hawa askari hawapandishwi vyeo? Hii inawakatisha tamaa vijana wetu, na kama tatizo ni kuwapandisha vyeo, basi tuwalipe misharaha kutokana na miaka aliyotumikia kama ni miaka tisa apewe mshahara wa *S/SGT* na miaka 12 apewe mshahara wa Meja – *A/INSP.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara ya askari wetu ni midogo sana ulilinganisha na gharama za maisha zilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeambiwa askari wanaokaa nje ya Kambi (uraiani) hupewa Sh. 45,000/= wengine Sh. 30,000/=. Pesa hizi bado ni ndogo sana, wote tunajua gharama za nyumba kwa sasa na nimeeleza toka mwanzo, chumba kimoja kwa familia ya askari hakitoshi. Hivyo, fedha hiyo haitoshi na ukizingatia wenye nyumba hawapokei fedha kwa mwezi moja,

wanapokea kuanzia miezi sita mpaka mwaka mmoja. Kwa utaratibu huu, askari wetu tunataka waishi vipi huko Wilayani?

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo yaliyokuwa yangu. Naomba yafanyiwe kazi ili Jeshi letu liwe la mfano na askari wetu wawezeshwe kwa kulipwa haki zao ili waweze kufanya kazi zao kwa moyo.

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kuipongeza Wizara na kumpongeza zaidi Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi - Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na Naibu Waziri wake - Mheshimiwa *Al-hajj Muadh'dham Al-habiyb* Khamis Kagasheki kwa umahiri, busara na hekima waliyokuwanayo katika kuiongoza Wizara hii. *Allah* awazidishie hekima hizo na awape afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia Kamanda Said Mwema *(IGP)* kwa busara alizokuwa nazo na wote wale walio chini yake. Naomba pia kuwapongeza Makamanda wote na Wakuu wa Idara zote zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote, naomba sana kuleta maombi kwa niaba ya Askari wa Mafia kuwa nyumba zao ni mbovu na hazifai, na wakati mwingine nasema hawana nyumba kabisa, wanaazima za Halmashauri. Hivyo naomba wizara ianze mchakato wa ujenzi wa nyumba za askari Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba sana, hivi sasa ujambazi na wizi wa uporaji mali upo au umeanza katika maeneo ya Baharini. Naleta ombi la kutaka kuanzishwe kituo maalum pale Mafia na kuweka Boti za *Patrol* ziweze kusaidia ulinzi katika bahari yetu na kitasaidia kuanzia maeneo yote ya Wilaya ya Mkuranga, Mafia, Kilwa na Rufiji. Maana hali ni mbaya sana baharini. Naleta maelezo haya na kukuomba hizi boti zilizopo Dar es Salaam japo mbili ziletwe Mafia na kuanzishwa kituo maalum cha ulinzi au uokoaji chini ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina zaidi, ila ni kuwatakia kheri viongozi wetu hawa wa Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jukumu kubwa la Mambo ya Ndani ni kuhakikisha usalama wa raia na mali zao kuwa usalama, ili Wizara kuwa imara, inahitaji vijana ambao wamesoma na wapo tayari kujitoa katika kulitumikia Taifa letu. Sasa zipo changamoto ambazo zinaweza kuwakatisha tamaa vijana wetu katika utendaji kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za kuishi watumishi wa Jeshi la Polisi ni mbaya/mbovu kupita kiasi. Je, Serikali ipo tayari sasa kufanya ukarabati na kujenga nyumba mpya kwa watumishi hawa wa Jeshi la Polisi? Ni mbaya/mbovu kupitia kiasi. Je Serikali ipo tayari sasa kufanya ukarabati na kujenga nyumba mpya kwa watumishi hawa wa Jeshi la Polisi hasa katika Jimbo langu ya Mufindi Kusini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mufindi Kusini lina vitu vidogo vya Polisi vitatu, navyo ni Kituo kimoja cha Kibao, kituo kidogo cha Malangali na Kituo cha Mgololo. Lakini tatizo kubwa ambalo linavikabili vituo hivi ni gari kwa ajili ya usafiri. Vituo hivi havina gari wala pikipiki, tukizingatia kwamba vinahudumia sehemu kubwa sana katika Jimbo. Naiomba Serikali kuwatafutia gari ili lisaidie katika shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru sana kama swala hili litatiliwa umakini wake.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuanza mchango wangu kwa kusema kwamba ninaunga mkono hoja.

Mheshimwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, yapo maeneo ndani ya Wizara hii yanayohitaji kupewa kipaumbele ili yaweze kumudu changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008, wakati nikichangia hoja ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani niliiomba Serikali kuangalia upya vipaumbele vyake vya kibajeti kwa majeshi yake ya ulinzi na usalama. Tofauti ni miaka ya 1960, 1970 na hata 1980 ambayo maadui wa nchi yetu walikuwa watu toka nje ya nchi ambapo fungu kubwa au bajeti kubwa ilitengwa kuwezesha Jeshi na Usalama wa Taifa, kuwezesha taasisi hiyo kutekeleza majukumu yake. Leo hii, maadui wa nchi yetu ni wa ndani humu humu, majambazi, vitendo vya uvunjifu wa amani. Hivyo ni wakati muafaka sasa Polisi, uhamiaji na hata Magereza wakapewa fedha nyingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, suala la vitendea kazi katika Jeshi la Polisi ni muhimu likatafutiwa ufumbuzi wa kudumu. Magari yapatikane ya kutosha, nyumba, mavazi na hata silaha. Haiwezekani na wala haingii akilini Wilaya kama ya Kahama kupewa lita 300 za mafuta kwa mwezi mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mambo haya yazingatiwe.

**MHE. RUKIA K. AHMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa sababu inaleta utulivu katika nchi na pia inalinda sana askari wetu wapewe taaluma nzuri ili wajue wajibu wao wasikiuke sheria. Pale askari anapovunja sheria, basi ndiyo panapotokea fujo ndani ya nchi na kusababisha maafa ambayo yangeliweza kuzuilika. Pawekwe adhabu maalum kwa askari Polisi, wanapovunja sheria ili iwe funzo kwao, mambo kama hayo yasitokee na kusabisha matatizo ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niishauri Serikali ijenge Magereza ya watoto ili tuondokane na ile hali ya kuwachanganya watoto na wafungwa watu wazima. Watoto wanapochanganywa na watu wakubwa, basi ni matatizo kwa sababu pale badala ya kupata mafunzo ambayo yangewafaa baadaye, wanakumbwa na majanga ya kufundishwa mambo ya kikubwa au pengine kufanyiwa mambo ambayo hayastahili kwao. Pia napenda niseme kwamba kuna baadhi ya Magereza wafungwa wanapewa kazi ngumu sana kiasi cha kuwa wafungwa wanapotoka pale wanakuwa ni wabovu, wagonjwa na inabidi wapewe matibabu makubwa wanapofika uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ucheleweshaji wa kufanya upelelezi wa kesi husababisha mlundikano mkubwa wa mahabusu ndani ya Magereza. Naomba mambo haya yashughulikiwe ili huu mlundikano wa mahabusu upungue.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hoja hii naomba nijikite katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali mbaya ya majengo ya nyumba za kulala na Ofisi za Askari Polisi, nashauri Serikali iongoze bajeti kwa ajili ya nyumba za ofisi na makazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa na mazoea ya Askari Polisi kupiga watu risasi kwa kisingizio cha kuwa ni majambazi, nashauri matumizi ya risasi za moto yakatazwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wa *Traffic* wanajazana barabarani, kila lori inalopita lazima lipigwe mkono, kwa nini? Lori linalosafiri kutoka Arusha kwenda Dar es Salaam linasimamishwa hadi mara 15. *Traffic Notification* inatumika kukomoa madereva wanaokataa kutoa rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Mbulu ni kubwa km. 6,000 za mraba ina gari moja tu. Tunaomba Wilaya hii ifikiriwe kupewa magari mawili au matatu. Moja iwe ya doria na nyingine iwekwe Dongobesh na nyingine Haydom.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuwe na *counter* mbili. Moja, ya wateja wa kawaida, pamoja na walalamikaji na nyingine ya washtakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi waache kupiga watuhumiwa. Mtuhumiwa siyo mkosaji, hata kama ni mkosaji, wakosaji wanaadhibiwa kisheria, siyo kupigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashauri Polisi wawe wapole na watumie lugha ya kistaaratubu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. ABUDL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii iliyowasilishwa leo. Naanza kuchangia hoja hii kwa kulizungumzia Jeshi la Polisi na hasa nilijikita kwenye Jimbo langu la Kibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Kibiti ndiyo kituo pekee katika Jimbo la Kibiti kinachohudumia Kata 15 zenye watu zaidi 150,000. Kituo hiki kina askari wasiopungua 36. Kituo hiki kina jengo ambalo lipo ndani ya hifadhi ya barabara *(road reserve).* Jengo hili la kituo limewekea alama kumaanisha kwamba linatakiwa libomolewe. Jengo hili ambalo hata Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani - Mheshimiwa Kagasheki analifahamu, jingo ni chakavu sana, wakati wa mvua linavuja jengo zima. Kibaya zaidi, kwa kuwa jengo lipo kwenye hifadhi ya barabara, hata ukarabati hauwezi kufanyika kwani, sheria ya ukarabati inakataza. Kwa hali hiyo basi, askari wa Kituo hiki hasa wakati wa masika husimama wima au kuhamisha majalada kutokana na kuvuja kwa jengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali ya Kijiji cha Kibiti ‘A’ kwa kuwaomba Askari hawa kupitia kwa Mkuu wa Kituo hicho waombe eneo lolote wanalolitaka kwa ajili ya kuhamisha kituo hiki. Namwomba Mheshimiwa Waziri afuatilie hilo na kuona namna ya kutatua tatizo hilo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jengo hili limewekwa alama (x), yaani bomoa, wananchi wa Kibiti ambao nyumba zao zimewekewa alama hizo wanakataa kuzibomoa mpaka jengo la kituo libomolewe kwa kuwa sheria ni msumemo, haibagui.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu madai ya Askari Polisi yanayotokana na malimbikizo yao mbalimbali. Askari wa Kituo hiki wengi wanadai marupurupu yao. Ni vizuri kwa Serikali kulipa madeni hayo ili askari wetu waishi kwa amani na wafanye kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu usafiri kwa askari hawa. Naishukuru Serikali kwa kutoa pikipiki chache ili kutumia kwa usafiri wa askari kwenda maeneo yao ya kazi. Ni vizuri kwa Serikali ikawapatia gari askari hawa, kwani wanahudumia eneo kubwa na gari la Wilaya lipo Utete ambako ni km 90 toka Kibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie Gereza la Kibiti. Naishukuru sana Serikali kusikiliza kilio changu cha kujenga Gereza hili ambalo mwanzoni lilikuwa na bati juu na chini. Hivi sasa jengo limekamilika na ni zuri, la kisasa. Hakuna tena mtondoo, kuna vyoo safi ambavyo vina *“flash*”, tatizo lake katika jengo hili ni uchakavu wa magodoro. Ni vizuri kwa Serikali ikazingatia hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Gereza hili kuna matatizo makubwa ya jengo la utawala na nyumba za askari. Jengo hili ni la udongo na limechakaa sana, baadhi ya kuta zimepinda na wakati wowote jengo hili litabomoka. Aidha, hata nyumba za watumishi ni za udongo na ni hatari kuishi. Naiomba Serikali, kwa kuwa imejenga gereza la kisasa, basi pia waboreshe ofisi na nyumba ili zilingane na Gereza ambalo wafungwa wanakaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Gereza hili ni la kilimo na wana ardhi kubwa, ni vizuri kuwapatia angalau trekta la mkopo ambalo watalitumia kwa ajili ya kilimo. Gereza hili lina ardhi kubwa yenye rutuba nyingi, naamini wakipewa trekta hata kama la mkopo wanaweza kurejesha kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri yeye binafsi na Jeshi letu la Polisi kwa utendaji mzuri wa Askari polisi wetu. *Please keep it up*. Wasichoke, pamoja na kwamba wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Askari Polisi wetu wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mishahara ya Askari Polisi wetu, hasa wale wa kima cha chini iboreshwe. Pia posho na stahili zao ziwe zinalipwa kwa muda unaostahili. Siyo jambo jema kumkopa askari posho zake halafu huku unampa bunduki. Hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi wetu waongezewe mishahara na posho, kwani hii itasaidia sana katika kuboresha utendaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la wakimbizi kwa niaba ya wananchi wa Ludewa, sisi sote na mie mwenyewe kama Mbunge wao, hatuwataki hao Wwakimbizi kwa sababu zifuatazo:-

Mpango wenyewe ambao unalenga kuwaleta wakimbizi 350 Ludewa haujawa shirikishi. Wananchi wa Ludewa hawajaandaliwa kisaikolojia namna ya kuwapokea wageni/wakimbizi hao. Mila na desturi za watu hawa (wakimbizi) hazifanani na mila zetu kule Ludewa. Wakimbizi ni watu wa vita na ni watu walioshindikana kwa makosa mbalimbali ya jinai na kadhalika. Ludewa hatutaki vita. Tanzania hatutaki vita. Hatuwataki wakimbizi Ludewa.

Sisi tunaamini kuwa Rais ameshauriwa vibaya kuhusu mpango huu, na tunaamini Wizara itamshauri asitishe maamuzi yake ya kuwapokea hawa wakimbizi. Hawa wakimbizi hawana tija wala manufaa yoyote kwa Wanaludewa. Ahsante

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo katika Bunge lako Tukufu nami nikawa miongoni mwa wawajibikaji wa kusimamia utumishi wa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia hii ya maandishi, naomba nichangie kwa kutoa shukrani za dhati, kwa upande wa Jeshi letu la Polisi, kuhusiana na kusimamia vyema uchaguzi wa mwaka 2010 kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi ulisimamiwa vizuri sana japokuwa kulikuwa na kasoro ndogo za kibinadamu. Kwa shukrani hizi, naomba kwa heshimwa zote niishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya CCM isimamie zaidi utaratibu huu mzuri wa kusimamia amani na utulivu katika shughuli hii ngumu ya suala zima la uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda huu mfupi, napenda nieleweshe Bunge lako kwamba Zanzibar imeanza ukurasa mpya ambao ni heshima kwa Wazanzibar, Tanzania na duniani kote.

Mheshimimiwa Naibu Spika, pili nataka nieleze masikitiko yangu kwa upande wa Serikali, pamoja na mpango mzuri wa Mheshimiwa Waziri na taasisi zake zilizo chini yake kwa kujiandaa na mwaka huu wa fedha katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ielewe kwamba Wizara hii ni Wizara nyeti, na Wizara yenye majukumu magumu. Kwa hiyo, naishauri Serikali ielewe kwamba jeshi letu linakabiliwa na changamoto nyingi kama vile majengo chakavu ya vituo, hawana nyumba za kuishi Askari Polisi, posho zao ni ndogo zilizoendana na kazi yao ngumu, mishahara midogo isiyokidhi haja sana, wanaofaidika ni maafisa peke yao. Hawana vyombo vya mawasiliano vya kisasa kama vile redio, vyombo vya usafiri kama magari, pikipiki, sasa wanatumia simu za mikononi zisizo na uhakika wa mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi letu limekabiliwa na rushwa kupita kiasi. Hasa wale wa usalama barabarani. Lakini hakuna kosa, hii imesababishwa na Serikali yenyewe kwa sababu hawashughulikiwi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali sikivu ya Jamhuri ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itenge fungu la kutosha kwa askari wetu ili waweze kumudu shughuli zao vema, askari wetu walipwe malimbikizo ya madini ambayo wanadai, posho, malimbikizo ya tatizo na mahitaji yao wapatiwe kwa wakati na posho ziongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wale askari wastaafu wapatiwe haki zao za viinua mgongo na pensheni, wapatiwe mapema kwa wakati unaofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano iendelee kulinda, kudumisha na kusimamia amani na utulivu uliopo Zanzibar kwa sababu ndiyo roho ya Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba nzuri na mikakati madhubuti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kulipongeza sana Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri nchi nzima na hasa Mkoa wa Dar es Salaam ambapo imekuwa shwari kwa muda mrefu. Naomba nimpongeza sana Kamanda Selemani Kova na wenzie, Makamanda wa Mikoa ya Temeke, Ilala na Kinondoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Maslahi duni, hawana nyumba, mimi nakaa karibu na Kituo cha Polisi Mabatini, jina hilo linatokana na kwamba nyumba za Polisi wa Kituo hicho ni *full suit* ya mabati chini hadi juu, unaweza kufikiria ni aina gani ya nyumba, Polisi hao wanakaa vyumba vinakatwa kwa njia ya shuka na kanga. Mara nyingi unakuta wamelala nje kwa joto. Lakini hali hii ipo kwenye vituo vingi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa Wizara kurekebisha hali hii. Inawezekana hata ikiwa kwa awamu. Wenzangu wanasema adhari ya Polisi kukaa nje ya Kambi tunawatia kwenye majaribu makubwa sana, lakini Polisi wana maeneo makubwa mazuri kama *Oysterbay Police*, Kawe, *Kilwa Road*, pale *opposite* na *petrol station,* kote kunaweza kujengwa majumba mazuri na makubwa kama yale ya *Kilwa Road* ambayo yanaweza kuwaweka polisi katika hali ya heshima na kuwaondoa kwenye mazingira ya ushawishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi ni binadamu na wana mahitaji ya kawaida na maendeleo kama wengine. Kwa nini Serikali isizungumze na vyombo vya fedha na siyo lazima mabenki, lakini hata mifuko ya pensheni ili ikawakopesha wakaweza kujenga nyumba zao nzuri, wakanunua usafiri na hata mitaji ya biashara kwa wenza wao ili waweze kuongeza kipato kama wenzao wengine. Naomba hili liangaliwe kwa karibu, linawezekana na Wizara kama mwajiri ndiyo iwe dhamana yao na mikopo hiyo isiwe ya miaka miwili mitatu, hapana iwe ya miaka 15 mpaka 20, na Wizara ihakikishe inakata mishahara ili kulipia madeni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza yetu yana hali mbaya sana. Mimi nilikwenda pale Segerea kumwangalia mtu ambaye alikuwa kakamatwa hata Mahakamani hajapelekwa. Dirisha la kuangaliana na kuzungumza lilinifanya nipandishe *pressure,* maana hali yake ilikuwa mbaya sana, limejaa vumbi na kila upande umejaa watu wanaongea, hata pombe *shop* watu wanasikilizana. Huyu alikuwa mahabusu tu, alikaa pale kwa mwaka mmoja bila dhamana, na baadaye akaachiwa kuwa hana hatia. Mimi sielewi kama wakitoka kule, akili za wale ambao siyo wahalifu bado zinakuwa timamu, maana mimi nadhani wanaweza kufa kwa *depression.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza ni sehemu ya kumrekebisha mfungwa ili abadili tabia. Kwa nini basi kwa makosa madogo madogo tusiwapeleke kwenye *community centre* ili kuondoa msongamano, na wanaweza kupewa mafunzo huko?

Mheshimiwa Naibu Spika, wafungwa wanachanganywa vijana wadogo na watu wazima. Kuna uvumi wa vitendo vya kuvunja haki za binadamu kwa vijana wadogo vinavyofanywa na watu wazima. Naomba jambo hilo lichunguzwe na kwa nini kusiwe na sehemu tofauti kwa watu wa rika tofauti?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba masuala yafuatayo yashughulikiwe na Wizara.

(1) Gari la Uhamiaji la Wilaya Nkasi kuwa Sumbawanga;

(2) Kutokuwa na Afisa Uhamiaji wa Wilaya kwa muda mrefu; na

(3) Upungufu wa askari katika Vituo vya Mwambao mwa Ziwa Tanganyika katika Vituo vya Kirando na Kabwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuongezwe Vituo vya Polisi katika Vijiji vya Korongwe na Mkinga Mwambao mwa Ziwa Tanganyika kutokana na vitendo vya mara kwa mara vya ujambazi hasa katika nchi jirani ya Congo na kuwapora wananchi mchana au usiku pia itasaidia hata raia kutoka Congo kutoingia katika vijiji hivyo bila mpangilio.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni Askari Polisi kukaa katika Kituo cha Wilaya kwa muda mrefu sana wengine hata zaidi ya miaka 15 na askari kupandishwa vyeo, lakini mishahara kusalia kiwango hicho hicho cha mwanzo kwa muda mrefu.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuleta hotuba nzuri sana hapa Bungeni. Pamoja na kuunga mkono hotuba hii, ninayo machache ya kuiomba na kuiasa Serikali kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu niingie Bungeni mwaka 2005, hadi leo hii nimekuwa nikisema tatizo la wahamiaji haramu wa mifugo yao kutoka nchi ya Rwanda na Uganda kuingia katika nchi yetu kama wanavyotaka. Wahamiaji hawa haramu wamejitwalia maeneo ya Wilaya ya Karagwe, Ngara, Biharamulo, Muleba, Kyerwa, Chato na Misenyi. Wameingia maeneo haya na kuvamia malisho ya mifugo kwa nguvu. Ni wababe sana, wanapiga watu, wanadharau na wameamua kuanza kuua Watanzania. Mfano halisi ni mauaji yaliyotokea Wilayani Ngara, watu sita, raia wa Tanzania waliuawa kinyume na wahamiaji haramu hawa kwa kutaka kuhalalisha uvamizi wa ardhi ya nchi yetu. Walioumizwa sasa ni wengi sana. Pia wavamizi hawa haramu, wengi wao hujihusisha na ujambazi na wizi wa mali za Watanzania waishio Mikoa ya Kagera na Kigoma. Wizi ndiyo usiseme kabisa. Sasa hivi ninavyoandika, raia wawili wa Rwanda ambao wanafuga ng'ombe wao katika ardhi ya Tanzania Wilayani Ngara wamekamatwa kwa wizi wa mifugo na kesi inaendelea katika Mahakama ya Wilaya ya Karagwe. Ng'ombe wanaotuhumiwa kuibiwa na Wanyarwanda hao walikamatwa katika mazizi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuwa watu hawa wana nguvu ya fedha sana kuliko wananchi wetu wa kawaida. Nasema hivyo kwa sababu hata viongozi ngazi ya vijiji, Kata, Wilaya Mkoa hata Taifa wamezidiwa nguvu kwa sababu ya rushwa. Hata viongozi wa TAKUKURU mfano Bosi wa TAKUKURU Wilaya ya Karagwe anawalinda kwa nguvu zote kwa masikitiko ya raia wa Watanzania. Wakikamatwa wezi kutoka Rwanda anatumia nguvu za ofisi ya TAKUKURU ili kuwalinda wasifikishwe Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Kagera, imeshindwa kudhibiti hali hii. Baadhi ya Wakuu wa Idara hizi za Wilaya, siyo wazalendo hata kidogo. Hata baadhi ya Wakuu wa Wilaya ni wasaliti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali iamke sasa, iondoe wahamiaji haramu wote na mifugo yao kama ilivyofanya mwaka 2006. Pia iweke mkakati madhubuti wa kukomesha

hali hiyo moja kwa moja *(once and for all).* Sisi wananchi wa Wilaya ya Karagwe na Mkoa mzima wa Kagera tunataka kuishi na kutumia ardhi ya Tanzania kwa manufaa yetu na siyo kunufaisha Wanyarwanda na Waganda. Serikali iache uzembe wa kushindwa kulinda mipaka ya nchi yetu. Serikali isiruhusu Wanyarwanda na Waganda kufanya shughuli, ni dharau kubwa sana kwa Taifa letu. Serikali ifanye utafiti haraka katika nchi ya Rwanda ili ione jinsi Rwanda ilivyoamua kuondoa mifugo yote ya kuchunga na badala yake mifugo inayoruhusiwa kwa kila kaya ni ng'ombe wasiozidi wawili. Baada ya uamuzi huo wa Serikali ya Rwanda, mifugo yote ya Wanyaranda iko Tanzania. Ni kwa nini Tanzania iruhusu hali hii? Wananchi wa Karagwe, Ngara, Muleba, Biharamumo, Misenyi wametutuma sisi Wabunge wao tulete kilio hiki cha siku nyingi.
Tunasubiri operesheni ya nguvu ya uhakika ya kumaliza tatizo hili.

Mwisho, nakumbushia tena madai ya fedha za uhamisho za maaskari wa Karagwe na wenzao sehemu nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa maoni yangu kuhusu hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuwapatia wananchi mafunzo ya ulinzi shirikishi ili wawe tayari kujilinda katika maeneo yao ni mzuri. Lakini utaratibu wa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Kitengo cha Polisi Jamii kusambaza vitabu vya mpango huo kwa wananchi, siyo utaratibu wa kuweza kufikia wananchi wengi. Wananchi wengi zaidi wahamasishwe na kuelimishwa kwa kutumia Vyombo vya Habari kama vile redio, njia ambayo wananchi wengi zaidi wanaweza kufikiwa kwa wakati mmoja. Napendekeza Polisi jamii wawe na kipindi chao maalum cha redio cha kila wiki na kitangazwe mapema ili wananchi wengi waweze kukifuatilia. Hii itasaidia kupunguza uhalifu ambao wamekithiri na hasa Mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Polisi vina hali mbaya sana. Kwa mfano, Kituo cha Mwenge jijini Dar es Salaam, hakina vitendea kazi, jengo lenyewe lina hali mbaya, sakafu imebomoka na kubakia udongo. Mazingira mabaya ya kazi yanaweza kuwa kichocheo cha Polisi wetu kukubali kupokea rushwa. Fedha ya kutosha itengwe na Vituo vya Polisi nchi nzima viboreshwe, viwe vya kisasa, vyenye vitendea kazi kama vile karatasi kompyuta na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kituo cha Polisi cha Mbuguni Arusha kina Polisi wawili wa kiume na hakuna Polisi wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahabusu wa kike hawatendewi haki kuhudumiwa/ kushughulikiwa na askari wa kiume. Nashauri vituo vyote nchini visivyo na askari wa kike vifikiriwe kupatiwa askari wa kike ili kulinda haki za binadamu kwa mahabusu wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho vya Taifa ambavyo vitatengenezwa na kampuni kutoka Malysia ya *Iris Corporation*, mradi huo uharakishwe, kwani vitambulisho vya Taifa vitasaidia sana kupunguza uhalifu, kwani itakuwa rahisi kubaini wale wote ambao siyo raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya *biogas* na nishati nyingine mbadala zitasaidia kupunguza ukataji wa miti kwa lengo la kuhifadhi mazingira. Ningependa kujua, kwa nini mradi wa matumizi ya nishati mbadala Magerezani haujapewa umuhimu, kati ya Magereza mengi tuliyonayo hapa nchini? Mpaka sasa nusu karne ni Gereza moja tu la Ukongwa limekamilishiwa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba kuna kero ya usafiri wa abiria ya kusimamishwa katika sehemu mbalimbali kutoka Mkoani kwenda Chake Chake ni karibu 29 km. Gari ya abiria katika hali ya kawaida kutoka Mkoani husimamishwa mara nne! Husimamishwa na askari wa usalama barabarani sehemu ya Mtuhaliwa

Kituo cha pili ni Polisi Tutambile, sehemu ya tatu ni meli mbili karibu ya Chake Chake na sehemu ya nne ni Polisi Chake Chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zinazofanywa na askari wa usalama wa barabarani za kusimamisha gari za abiria wacha ziendelee. Lakini ule utaratibu wa kudumu katika Vituo vya Polisi gari za abiria kusimamamama, uachwe kwani unasababisha usumbufu usio wa lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kuwa kusimamishwa kwa magari kwenye vituo vya Polisi ni kulinda usalama wa nchi, haina uzito. Mkoa wa Kaskazini Pemba wanaofanya kazi za barabarani ni askari wa usalama barabarani. Bado usalama katika Mkoa wa Kaskazini Pemba ni salama. Kwa hiyo, naomba Serikali iondoe utaratibu huo wa gari za abiria kila zikifika Kituo cha Polisi Chake Chake, Mtambile na Mkoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka 2010/2011 ya Wizara hii iliahidi kufanyia matengenezo Kituo cha Polisi Kengeja. Bahati mbaya kituo hicho hakijafanyiwa matengenezo na hata bajeti ya mwaka huu 2011/2012 kituo hicho hakikupangiwa kufanyiwa matengenezo. Je, ni sababu zipi zilizosababisha bajeti iliyopita kituo hicho hakikufanyiwa matengenezo? Kwa nini bajeti ya mwaka huu kituo hicho hakikupangiwa kufanyiwa matengenzo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kusini Pemba una Wilaya ya Chake Chake na Mkoani. Wilaya ya Chake Chake wameshajengewa nyumba huko Mfikiwa. Jambo la kusikitisha Wilaya ya Mkoani bado haikujengwa nyumba mpya tokea uwepo huu Muungano wa Tanzania. Hali ya nyumba (makazi) za Polisi Mkoani ambapo ndiyo Makao Makuu ya kijeshi ni mbaya mno. Kuna mabanda mawili yaliyojengwa kwenye miaka 1928 na nyumba mbili za ghorofa zilizojengwa katika miaka ya 1950. Hali ya makazi ni mbaya sana. Askari anaishi na familia yake yenye watoto wakubwa wa kike na wakiume katika chumba kimoja. Hali hiyo inasikitisha na ninauliza Serikali ni lini wataanza kujenga makazi ya Polisi Mkoani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja ya Wizara kutokana na mabadiliko ya ujanja wa wahalifu askari wa upelelezi wapewe taaluma ya kukabiliana na wahalifu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili la mafunzo, naomba askari wa Upelelezi wa Polisi Mkoani wawe wa mwanzo kwani inayoonekana wametetereka katika upelelezi wa kesi, badala yake upelelezi kwao ni kulundika wananchi ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, naomba mtoe mfano hai, vipi Askari wa Upelelezi Mkoani, siku moja alikwenda kijana mmoja na kutoa taarifa Polisi kuwa amepigwa na vijana watatu. Wasifu wa kijana huyo unaeleweka katika Mji wa Mkoani kwamba ni mropokaji (msema ovyo) na pia inaonekana ana athari ya akili inayoonekana. Mfano baadhi ya kanga huwa na karatasi yenye picha ya mwanamke. Karatasi hiyo amewahi kuonyesha watu mbalimbali nikiwemo mimi na Mheshimiwa Haji Faki kuwa huyo ndiye mke wake. Pia mazungumzo yake kwenye simu hujifanya kuwa ni mfanyabiashara mkubwa na anategemea kupokea makontena. Pamoja na hali hiyo aliyo nayo kijana, Polisi baada ya kuripotiwa tu bila ya upelelezi waliwaweka ndani vijana watatu ambao ni Mohamed Kenya, Salum Abudulla na Ali Ame kuanzia Ijumaa mpaka Jumatatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumpokea huyo kijana hapo Polisi ni haki yake na kuchukuliwa na kuhojiwa hao vijana pia ni haki ya Polisi kufanya hivyo. Ninachotilia mashaka, ni kwa misingi gani vijana hao kuwekwa ndani ikitiliwa maanani mpelekaji habari, hali yake ni kama nilivyoelezwa hapo juu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, ndio naomba kuwa askari wa upelelezi wa Mkoani wapatiwe mafunzo ya upelelezi.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na kumpogeza Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Vuai Nahodha - Naibu Waziri Mheshimiwa Balozi Kagasheki Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa hotuba nzuri na fupi aliyoiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na yafuatayo: Hali ya nyumba za Polisi kwa kweli inasikitisha. Nilichangia kwa uchungu sana katika hotuba ya Waziri Mkuu. Ningeomba askari wetu wakumbukwe. Nasikitika kuona askari wanaishi uraiani, maeneo yalipo nyumba za askari yangejengwa maghorofa, ingezaidia hata kupata maeneo ya viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilolo ni mpya, lakini haina Ofisi za Polisi za Wilaya, hakuna nyumba za kuishi askari, Mkuu wa Kituo anaishi nje ya Makao Makuu ya Wilaya. Naomba kama kuna mpango wowote, tupatiwe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Kihesa Mgagao ambalo lilitumika kama kituo cha wapigania uhuru wa Afrika ya Kusini, leo hii Serikali yetu imegeuza kituo hicho kuwa Gereza. Serikali haioni kuwa inavunja heshima kwa wapigania haki hao kama Nelson Mandela Walter Sesulu, Thabo Mbeki na kadhalika ambao walipita na kukaa katika ile Kambi? Lile eneo lingetumika kuwa eneo la kutoa elimu ili kuenzi viongozi hao kama ilivyofanya eneo la Dakawa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wafungwa wanawake, hivi huwa siku zote najiuliza wanawake wajawazito wanapofanya kosa wakahukumiwa kufungwa; hivi watoto wao wanawekewa utaratibu gani? Kuna bajeti yoyote wanayotengewa wafungwa wanawake kwa ajili ya kupata vifaa vya kujihifadhi kwa mwezi? (Wakati wa hedhi).

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa sana kuhusu wiki hii ya usalama barabarani, askari wametumia muda huo kuuza stika na siyo kufanya ukaguzi. Inatia aibu sana kwa Serikali yetu, utakuta magari mabovu yanawekwa stika na stika zinauzwa kama maandazi, kama vile Mradi wa Polisi kuwasaidia askari wake kupata pesa. Naomba jambo hili lisipuuzwe, sababu askari ana vitabu viwili. Hili siyo siri, naamini mnalifahamu na ndiyo maana ajali nyingi zinasababishwa na ubovu wa magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, adhabu anayopewa dereva anayesababisha ajali ni ndogo sana, hivyo husababisha kuendelea kurudiwa kwa makosa hayo kwa makusudi. Pia umekuwepo uvunjifu mkubwa sana wa sheria kwa madereva hasa wa magari ya madaladala, kwa sababu adhabu ile mtuhumiwa haimtambui. Napendekeza kiwango cha adhabu kiongezwe kama wanavyofanya *SUMATRA* ikisaidia sana kupunguza vurugu barabarani.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika hoja hii maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza Sekta hii ya Zimamoto kwa maana ya vifaa vya kutendea kazi pamoja na raslimali watu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko ya mara kwa mara kwa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia hasa kwa askari wa kike, hasa pale wanapotaka kujiendeleza kielimu. Je, Waziri anatoa ufafanuzi gani na Wizara ina mikakati gani ya kuwaendeleza askari wake wa kike ili waweze kufikia ngazi za juu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango gani wa kutoa mafunzo ya awali ya ulinzi shirikishi kwa wananchi/raia wasio askari wanaoshiriki katika ulinzi? Pia ni kwa namna gani wananchi hao wanashirikishwa? Kwani kumekuwa na malalamiko kwamba wananchi wamekuwa wakitozwa michango mbalimbali kama betri na vinavyofanana na hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara hii itoe ufafanuzi wa suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha - Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba yake nzuri yenye mwelekeo thabiti na inayotoa matumaini kwa Watanzania. Aidha, nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Inspekta Jenerali wa Polisi, Makamanda, Askari pamoja na Watendaji wote

wa Wizara hii yenye jukumu kuu la kulinda usalama wa raia na mali zao. Nawapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, natamka kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mchango wangu utajikita katika maeneo mawili ya Hotuba ya Waziri. Maeneo hayo ni Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri linalofanya katika mazingira magumu, hasa katika kukabiliana na uhalifu wa aina mbalimbali, licha ya uhaba wa raslimali, uchache wa vitendea kazi na idadi ndogo ya Askari Polisi katika nchi yenye watu wanakisiwa kuwa milioni 42, ikilinganishwa na idadi ya askari wasiozidi 39,000 ambao ni askari mmoja kwa watu 1,105.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hii, Jeshi la Polisi lina changamoto nyingi na Bunge lako Tukufu lazima lijipambanue kama mtetezi Mkuu wa Jeshi la Polisi. Naungana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, ulinzi na usalama kuiomba na kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Jeshi la Polisi. Napendekeza ongezeko la bajeti lielekezwe katika maeneo ya vipaumbele vya jeshi hilo hasa upanuzi wa vyuo vya Polisi nchini. Upanuzi wa vyuo hivyo, utawezesha kuchukua kuruta wengi na hatimaye kujenga uwezo wa kukuza ajira ya askari. Jeshi la Polisi sharti liwe na mpango wa muda wa kati na muda mrefu wa kupanua ajira ya askari kulingana na idadi ya watu inavyoongezeka (2.9% pa).

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa nyingine ni ile ya kuboresha makazi ya Askari Polisi na Magereza kwa kujenga nyumba bora. Nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kubuni njia mbalimbali za kupunguza tatizo hili ikiwa ni pamoja na kushirikiana na baadhi ya Mifuko ya Pensheni ili kuboresha makazi ya Askari Polisi. Nashauri juhudi ziongezwe kwa kubuni mikakati itakayowezesha Jeshi la Polisi na Magereza pia kuingia ubia na sekta binafsi *(through public – private partnership)* ili kuboresha makazi ya askari hao.

Aidha, Jeshi liangalie uwezekano wa kununua mashine za kufyatua matofali ya aina ya *hydroform* ili kuwezesha kuwa na *building brigade* itakayofanya kazi ya ujenzi wa kujenga nyumba bora. Wenzetu nchini Rwanda wamepiga hatua kubwa katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie kwa kifupi suala la uhalifu nchini. Mikoa ya nchi yetu inatofautiana kwa ukubwa wa maeneo pamoja na idadi ya watu. Kutokana na uchache wa Askari Polisi hapa nchini Mikoa ya Shinyanga na Mwanza na mingine inakuwa na matukio mengi ya uhalifu yanayowaelemea Polisi. Je, Waziri anasema nini kuhusu hali hii? Je, haingekuwa vizuri Idadi ya Polisi ikaongezwa katika maeneo hayo kwa kuwa yana matukio mengi ya uhalifu?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Bariadi Magharibi lipo Gereza katika Kijiji cha Matongo. Gereza hili lilianzishwa mwanzoni mwa miaka ya themanini kama Gereza la Kilimo. Gereza hili linamiliki eneo kubwa sana la ardhi. Hali ya Gereza hili ni ya kutisha na huko nyuma Serikali iliwahi kulaumiwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kama hili halitoshi, Gereza hilo halina zana za kilimo na kusema kweli halifanyi tena kazi ya kuzalisha chakula kama ilivyokusudiwa wakati linaanzishwa. Mwaka 2006 wananchi waliomba warejeshewe eneo hilo. Majibu ya Serikali yalikuwa ni kwamba Jeshi la Magereza lilikuwa linatafuta mwekezaji wa kuingia nalo ubia kwa shughuli za kilimo. Hadi leo hakuna shughuli yoyote ya kilimo inayoendelea pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu na wananchi wa eneo la Matongo, hatima ya Gereza hilo na eneo linalomilikiwa na Gereza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata ufafanuzi toka kwa Waziri juu ya malalamiko kutoka kwa Polisi wa Wilaya ya Karagwe. Mkoa wa Kagera wana tatizo la umeme, ambapo kila familia ya watu kumi askari wanatumia mita moja ya luku. Matokeo yake askari wanalazimika kununua umeme wa Sh. 20,000/= kila wiki wakati kila familia ina matumizi yake

binafsi ya umeme. Wameomba kila familia iweke mita yake, Mkuu wa Polisi wa Wilaya *(OCD)* amewaambia kila askari atoe Sh. 500,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua vipato vidogo vya askari wetu. Naomba Waziri alifanyie kazi jambo hili kwa umakini. Vile vile ningependa kujua ni Shilingi ngapi zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za askari wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimboni kwangu Kawe, Serikali imekuwa haitoi huduma ya kulipia bili ya umeme katika baadhi ya Vituo vya Polisi, matokeo yake askari pamoja na kipato chao kidogo wanalazimika kununua umeme wa luku kwa gharama zao wenyewe. Naiomba Serikali ifanyie kazi hii kero inayowakumba askari wetu Jimbo la Kawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko dhidi ya Kampuni ya *Zantel,* kwa nyakati tofauti kumekuwepo na hujuma kwa Watanzania wenye uwezo wa kufanya kazi. Hivi sasa, kitengo cha *Human Resources* kinaongozwa na Mhindi ambaye ameapa kuwafukuza Watanzania na kuleta Wahindi (kitu ambacho kinaendelea kwa sasa). Hoja yao kubwa ni kwamba wameweka Serikali ya Tanzania mfukoni mwao, hasa Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili suala lifuatiliwe kwa umakini hasa ikizingatiwa kwamba *Zantel* inamilikiwa kwa pamoja na Kampuni ya *Etisalat* ya Abudhabi na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tuhuma kwamba kuna Mhindi ameletwa kinyemela anaongoza kitengo cha Manunuzi, amepewa cheo chake cha *Procurement Director*, lakini yeye ni *Accountant* na taarifa zote zipo. Alipokuja nchini alipewa kibali cha kufanya kazi Tanzania, kibali kilikwisha tarehe 18 Juni, 2011, ajabu ni kwamba anaendelea kuwepo nchini licha ya muda wa kibali kwisha. Uhamiaji walikwenda *Zantel* tarehe 21Juni, 2011 wakafanikiwa kumkamata na kwenda naye uhamiaji na kumpatia kibali siku hiyo hiyo. Tumeikashfu Serikali na Idara husika kwamba pesa inaongea! Huu ndio utaratibu? Sheria ndizo zinasema hivi? Huyu Mhindi anaitwa Nanshad Mohamed. Kama hiyo haitoshi, kuna mfanyakazi kutoka Ireland anaitwa Alina Malan, yeye anafanya kazi kwa kujificha. Wafanyakazi wa kigeni wamekuja nchini kwa malengo ya kufanyia kazi Kampuni nyingine, lakini wanafanya *Zantel*. Naiomba Wizara ichunguze kampuni hii kwa umakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kupata maelezo ya kina, ni kwanini Gereza la Mahabusu Mpanda Kalila na Magereza nyinginezo nchini hazifanyiwi ukarabati? Gereza la Mahabusu Mpanda ambalo nimekuwa nikilisema mwaka hadi mwaka, leo ni mwaka wa sita hakuna hatua imechukuliwa kukarabati Gereza hili. Mbali na ahadi nyingine, kule Gerezani wapo Watanzania wenzetu, kesho mimi au wewe utajikuta ni mgeni wa Gereza. Hali ni mbaya sana. Kadhalika makazi ya askari wa Magereza na Polisi Mpanda hazitoshelezi na zipo katika hali mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipotembelea Gereza la Mahabusu Mpanda yamekuwepo malalamiko mengi dhidi ya Jeshi la Polisi, Idara ya upelelezi kwa kuchelewesha kesi zao kwa kisingizio kwamba upelelezi haujakamilika. Wanadai pia wanapata mateso na uvunjaji wa haki za binadamu kwa kiwango cha hali ya juu kabisa, wanakaa mahabusu kwa muda mrefu hata kwa kesi ndogo ndogo na mlundikano unatisha katika Gereza ambalo uwezo wake ni watu 90. Nimekuta wafungwa na mahabusu kwa karibu zaidi ya 100 ya uwezo wa Gereza. Ipo haja kuongeza ufanisi katika Idara ya Upelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo malalamiko na stahili za askari wa Zimamoto ambao ni waajiriwa wa Halmashauri zetu. Hivi kwa sasa hatuoni upo ulazima sasa Jeshi hili la Zimamoto kuwa chini ya Komandi moja badala ya mfumo wa sasa wa kila taasisi kuwa na jeshi lake. Nadhani sasa ni wakati muafaka kuliangalia upya suala hili la kuwa na Komandi moja ili malalamiko/ Stahili/Madaraja vyeo na kadhalika vingekuwa vinasimamiwa katika mfumo mmoja ili kuondoa hizi kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lipo tatizo la muda mrefu wa mipaka ya Gereza la Kalila limehodhi ardhi isiyotumika na wananchi wanaozunguka Gereza hili kukosa ardhi kwa ajili ya Kilimo. Ni vyema sasa suala hili likapata ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, dhuluma ambayo wanafanyiwa waliokuwa wakimbizi katika makazi ya Katumba na Mishamo wanaotakiwa kuhama kupewa Sh. 300,000/= na kuvunja makazi yao bila kujali thamani halisi ya mali watakazoharibu kabla ya kuhama na Sh. 300,000/= ndiyo nauli na akajenge makazi mapya aendeko bila kujali gharama za maisha leo, lakini kumbukeni mmewapa wenyewe uraia tena kwa kutupa kwa ada ya dola 50, badala ya ada ya dola 800, tumewafurahisha wakubwa *UNHCR*.

**MHE. HAROUB M. SHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *(SW)* kwa rehema na neena zake nyingi anazoendelea kunijalia *(Alhamdulillah).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa utulivu na amani yetu iliyomo ndani ya nchi kama ilivyo nembo ya Jeshi la Polisi, usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze Wizara hii hasa Jeshi la Polisi kwa kushiriki kusimamia amani na utulivu katika Uuchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Shukrani za pekee ziende kwa Inspekta Jenerali wa Polisi (*IGP)* - Said Mwema kwa kufanya *restructuring* katika Jeshi la Polisi na kujitahidi liwe Jeshi la kisasa lenye kuaminiwa machoni mwa jamii. Wameonyesha mwanzo mzuri, nawapongeza na mimi nasema hongereni sana na endeleeni kutenda mazuri na haki kwa raia ili wananchi wazidi kuwaamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifanye wajibu wake ili Wizara hii na taasisi zake zifanye kazi vizuri. Jeshi la Polisi wapewe elimu ya utendaji, wajue haki zao na za wanaowalinda (wananchi), wapewe mafao yao kwa wakati na usawa. Waongezewe mafao yao yalingane na hali ya maisha. Waboreshewe makazi na sehemu za kazi. Ajira zitolewe kwa usawa, bila kuajiri kwa kujuana, upendeleo, rushwa na kadhalika. Askari wapandishwe vyeo kulingana na elimu na uwajibikaji wao na siyo vinginevyo. Askari wanaofanya uzembe kazini washushwe vyeo ili iwe ni mfano kwa wengine wawajibike.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo changamoto nyingine nyingi zinazohitaji kuangaliwa ili Jeshi letu la Polisi liwe la kisasa na lisiendelee kulaumiwa bali lisiwe ni Jeshi la kupongezwa. Liendane na nembo yao *Crown* wanayovaa Usalama wa Raia na mali zao. Kuwe na *accountability* ili viongozi wawajibike kwa makosa yaliyo chini yao ili kujenga heshima ya Jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara hii ni muhimu sana kwani isipokuwa na uaminifu inaweza ikawapa uraia watu wabaya na kuliletea maafa Taifa letu. Ni lazima Uhamiaji wawe waadilifu kwa pande zote. Wasiwasumbue raia wema kuwapa hati za kusafiria baada ya kukamilisha taratibu kwani ni haki yao, wasiwape wageni uraia kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza pia inapaswa kufanya kazi kwa uadilifu. Mahabusu wasiwatese na wawape mahitaji ya lazima kama binadamu. Chakula bora, malazi, vyoo, matibabu, yote haya ni haki za msingi kupatiwa mahabusu na hata wafungwa kwani ni haki zao za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu wengi waliondoka nchini kwa namna moja au nyingine na kwenda Uughaibuni ili kutafuta malisho bora. Wapo walioondoka baada ya kusomeshwa na Taifa, na wapo walioondoka hawajasoma vizuri, huko nje wakajiendeleza na masomo katika mazingira magumu, lakini sasa ni wataalam. Ili waweze kupata malisho mazuri huko nje, iliwabidi waombe uraia wa nchi hizo na uraia wao wa asili ukafa ghafla! Kati yao kuna wengi uzalendo umewazidi na wameanza kurudi nyumbani na kulitumikia Taifa katika fani mbalimbali katika hali ya kuwa wao ni wageni nyumbani kwao walikozaliwa wao pamoja na wazazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, *"mwenda tezi na omo hurejea ngamani."* Mtu hawi mgeni kwao hata akiondoka kwa karne nzima. Ndugu zetu hawa ni wataalam katika Vyuo Vikuu, mabenki, na taasisi mbalimbali. Wakati sasa umefika kuwatambua ili tuwarejeshee uraia wao ambao ndiyo asili yao ili wapate nafasi na kulitumikia Taifa lao vizuri. Hatuoni kuwa hiyo ni nguvu kazi muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, lakini siyo kwa umuhimu ni Askari Polisi wanapokuwa katika misafara ya kupitisha au kusubiri viongozi wakuu barabarani huwa hawalipwi *lunch allowance*, wakati wenzao Askari wa Usalama Barabarani wanalipwa Sh. 5,000/=. Huu ni ubaguzi na unaleta fitna miongoni mwa askari wetu. Tatizo hili lirekebishwe mara moja ili kujenga usawa na kuondoa tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii. Nachangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuilinda nchi na kudumisha amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iwape moyo askari wa vyeo vya chini kwa kuwajengea nyumba, kuwapandisha vyeo, kufuata kanuni za utumishi na kuwalipa stahili zao inapotokea kuhamisha, kwani asipolipwa ndipo inatokea wanachukua na hata kudai rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu ambao sio raia wa nchi hii, huingia nchini bila kibali na wengine huingia kwa kufanya biashara. Naomba Serikali iweke utaratibu wa ukaguzi wa mara kwa mara ili kubaini wahusika na kuwachukulia hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua, suala la kutoa *passport* ni haki ya kila mwananchi au ni yule tu mwenye shughuli ambayo inamlazimu mwananchi atoke nje ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ya usafiri ni muhimu kwa kila askari, hivyo naishauri kuwapatia mikopo ya gari, pikipiki ili waweze kufuatilia matukio ya uhalifu haraka.

Suala wa madaraka ya kulevya hujitokeza mara nyingi. Naiomba Serikali ileze ni wangapi waliokamatwa? Tunaomba Jeshi la Zima Moto lipatiwe vifaa ili kutekeleza wajibu wao na wapelekwe wakasome ili kuongeza ujuzi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Jeshi la Polisi lijitahidi kuzima maandamano kwa uangalifu ili wasije wakazidiwa na waandamanaji. Hata hivyo, nalipongeza Jeshi la Polisi, linavyojitahidi kuanya kazi ya kuzima maandamano yaliyojitokeza katika maeneo mbalimbali. Nawatia moyo, waendelee kuilinda nchi na Mwenyezi Mungu atawalinda na nawaomba wamtangulize Mungu wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi bila kumsahau Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote kwa kazi nzuri inayofanyika katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Busanda Wilayani Geita vipo, Vituo vya Polisi ambavyo vinafanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha raia wanaishi kwa usalama. Mara nyingi maeneo ya machimbo huwa yana matukio mengi ya ujambazi. Lakini kutokana na kazi nzuri ya Askari Polisi wanayofanya, ndiyo maana hali ni shwari. Vituo vilivyopo ndani ya Jimbo la Busanda ni Kituo cha Polisi, Katoro, Chigunga, Lwamgasa, Bukoli na Nyarugusu. Katika vituo hivi pamoja na kazi nzuri inayofanyika, wana upungufu wa vitendea kazi. Hivyo, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Sasa basi, naomba Wizara iboreshe mazingira haya kwa kuwanunulia pikipiki katika Vituo vya Chigunga, Bukoli na Lwamgasa. Kulingana na idadi kubwa ya watu katika Kata ya Katoro, hivyo hata matukio ya ujambazi yanakuwa mengi ukilinganisha na maeneo mengine. Naomba Wizara katika bajeti hii inunue gari moja na pikipiki moja kwa ajili ya Kituo cha Katoro.

Katika Kituo cha Nyarugusu ninaomba Serikali inunue pikipiki mbili ili kuboresha utendaji kazi wa Askari Polisi katika Kituo hicho. Hii itaboresha huduma kwa wananchi kwa kuwa na usafiri wa uhakika pale ambapo unahitajika. Jambo la pili ninaomba Serikali iboreshe maslahi ya watumishi katika Wizara hii. Askari Polisi maslahi yao yako chini sana kiasi kwamba wanaweza kujikuta wanapata vishawishi vya kuingia katika rushwa. Bila kusahau Magereza, naomba wapewe *hardship allowance* pale inapobidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naunga mkono hoja.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa uwasilishaji wa hotuba yake ya Bajeti. Pia namshukuru Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu Kituo cha Polisi cha Mazizini – Zanzibar. Kituo hiki ni kikubwa au cha tatu kwa kuhudumia wananchi wengi na viongozi wetu wanaoishi eneo hili. Kituo hiki kimejengwa toka wakati wa mkoloni. Mandhari yake ni ya kizamani na nyumba yake ya ofisi ni mbovu sana, hailingani na eneo la Mazizini wanapoishi viongozi wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu makazi ya polisi Mazizini. Namba yao ni wengi kuliko idadi ya vyumba vilivyopo inasababisha kupanga uraiani ambapo kunahatarisha maisha yao na familia zao. Pia hizo nyumba zilizopo kituoni, vyumba vyao ni vidogo na wanaishi familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye nyumba iliyoachwa na mkoloni hali ni mbaya sana kwani hivi sasa makaro yote ya choo yanavuja uchafu mwingi ambao unaenda mpaka sehemu wanayoishi watu hali hii inahatarisha maisha yao kwa maradhi ya kuambukiza. Pia *roof* ya nyumba hiyo inavuja kupita kiasi. Mimi Mbunge niliitwa kuona hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nashauri Wizara hii ifanyie matengenezo makubwa nyumba za kuishi hawa polisi wa Mazizini. Pamoja na ofisi yao iendane na hadhi ya eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naushauri Mazizini Polisi kuna eneo kubwa la kuweza kujenga nyumba itakayoweza kuishi askari wengi kwa pamoja kama itajengwa nyumba ya ghorofa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka nichangie kuhusu kupatiwa vyombo vya usafiri kwa askari au wafanyakazi wa Idara ya Uhamiaji. Wafanyakazi hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu ambapo hawana usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia askari wa uhamiaji wanapata posho lakini wafanyakazi wa Idara ya Uhamiaji hawapati posho. Hivyo naishauri Wizara hii kuwapatia posho wafanyakazi wasiokuwa askari wa uhamiaji nao walipwe posho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuchangia kuhusu askari wanaokamata dawa za kulevya. Kwa kweli inasikitisha sana kuona wahalifu hawa wanakamatwa, baadae wanaachiwa kwa muda mfupi. Inasikitisha sana kuona hali hii inaendelea ya kuletwa dawa na askari wetu polisi ndio wanaowalinda wahalifu wa dawa na wakati mwingine wanawapa *escort* mpaka wanapokwenda. Hivyo hili ni tatizo kubwa na Serikali iangalie eneo hili au nchi yetu itaharibika sana. Lakini napenda kufahamu hizi dawa zinazokamatwa zinapelekwa wapi? Au wanarejeshewa wenyewe wahalifu au zinachukuliwa na polisi wanafanya biashara. Naomba nipate jibu la hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja wa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza hotuba nzuri ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba hii kwa machache yafuatayo:-

Napongeza askari wa Wilaya ya Kasulu kwa kujituma sana hasa ukizingatia ni mpakani, ninaloliomba Serikalini ni kuongeza gari la askari wa Manyovu ili waweze kufikia maeneo yote kirahisi, kwani ni tatizo kubwa (Kituo cha Polisi Manyovu).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma unao matukio makubwa ya ujambazi ambao hata Serikali inayajua. Ombi langu, tuanzishe vituo vya polisi katika *strategic areas* pamoja na doria inayofanywa hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa ofisi, Jimbo la Manyovu limepewa wilaya mpya ya Butigwe, ninaomba ujenzi wa Kituo cha Polisi kianze kujengwa kuimarisha huduma ya ulinzi na usalama katika wilaya hiyo mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira, katika Jimbo la Manyovu, tunao vijana ambao wanapenda kuajiriwa na jeshi hili lakini fursa hizo hawazipati kabisa hasa ukizingatia wanao uchungu wa kulinda amani kwani adha za uhalifu wanaujua kwani wananchi wote wapo mpakani mwa Tanzania. Mheshimiwa Waziri naomba nafasi za ajira katika Jimbo la Manyovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nathamini uwezo wako na ninakuamini. Naunga mkono hoja.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru sana Mungu kwa zawadi ya uhai anayoitoa kwetu hadi muda huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu sana kwa raia walio ndani na nje ya Tanzania, nasema wa ndani kwa kuwa usalama wao na mali zao unasimamiwa na Jeshi la Polisi na walio nje wamepata pasi kutoka Idara ya Uhamiaji ambavyo vyote ni vyombo vinavyofanya kazi chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kikatiba Jeshi la Polisi limeanzishwa kwa madhumuni ya kulinda raia na mali zao na pia usalama wa wageni na kuondoa au kuzuia kabisa uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii imeanza kutia shaka hasa pale juhudi za jeshi na jukumu lake linapopelekwa kwa raia kwa kivuli cha polisi jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo umuhimu mkubwa sasa wa kuongeza wingi wa askari wenye mafunzo ya kutosha na ujuzi kwa ajili ya kuwalinda raia na mali zao na si raia kujilinda hadi pale ambapo italazimu raia kujilinda kwa maana ya Jeshi la Polisi na Serikali yao kushindwa kutimiza dhumuni hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama sio nzuri sana kwa kudhibiti na kumaliza kabisa uhalifu uliopo hivi sasa kwa sababu ambazo ni vyema sasa kwangu kuziweka wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, imani ya wananchi kwa jeshi imekuwa ikipungua siku hadi siku na hii imepelekea raia wengi kujichukulia hatua/sheria mikononi kwa kuwaadhibu na hata kuwauwa watuhumiwa kabla ya kuwapeleka kituo cha polisi au kuvamia kituo na kuua watuhumiwa. Hii inaonesha kuwa kumekuwa na taratibu za upendeleo unaotafsirika unachochewa na rushwa kwa walio na nafasi ya madaraka ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja kwa Serikali kuendesha au kutoa matokeo ya upelelezi haraka kwa kuhakikisha kuwa hakuna dalili ya rushwa wa upendeleo wowote wa zoezi zima kabla ya kupelekwa kwa hatua ya mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya askari wetu ni duni sana na hasa katika kada ya askari wenye vyeo vya chini. Hali ya polisi na wategemezi wao ni duni sana, sio kwamba polisi wetu wanatakiwa kulipwa mamilioni ila kupata huduma bora kwao na wategemezi wao, hasa elimu kwa watoto wao na wategemezi wao, huduma za lishe bora kwa askari ambao wanafanya kazi zao usiku na mchana. Posho ya chakula iongezwe kulingana na hali ya kupanda kwa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, umiliki holela wa silaha, kwa mujibu wa sheria za nchi zinazomruhusu raia kumiliki silaha na ninaupongeza utaratibu unaoanza kumjadili mwombaji kuanzia Serikali ya Mtaa anaoishi mwombaji anajadiliwa na wanaoishi naye na kumjua vizuri mwombaji kwa tabia na staha pia ustaarabu na uvumilivu kwa jamii inayomzunguka pia mali anazomiliki zinazohitaji ulinzi binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa umetokea utaratibu mbaya na hatari sana kwa umiliki wa silaha kwa sasa ambao mtu anayeishi sehemu fulani ya nchi anapata kibali kwa muhtasari wa mahali ambapo yeye hakujadiliwa na watu anaoishi nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kuielekeza Serikali kukagua majalada yote ya umiliki wa silaha binafsi na kupitia mchakato wa kujadili wamiliki hawa kama wamemilikishwa tofauti na utaratibu uliopo basi hatua za haraka zifuatazo zichukuliwe kama kufuta kibali cha silaha anayoimiliki, kutoa adhabu kali kwa waliohusika katika kughushi nyaraka za Serikali na kuwapa adhabu wamiliki wa silaha hizo kwa kumiliki silaha kinyume cha utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi ikiwemo ukaguzi wa kustukiza na wa mara kwa mara na alama za ukaguzi ziwekwe katika silaha. Vitabu vya umiliki wa silaha ubadilishwe na kuwe na kadi za ki-*electronic* kama iliyo katika leseni za udereva ili kiwe na taratibu za kuweka rekodi kwa utumiaji na idadi ya risasi pamoja na malipo ya silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zimamoto bado hali ni mbaya kivifaa na mafunzo kuhusu Idara ya Zimamoto na Uokoaji. Jimbo ninalotoka lipo Kando ya Ziwa Victoria ambapo kuna usafiri wa majini kati ya Musoma Mjini na Wilaya nyingine, lakini hakuna kikosi cha uokoaji majini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Jimboni Musoma Mjini)ilikuwepo miundombinu ya maji kwa ajili ya utayari wa maji ya kuzima moto, lakini hadi leo haipati huduma na kukarabatiwa wala kuongezwa kulingana na ukuaji wa nchi na mahitaji ikiwemo ongezeko la watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Ndege wa Musoma unalo gari la zimamoto ambalo lipo tangu mwaka 1970 na chakavu na bovu sana na haliwezi tena kufanya kazi yake kwa ukamilifu na askari wa zimamoto wapo, hakuna kazi ifanyikayo zaidi ya kuorodhesha matukio.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda muafaka sasa kuleta askari wa uokoaji majini na kikosi cha zimamoto bandari. Kuna haja ya kuongeza askari na mafunzo kwa ajili ya idara hii. Jeshi la Magereza mbali na kuwachunga wafungwa pia wana jukumu la kumpa mbinu mbadala ya maisha kwa kuwapa tu mafunzo ya ujasiriamali na ufundi ili akitoka akafanye kazi tofauti na uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na wafungwa wa kujirudia rudia kwa makosa yale yale kwa wafungwa kwa kuwa hawakupatiwa njia mbadala ya maisha ya kujitegemea kuliko kutegemea uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Musoma Mjini lipo Gereza moja katika Kata ya Mkendo na ipo kambi katika Kata ya Nyasho. Askari hawa hawana gari la kuwachukua usiku kwa ajili ya kutekeleza jukumu lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika majumuisho ya Waziri nipate ufafanuzi wa gari kwa ajili ya askari wa Musoma.

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kutambua umuhimu wa Wizara hii kwa usalama na hivyo amani na hatimaye maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini inasikitisha kuona kwamba hali halisi ilivyo sasa Wizara yako ambayo wahusika wakuu ni Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji, Usalama wa Taifa, Jeshi la Wananchi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijadili Jeshi la Polisi. Hili jeshi kusema kweli limeelekea kupoteza misingi ya kazi zao kwani Jeshi hili limejaa shutuma za rushwa na ukatili uliokithiri. Wananchi wakisikia au kupishana na polisi badala ya kuwaona ni rafiki kimbilio bali kinyume chake huwaona kuwa ni adui na hivyo kila wakati kuwa tayari kukabiliana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hayo niliyoyaeleza hapo juu polisi inapoteza umuhimu wake mfano polisi wanatuhumiwa kuongoza ulaji rushwa na unyanyasaji wa raia sio hivyo tu bali pia kwa kuletea vilema wananchi na mara nyingine kuua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo ambalo linailetea fedheha nchi yetu kuona kwamba Serikali imeshindwa kulitumia jeshi hili vema. Serikali hii imeingia katika mtego wa kumeza ndoana ya kutumia chombo hiki cha dola kukandamiza raia wake wema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo lililo wazi kuwa wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, Chama Tawala cha CCM kililitumia vibaya jeshi hili na hasa Jeshi la FFU ambalo kila mahali ambapo ilionekana kuwa chama cha upinzani kinaelekea kushinda basi jeshi hili lilitayarishwa kwenda kutisha wananchi au kuvuruga uchaguzi na hili ni wazi mfano karibuni washindi wote wa Ubunge CHADEMA walishinda kwa mbinde kutangazwa, kwa vile viongozi wa juu wa CCM na Serikali yake waliwashinikiza polisi na wanajeshi kufanya wizi wa kura kwa faida yao. Lipo hili linapaswa lizingatiwe la sivyo kutakuwa na matokeo mabaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, umaskini wa jeshi hili unalifanya Taifa hili kuingizwa katika majanga mengi. Kwa mfano majangili wakubwa ni Wasomali toka Somalia ambao inasemekana wametumia fedha zao kuwahonga askari wetu kuanzia *immagration* hadi polisi wa maliasili kuhujumu nyara za Serikali kuua tembo, faru, twiga na kadhalika. Na kwa kweli Wasomali wana ujasiri wa aina fulani kwani ni watu wa vita tofauti na Watanzania ambao hawajazoea vita. Hivi wanapoingia mahali fulani hujiimarisha na kuteka maeneo hasa hoteli ambayo huficha mitandao haramu ya kuhamisha mali za asili za Watanzania kwenda mahali mbalimbali nchini kwao na nchi nyingine ambako wana uraia huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui, sielewi, hivi Wizara yako haina hata wapelelezi, majasusi wa kuyaona haya? Kwa nini? Tunasubiri mpaka donda liwe kubwa lishindwe kutibiwa. Tunakuwa na kigugumizi kushughulikia mambo muhimu ya maslahi ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia tena kuwa ni wakati muafaka wa kuwashughulikia wahalifu wote bila kujali vyeo vyao, vyama vyao au hata ikiwa ni polisi pia washughulikie. Mfano wale wote ambao wametuhumiwa kuua wananchi kama kule Arusha, Tarime na kadhalika. Mafisadi wa mali ya umma kama wale waliowaletea wananchi mateso makubwa ya kutowapatia umeme. Jambo hili ni hatia kubwa, halipaswi kufumbiwa macho. Wizara yako ni zaidi ya kutumwa kupiga watu, kuua, kunyanyasa *(harass)* bali inapaswa kuona kuwa nchi inakuwa salama. Ni muhimu kubuni njia za kuzuia uhalifu kuliko kuutibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ni yetu sote masuala ya *propaganda* ya kuwa nchi hii ni ya amani, si kweli kwani kilichopo hapa ni nidhamu ya woga tu. Lakini Wizara ya Polisi mnajua kabisa ni mazingira gani yanaweza kuondoa amani katika jamii. Mojawapo kubwa sana ni ukuaji wa matabaka katika jamii. Hali halisi sasa hivi ni kupanuka kwa matabaka haya, sasa hivi tabaka la matajiri linakuwa dogo lakini lenye utajiri wa kutosha, lina utajiri pia limeshika mamlaka ya kiuchumi, kisiasa hii ni mbaya na haya matabaka yanaishi sambamba huko mijini na vitongojini. Hii ni hatari sana kwani hili ni bomu lililotayari kulipuka kufuatia mwenendo ulivyo sasa. Kwa nini kunakuwa na tabaka ambalo lipo juu ya Sheria (Katiba).

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wakimbizi pia ni tete mno, si la kuongelewa tu Bungeni na kuondoka na kuacha kwenye *Hansard*. Mambo yalivyo katika uhalisia amani haipo ndiyo

maana watu wanaandamana, wanagoma. Inakuwaje, wazee wastaafu wagome, walimu wagome, wanafunzi sekondari na *primary* wagome, vyuo wagome, madereva wagome na kuandamana lakini ninyi hamna majibu. Tafakarini hili ni jukumu la Wizara ya Mambo ya Ndani si kuumiza watu kwa kuwakata miguu, kutia umaskini na kadhalika. Yachukulieni matukio na kuona vipi yanaweza kushughulikiwa kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, *intelligence* ya nchi hii pia ni ya mashaka sana kwani mambo mengi ya hujuma kubwa kama hili la watu kuamua kuingia mikataba mibovu ya kiuchumi kama ile ya madini, kuuza ardhi kwa wageni, kuwaingiza wakimbizi kwa njia za hila, kukiuka taratibu za msingi kama kutumia vyeo/madaraka, kujisimika kwenye uongozi/nyadhifa za juu kwa mabavu au hila. Mambo yote hayo ni kazi za msingi za Usalama wa Taifa na viongozi wa CCM kutimiza azma zao za kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache naomba nisisitize kuwa Wizara yako kama kweli inazingatia amani iachane na kufungamana na chama chochote cha siasa hata kama ni tawala. Ahsante.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja. Lakini nina mambo matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za askari magereza Gereza la Mpwapwa lina nyumba zaidi ya 20 ambazo zimejengwa na askari wenyewe na zipo usawa wa *renter* kwa muda mrefu sasa zimebaki hivyo hivyo, sasa zinaharibika kwa kubomoka, naomba Wizara iangalie uwezekano wa kuzimalizia maana askari wengi hawana nyumba na zilizopo zina hali mbaya na wala hazistahili kuishi binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la vyombo vya usafiri katika vituo vya polisi vilivyopo jimboni kwangu Kibakwe, jimbo langu lina vituo viwili vya polisi, Kituo cha Polisi kidogo cha Kibakwe na Kituo kidogo cha Polisi Chipogoro, vyote hivi havina usafiri hata wa pikipiki. Naomba Wizara iangalie namna ya kutusaidia gari kwa ajili ya vituo hivi viwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme Kituo Kidogo cha Polisi cha Kibakwe. Nimeshasema humu ndani mara tatu, Naibu Waziri ulinijibu mara mbili na kwamba fedha ipo lakini hadi leo hakuna kilichofanyika. Kwa masikitiko makubwa nakuomba tena uangalie namna ya kutatua tatizo hili la umeme Kituo cha Polisi Kibakwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, fungu la Bajeti ya Wizara iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa ajira uwekwe vizuri ili ajira zisiwe na upendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupandishwa vyeo kanuni zizingatiwe ili kutenda haki. Jimbo la Mtera vijengwe vituo vya kutosha walau kila tarafa tupate kituo kimoja pamoja na usasfiri iwe gari au pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya kufungua kesi ipitiwe upya kwani inaondoa nguvu ya polisi wetu katika kumpeleka mtuhumiwa mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara ya polisi iwe sawa na JWTZ, nyumba na zana za kazi polisi jamii iimarishwe na haki za binadamu zisipunguze nguvu ya Jeshi la Polisi katika kuhoji watuhumiwa wa kesi za ujambazi ni vema mkong'oto kidogo ukawepo. Nawasilisha.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri na makamanda wote wapiganaji kwa kazi kubwa wanayofanya kuwalinda Watanzania na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapiganaji wetu wanafaa wapongezwe kwa kufanyakazi katika mazingira magumu kiasi kwamba kama isingekuwa nidhamu ya kiaskari wangeweza kufanya maandamano kama wanavyofanya Watanzania wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko makubwa ya uajiri kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Hata kama haiwezekani nafasi za ajira za Zanzibar na Tanzania Bara ziwe sawa lakini kuna ushahidi wa kimazingira kuwa wanapelekwa waombaji wa nafasi za uaskari kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar ili waajiriwe kama Wazanzibari na hatimaye wanarudi kwao bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni dhuluma kwa Wazanzibari na naomba viongozi wahusika wahakikishe kuwa haki inatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha pia kuwa waajiriwa wapya wanatakiwa kukaa bila kuoa/kuolewa kwa muda wa miaka mitatu kwa namna yoyote ile sheria hii inavunja haki za binadamu. Katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya UKIMWI, naishauri Serikali suala la ndoa lisiwe ni sharti katika uajiri, waliooa/kuolewa waajiriwe pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi ya askari, naishauri Serikali iwaweke askari wote kambini katika nyumba bora na za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo sasa ambapo Jeshi la Polisi linaruhusu askari wakae uraiani ni hatari sana. Moja katika ya matatizo wanayopata askari wanaoishi uraiani utendaji wao wa kazi sio mzuri kwa kule kujuana sana na raia yaani wanaoneana haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhamisho kuna malalamiko ya muda mrefu kuwa baadhi ya askari wanakaa sehemu moja kwa muda mrefu. Inawezekana kukaa huku kunatokana na msukumo wa askari mwenyewe kulingana na maslahi. Lakini mara nyingine inashindwa kumhamisha kwa kuogopa kulipa posho. Naomba Serikali ifuate sheria ili uhamisho uendane na sheria za Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi na siasa, lazima tukubali kuwa Jeshi la Polisi limekuwa likitumiwa na viongozi wa CCM kufanikisha ushindi wa chama hicho kwa njia mbalimbali kwa mfano kubambikizana kesi za uongo, wakati wa uchaguzi, kutoa vitisho na kusaidia wizi wa kura. Hii sio kazi ya Jeshi la Polisi, naiomba Serikali isiliingize Jeshi la Polisi katika siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi na rushwa. Kuna malalamiko pia kuwa Jeshi la Polisi linaongoza kwa kuomba rushwa, sababu za msingi ni hali duni ya maisha ya askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipato cha askari hakilingani na vipato vyao. Hivyo wanatumia nafasi zao za uaskari kushawishi/kuomba rushwa. Serikali iwalipe askari mishahara mizuri na posho muafaka.

**MHE. SHAWANA BUKHETI HASSAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa hotuba yake nzuri yenye kuleta matumaini katika suala zima la kuendeleza amani katika nchi yetu na naunga mkono hoja asalimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi mambo yafuatayo naomba yachukuliwe hatua pia yafanyiwe kazi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kupatiwa vyombo vya usafiri askari waliopo katika vituo ili wanaporipotiwa kuwa kuna tatizo waweze kufika kwa wepesi eneo la tukio, hata kama uwezo wa magari hakuna, wapatiwe japo pikipiki, Mheshimiwa Waziri wiki mbili zilizopita eneo la hoteli moja iliopo Mbweni wameuwa watu watatu na majambazi, raia wamepiga simu polisi katika Kituo cha Kiembesamaki waende wakahami hali ilipo wamejibu hawana usafiri wa kufikia kwenye tukio, hili ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mikakati ya kujenga majengo mengi ya makazi ya askari wetu na ujenzi wa vituo vya Daraja C, lakini pamoja na juhudi za ujenzi uliopangwa, kuwepo na utaratibu wa kukarabati majengo. Mfano majengo ya polisi Mwera ni makubwa yanakidhi haja lakini hali ya majengo hayo sio nzuri hata kidogo, yanahitaji ukarabati mkubwa au tutayapoteza, pia hali hiyo hiyo nayo ipo nyumba za askari za Fuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimewasilisha jina kwa *IGP* Mwema la mstaafu aliyekuwa hajapata mafao yake. Naomba hatua zichukuliwe ili apatiwe haki zake. Ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na wataalam kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, msongamano wa mahabusu na wafungwa gerezani upunguzwe kwa kutumia kifungo cha nje zaidi na hata mahabusu wawekewe utaratibu kubaki makwao na kuripoti polisi kila mara wanaposubiri hukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi lidhibiti vitendo vya baadhi ya askari wake Wilayani Kiteto ambao wamekuwa wakituhumiwa kushiriki katika vitendo vya kiuhalifu hasa usafirishaji wa Wasomali haramu na pia uporaji wa malori ya mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi Wilayani Kiteto wapatiwe gari na mafuta ili waweze kukimbia kwenye matukio yanapotokea hasa katika maeneo yenye migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamisho utolewe kwa baadhi ya askari ambao wamekaa Kiteto zaidi ya miaka kumi na kuwa wenyeji zaidi ya askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vitambulisho lishughulikiwe haraka na hatimaye vianze kutumika ili kubaini nani raia na nani siye.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uraia wa nchi mbili liharakishwe na kuanza kutumikia.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kikosi cha Polisi Wanamaji *(Marine Police)* kinahitaji kuboreshwa. Uvuvi haramu umekithiri katika Pwani ya Jimbo la Kigamboni. Kikosi hiki kikiboreshwa doria zitaongezeka na hivyo kudhibiti uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi za polisi za Wilaya za Kigamboni na Mbagala ni chakavu na hazina nafasi ya kutosha. Naomba ofisi hizi ziingizwe katika mchakato wa ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo la wahamiaji holela nchini, vilevile kuna tatizo la wageni kuingia na kufanya kazi bila ya kuwa na vibali. Tatizo hili linachangiwa pamoja na mambo mengine na maofisa uhamiaji wasio waaminifu kuna haja ya kuwa na mikakati madhubuti ya kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ulinzi shirikishi, ni dhana nzuri yenye manufaa makubwa katika jamii. Jeshi la Polisi liendeleze kuhamasisha dhana hii na kutoa elimu kwa jamii.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu, Vitambulisho vya Taifa, je, hakutakuwa na haja ya kuwa na sheria au mabadiliko ya sheria kabla ya vitambulisho hivyo havijatolewa? Vitatolewa kwa sheria ipi? Na makosa yanayotokana na matumizi mabaya ya vitambulisho hivyo kwa mfano kutoa maelezo ya uongo, kutumia kitambulisho cha wizi na kadhalika, yatashughulikiwaje? Aidha, ningependa kujua taarifa muhimu zitakazojumlishwa katika kitambulisho ili kuepuka mtu kuwa au kubeba vitambulisho vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa mtindo wa kutoa uraia kwa wakimbizi *"en mass"* hautarudiwa. Lakini hao waliopata uraia waachwe mahali walipozoea. Kuwalazimisha

au kuwagawa mikoani ni sawa na *deportation* kama ilivyokuwa kwa wezi wa mifugo na wachawi waliopelekwa mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya *dual citizenship* italetwa lini Bungeni? Mnahakikishaje wale wageni wanaopewa uraia wa Tanzania hawaendelei na uraia wa nchi zao za zamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, lawama zinazoelekezwa kwa Wizara hasa Polisi, Magereza na Uhamiaji ni lawama zinazotolewa na wavunja sheria, msivunjike moyo. Maneno hayo ni ya kuwavunja moyo ili muwaogope wapinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, *keep it up.* Kwa kweli kama wapinzani wangewasifu tungeshangaa.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Itigi hakina usafiri wa uhakika. Ni jimbo kubwa lenye kilomita za mraba 18,000. Tunapakana na Chunya na Tabora. Tumeomba siku nyingi kituo hicho kipatiwe gari ili askari waweze kutekeleza kazi zao kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ya ujambazi yamekuwa yakitokea mara kwa mara lakini askari wanashindwa kufuatilia majambazi kwa sababu ya tatizo sugu la usafiri. Naiomba tena Serikali ikipatie Kituo cha Itigi usafiri wa gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Itigi kinatumia kazi zake kwenye magofu ya nyumba za *TRC* kutokana na kukosekana kwa majengo. Mwaka jana katika ziara yake Itigi, Waziri Mkuu alichangia shilingi milioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi na nyumba za askari, lakini ujenzi huo haujaanza kwa sababu Serikali ya Wilaya na Mkoa haijahamasisha wananchi kuanza ujenzi huo. Nashauri *DC* na Kamati ya Ulinzi na Usalama ilisimamie suala hili. Pia fedha kwa ajili ya kazi hiyo bado ni kiduchu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itenge fedha za kutosha kuanza ujenzi wa kituo hicho na nyumba za askari. Bado tuna matatizo ya askari na vyombo vya dola kuelewa vizuri dhana nzima ya utawala bora hivyo kuwataka wananchi wao wenyewe tu wajenge Kituo cha Polisi na nyumba za askari, hawaelewi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kesi ya siku nyingi inayomhusu Bwana Mgullu wa Ipande ambaye mwaka 2008/2009 alidhulumiwa mifugo yake 47 Kituo cha Polisi Manyoni. Makamishna wa Polisi Makao Makuu walipewa kazi ya kuchunguza suala hili na walifika Mkoa wa Singida na Wilaya ya Manyoni. Hadi leo hii hakuna taarifa yoyote juu ya uchunguzi huo na Bwana Mgullu amebakia mtu maskini na kuilalamikia Serikali kila siku, hawezi kufungua kesi mahakamani kwa sababu ni maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba jibu la Serikali kuhusu suala hili na Naibu Waziri analifahamu suala hili. Tafadhali mtu huyu apatiwe haki yake ili afidiwe haki yake. Nawasilisha.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitangulize shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu na pia kwa wananchi wa Jimbo la Babati Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanda Peter Pinda kwa kazi nzuri na jitihada kubwa wanayofanya kuboresha huduma mbalimbali inayotolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Pamoja na kuboresha maslahi ya watumishi wake waliopo chini ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa juhudi ya kuendelea kufanya kazi katika Wizara hiyo yenye changamoto nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwanza kwa Jeshi letu la Polisi, naishauri Serikali iangalie namna ya kuboresha maslahi ya askari wetu ili wasiwe na ushawishi wa kupokea rushwa kutokana na hali ngumu ya kimaisha kwa askari wetu. Makazi ya kuishi yangeboreshwa,

huduma ya afya, huduma ya elimu kwa watoto wa askari na pia sehemu ya *community centers* kwa ajili ya askari wetu ili na wao waone wanapata huduma muhimu zote kama binadamu anazostahili. Pia wakati wa kudahili *(interview)* wanaojiunga na Jeshi hilo vigezo zaidi vingetumika kuchuja ili tupate askari waadilifu na baada ya hapo haki wakati wakiwa chuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya namna ya kuishi na raia na kuondoa sifa mbaya jeshi linapata kwa ajili ya askari wachache. Pia jeshi lianze kwenda na wakati, vifaa vya kisasa vitumike kote nchini na hasa ngazi ya mkoa, wilaya na *center* kubwa. Teknolojia ya kutumia *computer* na mtandao wa *internet,* vituo vyetu vingi havina *internet* na *computer* za kutosha. Pia polisi ingetumia *internet* kutangaza matukio mbalimbali pamoja na taarifa kwa umma ili kuleta mafanikio zaidi kwa usalama wa raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya usafiri na vingine kwa ajili ya utendaji bora wa Jeshi la Polisi vingefanyiwa kazi ili mafanikio yaonekane. Sehemu nyingi nchini bado tatizo la vitendea kazi ni kubwa. Askari hulazimika kuomba msaada na dhana potofu ndipo inajengeka kuwa wanapenda rushwa na ile wanayopatiwa na Serikali wanakula au kutumia kwa matumizi binafsi. Pia uongozi wa wilaya chini ya Mkuu wa Wilaya wangepatiwa taarifa ya kiasi cha vifaa, matuta ya magari na *stationery* kila kituo ikapata ili kama ni upungufu wa Bajeti na mahitaji ni mengi zaidi waweze kusaidiana na jeshi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wote wanaotajwa mara kwa mara kwa rushwa basi bila kujali kama kuna ushahidi au hakuna wachukuliwe hatua. Wanasema penye moshi pana moto, ndiyo wanaoharibu sifa ya jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho Jeshi letu lingepatiwa mafunzo ya *customer charter* ya namna ya kutoa huduma bila lugha chafu, kwa muda na kuongeza imani kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi kwa upande wa usalama barabarani ndiyo kwa sehemu kubwa linatuhumiwa kuongoza kwa rushwa na kushindwa kufanya kazi kwa uadilifu kupunguza ajali za barabarani. Vifaa vya kisasa vingetumika ili kuleta tija na kuondoa lawama kwa jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Idara ya Upelelezi na Mashitaka *(PP)* wangepatiwa vifaa vya kisasa na *(prosecutors) PP* wangepata elimu ya sheria zaidi na namna ya kuandaa mashitaka. Pia taarifa zao zingekuwa zinatolewa kwa jamii ili jamii ielewe kazi ngumu wanayofanya hao askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Jeshi la Magereza, napenda kuchangia jeshi hili kwa jitihada kubwa wanayofanya kuleta maendeleo kwa nchi yetu. Wanakabiliwa na changamoto nyingi. Jukumu lao ni kuwapa elimu wanaoletwa kwao ili wakirudi katika jamii wasiendelee na uhalifu ili waweze kufanya hivyo, ni vema wangepatiwa vitendea kazi vya kisasa kwanza ili wawe na maktaba yenye *internet* iliyokamilika ili wafungwa, mahabusu na askari magereza wenyewe wapate elimu na waweze kujiendeleza. Pia vifaa mbalimbali mfano vya kufundishia ufundi mbalimbali, kilimo, ufugaji na usindikaji wangepatiwa jeshi letu ili waweze kutoa mafunzo ya kisasa na watakaopata hayo mafunzo wakirudi katika jamii basi wataweza kupata ajira kinyume na ilivyo sasa wakirudi kuendelea na uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi ya askari wetu na gereza ambalo huhifadhi wahalifu na mahabusu ambao kabla ya kuhukumiwa bado wana haki ya kupata huduma zote muhimu hadi hapo watakapohukumiwa. Magereza zetu nyingi zina wafungwa na mahabusu wengi kuliko uwezo wa gereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri, Jeshi la Magereza kwa sababu lina kitengo cha ujenzi kizuri sana, wangeomba tu vifaa vya kununua madukani na viwandani na wao wana uwezo wa kutengeneza tofali, nguvu kazi wanayo na tungeanza kuboresha magereza yetu na kwenda na wakati. Waboreshe katika magereza yote suala la kutumia *bio latrins,* (nishati mbadala).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo watapunguza matumizi ya kuni na kuboresha mazingira magerezani na taasisi zingine zitafuata nyayo kama shule za sekondari, vyuo na nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia magereza ipate wataalam wa kilimo na ufugaji ili wawe mstari wa mbele kuzalisha mbegu bora, mifugo bora na tayari sifa ya ufugaji wa samaki wanayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kuchangia Idara ya Uhamiaji, ni idara muhimu na nyeti, ningependa suala la uraia wa nchi mbili uchukuliwe kwa uharaka na umuhimu wake, suala la uraia wa nchi mbili ungeletwa mapema ili kuwapa fursa Watanzania na waliokuwa Watanzania wapate haki na fursa ya kuleta maendeleo katika nchi yao na huko wanakotarajia kufanya makazi *(dual citizenship).* Pia sheria ya uraia ingebadilishwa kwa wale waliozaliwa Tanzania, leo hii ni lazima moja kati ya wazazi wake awe raia wa Tanzania wakati anazaliwa, la sivyo kama wazazi wake kama si raia wakati wanazaliwa itabidi aombe uraia wa Tanzania.

Nashauri kuwa mtu apate haki ya kuwa raia kwa kuzaliwa ndani ya Tanzania. Pia muda wa kupata uraia wa mke au mume wa Mtanzania, unachukua muda mrefu mno. Kwa wale ambao wameoa au kuolewa na Mtanzania, wangepata fursa ya kupata uraia mapema wakati masharti yote yametimizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba Jeshi letu la Zimamoto na Uokoaji lipatiwe vifaa vya kutosha na vya kisasa, pia watoe elimu kwa makundi ya raia, mashuleni, misikitini, kanisani na kwingine kote juu ya huduma na uokoaji.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Chunya ni moja kati ya Wilaya chache sana kongwe nchini. Ni kati ya wilaya tatu za kwanza kabisa kuitwa wilaya. Lakini Chunya haina Kituo cha Polisi yaani haina jengo la Kituo cha Polisi. Jeshi la Polisi limejibana kwenye ofisi chache za jengo la Mkuu wa Wilaya. Hii ina maana kuwa hata mahabusu wanapelekwa Mbeya kilomita 72 na ni gharama sana kwa Jeshi la Polisi.

Namwomba sana Mheshimiwa Waziri atoe kauli ya Serikali ni kwa nini Chunya haina jengo la Kituo cha Polisi? Nikiangalia hotuba ya Waziri ukurasa wa 18, vituo vya polisi vitakavyojengwa mwaka huu Chunya haimo. Nimekuwa Mbunge katika Bunge la Tisa na kila mwaka niliomba Chunya tujengewe jengo la Kituo cha Polisi. Naomba Mheshimiwa Waziri aseme ni lini Serikali itatenga fedha za kujenga Kituo cha Polisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Magereza ya Wilaya ya Kyela, Serikali imejenga Magereza ya Wilaya ya Kyela. Hii inapunguza gharama za kupelekwa mahabusu Tukuyu Wilayani Rungwe. Hata wafungwa wa Wilaya ya Kyela wanapelekwa Rungwe. Sasa magereza ipo tayari na Serikali ilisema kuwa Magereza itaanza tarehe 30 Juni, mwaka huu. Kwa nini haijaanza? Isije ikawa mbinu za watu wachache ambao wanataka mahabusu na wafungwa wa Kyela waendelee kupelekwa Tukuyu. Naiomba sana Serikali Gereza hili la Kyela lianze kazi mwaka huu. Naunga mkono hoja.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ni Wizara ambayo inakabiliwa na changamoto nyingi sana. Changamoto nyingi hizo zinapelekea taasisi zilizoko chini ya Wizara hii kutotimiza kazi zake inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Jeshi la Polisi, kama tunavyotambua Jeshi la Polisi limekuwepo kwa ajili ya kulinda raia na mali zao. Watu hawa wasipotendewa haki katika maslahi yao hawataweza kufanya kazi yao kiufanisi. Tunajionea wenyewe jinsi wanavyoishi katika kambi zao, chumba kimoja askari anakaa na familia yake yote hili jambo linadhalilisha askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali haioni taabu ambazo wanazipata na kuona sasa kuna umuhimu wa kuwajengea nyumba bora zenye hadhi yao? Mbali na makazi yao askari hawa wamekuwa wakipunjwa na muda mwingine hawalipwi stahili zao wanapostaafu. Wapo askari ambao wamestaafu na wamelitumikia jeshi kwa zaidi ya miaka 30 wamelipwa shilingi milioni 1.6 kwa kazi aliyofanya miaka 30? Haiingii akilini. Naomba hili suala liangaliwe kwa makini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu utoaji wa leseni mpya za udereva. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuanzisha mchakato wa kuboresha leseni kwa madereva na kuzifanya za kisasa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo limejitokeza katika zoezi hili, suala lenyewe ni sifa za kupata leseni yenyewe. Kuna madereva ambao wana miaka zaidi ya 30 – 40 wanaendesha magari, hii ina maana maisha yao yote wameyatumia wakiwa madereva, cha kustaajabisha watu hawa wanapokwenda kuomba leseni mpya wanaambiwa warudi tena chuoni wakapate vyeti, hii haijakaa vizuri, kwa nini warudishwe chuoni na wakati muda wote wa maisha yao wamekuwa wakiendesha magari na kutunza familia zao mpaka sasa wameota mvi Serikali inataka kuwarudisha vyuoni? Wakafanye nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuzungumzia sasa Jeshi la Magereza. Jeshi la Magereza linatakiwa liboreshwe kwa kukarabati magereza yote nchini ambayo yapo katika hali mbaya. Magereza mengi yamekuwa katika hali isiyoridhisha kabisa. Ndani ya magereza kumekuwa na mambo ya ajabu yanayoendelea baina ya wafungwa na askari, vilevile wafungwa na wafungwa wenzao. Tabia hizi ambazo naweza kuziita ni za kudhalilisha Jeshi la Magereza kwani zimekuwa zikiendelea kuota mizizi katika magereza yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Zimamoto limekuwa likibakia nyuma kweli kweli, sababu nini? Nafikiria sababu ni kuwa halitengewi fedha za kutosha kwenye Bajeti ya kila mwaka mfano mwaka huu Bajeti yao ni shilingi 3,095,792,000 kiasi ambacho ni pungufu kwa miaka ya nyuma yaani mwaka 2009/2010 na mmwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonyesha ni jinsi gani Serikali haijalipa kipaumbele Jeshi hili la Zimamoto. Tunajionea wenyewe bila hata ya kuambiwa, hakuna magari ya kuzimia moto maeneo mengi magari haya hata kama yapo ni chakavu hayawezi kukidhi haja panapotokea janga la moto na uokoaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa ione haja ya kuweka mpango ambao utaliwezesha Jeshi la Uokoaji na Zimamoto kufanya kazi zake kiukamilifu bila kutoa manung'uniko. Serikali iweke fungu *at least* kila Bajeti yapatikane magari ya zimamoto kwa ajili ya manispaa kote nchini pamoja na halmashauri zote. Magari haya pia yaendane na wakati kutokana na ujenzi wa maghorofa katika miji mikuu ya nchi yanavyoendelea, hii ina maana kuwa magari yawepo ambayo hata kama moto ukitokea ghorofa ya 30 gari linaweza kuzima moto huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tabia ya askari wa usalama barabarani kusababisha ajali kwa kukiuka baadhi ya taratibu zao za kazi. Nimewahi kushuhudia askari wa usalama barabarani akisimamisha gari ghafla baada ya kutokea kichakani ambako alikuwa amejificha na tochi yake. Hii ilisababisha tafrani kwa abiria tuliokuwemo ndani ya basi hilo. Kwa nini hawa askari wasikae peupe na wakaonekana na madereva wakiwa mbali ili waanze kupunguza mwendo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu huu na ningependa nipatiwe majibu ya maswali yangu.

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze kwanza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu na Magereza ya Watoto (vifaa vya mafunzo kwa watoto) kwa kweli naomba nielezee masikitiko yangu makubwa sana kwa vijana chini ya miaka 18 wanapofanya makosa na kutiwa hatiani kwanza hivyo vituo vyao wanavyopelekwa haviridhishi hata kidogo. Tanga Mjini lipo Gereza la Watoto ni baya sana endapo mtoto wako amepatwa na hatia na akaenda hapo, mtoto huyo maisha yake yameshaharibika kabisa. Mazingira yake ni mabaya sana, vitendo vilivyomo humo ni vya ajabu mno, tabia zote mbaya na chafu zimo humo badala ya kwenda kumfunza mtoto huyo ndio unakwenda kummalizia kabisa maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali iviangalie kwa makini mkubwa vituo hivyo (Magereza ya Watoto). Inachotakiwa Serikali kufanya kwa vitendo sio maandishi ni kuwarekebisha kitabia kwa haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa na programu za mafunzo ya shule ya kisaikolojia ili watoto hao wajitambue kuwa ni watoto na hawapaswi kufanya vitendo hivyo vitakavyowaharibia maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni vizuri kuwa na programu za mafunzo kwa njia ya vitendo katika miradi mbalimbali ambayo itakuwa kama adhabu lakini itawajenga sana kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwe na mafunzo ya kuwajenga kiimani. Vituo vya Polisi hasa vya Kata havina msaada mkubwa kwa raia hasa nyakati za usiku. Raia wanapovamiwa na majambazi na kuwapigia simu kuomba msaada wanachukua muda mrefu sana kuja kwenye tukio mpaka raia wanafikia kuwa askari hawa wanakula njama na majambazi. Pia utakuta askari kwenye vituo hivi vya kata hawana silaha (Bunduki) sasa hiyo inapunguza sifa za askari huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli tumedhamiria kusogeza ulinzi kwa raia basi tufanye kwa ukamilifu wake, tusijenge vituo vingi tukawapa matumaini raia wakati hakuna askari wa kutosha wala hakuna silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu dawa za kulevya. Kusema kweli hili ni tatizo sugu na askari wanachangia kwa kiasi kikubwa kuendeleza shughuli hizi na kuteketeza jamii ya Tanzania kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, askari hao wanaotakiwa kukomesha biashara hiyo kwa kuwakamata wafanyabiasha hao ndio hao hao nao wafanyabiashara kwani wanapowakamata kama ni miraa au dawa za kulevya wanazichukua wao na kuziuza. Kwa mfano askari wa njia ya Horohoro - Tanga wapo pale kwa ajili ya kukamata miraa tu na wanaikusanya na kuchukua wao, mingine wanagawa kwa marafiki zao na mingine wanauza, hii ni hatari sana. Je, biashara hizi za dawa za kulevya zitakwisha kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali (Wizara) wajitahidi sana kuhakikisha polisi wapatae mshahara wao mapema kwani hali zao ni duni wengi wao wanaishi kwenye mazingira magumu hivyo wajengewe nyumba zitakazokuwa na hadhi kwa mfano Tanga askari jeshi nyumba zao ukaziona zinatia imani ndogo, vijumba vidogo sana vya tangu enzi ya mkoloni, tafadhali Mheshimiwa Waziri wajengewe nyumba zinazoendana na wakati wa sasa ili waweze kufanya kazi kwa kujituma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la vitambulisho ni muhimu sana ukiangalia wahamiaji ni wengi sana kwa sasa humjui Mtanzania ni yupi na mhamiaji ni yupi kwa kweli ni vurugu mechi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri lazima wawe makini sana na uhamiaji wa wasomali ni hatari, wanatawala uchumi wetu kwa nguvu zote, sasa hivi kwa mfano eneo lote la gerezani wamelinunua sijui kama Serikali ina taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo vitambulisho ni muhimu sana ili kuwatambua wahamiaji ni wapi. Ahsante.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri, Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mkurugenzi Mkuu wa *NIDA* na Serikali kwa ujumla kwamba kwa mara ya kwanza Watanzania watakuwa na Vitambulisho vya Taifa. Kwa kuwa kampuni itakayohusika na utengenezaji huo imekwishateuliwa naamini kazi hiyo itafanyika

kama ilivyopangwa na Serikali. Nawapongeza tena Mkurugenzi Mkuu Maimu, nakuombea kwa Mwenyezi Mungu ufanikishe hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, msongamano wa wahalifu katika mahabusu (Magereza) ni tatizo sugu katika nchi yetu. Msongamano huu unatokana na Askari Upelelezi kuchelewesha sana upelelezi. Ucheleweshaji wa upelelezi hujenga pia mazingira ya rushwa katika kesi. Uwepo utaratibu wa kupeleleza kesi hasa zile ndogo ndogo wa wizi wa kuku na kadhalika na ni ukweli usiopingika kuwa mahabusu waliojaa magerezani ni wale wenye kesi ndogo ndogo ambazo upelelezi wake unaweza kukamilika kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wetu wanaishi katika nyumba duni mno, Serikali iendelee na ujenzi wa nyumba za askari kila mkoa. Nina imani Jeshi la Magereza likipewa kazi ya kujenga makazi kwa ajili hiyo wanaweza wakafanya kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la dawa za kulevya bado ni kubwa kwa vijana wetu wauzaji wa dawa ya kulevya wanaweza kufahamika kupitia kwa utumiaji wa dawa hizo, nadhani Serikali haijafanya operesheni ya nguvu kuwatambua wahusika hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahamiaji haramu ni tatizo kubwa nchini kwetu. Hivi karibuni kumekuwepo na matukio mengi ya wahamiaji haramu, wengi wao wamekamatwa Kusini mwa nchi wakiwa wamekwisha tembea mikoa zaidi ya kumi kutoka Somalia. Nashauri udhibiti katika mipaka yetu uimarishwe zaidi. Pamoja na hayo yanayotokea nampongeza sana *IGP* kwa kazi nzuri anayofanya kwani uhalifu umepungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika sasa wa Serikali kukubaliana na ombi la Watanzania wa uraia wa nchi mbili. Hii itatoa fursa kwa Watanzania waliozaliwa nje ya nchi kufaidi matunda ya nchi yao, pia waliooa wasio raia wa Tanzania kuishi bila kulipishwa kodi kwa familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Jeshi la Polisi ndio lenye wajibu wa kutoa leseni za udereva kwa vyombo vya usafiri vya moto, nashauri Jeshi la Polisi kufanya mafunzo kwa vijana waendesha pikipiki nchini ili kupunguza ajali hizo. Vijana wengi hawana leseni na wenye leseni hawajui sheria ya usalama barabarani. Kwa kuthibisha hili naliomba Jeshi la Usalama barabarani kufanya mahojiano ya ghafla kwa waendesha pikipiki watashuhudia ukweli huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia kuwa katika hali ya uzima wa afya, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba yake nzuri ambayo imejaa matumaini ya Watanzania ambao wengi wao ni wapenda maendeleo ya nchi yao ambayo ni tulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia hotuba hii kwa kujielekeza upande wa nyumba za askari polisi. Nyumba wanazoishi askari hawa ni za kutisha hali ambayo inapelekea kuwa hatarishi kwa upande wa maisha yao. Kama maisha yao ndio hali hiyo halafu tunataka wawe watiifu, wapenda kazi, askari huyu anaenda kazini (zamu) hajui familia yake inakula nini na wala hafahamu wageni ambao wamemtembelea watalala wapi, askari hao ndio walinzi wetu ambao sisi tumelala wao wapo nje wanatulinda. Namuomba Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho, naomba atueleze ni lini askari hao watapatiwa nyumba za kuishi ambazo zinaendana na kazi zao ambazo wanazifanya, ili waweze kufanyakazi kwa kuipenda bila ya kuhisi ugumu wa kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niendelee kuchangia upande wa maslahi ya askari. Maslahi ya askari polisi bado hayajaridhisha, askari wamekuwa hata kazi yao hawaifurahii kutokana na uduni wa mishahara yao, hizi tuhuma za rushwa ambazo wanapewa askari polisi na mazingira ambayo yamewazunguka basi unaweza kusema ni kweli, kutokana na maisha waliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri afanye iwezekanavyo askari hao wapate maslahi mazuri ili waweze kufanya kazi zao vizuri, hata hivyo tuhuma ya rushwa zitaondoka miongoni mwao, ndipo raia watakuwa na imani na askari hao. Pia namuomba Mheshimiwa Waziri, ayafanyie kazi haya ambayo nimependekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika Wizara hii hasa kwa baadhi ya vipengele ambavyo nahisi vinali-*turnish* Jeshi letu la Polisi. Katika kupitia kitabu cha Taarifa ya Hali ya Uhalifu kwa Januari hadi Desemba, 2010, kwenye Jarida la nyuma la kitabu hiki imeainisha kuwa nanukuu; "Dhima ya Jesho la Polisi la Tanzania ni kuwa na jeshi lililopanuka, linaloonekana, linalofikika, linalojali wateja/umma na linaloshirikiana na wananchi katika kulinda mali na maisha ya wananchi." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhima hii napenda kueleza masikitiko yangu juu ya ueledi na uadilifu wa Jeshi la Polisi. Nilitegemea kwa maneno matamu na yenye kutia imani kubwa kwa wananchi, lakini hali si hivyo kwa kuwa mgodi wa Buhemba ambao mara ya mwisho ulikuwa unamilikiwa na Kampuni ya Meremeta. Baada ya utelekezaji wa mgodi huu ambao ni rasilimali adimu kwa maendeleo ya nchi yetu, na hivyo nilitaraji Serikali ilikuwa na malengo mazuri kabisa kwa kupeleka ulinzi wa Jeshi la Polisi ili kulinda samani na hali za ule mgodi *(all fixed and tangible assets).*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa fedheha kubwa sana kwa Serikali na inatia uchungu kuona mali zinatembelea na kutojaliwa wala kuchukuliwa hatua. Kwa dhima ya kulinda mali ya umma, wananchi na kadhalika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliamua kupeleka askari wake pale ili kulinda mali za mgodi ule na ikumbukwe kwamba mali ziliachwa zikiwa katika hali nzuri ya kuruhusu mwekezaji yeyote kutake *over* na nadhani ni matarajio ya Serikali na wananchi ama *all property will be kept in the safety hand.*

Naomba kuainisha baadhi tu ya mali zilizokuwepo ambazo ni magari yakiwa katika *excellent condition,* magari haya kwa sasa vipuli vyote vimeshaibwa na sasa yamebaki kama vyuma chakavu *with only sample showing that* ile ilikuwa ni gari. Pia kulikuwa na *computer* nyingi tu lakini sasa ukienda hamna kitu kama hicho, nyumba zilizokuwepo tena nzuri na imara za kisasa ila sasa imebaki magofu tu maana mabati, nondo, vyoo kwa maana ya *toilets* yaani ni aibu sana tena sana kwa nchi, leo hii mitambo ambayo ilikuwa inatumiwa kuendeshea shughuli za mgodi ule leo ukifika utatoa machozi, maana vinu vimeuzwa aidha, vipuli vyake au vinu vyenyewe, sasa tujiulize hawa polisi ndio wameenda kulinda mali ile lakini wao ndio wamekuwa mstari wa mbele kuuza vipuli na vifaa vinginevyo vilivyokuwepo katika mgodi ule tena kwa bei ya uharibifu yaani mtaani wanasema kuwa ni bei ya kutupa au ya kumwangusha mlevi.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi hapa tuliona kwenye vyombo vya habari hususani *ITV* wakionyesha mgodi huu na masikitiko ya wananchi juu ya uharibifu huu mkubwa wa mali ya umma. Hivi ni mwekezaji gani atawekeza pale? Hata Serikali leo ikifanya *evaluation of property* pale ni hasara kiasi gani itapatikana? Lakini cha ajabu na cha kujiuliza ni kuwa Jeshi la Polisi limechukua hatua gani kwa hawa polisi wanaolinda doria katika eneo lile la mgodi? Kwani wakati wanaanza kulinda sehemu ile walikabidhiwa mali za mgodi huo na ni imani yangu kila askari aingiapo doria hukabidhiwa hivyo ni kwa ku-*trace* hiyo *chain* ya wote waliolinda huo mgodi kwa kutokuwa mwaadilifu/waadilifu na hivyo wanastahili kuwajibika na si kuwa kazini hadi leo.

Sasa napenda katika majumuisho ya Waziri nijulishwe maana askari hao hao ndio wapo mstari wa mbele kuwapiga risasi wananchi hata wale wanaotuhumiwa kwa kuiba kuku na kuuwawa, hii jamani ni uvunjifu wa haki za binadamu na hao askari inabidi wapigwe risasi pia na wapelekwe gerezani na wao kama Watanzania wengine wanavyochukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Naomba sana majibu kwa hili.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote walioshirikiana na Waziri kwa kuandaa hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Jeshi la Polisi kwa kujitahidi kufanya kazi kwa uzalendo na umakini mkubwa wa kulinda raia na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wetu wanafanyakazi wakati mwingine kwa mazingira magumu ya vitendea kazi makazi kwa maana ya mazingira yenyewe hayaendani na mila na desturi za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Tumbatu limegawanyika sehemu mbili, kuna eneo la juu na Kisiwani Tumbatu na Kituo cha Jeshi la Polisi kipo Mkokotoni yaani kipo eneo la juu ndani ya Jimbo la Tumbatu na lile eneo la Kisiwa ambako pia kuna wananchi wengi hakuna Kituo cha Polisi kunapotokea machafuko huwa hakuna chombo cha haraka kuweza kufika katika eneo la tukio. Mimi ninaiomba Serikali kukipatia bodi kituo hiki kilicho karibu na bahari ili linapotokea tatizo waweze kufika kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara na posho kwa jeshi ni midogo sana na hupelekea askari wetu wadogo yaani kipato cha chini wanapostaafu wanapata kiinua mgongo kidogo sana, lakini pia pensheni huwa ndogo sana kupelekea kupata shilingi 60,000/= kwa miezi mitatu na Wizara ya Fedha walisema humu Bungeni kipindi cha Bunge 2005-2010 kwa wastaafu wa kipato cha chini walipwe pensheni ya shilingi 50,000/= kwa mwezi mbona mpaka sasa kuna wastaafu bado wanapata shilingi 20,000/= kwa mwezi hivi ile nyongeza ilikuwa ni ya wastaafu wa kiwango gani cha wastaafu ambao wameongezewa posho hiyo kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu makazi ya askari, nyumba wanazoishi zipo katika hali mbaya sana, naomba ukarabati wa nyumba hizi ufanyike haraka ili askari hawa wajisikie vizuri wanapotoka kazini kwa sababu askari wengi wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar kulikuwa na makubaliano ya kuchangia Kamishna mmoja na Naibu Makamishna wanne je, suala hili utekelezaji wake umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna askari kafariki toka tarehe 24/06/2005 anaitwa *PC* Tatu Saidi Abeid *WP* 4857 mpaka hivi leo bado warithi wake hawajapata kiinua mgongo hawajalipwa, naiomba Serikali iliangalie hili suala kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri. Pia naomba nilipongeze Jeshi la Polisi kwa kazi kubwa wanavyoifanya hasa katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana nizungumzie suala la maslahi ya watumishi wa Jeshi la Polisi hasa mishahara yao ni midogo mno. Niiombe sana Serikali iwapandishie mishahara sambamba na kuwalipa madai mbalimbali wanayodai Serikali, ninaomba Serikali iwalipe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wakimbizi, Mpanda kuna wakimbizi wa makazi ya Mishamo na Katumba. Wakimbizi hawa waliamua kuendelea kuishi Tanzania na hawataki kurudi Burundi. Kulingana na wakimbizi hawa kuomba uraia wa Tanzania na kukubaliwa, kuna changamoto kubwa zinazowakabili kwani wanatakiwa waondoke kwenda katika makazi mapya tofauti na maeneo wanaoishi sasa. Niiombe Serikali itoe rasmi tamko la wakimbizi kama mwaka huu Serikali haina nafasi ya kuwahamisha basi itoe tamko la kuwaarifu ili waanze kufanya maandalizi ya kilimo. Tusipowaandaa mapema watashindwa kujua kama wanahamishwa au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni muhimu sana kwa jamii hii ya wakimbizi wa Mishamo na Katumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, jimboni kwangu kuna gereza la kilimo la Kalilankulunkulu. Gereza hili limechakaa sana pamoja na nyumba za watumishi. Naomba sana Serikali itenge fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa nyumba za watumishi na kuboresha gereza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali kutatua mgogoro wa Ggereza la Kalilankulunkulu na wananchi wanaozunguka gereza hilo juu ya kugombania mpaka wa eneo ambao bado kuna mgogoro baina ya vijiji vya Sijonga, Iloba, Kasinde. Niiombe Serikali iandae ustaaratibu wa kusuluhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Uhamiaji, naomba idara hii iboreshwe kwa kuwapa vitendea kazi kwani wanafanyakazi bila vifaa, mpaka wa nchi yetu Magharibi ni mpaka mrefu sana ambao ni vigumu kuudhibiti bila vifaa, niombe Serikali iwanunulie vyombo vya kurahisisha usafiri kama boti na magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Waziri kwa hotuba nzuri ya Bajeti japo nikiri kuwa fedha iliyotengwa kwa Wizara hii ni ndogo, tena ndogo sana ukilinganisha na majukumu wanayotakiwa kuyatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuwekwa kwenye kumbukumbu ya mahitaji ya nyumba za polisi katika Kituo cha Lamadi ambao sasa umekuwa Mji Mdogo. Hili ni tatizo na kero kwa askari, naomba maelezo ni lini kituo hiki kitaingia kwenye mpango. Hata hivyo napenda nishauri Wizara kufanya utaratibu wa kushirikisha zaidi jamii ili kupata fedha za kujenga nyumba na vituo vya polisi kwa haraka zaidi badala ya kusubiri mgawo wa Bajeti ya Serikali pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka ya karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la biashara ya dawa za kulevya. Imefikia wakati hata viongozi wakuu wa Serikali wanapata kigugumizi kuwataja au kuelekeza kukamatwa kwa wafanyabiashara wa dawa za kulevya. Hivi ni kwa nini polisi wanawagwaya hawa? Inakuwaje wanakuwa wepesi kukamata wapika gongo au waandamanaji halafu wanaacha kuwakamata vigogo wa dawa za kulevya? Mtazuiaje jamii kwa nini polisi nao wanashiriki katika biashara hii chafu? Naomba jeshi letu lijisafishe kwa lawama hii na lichape kazi kwa umakini na kuwadhibiti vigogo wa biashara hii ili kuilinda jamii yetu kwenye madhara ya dawa hizi. Mbinu mnazo na uwezo mnao, ebu amueni sasa!

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia Jeshi la Magereza. Napenda nipongeze kwa kazi mnayoifanya. Hata hivyo napenda kuhamasisha jeshi hili lidhamirie kujitegemea sasa kwa kutumia rasilimali watu ilizonazo. Miradi ya uzalishaji chakula, mbegu, samani na ujenzi inaweza ikakuzwa kwa kutumia utaalam sahihi na uwekezaji stahili, miradi hii iende sambamba na kufundisha wafungwa ili waanze kujitegemea na kuishi kama raia wema. Hakuna sababu kwa watendaji wa Jeshi la Magereza kuishi katika nyumba duni, kwani wangeweza kushindana na SUMA JKT katika miradi ya kiuchumi. Naomba magereza watengeneze mpango mkakati unaoelekea kulifanya jeshi hili kuwa wakala *(agency)* ili liweze kujitegemea zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliposema Bajeti ya Wizara hii ndogo inaathiri sana uwezo wa Jeshi la Polisi kutenda kazi. Uhaba au ubovu wa magari pamoja na mafuta ya kuendeshea kazi ni tatizo la kudumu katika vituo vyetu hasa vile vya vijijini. Naomba sana Serikali iviwezeshe vituo hivi vifanya kazi kwa uhuru. Inafikia wakati polisi wanaomba mafuta kutoka kwa wananchi ili kufuatilia matukio ya uhalifu. Japo ni vyema wananchi kuchangia, lakini madhara yake ni kulifanya jeshi letu kuwekwa mfukoni mwa wafadhili hawa na hivyo kuathiri haki za raia wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine sasa hivi taasisi za Serikali zinahujumiwa kiuendeshaji na vyama vya siasa, vyama vya upinzani. Uwezo wa kupeleleza na kubaini mambo ya kuhujumu mipango ya Serikali unaofanyika katika taasisi na vyuo vya umma mbona haubainiki mapema na kudhibitiwa. Naomba idara ya upelelezi ifanye kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba nizungumzie suala la haki na usalama wa polisi. Hivi karibuni kunaonekana kuibuka dhana ya haki za binadamu kuwa ya maana zaidi pale mhalifu anapodhaniwa na askari anayotoka kumkamata au anayepambana naye. Hivi haki ya polisi wetu ipo wapi? Nani anayewalinda wanapotekeleza majukumu yao? Ni vema sheria zetu zikae sawa ili polisi wawe na ulinzi wa kisheria wanapotekeleza majukumu yao. Haki za binadamu ni kwa wote na siyo kwa wahalifu tu! Itakuwa ni ajabu sana kama polisi watashambulia tu watu waliotulia, siyo kitu cha kawaida labda kama atakuwa na matatizo ya akili. Hivyo ni vyema taasisi hizi za haki za binadamu vijue kuwa hata polisi ni watoto wa Watanzania na wana haki ya kulindwa na kuthaminiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba askari wetu wa Jeshi la Polisi Wilayani Meatu wajengewe nyumba ili watoke uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata *OCD* anaishi uraiani nyumba za kupanga. Naiomba sana Serikali ilione hili kuwa ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kufanya kazi katika mazingira magumu. Naiomba Serikali kuhakikisha kuwa jeshi hili linawezeshwa kuwa na miundombinu ya kisasa katika kulinda na kudumisha amani ya nchi hii katika misingi ya haki na uhuru. Pili, maslahi yao yaboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maadili ya kazi yao jeshi hili linapaswa kutojihusisha na siasa. Hivyo si vyema kwa Serikali kutumia jeshi hili isivyostahili katika kunyima haki za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusemea *case study* ya mambo yanayotendeka katika Jimbo la Karatu – Kata ya Rhotia na kijiji cha Chemchem.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu wananchi wa Kijiji cha Chemchem wamekuwa na mgogoro na Serikali yao ya kijiji wamepeleka malalamiko yao katika ngazi zote zinazohusika, matokeo yake hakuna hatua yoyote inayohusika na mamlaka husika. Hatimaye wananchi wakaamua kuondoa Serikali ya Kijiji chao na kuomba uongozi wa Halmashauri/Mkuu wa Wilaya/Mkuu wa Mkoa waweze kuwasaidia kutatua mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza ni pale ambapo Mkuu wa Wilaya anamtumia *OCD* kukamata wale wote wanaodai kuwa wasemaji wakuu wa wananchi. Je, utawala wa sheria uko wapi? Utawala bora uko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata jibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri la mgogoro wa Kijiji cha Chemchem wakati ambapo hadi sasa ofisi ya kijiji imefungwa na wananchi wakilinda kwa mikuki/mishale na kadhalika. Je, hali hii itaendelea mpaka lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonesha kuwa Mkuu wa Wilaya/Mkuu wa Mkoa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu wameshindwa kutatua mgogoro huo. Mheshimiwa Waziri, chonde chonde naomba jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri apate kufuatana nami ili kutatua migogoro hiyo pamoja na mgogoro wa Kijiji cha Mbuga Nyekundu kule Kata ya Baray Tarafa ya Eyasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro yote hii inahusisha kwa namna moja au nyingine kuwa Serikali inalitumia vibaya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji sana amani, haki na utulivu kuwapo kwa wananchi wetu. Pengisne suala zima la uwajibikaji bila kuahirisha tatizo mpaka tatizo linakuwa sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachelea kusema kuwa matumizi ya nguvu ya dola si namna muafaka ya kuleta amani/suluhu.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali kwa asilimia mia moja kwamba Jeshi la Polisi linafanya kazi katika mazingira magumu sana kama vile uhaba wa vitendea kazi (magari, mawasiliano, mafuta), uduni wa sayansi na teknolojia ya uhalifu wa kisasa *(cyber crime),* uhaba wa askari, uhaba wa majengo ya vituo na nyumba ya makazi, mishahara midogo, posho ndogo za chakula na nyumba, ukosefu wa fedha za mafunzo, pamoja na matatibu lukuki. Pamoja na matatizo yote haya na changamoto zote hizi yapo mambo ambayo napenda kushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ili kupunguza malalamiko yasiyo ya lazima juu ya mauaji ya raia yanayosadikiwa kufanywa na Jeshi la Polisi ni vema Jeshi likawekeza katika kupunguza vifo vya namna hiyo labda katika mazingira yasiyoepukika kama ifuatavyo:-

Mosi Kikosi cha Kutuliza Ghasia kiwe na utaratibu wa mara kwa mara labda kila baada ya miaka miwili hivi kufanya maonyesho ya *riot* kama utoaji wa elimu kwa umma mikoani ili wananchi wajue ni mazingira gani wanatakiwa kutii amri za Jeshi la Polisi katika kusitisha au kutawanyika katika maandamano yao. Wananchi walio wengi hawajui sheria na kanuni zinazotawala *riot* na wanadhani kundi kubwa la watu haliwezi kudhibitiwa kwa risassi za moto japo kutojua sheria siyo kinga, *riot drill* isiishie tu vyuoni wakati wa kumaliza mafunzo au katika makambi yao.

Pili katika hili ni elimu ya *riot* kutolewa shule za sekondari na vyuo kwani huko ndiko yaliko makundi ya umri unaopenda na kukubali kushiriki maandamano yasiyo halali. Tatu tumieni vyombo vya habari (redio, televisheni, magazeti) kutoa elimu hii kwa umma kwa sababu *riot* siyo siri ya kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili ni kuimarisha Kitengo cha Intelejensia. Kitengo hiki kinaonekana kama hakipewi umuhimu sana na Jeshi la Polisi. Bila ukusanyaji wa taarifa za kihalifu mtazuiaje uhalifu. Katika *organization structure* ya Jeshi iwe ni Idara inayoripoti kwa *IGP* sawa na *CID* na siyo kuwa Kitengo ndani ya Mkurugenzi wa *CID* yaani *DCI.* Vivyo hivyo kishuke mikoani kama alivyo *RCO,* vivyo hivyo kishuke Wilaya kama alivyo *OC-CID* na kishuke chini kwenye vituo vidogo walipo wananchi na kufanya *chain of command* na *chain of reporting* kuwa ya kila siku kila dakika kwani watakuwa wanawasilisha taarifa polisi wakamataji na wapelelezi. Kitengo hiki kiwe na fedha za kutosha na vifaa vya mawasiliano ya kisasa na wasomi na ikibidi matumizi ya kazi hizi nayo yasihojiwe kwa ajilia ya usalama wa nchi. Mkitegemea *CID* tu hamtaweza kwani *CID* wa sasa wote ni kama *GD* kwani wametambulika kwa vile wengi wanaishi kambini. Hwa wa intelijensia wasiishi kambini na ikibidi hata wawe wanafanya hata bidii ya kuwa mbali na askari wenzao kimahusiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, ni kutokuwepo na vituo vya polisi wanamaji *(Marine Police)* kwenye kila wilaya angalau ambazo zipo kwenye maziwa na bahari ambako hufanyika uhalifu wa majini. Kwa mfano Ziwa Victoria kuna vitatu tu, kimoja kila mkoa Sota – Mara, Mwanza na Kagera pale Bukoba. Kutoka Sota Wilaya ya Rorya hadi Kisiwa cha Najuba Wilaya ya Bunda (Jimbo la Mwibara) ni zaidi ya kilomita 150. Ni wakati gani watashughulikia tukio kwa wakati. Hii siyo sahihi lazima tuweke angalau kituo kimoja kila Wilaya yenye ziwa na bahari kwa kuanzia. Kwa mfano Jimbo la Mwibara ambalo lina ziwa kubwa katika jimbo la Bunda ambapo ndipo kuna Makao makuu ya Wilaya ndio panastahili kuweka hicho Kituo cha Polisi cha Wanamaji. Aidha, kwa sasa tunashukuru Serikali mmetuletea boti za kisasa za doria Ziwa Victoria kwa ajili ya kudhibiti uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni lini Kituo cha Polisi cha Daraja kitaanza kujengwa Kibara licha ya ramani na kiwanja kupatikana, je, Bajeti hii imetenga fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono, ahsante.

**MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na Naibu

wake, Mheshimiwa Balozi Kagasheki kwa kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yao kwa mwaka 2011/2012 kwa ufasaha mkubwa. Naunga mkono hoja!

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeamua kuchangia kuikumbusha Wizara kuhusu ahadi yake ya kufungua Gereza la Kyela kabla ya tarehe 30 Juni, 2011. Ahadi hiyo ilipokewa na wananchi Wilayani Kyela kwa furaha, nderemo na vifijo kwa sababu wana imani kubwa na uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne. Vilevile wananchi wamechoshwa na adha kubwa wanayopata miaka nenda rudi ya watuhumiwa wa makosa mbalimbali Wilayani Kyela kupelekwa Gerezani Tukuyu, Rungwe ambako hukwama Kyela kuendelea na kesi zao! Matokeo yake ni kesi za jinai Kyela kuchukua muda mrefu mno! Ndugu na jamaa wa mahabusu huingia gharama kubwa kufuatilia afya na kesi za ndugu zao ambao wanarundikwa Wilaya nyingine ya Rungwe bila uhakika wa kuwahishwa kwenye kesi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetembelea Gereza la Kyela likiwa kwenye matengenezo. Gereza lipo tayari kufunguliwa, hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri afuatilie kwa karibu suala hili ili kurejesha imani ya wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kwa kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani na kuniwezesha kuwa nimo ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie Bajeti ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja mbele yako anijibu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la posho ni shilingi150,000/= au shilingi 100,000/=. Ni muda gani posho hiyo ya laki moja na nusu imeanza kutolewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anaelewa kuwa kuna Kituo cha Polisi Kombeni ambacho kimejengwa kwa nguvu za wananchi na viongozi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Jeshi la Polisi Zanzibar kwa kufanya kazi nzuri sana ya kusimamia amani katika Visiwa vya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kutufafanulia michango yetu hii atueleze ni lini vituo vyetu vya polisi vitaboreshwa kwa kupatiwa vitendea kazi ili kuboresha jeshi letu, kwani vituo vingi nilivyotembelea kwa wakati wangu nimegundua kuwa karatasi za kuandikia mahojiano na walalamikaji na walalamikiwa askari mhusika ndio anaetoa pesa zake kwa ajili ya kununulia karatasi hizo, hivyo inaonesha wazi kuwa kwa utaratibu huo unachangia rushwa kwa Jeshi letu la Polisi kwa jumla.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Mheshimiwa Waziri naomba ufafanuzi katika yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gari la polisi Wilaya ya Lindi Vijijini, gari iliyopo ni moja na ni chakavu aidha, hupewa mafuta lita tano kukiwa na matukio unalazimika kuchangia mafuta, je, kwa nini basi pikipiki za polisi zisipelekwe Kituo cha Rutamba na Mchinga ili kukabiliana na changamoto za usafiri katika Wilaya ya Lindi Vijijimi?

Mheshimiwa Naibu Spika, polisi kuwabambikia raia kesi, yako matukio mengi ya namna hii, ni hatua zipi zinachukuliwa dhidi ya askari wenye kuendesha vituo vya namna hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ukosefu wa *solar power* kwa nyumba za watumishi wa Magereza Kingulungundwa lililopo kata ya Kitomanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa nyumba kwa askari polisi Wilaya na Lindi Vijijini. Kwa muda mrefu Serikali haina mkakati wa kujenga nyumba kwa ajili ya watumishi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, hongera Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, *IGP,* Mkuu wa Magereza, Mkuu wa Uhamiaji na watumishi wote kwa kazi nzuri mnayoifanyia nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Ndagalu Jimbo la Magu ina Kata nne za Shishani, Jinjimili, Kabila na Ng'haya. Tarafa hii ilikuwa na kituo kimoja tu cha polisi katika Makao Makuu ya Tarafa – yaani Kijiji cha Kabila. Kwa bahati mbaya kituo hiki kiliungua moto. Hivi sasa tarafa nzima haina Kituo cha Polisi, kwa kuwa kiwanja kipya kimeshapatikana na michoro ya kituo kipya ipo tayari, je, Wizara ipo tayari kushirikiana na mimi, Halmashauri ya Wilaya ya Magu kuhakikisha kwamba kituo kipya kinajengwa na kukamilika mwaka huu wa fedha? Tunapata adha kubwa sana. Tunaomba msaada na ushiriki wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linafanya kazi kubwa hapa nchini kwetu. Naiomba Serikali yafanyike yafuatayo ili kuboresha utendaji kazi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa makazi ya Jeshi la Polisi hususani kwa askari walio katika ngazi za Wilaya kwani nyumba nyingi zimejengwa maeneo ya mijini tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya polisi yaboreshwe ili kuongeza ari ya utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kutokuwa na pesa za maendeleo kwa Kitengo cha Zimamoto ni kuzorotesha utendaji wa kazi wa kitengo hicho na kuashiria upotevu wa rasilimali wakati majanga ya moto yanapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba askari polisi wasiwe wanakaa kituo kimoja kwa muda mrefu kwani kitendo cha askari kukaa kituo kimoja kwa muda mrefu kinapunguza utendaji kazi wa askari wetu. Pia nashauri mishahara ya polisi iweze kutazamwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu katika Wizara tajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze na askari wetu wa usalama barabarani. Napenda kusema kuwa chanzo cha ajali barabarani si uzembe wa madereva tu kama inavyoonesha, bali askari wetu wa usalama barabarani nao ni chanzo kikubwa. Askari hawa baadhi wamekuwa na tabia ya kupokea rushwa kwa wamiliki wa magari mabovu na kuwaruhusu waendelee na safari huku wakijua ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, gari inapoendelea na safari zake ndipo ajali sasa hutokea na kuteketeza roho za wasio na makosa. Je, hapo ni kosa la dereva au askari aliyepokea rushwa na kuruhusu gari ifanye kazi? Ubovu wa barabara nayo ni sababu kubwa inayosababisha ajali. Serikali nayo kwa uzembe wa kutotengeneza barabara kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, alama za barabarani haziwekwi kuonesha ishara kwa madereva hasa wanaosafiri usiku. Makandarasi wanaotengeneza barabara wamekuwa wakijenga miinuko ya kudhibiti mwendo wa magari ambayo haina uwiano mzuri na badala yake imekuwa ikisababisha ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mapato imekuwa ikitoa leseni kwa madereva wanaojifunza mitaani tu na hayo yote ni mapungufu ya Serikali na mipango yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipozisba ufa tutajenga ukuta. Serikali isilie na mchawi, mchawi ni mipango ya Serikali yenyewe ijipange katika ufuatiliaji ili ajali zipungue.

Mheshimiwa Naibu Spika, polisi wa kawaida huyu kazi yake ni kumlinda raia na mali zake. Lakini polisi hawa wamekuwa na tatizo la upuuzaji hasa raia anapovamiwa na majambazi. Raia anaweza kupiga simu kituoni lakini polisi hawaonekani mpaka raia anaibiwa mali zote ndipo askari wanatokea bila faida yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo yote ni ukosefu wa vitendea kazi vya kutosha kwa idara hii. Hivyo badala ya kuwalaumu bure, naiomba Serikali kwanza iongeze magari ya kutosha kwa idara hii kila wilaya ili wakabiliane na uhalifu kwa upana zaidi, pia wapewe mafuta ya kutosha yakae tayari kwa safari za dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wajengewe nyumba hasa Jeshi la Magereza kwani Jeshi la Magereza wanaishi katika nyumba zilizochoka na mazingira yao wanayoishi ni magumu, vyoo vimechoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwaangalie sana askari wa magereza na iboreshe maisha yao kwa kuwaongeza mishahara, kuwajengea majengo ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia shughuli zinazofanywa za ulinzi na usalama, zinaleta matumaini ya kulipongeza Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ambalo lilimtoa Nduli Iddi Amini Dada, Rais wa Uganda alipotandikwa na kuikimbia Uganda. Mpaka leo limekuwa ni Jeshi la Wananchi kweli linaloheshimika na kuleta mategemeo ya ulinzi wa mipaka yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni kwa Jeshi la Ulinzi linalosimamia Usalama wa Raia na mali zao (polisi). Jeshi hili limekuwa likilalamikiwa sana na raia kwa kunyanyasa raia badala ya kuwalinda. Kumekuwa na matukio mengi yanayotendwa na jeshi hili kwa kuwapiga na kuwaua raia bila huruma na Serikali ya Chama cha Mapinduzi haichukui hatua yoyote ile. Kana kwamba wananchi wamekuwa kama wanyama wa porini. Hata wanyama wana unafuu sababu wanalindwa na kukatiwa leseni ya kuwindwa na kuwaua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limekuwa ni jeshi linalotafuta fedha kwa nguvu kutoka kwa raia kwa kuwabambikizia kesi raia na wapo tayari hata kuwawekea raia misokoto ya bangi ili mradi wapate fedha tu na kama raia hana fedha ya kutoa basi atapelekwa mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Usalama Barabarani ndiyo kabisa, wananchi wamekuwa wakipoteza maisha yao na wengine kupata ulemavu wa maisha kwa kuwafumbia macho madereva wanaokwenda mwendo wa kasi, wanaobeba abiria kupita kiasi, wanaoendesha magari mabovu barabarani kwa sababu tu wanapewa rushwa. Hao ndiyo askari wetu wanaolinda raia na mali zao. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa askari wanaobainika kuwaua raia au kupokea rushwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 21 Juni, 2011 niliuliza swali katika Bunge lako Tukufu linalohusu wakimbizi kurudi kwa njia za panya. Wakimbizi wamekuwa ni tatizo kubwa wanapoingia kutoka Burundi wamekuwa hawana makazi maalum na badala yake wamekuwa wakijichanganya na wenyeji matokeo yake baadhi yao wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya uhalifu kama ujambazi wa utekaji magari, unyang'anyi wa kutumia nguvu na uwindaji haramu. Ninaomba Jeshi la Uhamiaji lichukue hatua ya kuwasaka wakimbizi hawa walioingia Tarafa ya Karema, Tarafa ya Mpimbwe, Tarafa ya Kashaulili na katika makazi ya Mishamo na Katumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naiomba Serikali iwajengee nyumba za kutosha askari ili kulinda heshima yao kwani wengi wao wamekuwa wakiishi katika mazingira yasiyo ya heshima. Pia waongezewe mishahara na kupewa marupurupu yanayostahili ili kuwaepusha na tamaa ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho namuomba Waziri anieleze tangu nilitoa taarifa ya kurudi wakimbizi Tanzania kwa njia za panya, je, Serikali imechukua hatua ipi ya kiutafiti ili kubaini wakimbizi hawa walio rudi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nini hatima ya Serikali kuongeza askari wa kutosha katika mikoa yenye upungufu wa askari hususani Mkoa wa Rukwa ambao umepakana na nchi jirani?

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono mpaka pale nitakapoona Jeshi la Polisi limeacha kuwanyanyasa wananchi na kuwaua, kana kwamba wao ni nzige. Ahsante na nawasilisha.

**MHE. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia mambo ya Wizara ya Mambo ya Ndani hasa upande wa magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiambatanisho Na.1, ukurusa wa 41 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kinaonesha kwamba wapo mahabusu wengi sana katika magereza yetu kuliko wafungwa wenyewe. Napendekeza kuwa muda wa mahabusu upunguzwe ili kupunguza mrundikano wa mahabusu katika magereza yetu. Mfano, miezi mitatu inatosha, kama upelelezi bado haujakamilika, basi mahabusu waruhusiwe na wanaweza kurudishwa mahabusu tena upelelezi ukiishakamilika, ili kesi ziendelee wakati watuhumiwa wakiwa mahabusu.

Katika Gereza la Isanga (Dodoma) wapo mahabusu ambao wamekaa gerezani kutoka miaka ya 1960, hii siyo haki. Hawa tayari wamekwishatumikia kifungo cha muda mrefu, kabla ya kesi kusikilizwa. Kwa nini watu wa aina hii wasingeachiwa huru tu maana hata adhabu yao tayari imekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahabusu wanatengana sana na familia zao kwa muda wa miaka mingi. Wakirudi wanakuta wenzi wao wameoa au kuolewa na kuzaa watoto wa nje. Ni hatari kwa mwanamke kuzaa mtoto wa nje, maana mume aidha atamfukuza mke au kuwachukia watoto wa nje. Watoto wa nje wakati wote wataishi kama jamii ya watoto wasiotakiwa na familia au ukoo *(Social outcast).* Watoto wa namna hii huwa ni hatari sana katika maisha ya jamii, wao wenyewe wanaweza wakawa majambazi, wavuta bangi na unga na ni vigumu sana kusoma shule, maana hawana mtu halisi wa kuwahudumia, kutokana na baba na ukoo kuwatenga. Kuliko kuwa na utitiri wa mahabusu, ni bora kujenga nyumba nzuri na safi za askari na pia kuboresha usafiri na mishahara ya askari, ili kuwapa motisha ya kuipenda na kufanya kazi yao vizuri, kuliko fedha nyingi kutumika kulisha mahabusu ambao wangeweza kurudi nyumbani kulima, kutunza familia na kuchangia kuinua uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na suala la sare za Askari Magereza ya Ngudu Mjini. Sare za Askari Magereza wa Gereza la Ngudu zinatia aibu. Pamoja na kwamba wafungwa nao wanavaa masempele, ni jambo la kushangaza kuona wafungwa wametangulizwa na askari mwenye viraka vinavyokwenda mpaka *layers* tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali izingatie jambo la sare zenye hadhi ili tuepushe aibu kwa jeshi letu la magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho za Askari wa Magereza za Mkoa wa Mwanza kwa ajili ya chakula hucheleweshwa sana. Badala ya kupata posho hiyo kila tarehe 15 ya mwezi, posho za askari hawa hucheleweshwa kwa mwezi mzima. Mheshimiwa Waziri afanye utafiti ni kwa nini posho hizi zikifika mkoani zinazamishwa kwa mwezi mzima. Hivi kuna mtu anafanyia biashara hizi posho za chakula kabla ya kuwapelekea walengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni kwa nini Serikali yetu imechelewesha uamuzi wa suala la uraia wa nchi mbili. Wakati sasa umefika raia wetu wenye uraia wa nchi zingine wapewe uraia wa Tanzania bila kuwataka kujivua uraia wao wa nchi za nje kwani kufanya hivyo ni kuwadhulumu haki zao za kiuchumi katika nchi hizo. Tunapoona Watanzania wanapigania kurudi nyumbani, tusiwazuie kuja nyumbani kutuletea maendeleo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa iache ubinafsi wa kuhofia kunyakuliwa vyeo vyao vya kisiasa. Basi kama Serikali ina hiyo hofu, basi waweke mipaka kwa walengwa lakini Serikali iwape Watanzania uraia ikiwa ni haki yao kama Watanzania waliozaliwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kuanza kusema kuwa askari polisi ni ndugu zetu au jamaa zetu, lakini walio wengi nina imani hawatekelezi wajibu wao, kwani wao ni walinzi wa raia na mali zao, lakini baadhi yao wamekuwa kero kwa raia na mali zao. Ni vizuri sasa Jeshi la Polisi likajitathimini, kwani imekuwa ni jambo la kawaida polisi akiwa doria mahali fulani lakini ukamkuta hayupo huko na yupo maeneo ya wavuvi. Mambo haya yanatokea sana maeneo ya Bwiru Ziwani, Kabangaja na maeneo ya Kayenze, Mjini Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ambayo wanasema imewapelekea ni nyavu, lakini cha kushangaza hubomoa hata milango na kubeba samaki wakavu. Wakiambiwa wawalete samaki hao huwezi kuwapata na kama wakiletwa sio ambao waliowachukua yaani kuchukua samaki wakubwa lakini kurejesha huleta samaki wadogo, hii ni kudhalilisha Jeshi la Polisi. Pia askari wa pikipiki nao pia baadhi yao ni kero, tena walio kero ni wengi sana. Kero nyingine ni askari wa barabarani, hawa kwa kitu kidogo hawawezekani na baadhi ya ajali sababu ni wao, kwani utaona gari lakini limepita mbele ya polisi na bila tatizo hata kama ubovu upo wazi sio wa kutafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu askari wa barabarani ni vizuri kuhamishwa mara kwa mara. Kumbukeni aibu alizozitoa Muro.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa niongelee nyumba za askari hasa wale wa Jiji la Mwanza eneo la Kigoto, Igogo na hata pale Mabatini. Kigoto ni bora na busara kujenga upya nyumba za polisi eneo la Kigoto na sio kuzikarabati, kwani nyumba nyingi ni mbovu sana, hazifai kwa maisha ya binadamu. Igogo nyumba zipo katika hali mbaya sana zinahitaji ukarabati wa hali ya juu. Pia nyumba za Mabatini zinahitaji matengenezo, kwani nyumba ya familia moja kutumiwa na zaidi ya familia moja, ni wazi huchoka kabla ya wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwaletea askari polisi lakini nao wana matatizo lukuki, tukiangalia wakati wa uchaguzi baadhi ya maeneo mengi, askari polisi ndio waliotumika kuwapatia ushindi waliokuwa wagombea wa CCM tena bila haya wala woga, kwani Watanzania sasa wanaelewa vyema nani anasaidiwa na polisi na ni nani mshindi.

Mheshimwa Naibu Spika, katika Jimbo la Newala kulitokea maajabu ambayo askari wa barabarani kwa kosa la kubeba mshikaki katika pikipiki, iliwaweka vijana ndani kwa muda wa zaidi ya siku saba na hata vijana wawili wa Kidato cha Nne kushindwa kufanya mtihani kwa kuwekwa ndani zaidi ya siku kumi na kunyimwa dhamana, eti tu hawamuungi mkono mgombea wa CCM wa kijiji hicho. Kama hiyo haitoshi, kosa hilo lilileta askari kijijini hapo, tena na silaha za moto, sio kuja nazo tu bali zilitumika. Siku hiyo hiyo gari ya Mheshimiwa Andrew Chenge akiwa mgombea ilisababisha ajali kwa mara ya pili, baada ya ile ya kugonga kibajaji na mara zote mbili kuua. Mtu huyo alifika kituoni kuhojiwa na kuachiwa, tusiwape wananchi wetu mtazamo hasi. Nini hatima ya vijana wetu wa Kidato cha Nne ambao hawakufanya mitihani yao ya kumaliza, kwa kesi ya mshikaki kwenye bodaboda ya pikipiki na kushikiliwa bila dhamana? Tunawafundisha nini vijana?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni bora askari wetu wakaongezwa mishahara yao na posho zao ili kuepuka mambo mengine ambayo sio mazuri. Maisha sasa hivi ni ghali sana na maduka yote tunanunua sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo ya Wabunge kuona ndugu zao wanapokuwa mahabusu. Usumbufu huo nimeushuhudia Magereza ya Urambo, Mbunge kumuona ndugu yake, eti mpaka amtafute Mkuu wa Wilaya na aruhusiwe. Hata kama amemuona Mkuu wa Magereza Mkoa. Ni bora Wizara ya Mambo ya Ndani ikatoa semina kwa Wabunge na kutueleza utaratibu ni upi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba Magereza ya Kilimo Urambo yaliyopo Kata ya Nzenda Wilayani Urambo yapatiwe umeme, kwani ni kilomita 14 tu toka Wilayani na ukizingatia ni magereza ambayo inalima sana mazao ya chakula na biashara pia ni wafugaji wakubwa. Hebu Wizara uione hili. Pia haina hata gari hivi sasa ya kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari hawa wanaishi na watu ndani ya magereza ni vizuri kuwa na usafiri mara zote. Muihurumie magereza hii, ni wazalishaji wakubwa na pia wafugaji wakubwa.

**MHE. *ENG.* ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ofisi na Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Wilaya ya Uyui Tabora, upo uhitaji wa kuwa na Ofisi za Jeshi la Polisi katika Wilaya kubwa ya Uyui na pia nyumba za askari, tunaomba hilo. Makao Makuu mapya ya Wilaya ya Uyui yako Isikizya. Tunaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutujengea Makao Makuu ya Wilaya na kutupatia umeme. Sasa maji safi na salama na barabara ya lami inapita hapo kutoka Nzega na kuelekea Tabora Mjini. Idadi ya wakazi ni zaidi ya 400,000 na ukubwa wa eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la ujenzi wa Gereza la Wilaya ya Uyui haina Gereza, kilimo ni shughuli kubwa wilayani. Mazao ni mpunga, mahindi, alizeti, tumbuku, karanga pia ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku. Utafiti ufanyike ili kilimo cha umwagiliaji na ufugaji kitekelezwe sehemu yoyote wilayani kama Kata za Goweko, Loya, Tura, Kizengi, Lutende na kadhalika kwani masika maji mengi na hupotea Mto Iwembele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tura na Loya tunaomba vituo vya polisi vilivyopo Kata za Igalula na Kizengi ni mbali kuhudumia watu 230,000 na eneo la kilomita za mraba 134,000.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu Makadirio ya Matumizi ya fedha ya ofisi yake kwa mwaka 2011/2012 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, nampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana kiutendaji. Huu ni mfano wa kuigwa kwa maana hachoki na amekuwa mstari wa mbele katika kulitetea Taifa letu ndani na nje ya nchi. Lakini siachi kumpongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Khamis Kagasheki kwa uwezo mkubwa aliouonesha kwa kipindi chote toka ameingia katika Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sote tunavyofahamu, Wizara hii zaidi inasimamia maslahi na utetezi kwa wananchi wote na usalama wa nchi yetu. Hivyo majukumu yake ni mazito na yanahitaji umakini mkubwa sana katika utekekelezaji. Ni kheri tuwaunge mkono na kusaidiana nao katika kurahisisha utendaji wao huku tukijua wajibu wa kila mwananchi kutii sheria lakini pia kuheshimu mamlaka zilizopo bila kubeza. Kwa kufanya hivyo basi, wenzetu walibeba jukumu watakuwa na kazi nyepesi katika utendaji wao wa kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba kubeba karibu kila kitu na kujibu hoja nyingi, napenda nami nitoe mchango wangu katika hotuba husika japo kwa uchache.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja sana tufanye sensa ya kujua wageni wangapi wapo nchini pamoja na shughuli wanazofanya ili tuweze kuondoa wimbi la uzagaaji na uzururaji wao hapa nchini. Napendekeza pia Wizara kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji iweke utaratibu wa kuchunguza wawekezaji kule wanakotoka ili tuwafahamu vema ni watu wa aina gani na ukweli wana uwezo kiasi gani kabla ya kuwapa vibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza pia sasa Wizara kupitia Idara zake kufanya utafiti maalum kwa wageni wanaojipenyeza kwa kujifanya ni Watanzania na kupata manufaa ama stahiki wasizostahili huku wakinyonya Watanzania katika nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali iliyopo sasa suala la kilimo ni muhimu sana na kama hotuba ilivyoainisha, napendekeza tulitumie vizuri jeshi letu la Magereza na Mafunzo (Zanzibar) kwa kulipa teknolojia na pia tuwaongezee mtaji ili wafanye ufugaji na kilimo kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo ambalo linahitaji majibu kwa muda mrefu *dual citizenship* ifike wakati Serikali iliangalie kwa umakini sana hili jambo na lipate ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi katika idara zote katika Wizara, Magereza, Polisi na Uhamiaji wanastahili sasa wapate nyongeza za mishahara haswa ukizingatia ugumu na mazingira ya kazi wanazofanya. Lakini pia inaweza kuwa ni kichocheo cha ukiukwaji mkubwa wa maadili miongoni mwao. Lakini pia Wizara ijipange vema katika kusimamia nidhamu za miongoni mwao. Lakini pia Wizara ijipange vema katika kusimamia nidhamu za watumishi hawa maana maadili yameshuka sana kiasi cha kukosesha imani kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hii pamoja na maombi ya Magereza Lindi kuomba ofisi lakini imeonekana hawajapangiwa fungu la kujenga ofisi yao. Lakini pia Gereza la Kilwa Masoko ni dogo sana na linastahili lipatiwe fungu ili lipanuliwe au lijengwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi kirefu wananchi wa Kipatimu wameomba wajengewe Kituo cha Polisi lakini hawajapata kutekelezewa lakini ikumbukwe ni kero kubwa sana kwao maana lazima watembee kilomita 117 ili kupata huduma za kipolisi na wamekuwa wanaishi kama tupo katika karne ya ujima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa kila siku hatumalizi kuzungumzia suala la wakimbizi hapa nchini ila ni wapi penye machafuko sasa? Ikiwa nchi zao zimepata amani warejee makwao, athari za ukimbizi ni kubwa na mzigo kwa Taifa kwa ujumla. Hata hivyo watu hawa hawana hisani wala wema pale ambapo wakiwa makwao ama hata wakiwa hapa nchini. Mfano tumeona kwa Msumbiji, Afrika Kusini, Namibia, Zimbabwe na wengine wengi. Nimesikia mara kadhaa kuna majadiliano ya kutawanya wakimbizi katika mikoa ya Kusini. Sisi kama Wilaya ya Kilwa hatupo tayari maana tulishapokea wafugaji ambao ni wakimbizi pia. Hata hivyo itatuwia vigumu kuishi na watu ambao mila na desturi zao zinapingana na zetu. Kwa lugha rahisi naomba nisema hatutaki wakimbizi wa aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba nikushukuru kwa kunipokelea maoni yangu kwa kuamini kuwa yatafanyiwa kazi stahiki. Nakutakia kila la kheri, namuomba Mungu atulinde sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakupongeza Waziri na timu yako kwa hotuba nzuri naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana muwaongezee magari vituo ambavyo vina watu wengi na uhalifu na maeneo. Kituo cha Kawe, Wazo na Oysterbay. Vituo hivyo vinafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kujengwa Kituo cha Polisi pale Merilisita Kata ya Machame Kusini kwani ujambazi umezidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali iwafikirie polisi kuwaongezea mshahara. Kusema ukweli wanafanya kazi katika maeneo magumu sana. Hii itasaidia kupunguza rushwa.

Mheshsimiwa Spika, napenda nipongeze sana Idara ya Uhamiaji kwa kazi nzuri wanayofanya, wanafuata taratibu na huduma ni nzuri sana. Mheshimiwa Waziri nampongeza kipekee Bwana Shayo kwa kazi nzuri mno, anayeshughulikia *resident permits,* kila *department* akipelekwa anafanya kazi nzuri mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHEIR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya majukumu ya Wizara hii ni kulinda usalama wa raia na mali zao. Ili kutekeleza jukumu hili imeandaliwa Sera ya Taifa ya Ulinzi Shirikishi na Polisi Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera hii imewataka raia kushiriki katika ulinzi ndani ya maeneo yao wanayoishi. Yapo maeneo ambayo wananchi wameitikia wito huo na kuunda vikundi ili kushirikiana na polisi, waliopangiwa kazi Jimboni kwangu kwa ushirikiano wao mkubwa na vikundi vya ulinzi vilivyoanzishwa. Hata hivyo vikundi hivyo vya ulinzi vimeshindwa kufanyakazi ya ulinzi ipasavyo kutokana na polisi kutatimiza ahadi yao wakijitoa wakati wa uhamasishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati maofisa wa polisi walipopita jimboni kuhamasisha raia kuanzisha vikundi vya ulinzi waliahidi kutoa askari angalau watatu kushirikiana na raia nyakati za usiku wakifanya doria. Miongoni mwao watakuwamo angalau wawili wakiwa na silaha. Hata hivyo askari hao hawakupelekwa na askari mmoja aliyekuwa akishiriki hakuwa na silaha ya aina yoyote. Hali hii imepelekea baadhi ya washiriki kuuliwa na kupigwa na wahalifu na baadhi yao kuumizwa vibaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri awatake maofisa wa polisi kutekeleza ahadi yao ya kuwapatia askari wenye silaha washiriki wa ulinzi wa doria jimboni kwangu ili kupambana na wahalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kituo cha Polisi *(Police Post),* kwanza naipongeza Wizara kwa hatua ya kuongeza kujenga vituo vya polisi katika maeneo ambayo hayana vituo. Lakini ninamwomba Mheshimiwa Waziri aangalie maeneo ambayo vituo vipo lakini vimefungwa. Katika jimbo langu kulikuwa na kituo kimoja tu cha polisi cha Shaurimoyo. Lakini kwa masikitiko makubwa sana kituo hicho kimefungwa na kupelekea Jimbo kukosa kituo cha polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa eneo hilo wameomba mara kadhaa kituo hicho kirejeshwe lakini hakuna mafanikio. Kwa niaba ya wananchi wangu ninamuomba Mheshimiwa Waziri akifungue kituo hicho kidogo cha polisi cha Shaurimoyo Jimbo la Kwamtupura ili kuwaondolea usumbufu wananchi wa jimbo langu kutembea masafa marefu kufuata kituo cha polisi. Kukosekana kwa kituo cha polisi jimboni kunawapa fursa wahalifu wa kujiimarisha kwa kuongeza nguvu wakijua kwamba wataweza kujihami dhidi ya walinzi wa raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za makazi, uamuzi wa kuwajengea nyumba za kuishi maofisa wa polisi ni wa busara, kwa vile utawaondolea adha ya kuishi uraiani. Pamoja na uamuzi huo bado tatizo la nyumba linaendelea na askari wanaendelea kuishi uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa askari ambao hawajapata nyumba za polisi baadhi yao wanalipwa posho ingawa ni ndogo na haikidhi haja. Hata hivyo wapo askari ambao wanaishi katika nyumba za kupangisha na hawalipwi posho la nyumba. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri atafute ni askari wangapi ambao wanaishi uraiani na ambao hawalipwi posho ya nyumba ili walipwe stahili zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kwa walinzi wa sheria kukimbizana na raia wakidaiwa kodi. Mambo kama hayo yanatakiwa wawe nayo raia na siyo askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamisho ni jambo la kawaida kwa watumishi. Lakini kumhamisha mtumishi bila ya kumlipa stahili zake siyo jambo la kawaida na wala siyo jambo zuri kwa mtu yeyote yule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwahamisha askari bila ya kuwalipa stahili zao ni kuwapa usumbufu na kuwasababishia ugumu wa maisha. Kitendo cha kuwakopa askari kinawadhalilisha maofisa hao na kuitia aibu Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inafahamu kwamba askari hawawezi kudai haki zao kwa njia zinazotumiwa na raia kutokana na maadili ya kazi zao. Kwa hiyo, ninamuomba Mheshimiwa

Waziri achukue hatua za haraka kuwalipa askari wote haki zao ambapo wengine tayari wamestahamili kwa zaidi ya miaka minne tangu walipopewa uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ninaunga mkono hoja.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khamis Kagasheki, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *IGP,* Mkurugenzi wa Uhamiaji, Kamishna Mkuu wa Magereza na viongozi wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri ya Bajeti, kazi kubwa na nzuri wanayoifanya na mipango mizuri sana ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Mwanga tunafanya juhudi kubwa ya kujenga Vituo vya Polisi angalau kimoja katika Tarafa. Tumekamilisha ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Msangeni, Ngulu, Kisangara, Lang'ata na Kifaru. Tunalishukuru Jeshi la Polisi kwa msaada wa mabati na *cement* katika kujenga Vituo vya Lang'ata, Msangeni na Kisangara. Vituo hivyo (kuacha Kisangara) vyote vinafanya kazi na kutoa huduma vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo wananchi wa Tarafa ya Usangi wanajenga Kituo kizuri sana cha polisi, waliahidiwa mabati 100. Naomba kupitia kwako nimwombe Mheshimiwa Waziri awapatie wananchi wa Usangi bati hizo ili wakamilishe ujenzi wa Kituo hicho cha Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzipongeza hotuba zilizotolewa na Waziri wa Mambo ya Ndani, Kamati ya Ulinzi na Usalama pamoja na ile ya Kambi ya Upinzani. Yote ni maoni, mawazo, ushauri yaliyotolewa kwa namna ya mtazamo kwa kila kambi. Tunaitaka Serikali isiibeze hotuba iliyotolewa na Kambi ya Upinzani kwani kwa yale mazuri yenye manufaa kwa Taifa letu yanaweza yakachukuliwa yakafanyiwa kazi na pengine yakaweza kuleta mabadiliko au unafuu fulani katika kuboresha Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania iliridhia mfumo wa vyama vingi na mnamo mwaka 1992 vyama vingi vilianzishwa. Kuanzishwa kwa vyama hivi inamaanisha tuliridhia uwepo wa sera mbadala, mawazo mbadala na kwamba kwa chama kilichoko madarakani hakiwezi kujikosoa, chama mbadala ndiyo kioo cha Chama Tawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini sasa tunaogopa kivuli chetu? Watanzania walioanzisha na kujiunga na vyama vya upinzani ni Watanzania halali ambao miongoni mwao walitoka katika Chama Tawala. Sasa vyama vya upinzani tunafikiri vingeundwa na watu gani? Ni kwa nini mtu anapokuwa Chama cha Upinzani awe ni adui, adhalilishwe, asiheshimiwe na viongozi wake wasiheshimiwe? Tunamtaka Waziri kwenye majumuisho yake atoe tamko ama kufuta usajili kwa Vyama vya Upinzani au kufutwa kabisa kwa mfumo wa vyama vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama Tawala au Serikali ya CCM imekuwa ikilitumia Jeshi la Polisi ili kufanikisha malengo yake ya kisiasa. Imejionesha wazi wakati wa chaguzi zilizopita jinsi Jeshi hili lilivyotumika kuwatisha watu kwa kuwapiga mabomu na hata risasi za moto ili mradi tu CCM ishinde.

Mheshimiwa Sspika, wakati mwingine raia wanapojichukulia sheria mkononi ni kutokana na vitendo vya polisi vya kikatili. Polisi wamekuwa wakidai rushwa kwa wananchi na hata wakati mwingine kutumia vitisho ili wapatiwe rushwa hizo. Matukio ya mauaji ya kikatili kwa raia wema sehemu za migodi kwa mfano mgodi wa *North Mara,* Mwadui wananchi wameuawa wakiwa katika harakati za kujitafutia riziki ni ushahidi tosha wa ukatili huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Temeke kumejitokeza mtindo wa polisi hasa wa Kituo cha Chang'ombe kupiga risasi raia wasio na hatia kwa kisingizio cha kufanya doria. Mtoto Juma Hamza alipigwa risasi na polisi, mtoto huyu anaishi Keko Mwanga. Je, polisi huyu alichukuliwa hatua gani? Kitendo hiki kimempatia mateso makubwa mtoto huyu hadi kupelekea kulazwa Muhimbili na kufanyiwa upasuaji mkubwa mara mbili ambapo kidonda kilikuwa

kikimsumbua sana japokuwa naendelea vizuri, tunamtaka Waziri aeleze ni hatua gani huyu polisi amechukuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwingine ni kijana Hamidu Abdallah mwendesha pikipiki eneo la Mwembeyanga Temeke alipigwa risasi ya kiuno mchana eti tu polisi walikuwa wapo doria, kijana bado risasi ipo mwilini, hivi sasa yupo nyumbani kwake Tandika mtaa wa Matumbi baada ya kutoka hospitali na polisi waligundua kuwa hakuwa mlengwa bali ni bahati mbaya. Sasa kwa nini asihudumiwe? Hao polisi wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, polisi wetu wataishi katika jamii gani baada ya kustaafu kazi? Ni nani atakayewapokea ikiwa wanatengeneza mazingira hasi kana kwamba wataishi kambini milele?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamtaka Waziri ama Serikali isikilize kilio cha Watanzania ifanyie kazi maoni yanayotolewa na Wabunge kwani ndio wawakilishi wa Watanzania. Mungu Ibariki Tanzania na watu wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ubungo hususan maeneo ya pembezoni mwa Kata za Kimara, Mbezi, Kibamba, Kwembe na Msigani yanakabiliwa na vitendo vya uhalifu. Kituo cha Mbezi kwa Yusuph ambacho kina hadhi ya Kiwilaya ya Kipolisi chini ya *OCD* wa Kimara kinazidiwa uwezo na hakina nafasi ya kutosha ya kuhudumia wananchi ipasavyo. Pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha tuliambatana kwa ajili ya *harambee* ya kuchangia Kituo cha Polisi Mavurunza, nashukuru kwa jitihada hizo. Hata hivyo, inaeleweka kwamba maeneo hayo ya makazi ya watu yanapanuka kwa kiwango kikubwa sana. Hivyo naomba kauli ya Serikali kuhusu mpango wa ujenzi wa kituo kikubwa cha Wilaya kwa ajili ya kuongeza kwa haraka ulinzi na usalama katika maeneo hayo. Mpango huu uendane na mpango wa Jiji na Manispaa *(master plan).* Mpango huu uambatane na ujenzi wa nyumba za askari na kutoa vifaa vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa tayari matangazo yameanza kutolewa kuwa vitambulisho hivyo vitatumika kama leseni chini ya mfumo wa *smart card.* Kwa kuwa Wizara imeongeza muda wa kutoa leseni mpya mpaka Disemba ni kwa nini isiunganishe mifumo hii miwili ili kupunguza gharama mara mbili kwa madereva.

Aidha, Wakala wa Usajili na Udhamini *(RITA)* nao umekuwa ukiainisha mfumo wa uwekaji kumbukumbu ambao unaweza kupunguza gharama na kuwezesha Watanzania wazawa kuwa na vitambulisho kuanzia mapema utotoni. Kwa upande mwingine, Tume ya Uchaguzi *(NEC)* imeeleza kusudio la kuanza mchakato wa kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura (DKWK), wakati ambapo *NIDA* nayo inatangaza kwamba Vitambulisho vya Taifa vitatumika kupigia kura. Ni muhimu ili kuepusha Taifa kuingia gharama mara mbili, maandalizi ya kuunganisha mifumo hii ni vizuri yakawa katika mwaka huu wa fedha. Aidha, Serikali ieleze inachukua hatua gani kuwasiliana na Manispaa ya Kinondoni ili kuweza kupata kiwanja kwa ajili ya kujenga ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho *(NIDA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya Mambo ya Ndani itoe ufafanuzi kuhusu malalamiko na tuhuma mbalimbali zinazoelekezwa kwa vyombo na taasisi zake. Mathalani, zipo tuhuma kwamba waliokuwa askari polisi ambapo walihukumiwa kwa kumuuwa Imram Kombe (aliyekuwa Afisa Mwandamizi wa Usalama wa Taifa) kwamba wameondolewa katika Gereza la Maweni Tanga bila utaratibu kufuatwa na kwamba zipo tuhuma kwamba wameachiwa huru. Jeshi la Magereza lieleze kama taarifa hizi ni za kweli na hatua gani zimechukuliwa kufuatia taarifa hizo.

Pia askari waliohusika na *operation* ya Comoro wana malalamiko kuwa hawajapatiwa kifuta jasho au pongezi kama ilivyokuwa kwa wanajeshi (JWTZ) kutokana na fungu kutoka katika Serikali ya nchi hiyo. Serikali itoe kauli kuhusu nini stahili za askari wote waliohusika na *operation* hiyo. Aidha, nielezwe matokeo ya uchunguzi wa jeraha la mwanafunzi wa shule ya sekondari

Mbezi ambaye alijieleza kuwa alipigwa risasi na polisi wakati wanafunzi hao walipotaka kuwekewa tuta katika barabara ya Morogoro mwaka huu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali mambo yafuatayo ili kuboresha huduma ya Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba askari wa Uhamiaji wawe wanapewa *radio call* kama wanavyopewa polisi na magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wa Uhamiaji wadumishe utaratibu wa kuvaa sare za kazi daima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wa chini hasa Dar es Salaam wawe na mabasi ya kuwapelekea kazini na kuwarudisha nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ghala la kutunza kumbukumbu za uhamiaji huko Kijichi Dar es Salaam. Napenda kuikumbusha Serikali kulitunza ghala la uhamiaji kwani ndilo linalotunza kumbukumbu za uhamiaji tena likarabatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawakala wa kutoa hati za kusafiria na cheti cha kuzaliwa. Napenda kutoa ushauri kwa Serikali kuacha utaratibu wa kuwa na mawakala wa kutoa hati za kusafiria kwani mwanzo wa kutoa hati za kughushi, kazi ya kutoa hati hizi ziwe zinatolewa na Idara ya Uhamiaji peke yake pamoja na vyeti vya kuzaliwa. Imejitokeza wageni kupata vyeti vya kuzaliwa wakati sio raia wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vituo vya polisi vilivyopo mipakani bado kuna uingiaji wa wageni majambazi kwenye njia za panya.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekwaji wa magari ya abiria, ni ukweli bado kuna matatizo ya majambazi kuteka mabasi ya abiria hasa kwenye misitu yenye umbali mkubwa usio na makazi ya watu hivyo napenda kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwe na *Antirobary patrol* kwa kila mkoa ili kufanya doria ya muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kutoa askari wa kusindikiza mabasi hasa maeneo yenye msitu na umbali toka kwenye makazi ya watu kwa tahadhari ya kusaidia unapotokea utekwaji wa abiria na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu polisi jamii, ninaunga mkono mpango wa polisi jamii kwani wananchi ndio wanaowajua wageni ambao wanahisia za ujambazi ni vema askari kushirikiana na raia lakini wanapopewa taarifa ya ujambazi mahali wasitoe siri ya yule raia mwema aliyetoa taarifa. Hii itawatia moyo wananchi kutoa taarifa pia Serikali kutoa zawadi kwa askari aliyefanikisha zoezi zito la kuwakamata majambazi pamoja na raia aliyetoa taarifa hata kwa siri.

Mheshimiwa Naibu Spika, magari ya Zimamoto, napenda kuikumbusha Serikali kuwa ni vema kuwa na magari ya Zimamoto kwa kila wilaya. Hii itasaidia pale panapotokea tatizo la nyumba au gari kuwaka moto basi unazimwa haraka kuokoa maisha ya raia na mali zao mfano gari la mafuta ya petroli liliwaka Manyoni watu walioenda kuiba walikufa sana na askari sita waliokwenda kujitahidi kuzuia watu walikufa na gari hili liliwaka usiku kucha bila msaada wa Zimamoto. Hivyo ninaomba Wilaya ya Manyoni na Wilaya ya Iramba ipate magari ya Zimamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninamalizia kwa kuunga mkono hoja hii nikitegemea Waziri na Naibu ataithamini michango yangu kwa kuitolea ufafanuzi wakati wakijibu hoja za Wabunge.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi naomba kuchangia kwa kukumbusha kwa maandishi kuhusu kufanya ziara Mkoani Kigoma hususani Jimbo la Kasulu Mjini, Wilayani Kasulu ili uweze kushuhudia na kusikia changamoto walizonazo askari wetu lakini pia usikilize matatizo au kero mbalimbali za wananchi zinazotokana na Majeshi ya Polisi na Uhamiaji Wilayani Kasulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wake ni kuwa siku zote fimbo iliyo mbali haiui nyoka. Ninaamini ukitimiza ahadi yako ya kuja Kasulu kama tulivyokwishazungumza na ukaahidi kuwa baada ya Bunge utakuja Mkoani Kigoma hususani Kasulu utaweza kuyajua mengi na hivyo kuweza kuona ni hatua gani uchukue ili kumaliza au kutatua matatizo. Naomba unisaidie kuelewa ni tarehe gani utakuja Kasulu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, nikupongeze wewe binafsi kwa kuongoza mjadala huu kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao katika masuala mbalimbali kuhusu Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, niishukuru familia yangu kwa kwa kunipa moyo katika majukumu yangu ya kuwatumikia wananchi. Pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Bukoba Mjini kwa kuniamini na kunichagua kuwa mtumishi na mwakilishi wao katika Bunge hili Tukufu kwa kipindi kingine cha miaka hii mitano, nawashukuru kwa imani yao kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru Viongozi wote wa Chama na Serikali Mkoa wa Kagera hasa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Waheshimiwa Madiwani wa Kata zote 14 na Viti Maalum na viongozi wa CCM wa Jimbo la Bukoba Mjini kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuonyesha kwangu. Naomba nimshukuru kwa dhati Mzee Samuel Mtambara Rwangisa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Bukoba Mjini kwa miaka 20, Mwenyekiti na Meya wa Bukoba Mjini kwa miaka 23. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Wabunge wote wa Viti Maalum, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Bernadetha K. Mushashu na Mheshimiwa Conchesta L. Rwamlaza kwa ushirikiano. Napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete kwa kuniamini na kuniteua kwa mara ya pili kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, namhakikishia kwamba sitamuangusha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichukue nafasi hii kujibu baadhi ya hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala wa hotuba hii. Hata hivyo, hoja nyingi hasa zile za kisera zitatolewa maelezo na mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba iliyotolewa au michango mingi iliyotolewa na napenda nitazame baadhi ya mambo ambayo yameibuliwa katika hotuba ya ndugu zetu wa Kambi Rasmi ya Upinzani ndani ya Bunge na kwa kweli niseme kwamba kwa *thrust* yake ile hotuba ina lugha ambayo kidogo ni kali sana lakini tunasema katika demokrasia basi watu wanaweza kuzungumza lakini naweza kusema kwamba taarifa nyingi ambazo zimo katika hotuba hii ambayo inaweka msimamo wa ndugu zetu wa Upinzani si sahihi kama nitakavyoeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi mkubwa wa hotuba hii ni kuvunja amani ya nchi na kuvuruga amani kwa kutumia falsafa isiyo sahihi. Mara kadhaa katika hotuba hii ambayo ilitolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani ndani ya Bunge, wamekuwa wanatumia jina la Dkt. Martin Luther King na ukitazama ukurasa wa tatu wa hotuba yao kuna mahali ambapo wamemnukuu lakini niseme kwamba Dkt. Martin Luther King nafikiri kule aliko akitazama jinsi anavyonukuliwa hapa nadhani kama wanavyosema, *he may be turning in his dream.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya ndugu zetu wa Upinzani ukitazama ukurasa wa tatu wanamnukuu Dkt. Martin Luther King kuwa alisema kwamba, *peace is not the absence of war* lakini msingi wa harakati zake ulikuwa *we call for the change through non violence,* huo ndio ulikuwa msimamo wake na nadhani ni vizuri kum-*quote* mtu huyo katika *context* yake na si vinginevyo. Hakuna katika hotuba za Dkt. King wala hakuna katika maandishi ya Dkt. King ambapo alizungumzia kwamba anataka pawepo na *violence* katika *movement* yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nilieleze pia Bunge lako Tukufu kuwa Dkt. King wakati watu wengi Ulimwenguni walipokuwa wanamwambia kwamba a-*lead movement* yake na aseme kwamba alikuwa ni *Human Rights Activist* au alikuwa ana-*fight for the Human Rights* alisema, *no, I am not fighting for the Human Rights but I am fighting for the Civil Rights* na cheo alichokuwa nacho aliitwa *a Civil Rights Leader not a Human Rights Leader* na hii imo katika vitabu, mnaweza mkaangalia mtaikuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kikubwa tena katika hotuba ya Upinzani ukurasa wa kwanza, kweli tunaambiwa kwa kauli ambayo nanukuu inasema, ni kheri ya vita. Sasa mimi nashangaa kwa sababu unaposema kwamba unataka vita ili uweze kuleta mageuzi ama ulete mabadiliko sidhani kama hiyo inam-*reflect* Dkt. Martin Luther King na sidhani kama hicho ni kitu sahihi kwani Dkt. Martin Luther King aliipenda sana America. Naomba nitoe mfano na naomba hili nilielezee kwa umakini kwa sababu ni Kiongozi ambaye Kambi ya Upinzani imemnukuu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Martin Luther King mwaka 1963 tarehe 28 August alipotoa hotuba yake, *the famous speech* ambayo ilikuwa inasema *'I have a dream'* kwa wale ambao wamesoma, wamemfuatilia Dkt. Martin Luther King alipokuwa anazungumzia kwamba alikuwa na *dream,* hakuzungumzia kwamba alikuwa na *dream* ambayo ilikuwa ni tofauti na America na alisema kwa maneno yake kwamba, *my dream is rooted in the American dream*. Kwa maana kwamba alikuwa na uzalendo ingawaje alipoitoa ile *speech* mwaka 1963 Dkt. Martin Luther King alikuwa hawezi kupiga kura *United States* kwa sababu *the Blacks* walikuwa hawawezi kupiga kura. Kitu kilichotokea ni kwamba alikuwa na uzalendo wa nchi yake na yeye mwenyewe alisema kwamba alikuwa na *dream* kuona kwamba America itakuwa *transform through non violence* na watapata yale ambayo wanayataka siyo katika lugha ambazo tunazitumia na ndiyo maana unaona kwamba *from the speech* yake ya 1963 unaona sasa *United States has a President who is an African America*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *speech* ya ndugu zetu wa Upinzani nimeisoma sana, wamem-*quote* Fredrick Deogratius na amekuwa *quoted* katika ukurasa wa sita wa hotuba hii. Ukurasa wa sita mwisho kabisa wanam-*quote* kwa kusema Deogratius alisema, *he is a lover of his country who rebukes rather justify its sins*. Natafsiri kwamba ni mpenzi yule anayekemea madhambi katika nchi yake na si vinginevyo. Hii nakubali, lakini Fredrick Deogratius alikuwa ni *Black American as well* lakini tunapowa-*quote* viongozi hawa ni vizuri tuwatazame *in totality* tusichukue sehemu tukaacha sehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nataka niseme kwamba Fredrick Deogratius huyo ambaye mnam-*quote* katika kitabu cha Upinzani, alisema kwamba na ninam-*quote* yeye, *a little learning indeed may be dangerous.* Sasa hiyo unaweza ukaipa tafsiri unayotaka kuweka mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Fredrick Deogratius huyohuyo ambaye anakuwa *quoted* na ndugu zetu wa Upinzani, wakati alipokuwa akihamasisha watu wake alisema kwamba, kwa sababu alikuwa anajua kuna *limits* na lazima kuheshima Mamlaka iliyo madarakani, Dkt. Martin Luther King alifanya hivyo, Fredrick Deogratius alifanya hivyo na nitam-*quote* katika maneno yake wakati anawaambia watu wake alisema waende katika taratibu ambazo zitawafikisha katika malengo na si vinginevyo. Alisema, *when men sow the wind* yaani unapopandikiza upepo *it is rational to expect that they will reap with wind*. Kwa maana nyingine wewe kama utapandikiza upepo na anawaambia watu kwamba matokeo yake ujue kabisa unaweza ukaleta gharika kutokana na upepo ambao unapandikiza. Kwa maana nyingine nasema kwamba ndugu zetu

twende sawasawa kuliko kuwa-*insult* na kujaribu kuwafanya Watanzania wawe *liberials* sidhani kama hiyo ni *philosophy* ambayo iko sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yoyote *by definition, authority,* unapozungumzia *state power* utake usitake unazungumzia mabavu. Hii haiko *different with the United States*, haiko *different with* German wala haiko *different with United Kingdom*. Serikali ni chombo cha mabavu na ndiyo maana wanasema kwamba chenyewe kinakuwa *regulated* na Sheria lakini pia iko pale ku-*enforce* Sheria. Hapa kuna *aspects* mbili yaani *regulated* na Sheria lakini pia yenyewe ina *enforce* Sheria. Sasa tatizo ambalo tunalipata, ndugu zetu wa Upinzani katika hotuba yao ambayo wameitoa na wana haki kabisa kutoa maneno ambayo wameyatoa lakini nadhani kwamba hatuwezi tukapingana ama tukaondokana na utashi wa kusema kwamba Sheria lazima zifuatwe. Nchi isiyokuwa na Sheria haipo na nchi ambayo haiwezi ku-*enforce* Sheria basi hiyo siyo nchi kwa sababu *it is not supposed to be there. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa nane, Wapinzani wanasema, Majeshi ya nchi yoyote duniani hayawezi kushindana na haki. Hili liko hapa kwani wanasema Majeshi yote duniani, katika *statement* wanasema hayawezi kupingana na ukweli na yakashinda. Wanasema Tanzania sasa Majeshi yote hayawezi kama wanavyosema, kushindana na haki lakini Tanzania haina Serikali ya Kijeshi, Tanzania kama kungekuwa na Serikali ya Kijeshi sidhani kama sisi tungekuwepo hapa, *we couldn't have been here!* Tumekuja *through a democratic process.* Sasa tunapozungumza haya mambo na mmetoa mifano na ndiyo nasema kwamba mifano iliyotolewa isipotoshe wananchi wa Tanzania bali ilenge mahali ambapo pako *correct*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba pia mmetoa mifano kuhusu mambo ambayo yametokea na *changes* zilizotokea. Mmezungumzia Afrika ya Kusini, mimi sijui Afrika ya Kusini inayozungumzwa ni ipi? Kwa sababu kama mnazungumzia Afrika ya Kusini ambayo iliitoa Serikali ya *Apartheid*, *the Legal Regime of Apartheid* ikaleta *Regime* ambayo wanayo sasa hivi, Tanzania ili-*participate very fully in that process*, *we participated very fully*. Wanapozungumzia Msumbiji sijui wanazungumzia Msumbiji gani kwa sababu uhuru na *struggle* ya Msumbiji tume-*participate fully as Tanzania* na ninaposema kwamba tume-*participate fully as Tanzania it means me, you and everyone else* kama Tanzania tume-*participate* katika uhuru wa watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia unapozungumzia Namibia *is the same thing* na unapozungumzia Zimbabwe *the same thing.* Sasa mimi nashindwa ku-*differentiate* na kujua ni kipi hapa kinachozungumzwa kwa sababu mchango wa Tanzania kama nchi na kama watu, hapa ndiyo ilikuwa *head quarters* ya ukombozi katika Bara la Afrika. Kwa hiyo, huwezi uka-*separate* Tanzania ukasema kwamba Tanzania ijifunze *from* wale waliokuwa wanajifunza kutoka kwetu na tulikuwa tunawasaidia hata kuwasemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumzia suala la Kenya, Kenya *is different* na ninafikiri unazungumzia vita ya Maumau. *Again* sisi tulikuwa na bahati kwamba nyote mnamtambua Marehemu Baba wa Taifa ali-*lead a process* iliyotupeleka katika kupata uhuru bila ku-*shade any blood*, Uganda walikuwa na matatizo ya Kabaka and *the Kingdom of Buganda*, kwa hiyo, hayo ndiyo matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naizungumzia hii mifano ambayo mme-*quote* humu, mmezungumzia Sudan ya Kusini. Sudan ya Kusini, *the differences* ziko *clear* na hazi-*apply* hapa Tanzania. Unazungumzia *North* ambayo ni Waarabu na Waislamu na unazungumzia *South* ambayo ni Waafrika na ni Wakrisho. *They had a long war* wakafikia mahali ikaonekana kwamba *of course* walikuwa na *referendum* na ndiyo ambayo imefanyika *recently* na *only* juzi wamekuwa-*adapted as a member* wa *AU* na *member wa United Nations.* Sasa ndiyo nasema vitu hivi tusipotoshe Watanzania, tuweke mifano ambayo iko *relevant*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wamezungumzia kuhusu nchi ya Misri. Misri tatizo ni Hussein Mubarak, wanasema alikaa katika madaraka zaidi ya miaka 32 hivyo walichoka. Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete amekaa miaka mingapi? *Legality is known* baada ya miaka mitano inayokuja atatoka kwenye madaraka tutakuwa na uchaguzi tena *and everybody else* atashiriki katika uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapozungumzia Tunisia kama mfano wao, *the same thing!* Yule kiongozi amekaa katika madaraka *more that 23 years,* wamechoka, wanataka aondoke, *the same thing!* Yemen miaka zaidi ya 20, Libya amekaa zaidi ya miaka 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapa kuna *iron*, Kambi ya Upinzani walimuuliza Waziri Mkuu hapa katika maswali kwa Waziri Mkuu, wakataka kujua kwa nini Tanzania imemtupa mkono Gaddafi? Liliulizwa swali na bado kuna swali likatoka *on the floor* kumuuliza Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, kwa nini Tanzania imeshiriki na kukubali *Resolution* ya *United Nations ya No-Fly Zone above Libya*? Sasa watu haohao wanasema kwamba *it is right* kwamba Gaddafi amepata misukosuko na amekuwa *overthrown,* hizi ni *contradictions* ndugu zangu ambazo sidhani kama zinatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumzia Bahrain, Bahrain ni nchi ya Kifalme lakini Tanzania siyo nchi ya Kifalme. Sasa nasema tumeleta mifano ndani ya Bunge ambayo ukiitazama kwa ukweli na kwa picha iliyokuwa kubwa haina uhusiano hata kidogo na nadhani haitakuwa vizuri kuwapotosha Watanzania kwa kusema hivyo ndivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa nne ambapo Mheshimiwa wa Kambi ya Upinzani amekuja hapa akazungumza ni juu ya taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na anasema hii Tume inaonyesha mengi yaliyopokelewa, hilo halihusu, Polisi kubambikiza raia kesi, mahabusu na Mahakama na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *report* ambayo wanaizungumzia ni *report* ya mwaka 2003, leo ni mwaka 2011 hivi ni vitu viwili tofauti. Ungekuwa unatuletea *information* hapa ambayo ni *recent report* ambayo imetoka mwaka jana na inaeleza hali halisi katika Tanzania, hiyo tungeweza ku-*debate* lakini unaleta *report* ambayo imetoka zaidi ya miaka saba au nane iliyopita, sidhani kama *that has any relevance* na wakati ule Mheshimiwa Jakaya Kikwete *was not even in power.* Kwa hiyo, nadhani tusijaribu kupotosha na kujaribu kuweka mambo mengine isivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii imetukana sana Askari wetu na sina haja ya kurudia lakini kila mtu ambaye amepata hotuba yao na akaisoma nadhani Askari *particularly* pale walipo watakuwa katika huzuni kubwa na watakuwa katika masikitiko makubwa. Maana imewatukana sana kwamba ni wala rushwa wakubwa katika Tanzania, ni wakatili wakubwa katika Tanzania, wauaji wakubwa katika Tanzania, watovu wa nidhamu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, *sincerely* nataka niwakumbushe kwamba mwezi Mei wakati kuna matatizo katika mgodi wa Nyamongo Tarime, Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambaye ametoa hotuba hii alikwenda kule na alipokwenda alisema anakwenda kutazama hali halisi na kadhalika lakini alipokwenda Sirali, Wilaya ya Tarime katika mpaka wa Kenya na Tanzania alifukuzwa na watu na alikimbilia kituo cha Polisi na Polisi ndiyo walimtengenezea njia ya kumtoa pale wakati Mheshimiwa Tundu Lissu anaingia kule huyu bwana alikuwa anakimbia, anatoka na ushahidi upo. Sasa unapowatukana Polisi na wakati ukiwa katika matatizo unakimbilia katika Kituo cha Polisi, nadhani kwa kweli hapo Polisi hatuwatendei haki hata kidogo. Mimi nadhani kwamba tusitukane chombo ambacho kinaleta amani katika nchi yetu na kinasimamia amani katika nchi sidhani kama ni chombo ambacho kinatendewa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 13 wa hotuba ya ndugu zetu wa Upinzani, wana uchungu sana kwamba Jeshi la Polisi, Polisi wa Kawaida wanapewa shilingi 5,000/= na wanasema inawauma sana na wanasema hii isifanyike kwa hawa Askari kwa sababu ni kinyume na hizi shilingi 5,000/= ni mchango ambao wanatoa kwa mazishi yao wenyewe Askari na familia zao. Wanasema kwamba kama Serikali haikuchukua hatua zozote za kuwarudishia Askari hawa shilingi elfu tano (5000/=) kwa hili peke yake wataandamana nchi nzima. Sasa mimi niombe tu kwamba nia ya kuandamana si mbaya na hapa kuonesha mahaba na mapenzi makubwa kwa Askari wetu pia si mbaya, baada ya kuwatukana kwamba mambo yao ni mabaya, wala rushwa lakini hapa tunajenga hoja juu ya ukweli ni upi?

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe ndugu zangu kabla hatujaja hapa, *to make firm and clear understanding position*, ni muhimu sana tufanye *research* kidogo. Suala la Askari anapofariki, au mkewe, wanawe na hata wakwe zake, gharama hutolewa na Serikali. *That has been the position and that is still the position* na si vinginevyo. Serikali inatoa jeneza, sanda na inasafirisha maiti mpaka kule yule Askari anakotoka na hiyo *it has nothing to do,* Askari hawatoi *contribution* yoyote. Jambo lililojitokeza ni kwamba baada ya hapo wanapopeleka maiti, Askari wakaona kwamba pesa hazitoshi, *of course* unakuwa na msiba, watu wanakaa, wanakunywa, wanakula, mnakuwa na matanga, wakaamua kwamba lingekuwa jambo jema wakawa na mfuko na mfuko huo ni wa hiari, hakuna mahali ambapo wanasema kwamba ni wa lazima. Wale Askari wanaotaka watatoa mchango wao na wasiotaka wasitoe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukitazama *arithmetically* ndiyo nasema fanyeni *research* kidogo, wale Askari ambao wamekuwa wanapata misiba wakitumia mfuko huu kila mmoja amekuwa anapata shilingi milioni moja (1,000,000/=) sasa ukitazama *five thousand shillings*, shilingi elfu tano anazotoa uka-*multiply* mara miezi kumi na mbili (12) yaani kwa mwaka inakuja *sixty thousand* (60,000/=) lakini anapopata msiba na wengine *of course* wanakuwa hawapati misiba, anachangiwa shilingi milioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme kwamba hili ndugu zangu wa Upinzani kabla hamjaenda katika maandamano kama mnavyosema, basi ningewaomba kidogo mfanye *research* kwa sababu si kweli kwamba Serikali inawatoza wale Askari shilingi elfu tano kwa sababu ya mazishi yao. Mimi nasema kwamba ni kitu ambacho hakiingii akilini, ni kitu ambacho hakipo *and it is highly immoral* na msitegemee kwamba Serikali hii inaweza ikafanya kitu cha namna hiyo. Hilo ni jambo ambalo mngelitazama vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 14 katika kitabu hiki Magereza wanatuhumiwa na ni tuhuma nzito kidogo au nisiseme kidogo, ni kubwa sana maana yake tuhuma yenyewe inawaita Askari wa Magereza ni mafisadi. Kitabu kinasema kwamba mfungwa chakula chake ni shilingi 650/= kwa kila siku. Kambi Rasmi ya Upinzani ndani ya Bunge inasema kwamba ni shilingi 2,420/=. Walivyoandika hapa ni kwamba ilikuwa imeidhinishwa na Serikali. Ni kweli hatujakataa iliidhinishwa na Serikali, lakini mngekwenda *a step further,* mngezungumza na *Controller and Auditor General* wa Serikali akawapa maelezo zaidi. Hizi pesa ziliidhinishwa lakini si pesa zilizokwenda Magereza na kwa maana hiyo ilikuwa ni ufinyu wa bajeti, zilikuwa zimeidhinishwa lakini sizo ambazo walipata. Kwa maana hiyo unapokwenda moja kwa moja ukasema kwamba humo ndani ya Magereza hao Askari Magareza ni mafisadi na unatumia lugha ambayo ni nzito kusema kwamba wanakula pesa ambazo ni za Wafungwa, mimi nadhani kwa kweli *charges* nyingine tungekuwa tunakuwa *fair*. Watanzania wakisikia mambo kama haya sidhani kama yanatujengea umaarufu, ama yanatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine katika ukurasa wa 16 hapa wanasema kwamba Jeshi la Zima Moto kuna pesa zaidi ya shilingi bilioni moja (1,000,000,000/=) zimeliwa. *My God!* Sasa mimi nasema kabla hatujafanya *accusations*, kabla hatuja-*point a finger* kusema kwamba hili jambo limetokea ni vizuri tufanye *research* mpaka dakika ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya magari yalinunuliwa. Wakati Mkaguzi Mkuu anafanya yale mahojiano na kuweza kutazama vitabu, magari yalikuwa hayajaja, lakini tangu mwezi Marchi haya magari yamefika na yapo nchini. Kwa hiyo, sasa kuwatuhumu Jeshi la Magereza tukasema kwamba ni mafisadi na kama tulivyofanya na kwa wengine wa Jeshi la Polisi, mimi nadhani *it is very unfair and is totally caughtfull*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naona muda unakwenda na kwa sababu mambo yaliyojitokeza ni mengi sana ambayo tungependa kwa kweli tuyajibu kwa kina, mimi nafikiri mengine ni *intellectually engaging*, ni mazuri kwa sababu yanasaidia, lakini pia yako mengine haya ya kuyaweka sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika hoja ambazo zimetolewa kumekuwa kuna wimbi kubwa la wahamiaji haramu. Sasa hilo ni jambo ambalo ni kweli tumekubali na tunajaribu kuweka mikakati ya namna ambavyo tunaweza tukalitatua. Tatizo tulilonalo ambalo siwezi

nikaficha ingawa tunakabiliana na hali halisi, ni la vitendea kazi. Hili inabidi kwa kweli tujipange kwa sababu hatuna *excuse* na pia tunajaribu kuongea na majirani zetu ambako hawa watu wanapitia kuingia katika Taifa letu. Hata hivyo, sidhani kama ni kitu ambacho tunaweza kuwa *accused off* kama Serikali na kusema kwamba kinafanyika kwa nia mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limekuwa *raised* na ndugu zetu wa Upinzani linahusu uraia wa nchi mbili. Hili ni suala ambalo tumelizungumzia sana na tumelijibia sana hapa. Hatua za kwanza za haraka ambazo zinafanyika sasa hivi ambazo Mheshimiwa Waziri alikwishazitaja hapa Bungeni na mimi pia nimekwishazitaja ni azma ya Serikali kuona kwamba ifikapo mwanzo wa mwaka unaokuja tuwe tumekwishapitisha Sheria ya kuwa na kitu ambacho kinaitwa *Permanent Residence*. Hiyo itakuwa ni hatua ya kwanza, wakati mchakato mzima wa suala zima hili la *dual citizenship* ambalo ni la Muungano na hivyo hatuwezi kusema kwamba litaamuliwa na Tanzania Bara peke yake au Serikali ya Mapinduzi Zanzibar peke yake. Kama alivyosema Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa alipokuwa anatoa hotuba yake, liko katika mchakato na tutafika mahali tutakuwa na jibu lakini ili kuondosha ile adha tumeona kwamba twende na utaratibu wa kuwa na kitu ambacho kinaitwa *Permanent Residence*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mkakati wa kupunguza msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani. Hili ni jambo ambalo kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge linawauma na kuwakereketa, ndivyo lilivyo hata kwa sisi ndani ya Serikali. *Population* imekuwa ni kubwa, lakini pia uhalifu umekuwa ni mkubwa na umeongezeka. Hata hivyo, hiyo siyo sababu, ziko njia ambazo sasa tumeanza kuzitumia na tutaona kwamba zinatupa matunda kwa sababu kila mwaka idadi ya msongamano inakwenda ikipungua na katika mambo ambayo tumedhamiria kuyafanya ni kutumia sheria za Mabaraza ya Kata ambayo Waheshimiwa Wabunge nafikiri mngetusaidia sana huko katika Kata zetu kuona kwamba hili kwa kweli linafanyika kupitia Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la wahalifu kupewa adhabu zisizokuwa za kifungo. Hiyo inatazamwa, lakini pia na washtakiwa wenye makosa madogomadogo kupewa dhamana bila masharti magumu ili waondokane na ule msongamano wa kuwekwa katika Magereza. Lililo kubwa ni kutekeleza utaratibu unaoruhusiwa kisheria wa mahabusu kuachiliwa baada ya siku sitini (60) iwapo upelelezi utakuwa haujakamilika. Sasa hivi kumekuwa na tatizo ambapo unakuta mtu anawekwa ndani, upelelezi unafanywa, ushahidi unakuwa hautoshi na mtu anaendelea kuwa ndani. Hilo tumeliona na tunasema kwamba twende kwa mujibu wa sheria ikifika siku sitini (60), ushahidi haujakamilika basi itabidi yule mtu aachiliwe na endapo kutatokea ushahidi basi mtu atakuwepo, kesi itakuwa *resumed* tena na itaweza kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa Vitambulisho vya Taifa. Niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutaanza kutoa Vitambulisho vya Taifa mwisho wa mwaka huu wa 2011, lakini tutakwenda kwa awamu, hatuwezi kusema kwamba tutaanza kwa nchi nzima. Ifikapo mwaka 2014 kwa mpangilio tuliojiwekea Watanzania wote watakuwa wamepata Vitambulisho vya Taifa. Mamlaka itaanza ujenzi wa ofisi za Utambuzi na Usajili katika Wilaya za Tanzania Bara na Zanzibar mwanzoni mwa mwaka 2012 na mkakati ni mrefu kwani kuna *consultations* ambazo zitahusu vyombo mbalimbali, lakini pia kutazama sheria ambazo zimekuwepo kwa sasa hivi na mambo mengine ambayo yanahusu Taasisi mbalimbali na kadhalika. Kwa hiyo, niseme kwamba tunakwenda vizuri na hatua zitakwenda vizuri katika jambo hili na ni jambo ambalo limechukuwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa kwamba Serikali ifanye ulinzi shirikishi kama nguzo ya ulinzi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Balozi Khamis Suedi Kagasheki, kwa shule kubwa sana ambayo umetupatia. Tunakushukuru sana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Shamsi Vuai Nahodha ili aweze kuzipitia hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri karibu sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine, ninayo heshima kubwa kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili bajeti ya Wizara yangu. Napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza na maandishi. Nimefarijika sana na michango mizuri waliyoitoa. Ukiachia michango michache yenye vionjo na ukakasi wa ushabiki wa kisiasa, kwa jumla michango mingi ilikuwa na ushauri wa kujenga. Ninaithamini michango ya Waheshimiwa Wabunge na niwaahidi tu kwa niaba ya Viongozi wenzangu wa Wizara tutaifanyia kazi ili kuimarisha utendaji na majukumu tuliyokabidhiwa katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kuishukuru sana familia yangu, mama watoto, watoto wangu Ahmed Nahodha, Ayun Nahodha na Aiman Nahodha, kwa msaada mkubwa wanaoutoa kwangu licha ya umri wao mdogo. *(Makofi)*

Mwisho ingawa siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru sana Naibu Waziri, Kaka yangu, Mheshimiwa Balozi Khamis Suedi Kagasheki, kwa msaada mkubwa sana anaoutoa katika kuongoza Wizara hii. Namshukuru sana kwa busara zake, ushauri na ushirikiano wa hali ya juu sana anaonipatia katika kuongoza Wizara hii. Kwa kweli nimebahatika sana. Ninayo bahati kubwa sana ya kupata msaidizi wa aina yake. Ni mkweli, muwazi na mchapakazi na makini sana. Nitaendelea kuienzi hazina na bahati hii niliyojaliwa na Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Wizara yangu imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 214. Waheshimiwa Wabunge 162 wamechangia kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge 30 wamechangia kwa kuzungumza. Waheshimiwa Wabunge 22 walichangia masuala ya Wizara yangu kwa kupitia hotuba ya Serikali, Ofisi ya Waziri Mkuu; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na hotuba ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kutokana na ufinyu wa muda, sitaweza kujibu hoja zote badala yake nitatoa maelezo ya jumla katika maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia. Halikadhalika Wizara yangu itaandaa majibu ya hoja zilizotolewa na kuwekwa katika kitabu na kuyawasilisha hapa Bungeni kama ilivyo ada ya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Rose Sukum, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mheshimiwa Abuu Jumaa, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Charles Kitwanga, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza na Mheshimiwa Amina Abdallah Amour. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Lameck Airo, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Dkt. Seif Rashid, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Josephine Chagulla, Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Rachel Mashishanga na Mheshimiwa Martha Umbulla. *(Makofi)*

Wengine ni pamoja na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Maulida Komu, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Herbert Mtangi, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Abia Nyabakari, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza,

Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi na Mheshimiwa Juma Othman Ally. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Eng. Athuman Mfutakamba, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Alphaxad Kangi Lugola na Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir. *(Makofi)*

Wengine ni pamoja na Mheshimiwa Said Mtanda, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa David Mallole, Mheshimiwa Mch. Israel Natse, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Amina Mwidau, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Albert Ntabaliba, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Azza Hamad, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mheshimiwa Zaynabu Vullu, Mheshimiwa Shawana Bukheti Hassan, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Ali Kheir Khamis, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Philipa Mturano, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mheshimiwa Ally Mohamed, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Abdul Mteketa, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Gosbert Blades na Mheshimiwa Mariam Mfaki. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Omari Nundu, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Salome Mwambu, Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema, Mheshimiwa Rukia Ahmed, Mheshimiwa Chiku Abwao, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe na Mheshimiwa Rashid Ali Omar. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Regia Mtema, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Dkt. Stephen Kebwe, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Dkt. Benelith Mahenge, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Tundu Lissu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa Muhammed Seif Khatibu, Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Yussuph Haji Khamis, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa , Mheshimiwa Ali Kheri Khamis, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Faida Mohammed Bakari, Felix Mkosamali, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Chiku Abwao, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Said Mussa Zuberi, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mheshimiwa Highness Kiwia, Mheshimiwa Vicent Nyerere, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Joseph Selasini, Mheshimiwa Haji Kai, Mheshimiwa Philipa

Mturano, Mheshimiwa Jaji Frederick Werema na Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kuhusu Wizara yangu wakati wa hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Assumpter N. Mshama, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Catherine V. Magige, Mheshimiwa Profesa Peter Msolwa, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Clara Mwatuka, Mheshimiwa Amina A. Amour, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mheshimiwa Mchungaji Israel Yohana Natse, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Mohamed Habibu Mnyaa, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda na Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa na Mheshimiwa Diana Chilolo ambaye amechangia kwa kuzungumza. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwatambua wachangiaji sasa naomba kupitia hoja zilizojitokeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza, Serikali inaua wananchi lakini haichukui hatua za kisheria na kinidhamu dhidi ya Polisi wanaosababisha vifo hivyo. Hoja hii ilitolewa na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Godbless Lema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua sana thamani ya maisha ya mwanadamu. Vilevile Serikali hii inaheshimu sana haki za binadamu. Kwa kuwa Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kuwa kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata ulinzi wa maisha yake. Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa mnasaba huo, haina sababu na haiwezi kuwa na sera ya kuua raia wake. Hii ni shutuma kubwa na kejeli kubwa kwa Serikali na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo wameipa Mamlaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuongoza nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Tanzania wanaopoteza maisha yao kwa sababu zozote sisi Viongozi tuliopewa dhamana ya kuongoza tunasikitika sana na hatufurahi hata kidogo. Kwa mnasaba huo nawapa pole jamaa na ndugu wa marehemu waliopoteza ndugu zao. Wananchi wetu wanapopoteza maisha Serikali ya Awamu ya Nne kama ilivyokuwa kwa awamu zilizotangulia imekuwa ikichukua hatua pale Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola vinaposababisha vifo vya raia. Tumekuwa tukifanya hivyo siku zilizopita na tutaendelea kufanya hivyo kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wa vyombo vya dola wanaposababisha vifo, sisi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tunakusanya taarifa za kifo au vifo hivyo na kuzipeleka kwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai kama taratibu zinavyoeleza. Mkurugenzi anapopata taarifa hizo anazipitia na kutoa ushauri wa kisheria kwa kuangalia mazingira ya tukio linalohusika. Iwapo atadhihirika kuwa Askari au kikundi cha Askari wamefanya uzembe basi Askari hawa wanashtakiwa kwa mujibu wa sheria. Ndiyo maana Askari wafuatao wamechukuliwa hatua na nitawaeleza.

Moja, *ACP* Abdallah Zombe na washirika wake waliwapiga risasi wafanyabiashara, walishtakiwa Mahakamani. Kama wameachiwa huru sasa si suala na wala si makosa ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Chombo chenye mamlaka ndicho kilichoamua hivyo na ndio utawala wa sheria unaposema maamuzi ya Mahakama yanapaswa kuheshimiwa hata kama haturidhiki.

Pili, Askari Namba F. 5073 *PC* Tumaini Mweta wa Polisi Manyara alishtakiwa Mahakamani tarehe 1 Juni, 2006 kwa kusababisha kifo cha raia. Tatu, Askari Namba D. 7248 *SGT* Pius na

wenzake walifikishwa Mahakamani Mkoani Mara tarehe 19 Novemba, 2007 baada ya kumpiga raia. Nne, Askari Magereza namba A. 7267 *SGT* Ismail Kibira wa Magereza Mkoa wa Mara alishtakiwa Mahakamani kwa kosa la kuua bila kukusudia pale alipomfyatulia risasi mfungwa aliyekimbia jela na risasi hiyo ikampiga Ndugu Mwabia Zome ambaye alifariki dunia, Askari huyu ameshtakiwa. Tano, Askari wengine 10 walishtakiwa kati ya mwaka 2006 – 2011, sasa mnataka ushahidi gani juu ya dhamira na hatua ambazo zinachukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli sisi Waheshimiwa Wabunge tunawapenda sana wananchi wa Tanzania na mimi naamini hivyo, tuendelee kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuendelea kuheshimu na kutii sheria. Naomba nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Viongozi wengine tushirikiane katika kuifanya kazi hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli zipo tuhuma za kwamba Serikali hii haina haki, inanyanyasa wananchi, mimi nasema si kweli kwamba Serikali hii haina haki na inanyanyasa wananchi wake. Kuwepo kwa Vyama vya Siasa ikiwemo CHADEMA na kufanya kazi zake moja kwa moja kwa uhuru ni kielelezo dhabiti cha kuwepo kwa haki hiyo. Serikali hii pia inaheshimika duniani kwa kuheshimu haki za raia. Nasikitishwa sana ninaposikia mtu mzima na Kiongozi ambaye anatakiwa kuwa mfano katika jamii kutoa kauli za dharau na kejeli kiasi hiki. Kiongozi makini siku zote anapaswa kuchunga na kutumia ulimi wake vizuri na kupima athari za kauli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujasiri wa kusema lolote linalokuja mdomoni ni ujasiri wa kiwendawazimu. Zipo tuhuma za baadhi ya Askari kufanya vitendo hivi na vile. Hata hivyo, malalamiko ya namna hii katika siku za karibuni naamini yamepungua kutokana na Serikali kuchukua hatua kwa kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji wa kesi. Kwa mfano, zamani Askari wa Jeshi la Polisi walikuwa wanatuhumiwa kuwabambikia kesi wananchi, lakini kwa utaratibu ulivyo sasa ni kwamba, kazi ya upelelezi inafanywa na Jeshi la Polisi. Kazi ya kuendesha kesi inafanywa na Mkurugenzi wa Mashtaka wa Serikali. Basi kama uwezekano huo wa kubambikizia kesi upo bila shaka kesi hiyo ambayo mtu amebambikiziwa itakapofika kwa Mkurugenzi wa Mashtaka bila shaka haki itatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA wamesema wataendelea kufanya maandamano mpaka kieleweke, sina tatizo hata kidogo la kufanya maandamano. Tatizo langu tu ni kwamba, wafuate taratibu na sheria. Mimi Waziri mwenye dhamana nasema jambo hili likifanyika bila utaratibu ni jambo la hatari sana na Viongozi wa Kisiasa kama tunataka tuendelee kuheshimiwa na naamini tunaheshimiwa tukiambiwa jambo tuwe na ustaarabu wa kusikiliza hata kama jambo hilo linalosemwa hatulipendi au wanaotuambia hatuwapendi.

Kuna msemo mmoja wa Kiingereza naomba niuseme kama ulivyosemwa kwa lugha ya Kiingereza. "*The human mind is like a parachute it works better when it is open*". Akili ya mwanadamu ni kama mwamvuli wa kijeshi unafanya kazi unapokuwa wazi. Sasa mwanadamu ambaye hapokei mawazo chanya, mawazo ya watu wengine, hawezi kujifunza. Tujifunze kusikiliza mawazo tunayoyapenda na tusiyoyapenda. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mbunge mwingine alisema, nisiposema kama mtoto aliyepigwa risasi atatibiwa watafanya maandamano. Sasa sijui tunamtisha nani! Hakuna haja ya kutishana. Mimi najiuliza hivi maandamano tangu lini ikawa dawa ya kidonda. Hivi maandamano ni kama muarobaini unatibu kila maradhi. Kama jua kali maandamano, mvua kali maandamano, kidonda maandamano. Kama maandamano ni tiba ya kila kitu kama muarobaini ulivyo basi tuwape hatimiliki ya maandamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge aliyelisema jambo hili kama ana huruma ya dhati kwa yule mtoto ambaye anataabika, nadhani taarifa hii asingesubiri Bunge tangu tarehe 6 Juni, 2011 tulipofika hapa angeleta taarifa hii ningemwona ana huruma kweli kweli. Waswahili wanaita huruma hii, hii ni huruma ya mamba anang'ata na huku anajidai analia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine nchi yetu ina vyombo vya dola katili kama ilivyothibitishwa na haki za binadamu na utawala bora. Napenda kutoa maneno yafuatayo: Tuhuma hizi si za kweli. Jeshi la Polisi linafanya kazi zake kwa kutumia sheria na taratibu maalum na hata pale Jeshi la Polisi linapopaswa kutumia nguvu kidogo basi wanapaswa kufanya kazi hiyo kwa umahiri na umakini wa hali ya juu sana na ikitokea kwa bahati mbaya mwananchi akapoteza maisha au mwananchi akajeruhiwa, haimaliziki hivi hivi tu kama nilivyosema pale awali ni lazima hatua zinazostahiki zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine Serikali kutokuridhia mkataba wa Kimataifa dhidi ya utesaji na matendo au adhabu nyingine za kinyama na za kudhalilisha. Serikali haijawasilisha kweli mkataba huo hapa Bungeni ili uridhiwe. Kwa kuwa mkataba huu unakataza adhabu ya kunyonga kwa watuhumiwa wanapopatikana na hatia ya mauaji. Nyote mnaelewa nchi yetu bado inatekeleza adhabu hii hivyo si busara kuleta mkataba huu hapa Bungeni wakati bado tunatekeleza adhabu hiyo ya kunyonga. Kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Serikali itaendelea kukusanya maoni iwapo ama tuendelee na utaratibu huo ama adhabu ya kifo ifutwe. Hata pale itakapofutwa Serikali sasa inapaswa kubadilisha sera hiyo inayohusu adhabu ya kifo na baada ya hapo basi Serikali ya Jamhuri ya Muungano inaweza sasa kuleta mkataba huu Bungeni ili uridhiwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, Jeshi la Polisi linashika nafasi ya kwanza kwa rushwa kama ilivyoelezwa katika (Ripoti ya *East Africa Bribery Index* 2010). Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala hili la rushwa kama ambavyo rushwa ipo katika jamii yetu pia inawezekana sana wapo maana mimi kama Waziri mwenye dhamana siwezi kulinda na kutetea maovu, inawezekana sana katika Jeshi la Polisi wapo Askari wasiokuwa waadilifu, inawezekana sana. Lakini pia hatuwezi kulizungumza jambo hili jumla jumla tu kama Askari wote wa Polisi hawafai, hapana. Wako Askari wazuri wanatekeleza majukumu yao ipasavyo na kwa maana hiyo wale ambao hawatekelezi majukumu yao ipasavyo wanakumbatia rushwa wanapaswa na ni lazima tuwachukulie hatua kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa upo utaratibu unaoshughulikia Askari wanaotuhumiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa, upo. Askari yoyote atakayethibitika kuwa amepokea rushwa hushtakiwa Kijeshi na hatimaye kufukuzwa kazi. Jeshi la Polisi limekuwa likichukua hatua zifuatazo kwa kupambana na tatizo hilo.

Kwanza, kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya rushwa kupitia vyombo vya habari.

Pili, kushirikiana na wadau wengine kama TAKUKURU.

Tatu, kutoa vyeti na zawadi kwa askari wanaokataa kupokea rushwa. Tumekuwa tukifanya hivyo si mara moja, si mara mbili na tutaendelea kufanya hivyo.

Nne, kuanzishwa kwa Kamati za Maadili ndani ya Jeshi la Polisi ili kuwafuatilia askari wanaotuhumiwa na kuchukua hatua dhidi yao. Mwaka 2010 jumla ya askari 22 walifukuzwa kazi na kufikishwa Mahakamani kutokana na kujihusisha na vitendo vya rushwa. Lakini kwa bahati mbaya sana na hili Waheshimiwa Wabunge mstahimili tu, sitalisema kwa nia mbaya, pengine natoa siri; Wako Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa wakiniletea majina ya watu ambao tumewafukuza kazi kuwatetea tuwaachie. Katika mambo haya haya ambayo sasa tunalaumu kwamba hatuyapendi, rushwa tumekuwa tukifanya hivyo. Wapo! Sisi ni watu wazima, wale ambao wananiletea vikaratasi wanajijua. Sasa kama kweli tunachukia rushwa, naomba tusiwatetee hawa, tuwe na sababu za msingi za kuwatetea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho, tumeshauriwa kuharakisha utaratibu wa kuwa na uraia wa nchi mbili haraka iwezekanavyo. Serikali mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi zinalifuatilia jambo hilo. Kama nilivyojibu katika jibu langu la ufafanuzi wakati tulipokuwa tukipitisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ni kwamba hivi sasa tumepewa kazi ya kutayarisha waraka maalum kwa ajili ya kuwa na utaratibu wa kuwa na hati za kudumu. Ni matarajio yetu kwamba ifikapo mwezi Januari au Februari mwakani, Mwenyezi Mungu akipenda, waraka huu utakuwa tayari na tunategemea kwamba wale wakereketwa, wale ambao wamekuwa wakilitetea jambo hili na wale ambao

wamekuwa wakitaka kunufaika na jambo hili, tuna imani kubwa tukianza utaratibu wa kuwa na hati za kudumu, pengine kiu yao inaweza kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya hapo, kama baada ya kuwa na utaratibu wa kuwa na hati za kudumu, tukiona bado ipo haja sasa ya kuendelea kuwa na utaratibu wa kuwa na uraia wa nchi mbili, basi suala hilo litafuata baadaye. Lakini, ni matumaini yetu sisi kama Wizara kwa kiasi kikubwa sana hati za muda mrefu zinaweza zikasaidia sana kukata kiu hiyo kwa sababu wako Watanzania ambao wamekuwa wakisema wazi kuwa wao haja yao ni kuja tu kupata fursa za kukaa hapa kwa muda mrefu kuendelea kufanya shughuli mbalimbali za uwekezaji, lakini wasingependa kupoteza uraia wa nchi hizo walizonazo, nchi za ughaibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiachilia pengine zaidi ya hao, wapo wale ambao pengine wao wana matarajio ya kisiasa, maana utaratibu wa hati za kudumu utawawezesha watu ambao wana uraia wa nchi nyingine kupata fursa zote, isipokuwa fursa ya kuchaguliwa katika nafasi za kisiasa kwa maana kwamba hawataweza kugombea nafasi za Ubunge, hawataweza kugombea nafasi za Udiwani, hawataweza kugombania nafasi ya Urais mpaka pale utaratibu wa kuwa na uraia wa nchi mbili utakapokubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kama nilivyosema, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kupitia hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Kabla hatujaendelea na hatua inayofuata, nitoe tangazo moja dogo la kuwatambua wageni wa Mheshimiwa Godfrey Zambi ambao wametoka Mbozi wakiongozwa na Ndugu Freddy Mgala, Mwenyekiti wa MVIKAMBO, Mbozi ambaye amefuatana na Waheshimiwa Madiwani wawili; Mheshimiwa Sunday Shura na Mheshimiwa Burton Sinienga. Karibuni sana, mwangalie Bunge letu na Mbunge wenu Mheshimiwa Zambi anafanya kazi nzuri hapa Bungeni.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na utaratibu wetu na ili kuwarahisishia, nimeona kwamba badala ya kuanza na mafungu yale mengine, tutakula muda bure, tutaanza na fungu lile la mshahara wa Mheshimiwa Waziri moja kwa moja. Hilo la kwanza.

La pili, nikumbushe makubaliano yetu ya dakika tatu kusema na Waziri kujibu, si zaidi ya dakika tatu. Kwa hiyo, kila atakayetaka kuzungumza, tafadhali ajitahidi kutumia muda mfupi inavyowezekana usiozidi dakika tatu na kama kutakuwa na jambo linalohitaji uchangiaji, hautazidi dakika mbili. Nikumbushe neno moja ambalo linatokana na Kanuni zetu, Kanuni ya 101(3), na nitaisoma ilivyo. Tunakumbusha tu kwa sababu ni muhimu kukumbushana kila wakati: "Mbunge atakayeamua kutumia kifungu chenye mshahara wa Waziri, ataruhusiwa tu iwapo ataomba ufafanuzi wa suala mahsusi la sera na hatazungumza zaidi ya jambo moja" Ukurasa wa 65, (kama vile tulivyokuwa tumekubaliana). Kwa hiyo kwa mshahara wa Waziri ni mambo ya sera, tukiwa kwenye mafungu mengine, ndiyo unaweza ukauliza mambo mengine.

Na 103, Kuhusu kutoa hoja ya kuondoa shilingi, kwa sababu hiyo ni hoja, tunaendela na utaratibu ule ule. Ili tusichukue muda wa Bunge, inabidi hoja hiyo angalau iwe inaungwa mkono na wenzako angalau kumi. Katibu, sasa tuendelee.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Kabla hujaendelea, kaa kidogo. Niwakumbusheni tu Waheshimiwa Wabunge, najua wengi mna nia ya kusema chochote kuhusu kitu fulani kuhusu Wizara hii. Dakika zetu ni zile zile, tutaishia kwenye *guillotine*. Kwa hiyo, tukichukua muda wetu mwingi katika malumbano, mjue kabisa tunakula muda wetu ule wa kawaida. Mheshimiwa uliyetaka mwongozo!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hilo hilo ambalo nilitaka mwongozo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na utamaduni wa siku kadhaa, hotuba nyingi sana zimepitishwa kwa *guillotine* na ni kwa sababu wakati wote Meza imekuwa ikiongeza nusu saa tu ile inayoruhusiwa na Meza bila kutengua Kanuni na kadhalika. Sasa, naomba mwongozo wako kuhusu jambo hili ambalo tunataka kulifanya hivi sasa. Kwa mujibu wa maelezo uliyoyatoa, ni kwamba tunakwenda kwenye fungu 51 na Wizara hii ilipaswa tuanze na fungu la 14. Tafsiri yake ni kwamba watu wakishashika mshahara wa Waziri kwenye fungu la 51 kwa wingi, tutafikia hatua muda utakwisha halafu moja kwa moja tutakwenda kwenye *guillotine* na vifungu ambavyo kiutaratibu tungeanza navyo, tunaanza na 51 badala ya kuanza na 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba mwongozo wako ili tuweze kwenda kwa kadri ya utaratibu, tuweze kuanza na fungu la 14 ili tukifika wakati ule wa fungu la 51, tupate fursa ya kutumia Kanuni kuongeza muda tuitendee haki hii Wizara ambayo ni Wizara muhimu sana kwa Taifa letu.

**MWENYEKITI:** Mimi niseme niko radhi, tutaanza kwa utaratibu ule. Nia yangu ilikuwa ni njema, suala la muda mtaniachia mimi. Nionavyo mimi, tutamaliza kwa wakati ule ule ambao tumepanga. Tunaanza na fungu lile la 14 na matokeo yake mtayaona, kwamba ushauri wangu uliwatakia mema zaidi kuliko ushauri wenu. Katibu, tuanze na fungu lililoshauriwa!

**FUNGU 14 – JESHI LA ZIMAMOTO**

Kif. 3001- *Fire and Rescue Services*……Sh. 2,479,935,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu 30, kifungu cha 3001, kasma ya 210100 pamoja na 210300. Katika maelezo ya Waziri kuhusiana na suala lililoainishwa kwenye ripoti ya *CAG* kuhusu magari ya Zimamoto, kimsingi maelezo ambayo Waziri ameyatoa hayajitoshelezi. Lakini, nia yangu siyo kuzungumza kuhusu hilo, nitazungumza katika hatua za baadaye.

Kuna jambo la pili ambalo tulilieleza la kukosekana kwa sera ya usimamizi wa vihatarishi ambavyo vinasababisha Idara ya Zimamoto inashindwa kukabiliana vizuri na majanga. Sasa, ningependa kupata ufafanuzi, inaonyesha hapa kwenye hizi kasma kiwango cha fungu la mishahara…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, twende taratibu! Kwa sababu kama unavyojua ni *issue* moja…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ndiyo *issue* moja hiyo Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, umesema fungu 210100!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Fungu ni 3001, *subvote*!

**MWENYEKITI:** Sawa sawa! Hapo kwenye zimamoto tuko pamoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kifungu 30100!

**MWENYEKITI:** Kifungu kidogo?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kifungu kidogo cha 210300 kinachohusu *personal allowances (non-discretionary)*. Sasa utaona kwamba kwenye hiki kifungu, kiwango cha posho kimeongezeka, lakini ukitazama kifungu cha juu yake kwa sababu nafanya *reference*, kiwango cha fungu la mishahara kimeshuka. Kwa hiyo, wafanyakazi wamepungua, lakini posho imeongezeka. Sasa nataka ufafanuzi kama kiwango hiki cha posho kinachoongezwa pamoja na wafanyakazi kupungua, kitasaidia Taifa letu kuwa na sera ya usimamizi wa vihatarishi ili kuiepusha nchi yetu na majanga. Ningeomba kauli, ni lini sera hii itakuwepo kama ambavyo *CAG* ameainisha na Kambi ya Upinzani imerejea?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kwamba Mheshimiwa Mnyika atauliza swali hilo. Jibu ni jepesi sana. Kama ulivyosema, ni kweli kwa mwaka uliopita, utaona fedha ambazo zilikuwa zimeidhinishwa katika 10100, zilikuwa pesa ambazo zimeidhinishwa. Lakini, hawakuweza kupata wafanyakazi hao, kwa hiyo, hizo nafasi zilibaki na hizo pesa zilirudi Hazina. Sijui, kama umenielewa Mheshimiwa?

**WABUNGE FULANI:** Endelea, endelea!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zile pesa ambazo tuliomba mwaka jana hazikutumika zote, lakini ingawaje hapa zinaonyesha kwamba hizi pesa zilitumika. Kwa kuwa zile nafasi hazikupatikana, hizi pesa tulizoomba mwaka huu ni katika nafasi ambazo zipo sasa hivi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 – *Fire and Rescue Services Training Instituion*……..................Sh. 546,057,000/=

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi. *Subvote* hiyo 3002, *item* 220400 - *medical supplies and services*. Naona pesa zilizotengwa pale ni milioni tano. Lakini hata kwenye *subvote* tuliyotoka kuijadili pia, pesa zilizokuwa zimetengwa ni hizo hizo milioni tano. Sasa, hiki ni Kikosi chote, nataka kujua, pesa nyingine kwa ajili ya suala hili nadhani linazungumzia *supply* ya dawa na nini, watazitoa wapi kwa kiasi hiki kidogo cha pesa kilichotengwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu Mheshimiwa Zambi ni kwamba, ni kweli hata sisi tunaamini kwamba kiasi ambacho tumepewa kwa sababu ya *medical services* hakitoshi. Lakini hiyo inatokana na hali halisi ya pesa ambazo tunazo katika bajeti.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 28 – JESHI LA POLISI**

Kif. 2001 – *Police Mainforce* …………….Sh. 89,915,073,300/=

**MHE. ASAA OTHMAN HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni jana nilizungumzia suala la watu waliofukuzwa kazi ndani ya Jeshi la Polisi na wamekwenda Mahakamani, Mahakama ikaamua kwamba warejeshwe kazini na walipwe haki zao zote. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wakati anafanya majumuisho hapa, ame…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamad, samahani!

**MHE. ASSA OTHMAN HAMAD:** Naam!

**MWENYEKITI:** Kule kwa Mheshimiwa Waziri ndiyo sera kama unavyotaka kuelekea. Hapa lazima twende kwenye fungu moja kwa moja liwe swali ambalo linajielekeza moja kwa moja kwenye fungu, ni jambo gani hasa ambalo unalilenga. Nia yangu ni kujaribu kukuweka sawa, lakini endelea kama una jambo.

**MHE. ASSA OTHMAN HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nia yangu ni kwamba sijaridhika na jibu la Waziri, kwa hiyo naomba kauli juu ya wale ambao wameamuliwa hivyo na mpaka sasa hawajarejeshwa, Serikali inasemaje?

**MWENYEKITI:** Nitakuomba usimame baadaye wakati...

**MHE. ASSA OTHMAN HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mshahara wa Waziri! *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ndio ulikuwa tuanze nao, Mheshimiwa Mnyika kasema, hapana, tuanze kinyume chake na mimi nikakubaliana naye!

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Subvote* 2001, *item* 220300 pamoja na *item* 230400 – *fuel oil lubricants*. Hii imetengwa kutumiwa jumla ya shilingi 2,614,800/= kwa ajili ya magari. Lakini tunakuta kwamba *routine and maintanance* ya haya magari ni *zero*. Je, Mheshimiwa Waziri, magari haya hayatoharibika yakahitaji kutengenezwa? Naomba maelezo yake!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kujibu swali la Mheshimiwa Rajab, ni kweli magari yanaharibika lakini ni hali halisi ambayo tulikuwa nayo kwa sababu huko tutakavyotazama hata hatuna pesa za kununua gari mpya katika kipindi cha mwaka huu. Kwa hiyo, tutazama jinsi tutakavyoweza, lakini kwa hali halisi ya bajeti tuliyokuwa nayo ndiyo maana tumeweka namna hii.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kinachohusiana na fedha zilizopangwa kw *RPC* Tanga sijaziona kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Polisi, hasa Wilaya ya Lushoto wanaishi katika mazingira magumu sana. Ningependa kujua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tuko kwenye *Police Mainforce.*

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Ahsante, basi nitaomba fursa ya kusimama tutakapofika panapohusika.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana nakushukuru.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru. Programu 20, kifungu 2001, kasma 2010300, *Personal Allowances Discretionary* ambayo inaonyesha kwamba kiwango cha fedha za posho kimepanda kutoka Sh. 44,000,000,000/= mpaka Sh. 48,000,000,000/=, ni ongezeko la takriban Sh. 4,000,000,000/=. Nataka kupata ufafanuzi tu, kwa sababu kuna kauli imetolewa humu Bungeni kwamba askari wanalipwa posho ya sh. 150,000/=. Lakini askari wengi wamekuwa wakitupigia simu kwamba ukweli ni kwamba wanalipwa chini ya kiwango hicho. Sasa nataka kupata ufafanuzi kama ongezeko hili la posho litaambatana sambamba na kuongeza kiwango cha posho kwa askari na ongezeko hili ni kwa kiasi gani? Kwa hakika kabisa tofauti na kauli za kisiasa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mnyika kama ifuatavyo:-

Suala la posho, ziko posho za aina mbalimbali na kwa kweli nasikitika siwezi kukwambia hapa *exactly* unazungumzia nini, maana ziko posho tofauti na zile posho ambazo tumeomba tumepata kiasi ambacho tumeweza kuongeza. Maana toka 100 zimekwenda mpaka mpaka 150. Siwezi nikakwambia kama unavyotaka kujua kwamba sijui zimekwenda katika sehemu gani. Lakini ninachojua ni kwamba, hizi ni posho ambazo tumejaribu kuwapa Askari na nyinyi wenyewe kila siku hapa mnasema kwamba posho za askari ni ndogo. Lakini pia yako masalia hayo na yako madeni ambayo pia bado hawa askari wanadai.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ni programu 20, hiyo hiyo, *sub-vote 2001,* lakini kifungu kidogo cha *221000, traveling in country.* Kwanza, nimefurahi kwa sababu pesa hizo ambazo ni kwa ajili ya safari naona zimeongezeka. Lakini kumekuwa na malalamiko ya Polisi hasa wa vyeo vya chini, kusafiri bila kulipwa posho zao kwa maana ya *per*

*diem* kule wanakokwenda kufanya kazi. Lakini nimeangalia vipindi vyote vya kusafiri ndani ya nchi vyote vimetengewa pesa. Je, Mheshimiwa Waziri anatueleza kwamba tabia ile ya Polisi hasa wadogo kusafiri bila ya posho ndiyo mwisho wake sasa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafunuzi ufuatao:-

Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, nadhani posho ya usafiri kwa askari kama ilivyo kwa wafanyakazi wengine wa Serikali ni haki ya wafanyakazi. Kwa hiyo, tutafanya kila lililo katika uwezo wetu kuhakikisha kwamba askari hawa wa Jeshi la Polisi wanapewa posho zao kama inavyostahiki na kwa kuwa imeidhinishwa katika bajeti hii.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Police Marine* …………………Sh. 1,410,881,300/=

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. *Sub-vote* hiyo hiyo. Fungu *2002, item 231100. Other routine maintenance expenses not as were classified.* Hapa pametengwa jumla ya sh. 60,000,000/=. Fungu lililopita niliambiwa kwamba fedha hakuna, bajeti ndogo. Je, nataka maelezo haya matumizi ambayo *not classified* yakoje?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Anataka ufafanuzi matumizi *not classified but classified* imeandikwa *else where classified* nafikiri? 231100 Mheshimiwa!

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni fungu dogo la 231100!

**MWENYEKITI:** Aaah *okay*! Ndiyo hilo hilo, tuko hapo hapo. Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemwelewa Mheshimiwa Mbunge, anauliza *other routine maintenance expenses not else where classified. Of course* hizi ni gharama ambazo tunazitumia wakati Askari, maana tumekuwa na hili suala la mjadala la shilingi 5,000/=, lakini hizi ni pesa ambazo zinatumika katika *expenses* ambazo zinahusu mazishi na usafirishaji wa Askari.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nazungumzia kifungu namba 220800 na hiyo 220900 ya *training domestic* na *training foreign* na pesa zilizotengwa kwa mafunzo haya ya ndani na ya nje nasema ni kidogo mno, hazitoshelezi chochote na hali tuliyonayo sasa hivi tunao mpaka ma-*local pirates* hapa ambapo wavuvi wetu huwa wanakamatwa, wananyang'anywa vifaa vyao na sasa sijui Jeshi la Polisi limejipangaje kusaidia kikosi hicho cha *marine* kiweze kusaidiana na Jeshi la wananchi kulinda wavuvi wetu wasinyonywe mali zao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa ufafuzi kwa Mheshimiwa Mbunge kuhusu hizi sehemu mbili, *training domestic and training foreign. Of course,* suala la *training* ni suala ambalo ni muhimu sana. Lakini hizi pesa ambazo umeona tumeweka hapa ni halisi ya pesa tulizonazo. Tunaamini kwamba hazitoshi, lakini imebidi tuweke kiasi fulani ambacho kinaweza kikasaidia katika *training* fulani. Lakini hazitoshi na hazikidhi lakini kwa sababu ya hali halisi ya pesa tulizonazo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 – *Railway Police Division*…………Sh. 642,134,100/=

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nipewe *clarification* tu hapo kwa sababu naona katika fungu hilo kuna *codes number* za mishahara peke yake. Sasa, sioni *allowances* zozote kwa hawa askari. Ina maana kwamba hawasafiri, hawalipwi *allowances* zozote? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hapa hakuna mafungu mengine, ni kwa sababu hawa wanakuwa katika zile *trains* ambazo zinapeleka abiria katika sehemu ambazo *trains* zinafanya kazi. Lakini mambo yao ya huduma nyingine kama mambo ya ugonjwa kama ni mambo mengine yanatoka katika kasma nyingine hapa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naona ndugu yangu Mheshimiwa pale ameniwahi. Nataka kuuliza hivyo hivyo kwamba inakuwaje hawa watu hawana vitu kama *maintenance* na vitu vingine! Nikasema au ndiyo ishara kwamba reli inakufa!

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2004 – *Police Signals Branch…………S*h. 4,163,820,300/=
Kif. 2005 – *Police Zanzibar………………..S*h.11,132,584,300/=
Kif. 2006 - *Police Air wing*………………….Sh. 2,218,707,700/=
Kif. 2007 – *TAZARA Police……………………S*h. 856,865,200/=
Kif. 2008 – *Field Force Unit………………...S*h. 8,706,889,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2009 – *Traffic Police……………………*Sh. 2,294,102,900/=

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Bado, bado naorodhesha. Nikishakutaja unakaa. Ili niweze kuwataja wengine halafu baadaye mtaanza kuzungumza. Nitajie Katibu. Mheshimiwa Kiwanga, Mheshimiwa Mtutura. Tuanze na Mheshimiwa Kiwanga.

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu hicho kikubwa 2009 kwenye kifungu kidogo 220600 - *Clothing, bedding, footwear and services*. Naona hakuna kitu chochote kwa hawa *traffic*. Sasa, sijui haya mavazi yao meupe kama nyangenyange ina maana hawatapata huduma hiyo? Naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba hizo *uniform* zao zinapatikana katika fungu hilo hilo. Au sikum…., sikum….

**MWENYEKITI:** Anasema katika fungu hilo la mavazi kwa mwaka huu hakuna fedha yoyote iliyotengwa. Je, hakutakuwa na *uniform* zozote? Ni ile *220600 - clothing, bedding, footwear and services.*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo, lakini zipo Makao Makuu ambazo zimetengwa karibu Sh. 100,000,000/=. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, limekwishajibiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mtutura?

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Wasemaji walionitangulia wameni-*pre-empt*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2010 – *Police Airport……………………..S*h. 783,270,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2011 – *Police Dog and Horses………..S*h.1,362,838,800/=

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kuhusu kasma 411200 inayohusu *acquisition of cultivated assets (breeding stock and live animals).* Fedha ambazo zimetengwa inaelekea ni sifuri kwa ajili ya kupata wanyama wa Kikosi hiki cha Mbwa na Farasi. Naomba ufafanuzi ni kwa nini Kikosi cha Mbwa na Farasi hakijatengewa fedha kwa ajili ya kupata wanyama wa kuzalishia hii *breeding stock* pamoja na Mbwa na Farasi wenyewe. Nashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge Lissu kwamba, hatukutenga fedha hapa *for the purposes* za kununua, lakini uzalishaji ni katika wale tulionao. Lakini kubwa zaidi ni kwa sababu hatuna pesa za kununulia. Lakini bado hili litafanyika kwa wale tulionao.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2012 – *DSM Special Zone…………….*Sh. 5,465,853,600/=
Kif. 2013 – *Police Ilala……………………..*.Sh. 4,329,087,700/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2014 – *Police Kinondoni……………...*.Sh. 4,362,446,800/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu hicho cha 2014 cha kuhusiana na *Police* Kinondoni. Kasma ya 210100, *basic salaries special post* ambazo zinaonesha kwamba ongezeko la mishahara ni takriban *gap* kutoka mwaka uliopita wa fedha, ni kama chini ya 60,000,000/=. Sasa nataka kuomba ufafanuzi tu, ilitolewa kauli inayoonesha kwamba mishahara imepanda, kauli ambayo ilijenga matumaini kwamba mishahara imepanda. Lakini kwenye kesi ya walimu kwa *pay slip* za mwisho wa mwezi huu wa kwao, Mwalimu wa kima cha chini amekuta mshahara umeongezeka kwa asilimia tisa tu kama shilingi 20,000 *or so*. Sasa nataka kujua kwa upande wa Polisi….

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, tuko kwa Askari. Sasa kwa Walimu huko rafiki yangu…..

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Nataka kujua sasa kwa upande wa Polisi, nipate ufafanuzi kwa sababu hapa kwenye bajeti inaonesha pesa za mishahara hazijaongezeka sana. Mishahara kwa Askari Polisi, kwa mujibu wa hili ongezeko lililotajwa hapa, itaongezeka kwa kiwango gani ili lijulikane wazi kabisa hili suala la mishahara. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni vigumu sana sasa hivi kukwambia zimeongezeka kwa kiasi gani. Kama tumetoa ahadi kwamba ongezeko litakuwepo, jitihada ambazo tunazifanya, najua maana yake mnaona kama tunafanya masihara, lakini ukweli ni kwamba ongezeko linakuwepo kutegemea pesa ambazo tunazipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka katika *intervention* moja ambayo tumeifanya hapa kuhusu chakula cha Magereza, pesa tulizoomba siyo pesa ambazo tumezipata. Imetuletea matatizo hapa kusema kwamba, hizi pesa zimetumika katika njia za ufisadi, ambayo si kweli. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge aridhike na hili ongezeko dogo ambalo tumekuwa nalo, lakini baadaye tutakapokuwa tumepata, maana tutakuwa tunatoa ripoti kuonyesha ni kiasi gani cha fedha, hali halisi ilivyo ya mishahara ya Askari.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2015 – *Police Temeke…………………*Sh. 3,242,010,900/=
Kif. 2016 – *Police* Arusha………………….Sh. 4,722,904,700/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2017 – *Police Iringa……………………*Sh. 3,709,510,700/=

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana!

**MWENYEKITI:** Bado, alikuwepo wa pili ee? Ni mmoja tu? Ahsante Mheshimiwa Mng'ong'o!

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimeona sehemu nyingine kuna kifungu kinachosema *clothing, bedding and footwear and services*. Naona Polisi - Iringa kifungu hicho hakipo. Kwangu nafikiri kwamba ni muhimu kuwepo ukizingatia kwamba ule Mkoa kuna baridi sana, kwa hiyo, wanahitaji mavazi yakiwemo ya kujihifadhi na baridi. Sasa ningependa kufahamu kiko kwenye kifungu gani labda?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumjibu swali Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o ni kwamba akitazama vizuri atakuta kuna sehemu kifungu hiki kipo na kuna sehemu nyingine ambapo kifungu hiki hakipo, hii inatokana na kwamba pale mahali ambapo bajeti iliyokwisha tulikuwa tumepeleka vile vifaa, bajeti hii inabidi sasa tupeleke mahali pengine lakini hii inatokana na ufinyu wa bajeti wala siyo kwa sababu nyingine yoyote.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2018 - *Police Kilimanjaro*…………….Sh.4,667,648,500/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2019 - *Police Kigoma*………………….Sh. 3,522,228,200/=

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata maelezo ya Waziri, Mkoa wa Kigoma ni Mkoa ambao una uwanda mkubwa sana ambao unahitaji ulinzi wa kutosha na naona kwamba gharama za mafuta katika mikoa yote hakuna umaalum wowote ambao unaonekana, nilitegemea kwamba pengine Mkoa wa Kigoma ungekuwa na umaalum wake kwa maana ya kiasi ambacho kinatengwa kwa ajili ya mafuta.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafulila ni fungu gani unalizungumzia hapa?

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni 220300 *Fuel, Oil and lubricants*. Kiasi ambacho kimetengwa kwa ajili ya mafuta kinakaribia kulingana katika mikoa yote, lakini Mkoa wa Kigoma una umaalum wake kwa maana ya kazi ya mafuta kwa ajili yak u-*patrol* eneo refu na kubwa la mpaka, sasa sijui ni kwa nini kiwango kimekwenda karibuni sawasawa na mikoa mingine. Naomba maelezo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anayoyasema ni sahihi kwamba Mkoa huu wa Kigoma na Mikoa mingine ya pembezoni kwa nchi yetu yapo matatizo na kuna kazi zingine za ziada, lakini tatizo ni uhaba wa fedha. Lakini ukitazama fedha ambazo tumeweka hapa ni Sh. 378,000,000/=. Kweli inaweza kuonekana ni kidogo lakini bado nafikiri Mheshimiwa Mbunge twende nazo hizo kwa sasa tuone tutafanyaje, lakini ni kwa sababu ya uhaba wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ningewaomba Waheshimiwa Wabunge sasa tukubaliane kwamba maswali ya kwa nini sungura mdogo angalau yatoshe sasa, kwa sababu jibu lake ndiyo hilo.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 2019, Kifungu 229900, *other operating expenses* ni kweli kama ulivyosema itoshe kusema habari ya sungura ni mdogo. Lakini kuna maeneo nadhani yana unyeti wake katika kulinda mipaka yetu. Ukiangalia Mkoa wa Kigoma wote tumekuwa tunapata matatizo makubwa ya majambazi wanaovamia kutoka nje ya nchi, upande wa Congo na Burundi, tungependa kujua wanapoweka hela kidogo za *operating expenses* haoni kwamba, tatizo la kupambana na hao majambazi kwa mikoa hii itakuwa ni shida sana. Pamoja na kwamba kuna sungura mdogo, lakini kupanga ni kuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini sasa wasiminye kwingine ili hawa wapate pesa nyingi zaidi ili tuweze kulinda watu wa Kigoma nao katika nchi yetu.

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hali anayoisema ya Kigoma kweli ni hali ambayo inatukabili katika mikoa yote ya Tanzania without *exception demands* ni zile zile, nina uhakika Wabunge wote wakinyanyuka kuhusu mikoa yao watasema vile vile. Lakini niseme kwamba hizi pesa ukizitazama hasa kwa hali waliyokuwa nayo katika Mkoa wao na mwingiliano mkubwa uliopo pale ni *expenses* ambazo tumeziweka kwa sababu ya shughuli ya upelelezi na mambo ya mazishi. Lakini ningeomba tu kwamba Mheshimiwa Serukamba aridhike na hilo na najua Wabunge wengine watakuwa na matatizo na jambo hili.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2020 - *Police Kagera*…………………..Sh. 3,649,956,700/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2021 - *Police Lindi*……………………......Sh. 2,910,911,600/=

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika kuchangia kwangu katika Mkoa wa Lindi, nyumba za Askari zipo katika mazingira magumu na nikiangalia hapa sijaona sehemu yoyote ambapo wametenga hizo pesa angalau kwa kufanya *maintenance*, ningependa kujua Waziri ana mkakati gani kwa ajili ya marekebisho katika nyumba hizi za Askari, Lindi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nilifika Lindi na hali ya nyumba pale nilivyoiona ni kama mahali pengine, lakini haziko hapa wala hazikukusudiwa kuwekwa hapa, hii ni katika *expenses* za mambo mengine ya kiutawala ya *maintenance* ya Polisi waliopo pale. Suala la majengo lipo mahali pengine katika *development*. Lakini hali tuliyokuwa nayo sasa hivi hatuna fedha na ningeomba hiyo ieleweke lakini huko tunakokwenda mbele ya safari tutatazama kuona ni jinsi gani tunaweza tukasaidia katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante tukiangalia saa yetu ya ukutani katika muda wetu wa kawaida, bado saa moja, bado tupo Mkoa wa Lindi, Katibu tuendelee na Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mtanda nimekusahau samahani sana.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wewe ni rafiki yangu hakuna neno. Katika *subvote* hii ya 2021 hatuoni hapa *repair* ya magari na kwa kweli magari ya Polisi, Mkoa wa Lindi yapo hoi. Katika *subvote* hii hatuoni kipengele chochote kinachoonesha basi hatupati mapya, basi hata hayo machakavu yawekewe fedha kidogo kwa ajili ya ukarabati ili yaweze kufika maeneo mbalimbali ya Wilaya yetu ya Lindi Vijijini na Mkoa mzima wa Lindi. Naomba Waziri atueleze, je, kuna eneo lingine zaidi ya hili ninaloliona hapa pengine fedha hiyo imetengwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hali tuliyokuwa nayo ya kifedha ni hali ngumu, maana ni jibu ambalo tutaendelea kuwapeni. Hakuna kitu kibaya kama kudanganya kwa kusema hili litafanyika na lisiweze kufanyika, isipokuwa katika mtazamo mwingine wakati mwingine kutoka *headquarter* ya Polisi wanaweza kusaidia katika maeneo ambayo kunakuwa na uharaka zaidi ama kuna *emergency* ambazo zimejitokeza. Lakini kwa mujibu wa pesa ambazo tumeweka katika bajeti yetu, hii inaeleza hali halisi tuliyonayo ya kifedha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2022 - *Police Mwanza*………………....Sh. 5,127,263,100/=

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 2022, Kifungu kidogo cha 221000, *Travel in country*, ongezeko la mwaka jana hapa ni shilingi takribani chini ya milioni tano, sasa ukiangalia Mkoa wa Mwanza ulivyo, ukienda mpaka Visiwa vya Ukerewe ambavyo viko vingi sana uende mpaka karibu na Mkoa wa Bariadi kwa upande mmoja, ongezeko hili naona ni dogo sana, ukizingatia kwamba matukio ya uhalifu ni mengi, hasa ukizingatia ukanda wa Ziwa kwa upande mmoja. Je, Waziri haoni kwamba, hili fungu la *travel in country* lingeongezeka na kwa sababu ukizingatia kwamba ni kwa vituo vyote vya Polisi Tarafa na kadhalika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge naweza hata nikatabiri majibu lakini Naibu Waziri ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kwamba Mkoa wa Mwanza ni Mkoa mkubwa na masafa yake ni makubwa pia, katika jitihada za pesa ambazo tumepata katika bajeti yetu ndiyo maana unaona tumeweza kuongeza kidogo. Ukitazama bajeti ya Mwanza, ukilinganisha na mikoa mingine unaona kwamba ni kubwa kuliko mikoa mingine ingawaje haikidhi ni kwa sababu ya ukubwa. Naomba Mheshimiwa Mbunge aelewe tu kwamba ni tatizo la kifedha wala siyo jambo lingine. Tungependa tufanye makubwa zaidi ili kuwawezesha askari wetu kuweza kufanya kazi zao vizuri lakini ni uhaba wa fedha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2023 - *Police Mara*……………………..Sh. 3,348,352,100/=
Kif. 2024 - *Police Tarime-Rorya*…………..Sh. 2,038,445,900/=
Kif. 2025 - *Police Mbeya*…..………………Sh. 4,114,671,000/=
Kif. 2026 - *Police Mtwara*………………….Sh. 3,063,052,400/=

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2027 - *Police Morogoro*……………….Sh. 5,158,534,800/=

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, sijaona kasma yeyote inayoonesha *travel out of country*, ina maana Polisi Mkoa wa Morogoro hawataenda nje ya nchi kujifunza?

Mwenyekiti:Kuna Polisi wa Mkoa wowote wamewekewa *travel out of country*, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA DANI YA NCHI:**Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba mahali ambapo anaona hiki hakipo basi hii inachukuliwa katika kifungu cha Makao Makuu.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Sub *vote* namba 221700, Mkoa wa Morogoro umetengewa milioni mia moja na thelathini na sita, lakini mikoa mingine yote wametengewa milioni elfu thelathini na sita, *subvote* hii inahusika na *food supplies and services*, naomba maelezo kutoka kwa Waziri, ongezeko hili la milioni mia moja kwa Mkoa huu wa Morogoro peke yake umetokana na nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA DANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru, ni *typographical error*, siyo laki moja ni zile kama mikoa mingine.

**MWENYEKITI:** Ni 36 kama mikoa mingine.

*(Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi ya Bunge zima bila Mabadiliko yeyote)*

Kif. 2028 - *Police Manyara*……………….Sh. 3,022,948,700/=
Kif. 2029 - *Police Singida*………………....Sh. 3,272,416,400/=
Kif. 2030 - *Police Pwani*…………………......Sh. 3,874,085,300/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2031 - *Police Ruvuma*………………...Sh. 2,955,591,800/=

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napongeza Wizara kwa kutambua umuhimu wa Jeshi Mkoani Ruvuma, kwenye *basic salary, non pensionable* kwa kuwaongezea fedha. Hoja yangu iko katika kifungu cha mavazi na huduma nyingine zinazofanana na hizo, mwaka huu naona wametengewa fedha kidogo sana ingawa mwaka jana hawakutengewa.

Ninachoomba tu ni ahadi ya Waziri kama Serikali mwakani itakuwa na hali nzuri, yupo tayari kuwatazama Polisi wetu wa Mkoa wa Ruvuma na kuhakikisha kwamba kifungu hicho wataongezewa ili waweze kufanya kazi nzuri ya ulinzi mpakani mwa Tanzania na Msumbiji ambako tumekuwa tukiingiliwa sana na Wasomali na mpakani mwa Tanzania na Malawi kupitia ziwa Nyasa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ambayo tunaweza kuitoa hapa, azma ni kuboresha nguo, *bedding* kwa askari wote. Sasa hivi tatizo tulilonalo nalo ni bajeti lakini endapo hali itakuwa nzuri nataka nimhakikishie Mbunge na Wabunge wengine kwamba tutafanya linaloweza kufanyika ili kuongeza hilo.

**MWENYEKITI:** Sungura akikua.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2032 - *Police Rukwa*………………......Sh. 3,107,244,800/=
Kif. 2033 - *Police Shinyanga*……………...Sh. 4,023,129,300/=

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2034 - *Police Tabora*………………......Sh.3,300,315,900/=

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Subvote* 2034, katika Mikoa mingine nimeona Polisi wanacho kifungu cha *clothing, bedding, footwear and service*, je, Polisi wa Mkoa wa Tabora hawahitaji nguo kwa mwaka mzima?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sakaya asifikiri kwamba kuna *discrimination* ama kuna watu ambao tumewaacha, lakini kama nilivyojibu katika kutoa maelezo ni kwamba, pale ambapo tuliweza kupeleka vifaa hivi mwaka jana, mwaka huu imebidi tupeleke mahali pengine ambapo hatukupeleka, hiyo ndiyo sababu tu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2035 - *Police Tanga*…………………....Sh.3,939,337,400/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2036 - *Police Mjini Magharibi*………..Sh. 3,556,561,000/=

**MHE. SELEMAN S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kufahamu vituo vyote *across* Zanzibar sioni *code number* ya *Office Utilities* ambayo inahusiana na matumizi ya maji, umeme pamoja na simu. Naomba ufafanuzi katika eneo hilo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ni kweli kama alivyosema Mbunge, lakini fedha za kulipa umeme na maji zipo Makao Makuu ya Polisi, Zanzibar na tumeanza utaratibu huo kwa sababu zamani masuala ya kulipia umeme ilikuwa inalipwa na Makao Makuu ya Polisi, sasa tumeanza na utaratibu huo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2037 - *Police Kusini Unguja*………….Sh. 1,987,465,300/=
Kif. 2038 - *Police Kaskazini Unguja*………Sh. 1,638,674,000/=
Kif. 2039 - *Police Kusini Pemba*…………Sh. 1,871,587,100/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka niulizie haya mafungu kwa ujumla wake Unguja na Pemba, lakini hapa nipo kwenye Mkoa wa Kaskazini Pemba, hivi vifungu vingine ambavyo vimepewa Mikoa mingine hawa hawahitaji kwa mfano *clothing, bedding, footwear and services* wao hawahitaji hawa askari wa huku? Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki ungerudia kidogo ili ueleweke vizuri zaidi.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye *sub-vote 2040* Polisi Kaskazini Pemba. Kuna vifungu ambavyo katika Mikoa mingine ambavyo wamewekewa kwa mfano kuna kifungu cha *clothing, bedding, footwear and services* hawa askari wetu walioko Mkoa wa Kaskazini Pemba na kwa ujumla wake Zanzibar nzima hawakuwekewa wao hawahitaji? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, mavazi ya askari Visiwani ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wanahitaji na fedha zao zinatoka Makao Makuu. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2041 Polisi Dodoma… … … ... … … … … … Shs. 361,814,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Police College Moshi*… … … … … … Shs. 8,856,349,200

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nipo fungu hilo hilo 3001, *item 221700 food supply and services*. Hiki ni Chuo cha Polisi Moshi mwaka juzi kwa maana ya 2009/2010 zilitengwa shilingi milioni 900 mwaka jana 2010/2011 zikatengwa shilingi bilioni moja na nusu. Mwaka huu zimetengwa shilingi milioni 900 pungufu zaidi kwa shilingi milioni 600. Sasa nataka kujua huu ufafanuzi tumepunguza idadi ya vijana wanaokwenda pale kwa *training* au tutakiendesha hiki chuo namna gani kama tunapunguza fedha kwa ajili ya chakula kiasi hicho? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Godfrey Zambi, hizi ni *concerns* ambazo sote tunazo. Lakini hii idadi ya wanafunzi ambao tutakuwa nao katika Chuo mwaka huu haitakuwa kama vile ilivyokuwa mwaka jana. Kwa hiyo, wengine watakuwa watakuwa katika Chuo chetu cha Dar es Salaam na wengine watakuwa Zanzibar kwa hiyo, ndio maana idadi ambayo itakuwa pale ina-*reflect* fedha ambazo tumeona.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3002 – *Police College*… … … … …. … … … Shs. 1,723,292,300
Kifungu 4001 - *Police Vehicles Maintenance* … … Shs. 3,122,213,700
Kifungu 5001 – *Police Medical Unit* … … ….. … … … Shs.1,935,623,700
Kifungu 6001- *Police Building Brigade* … ….. … … … Shs. 5,154,787,100

Kifungu 7001 – *Criminal Investigation Division* … Shs. 24,724,960,100
Kifungu 7002 – *Stock Theft Prevention Unit* ….. … … … Shs. 895,831,600

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 29 – Jeshi la Magereza**

Kifungu 1001 - *Administration and General* … … … Shs. 6,770,616,300

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kujua kifungu 220200 *utilities, supply and services* kwamba hamna fedha hata kidogo gharama ndogo ndogo kama umeme na kadhalika labda hawa wanalipa kutoka wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zambi hebu rudia kidogo.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyeiti, nimesema *program 10, sub-vote 1001, item 220200 utilities, supply and services* nimesema hakuna fedha iliyotengwa pale shughuli za umeme, maji na nini wanalipa kutoka wapi? Nataka ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zambi kuwa hizi zipo katika sehemu, ningeomba unipe muda kidogo niweze kutazama hapa lakini zipo katika fungu fulani, naomba unipe muda kidogo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ananithibitishia kwamba zipo katika fungu lingine masuala ya *utilities.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 – *Parole Department* … … … … … … … Shs. 588,308,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 – *Prison Welfare and Rehabilitation*… ... ... ... ... ... ... ... ... ... Shs. 88,594,234,600

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kifungu 2002 kasma 221700 *food supplies and services* kwa maana ya chakula na huduma nyingine. Inaonesha kwamba mwaka wa fedha uliopita fedha zilizotengwa kwa ajili ya chakula kwa wafungwa zilikuwa takribani shilingi bilioni 14.7 na sasa zimeshuka mpaka shilingi bilioni 13.4 sasa suala ambalo nataka ufafanuzi Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye maelezo yake alisema kwamba taarifa zilizoandikwa na Chama cha Wanasheria…

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa hebu anza tena. Fungu gani?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Fungu 2002 ukurasa wa 105 kasma 2217000 inayohusu fungu hili la vyakula. Taarifa za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu pamoja na Chama cha Wanasheria kinaonyesha kwamba wafungwa wetu hawapewi kiwango ambacho kinakusudiwa, maelezo aliyotoa Waziri ni kwamba fedha zinazotolewa na Serikali hazikidhi kile kiwango ambacho Serikali ilipitisha kwenye sera. Sasa ningeomba kupata ufafanuzi tu na kwa hili kwa kweli ni vizuri ikakubali tu ukaguzi ufanyike. Kwa sababu ukweli ni kwamba hali halisi ya kiwango cha matumizi ya mfungwa kwa siku ni chini ya kiwango halisi kinachotolewa na Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, unavyoji-*address* ni kama uko tayari kwenye mshahara wa Waziri kwenye sera.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Siyo kwenye sera, nazungumzia matumizi ya hizi fedha za wafungwa ambazo zimeshuka kiwango kulinganisha na mwaka uliotangulia, lakini pili maelezo ya ufafanuzi aliotoa Naibu Waziri hayakidhi kabisa mahitaji. Sasa nataka kupata ufafanuzi tu, kwa mwaka huu wa fedha mfungwa mmoja kwa hizi shilingi bilioni 13.4 ambazo tunataka kuzipitisha

mfungwa mmoja atatumia kiasi gani kwa siku ili wale watu wa magereza kule magerezani wasiwape tofauti na kiwango ambacho sisi tunapitisha Bungeni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Si itategemea kiwango cha watakaokamatwa kwenye maandamano na nini.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naona Mheshimiwa Mnyika amekazana maana yake kitu nilichokizungumza kabla sijajibu hii hoja yako nilisema kwamba fedha tulizopewa mwaka jana si fedha ambazo tuliomba, ambazo zimeonyesha katika kitabu kwamba tumeomba siyo fedha ambazo tulipewa.

Kwa hiyo, ilibidi wafungwa wale kwa mujibu wa fedha ambazo tumepewa na sasa hapa unapoulizwa mimi naona hakuna tofauti maana hizi ni fedha ambazo tumepewa na ni katika hali halisi ya fedha tulizokuwa nazo. Lakini bado nitakuambia kwamba hapa zipo fedha ambazo zinaonyesha kwamba zitatumika lakini pia magereza wana mashamba yao na wana vyakula vyao ambavyo wanapata kutoka kule ambavyo wakati mwingine vina *supplement* hivi ambavyo vinakuwa viko nje ya Bajeti. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2003 – *Resettlement of Offenders*………… Shs. 1,425,468,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Prison Staff College*……………. …… Shs. 1,850,895,800

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu namba 2217000 *food supplies and services* shilingi 600,000 nilitaka tu kujua shilingi 600,000 kwa *prison staff college* nilidhani watu wengi hizi zitafanya kitu gani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba hizi ni fedha ambazo zimewekwa kushika kasma, lakini hizi fedha zinatoka katika fungu lingine.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3002 – *Prisons Driving School*………………… Shs. 228,599,000
Kifungu 3003 – *Prisons Trade School*…….……………Shs. 542,191,900

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3004 – *Prisons College Kiwira……………….*Shs. 1,241,025,000

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia kifungu hiki cha *training domestic* 220800 hakijatengewa fedha kabisa naomba tu ufafanuzi labda kitaendeshwa namna gani ukizingatia kwamba ni Chuo cha Mafunzo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zambi ni kwamba hizi fedha hapa itabidi zitoke Makao Makuu kwa sababu Bajeti ambayo tumepewa ni ndogo lakini pia ni *training* ambazo wanapata ndani ya nchi wala siyo nje ya nchi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4001 – *Prison Building Brigade*…………….. Shs. 1,410,926,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4002 – *Prison Industries*………………………… Shs. 687,585,700

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kifungu kidogo 2215000 *Agricultural and Livestock Supply and Services*. Najua kwamba sungura ni mdogo lakini ninafahamu kabisa kwamba Magereza yetu haya na hasa yale ya kilimo sasa hivi yamekuwa yakitoa *support* kubwa ya kilimo cha uzalishaji wa mbegu. Sasa kwa msingi kwa kilimo kwanza Mheshimiwa Waziri yupo tayari fungu hili katika kipengele hiki mwakani sungura atakapoongezeka fungu hili liweze kuongezeka na kuweza kutoa huduma nzuri ya kuweza kutoa huduma ya kutosha kwenye *prison funds* katika kifungu cha *Agricultural, Livestock Supply and Services?*

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kweli tukipata tutaweka fedha zaidi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4003 – *Prison Farms*……………………………Shs. 947,167,900

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nipo kwenye hiki kifungu 221500 *Agricultural and Livestock Supply and Services.* Kwenye mashamba ya magereza ili yaweze kuwa na ufanisi kunahitaji vitendea kazi. Kwenye Gereza la Kilimo Urambo ambalo nime-*graduate* pale ni Gereza ambalo linazalisha sana na wana mifugo mingi lakini hawana hata chombo cha usafiri cha kupelekea maji shambani wala hata umeme kwa ajili ya kutunzia yale maziwa wanayohifadhi. Serikali inasemaje kuhusiana na hili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwamba majibu yangu ni yale yale, lakini hilo tutalichukua kwa kweli hili najua kazi kubwa ambayo inafanyika pale na tutatazama kama kutakuwa na uwezekano tutatazama jinsi tutakavyoweza kusaidia pale. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51- Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1001 – *Administration and General*………. Shs. 1,601,964,700

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa kuna posho mbalimbali wanazopewa polisi wakiwemo wale madereva wanaowaendesha wakuu wao wa polisi na posho hizi tumeelezwa kwamba zinapatikana kwa wakati muafaka. Lakini inasemekana hizi posho hawapewi. Sasa ninamuomba Waziri atuelezee vizuri kuhusu posho hizi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumjibu Mbunge ni kwamba kweli zipo posho mbalimbali na tatizo ambalo tumekuwa nalo kwa muda imekuwa ni kuzitoa hizo wakati muafaka na ndio maana kumekuwa na malimbikizo ya madeni. Kilichofanyika Mheshimiwa Mbunge mpaka kufikia madeni ya mwaka 2009 tumejitahidi tumeweza kuyalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa ndio tunaingia katika utaratibu wa kujaribu kulipa haya madeni, maana yake haya ambayo yamekwishalipwa ni kwa sababu Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali tayari amekwishakubaliana nayo kwa hiyo, hayo yamelipwa. Lakini hili tatizo ambalo si tatizo letu kama Wizara ni tatizo tu kwa hali halisi ilivyo kwa hiyo tunavyopata zile fedha kwa kuwa zinakuja zimechelewa ndivyo tunavyofikisha kwa wahusika. Ni jambo ambalo tunasikitika lakini ni jambo ambalo hatuna uwezo nalo.

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilimuuliza Mheshimiwa Waziri kwa kuwa Kituo cha Polisi Mwera kina majengo machakavu sana Serikali ina mpango gani wa kuyakarabati na kufanya askari wetu wawe katika mazingira mazuri. Ahsante.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika mchango wake wa maandishi Mheshimiwa Mabumba aliniuliza swali hilo kwamba Serikali ina mpango wa kukikarabati na kukitengeneza vizuri Kituo cha Polisi cha Mwera. Kama ambavyo tumekuwa tukisema mara kwa mara kwamba tunalijua tatizo hilo kwamba kuna mahitaji makubwa sana ya ujenzi wa vituo vya polisi, tuna mahitaji makubwa sana ya ujenzi wa nyumba za makazi za Jeshi la Polisi. Tunafanya kila lililo katika uwezo wetu kulitazama kadri uwezo wa fedha utakavyoturuhusu tutaliangalia suala hilo kwa makini. *(Makofi)*

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu wa maandishi katika mambo niliyochangia ni pamoja na kilio cha Wanakigoma cha kuitwa wakimbizi, siyo raia wa Tanzania. Ninaomba tamko la Serikali ili kuondoa adha hii kwa kuwa ni kero kubwa na hasa kwa sisi viongozi na wananchi wa Vyama vya Upinzani, ukiwa CCM utaitwa ni raia, ukiondoka CCM ukijiunga na Chama cha Upinzani unaitwa siyo raia. Hii nina ushahidi na hasa katika chaguzi mbalimbali zilizopita. Naomba tamko la Serikali ili kukomesha tabia hii kwa ndugu zetu wa Uhamiaji. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, watakubaliana nami kwamba mara nyingi tumekuwa tukiiambia Serikali hasa mikoa ya mipakani iliyopakana na nchi jirani ikiwemo hasa hasa Kagera na Kigoma ina matatizo makubwa sana ya wahamiaji haramu ndio maana wiki mbili zilizopita hivi nilifanya ziara maalum ya kwenda kuangalia jambo hili na nilibaini kweli kuna wafugaji wengi wa kigeni kutoka Rwanda. Sasa suala la Kigoma nalo halina tofauti kwa sababu Kigoma imepakana na nchi jirani. Kuna watu ambao siyo raia wa Tanzania wamekuwa wakiingia na kutoka. Sasa mimi badala ya kuwalaumu wenzetu hawa maana tuseme kwamba mimi nadhani tutoe *specific case* kama kuna watu ambao tunadhani wametendewa sivyo.

Lakini tukiwalaumu tu Maafisa wa Idara ya Uhamiaji, maana inawezekana kweli kwa sababu kuna watu tunaweza kudhania kwamba ni wahamiaji haramu, lazima watu tuwaulize maswali na hasa kwa kuwa sasa utaratibu wa kuwa na vitambulisho vya Utaifa bado, kwa hiyo, tutaendelea kuwahoji watu ambao tuna wasiwasi nao. Sasa Mheshimiwa Mbunge ana ushahidi kuna Afisa wa Uhamiaji hakutenda haki basi nafikiri hiyo tu-*deal* na Afisa huyo na kama analo jina mimi namuomba aniletee. Sisi Wizarani tutachukua hatua zinazostahili. *(Makofi)*

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabla sijamuuliza Mheshimiwa Waziri naomba ku-*declare interest* mimi ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Taifa *Tanzania Drivers Association*. Katika maandishi nimemuuliza Mheshimiwa Waziri, kwenye mchango wake ukurasa wa 13 na 14 amesisitiza madereva wafanye haraka kuchukua leseni. Lakini kuna madereva ambao wana miaka 30 wanaendesha magari na wamekuwa waki-*renew* leseni hizo toka wameanza kuendesha magari. Lakini wanapokwenda sasa hivi kubadilisha hizi mpya wanaambiwa waende tena chuo. Sasa nilikuwa naomba labda Serikali inazungumza nini kuhusu hili? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo; nafikiri tunakubaliana sana madhumuni ya kubadilishwa leseni hizi kulikuwa kuna wasiwasi wa muda mrefu kwamba watu wasiostahili wamekuwa wakipata leseni hizo. Kwa hiyo, tukabuni utaratibu wa kuwa na leseni za *electronic* ambazo itakuwa vigumu kidogo kuweza kuzighushi. Kwa maana hiyo, ndio tukaanzisha utaratibu huo. Sasa inawezekana mtu ameendesha gari kwa muda wa miaka 40 sasa la kujiuliza je, hiyo miaka 40 alikuwa na ujuzi unaostahili, alipata leseni katika njia zinazostahili?

Sasa tumechukua utaratibu huo ili kujiridhisha kama kweli huyu mtu ana ujuzi na maarifa yanayotakiwa, tunafanya hivyo kwa nia. Waheshimiwa Wabunge, hapa katika michango yenu wakati wa mjadala mlisema kwamba ajali za barabarani zimezidi na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ichukue hatua. Sasa hizi ni moja ya hatua ambazo tunazichukua. Tunaamini tukizichukua kwa dhati zinaweza kutusaidia sana katika kupunguza ajali.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi nimezungumzia vituo vya polisi katika Jimbo la Busanda vinafanyakazi katika

hali ngumu sana hasa Kituo cha polisi cha Katoro ambapo kinahudumia watu wengi sana hawana usafiri. Lakini vilevile Kituo cha Rwamgasa, Chigunga pamoja na Bukoli na Nyalugusu kwa hiyo, nilikuwa nahitaji ufafanuzi zaidi katika hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi katika hoja ya Mheshimiwa Mbunge Lolesia kwa kusema kwamba kweli hiyo hali niliwahi kuongea naye na ni hali ambayo inakabili vituo vingi hapa nchini. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba nia na azma ni kuboresha vituo vya polisi na kuhakikisha kwamba vitendea kazi vinakuwepo wala haina mjadala. Lakini tatizo kubwa ambalo tumekuwa nalo ni rasilimali fedha za kuweza kutumia kwa sababu *demand* inakuwa ni kubwa, ni ya nchi nzima. Kwa hiyo, tutakapokuwa tunakwenda awamu kwa awamu tutakwenda maeneo tunajaribu kufanya na kutengeneza na kuboresha hivi vituo vya polisi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Barway kabla hujauliza, kufuatana na Kanuni kwa kuwa zimebakia dakika kumi kufika mwisho wa *session* kwa mamlaka niliyopewa na Kanuni naongeza muda wa nusu saa kuanzia saa mbili kasoro robo hadi saa mbili na robo. *(Makofi)*

**MHE. SALIM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi na maelezo jana nilitaka kauli ya Serikali juu ya ukatili wa Jeshi la Polisi katika vituo vya polisi vya Kakonko, Katoro na Geita juu ya ukatili ambao unafanywa na raia ambao wanatuhumiwa na Jeshi la Polisi kitu kilichopelekea ndugu James pamoja na Mheshimiwa Mihayo kukatwa miguu na sasa wapo katika jengo hili Tukufu kuja kutaka kujua kauli ya Serikali inasemaje juu ya hali ambayo inatokea katika Jeshi la Polisi hasa huko Kakonko na Katoro? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi tumekuwa tukisema hapa na tunaendelea kusema kwamba hakuna mtu mwenye haki hiyo ya kutesa. Jeshi la Polisi linatekeleza wajibu wake wa kisheria na linapaswa kutekeleza wajibu wake kwa uadilifu na kwa kufuata misingi ya sheria.

Sasa kama kuna raia ambaye amefanyiwa kinyume na taratibu za kisheria zinavyoruhusu kama tunavyosema Serikali haitasita kuchukua hatua hizo kwa mujibu wa sheria. Tutafanya hivyo, mimi ninamuomba Mheshimiwa Mbunge atupe taarifa hizo, mimi ninamuahidi kwamba tutalishughulikia kikamilifu jambo hili ili haki na sheria ichukua nafasi yake. *(Makofi)*

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunitambua. Katika mchango wangu wa maandishi nilimueleza Mheshimiwa Waziri kwamba katika Jimbo la Bariadi Magharibi tuna Gereza la Kilimo katika Kijiji cha Matongo, kilianzishwa katika miaka ya mwanzoni ya 1980. Lilianza vizuri sana lilikuwa linafanya kazi vizuri sana. Sasa hivi shughuli pale za kilimo hazifanyika hawana zana, wanalimia jembe la mkono. Sasa tuliomba mwaka 2006 lirejeshwe kwa wananchi Serikali ikatuambia wana mpango wa kutafuta *partnership* na *private sector* lakini hadi leo eneo hilo bado liko vilevile. Ningependa nipate maelezo kutoka kwa Waziri tatizo hasa ni nini kama hamlitaki sisi tunahitaji eneo hilo. Nakushukuru sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi katika hoja ya Mheshimiwa Chenge, analolisema ni sahihi. Uongozi wa Magereza walijaribu kuweka *tenders* na watu wangekuwa *interested* kuingia katika *partnership* na bado haukufanikiwa lakini siyo kwamba ni kitu ambacho kimeachwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya mkutano huu tutafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba hili suala linakuwa *persuade,* limekwama kwa sababu ni suala la kupata wale *partners* ambao ni wa uhakika wale siyo *partners* ambao watakuja matapeli wana sababu ambazo siyo sababu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hili tutalifuatilia na bado hatujashindwa, ingawa nimuombe radhi kwamba tumechelewa lakini nimhakikishie kwamba tutalifuatilia kwa nguvu zote kuhakikishwa kwamba linafanyika. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kuhusu sababu hasa zilizoifanya Serikali kutokuleta Bungeni mkataba wa Kitaifa dhidi ya utesaji na matendo au adhabu nyingine za kinyama zinazotweza au za kudhalilisha wa mwaka 1984. Nimemsikia Mheshimiwa

Waziri akisema kwamba sababu iliyoifanya Serikali isiridhie mkataba huo ni kwa sababu huo mkataba unakataza adhabu ya kifo. Hata hivyo katika utaratibu wa Sheria za Kitaifa kama kuna jambo ambalo hulipendi lakini mengine unayapenda unasaini huo mkataba halafu unaweka kitu kinaitwa *reservations* kinachosema kwamba haya siyapendi sitabanwa nayo.

Kwa hiyo, Serikali ilipaswa kama kweli inakataza utesaji ungesaini huo mkataba *with reservations* kwamba sisi tunasaini huu mkataba hatupendi kutesa watu lakini kwenye suala la adhabu ya kifo hatukubaliani nalo. Sasa kuacha kusaini kabisa kunatuma *message* kwamba Serikali hii inaunga mkono mateso, inaunga mkono adhabu za kinyama na vitu kama hivyo. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa yote haya siyo huo Mkataba wa Kkimataifa. Msingi wa yote haya ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 14 haki ya kuishi, Ibara ya 13(vi) nitaisoma Mheshimiwa Mwenyekiti kwa ruhusa yako, najua nina muda mfupi lakini ni vizuri kuisema; "Ni marufuku 13(vi)(e), ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha." Nakubaliana na Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba mkataba ule wa mwaka 1984 na Sheria zetu *Bill of Rights and Duties* Sheria Na. 15 ya mwaka 1984 ni bora zaidi kuliko ule mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ule mkataba utaletwa Bungeni na si lazima, hatukusaini kwa sababu ya adhabu ya kifo. Kwa sababu adhabu ya kifo ina *protocol* yake. Kwa hiyo, unaweza kusaini ule mkataba mwingine lakini hii *protocol* uka-*deal* nayo tofauti. Kwa hiyo, nakubaliana na wewe kwamba tutaleta, hatukuleta kwa sababu tulikuwa tunaifanyia kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilichangia kwa maandishi lakini suala lenyewe ni kwamba mwaka 2009 kwa ushauri wa *IGP* baadhi ya Wabunge wa Mkoa wa Singida, kilikuwa kipindi cha Bajeti, tulikaa na Makamishna Waandamizi watatu kujadili suala la wizi wa mifugo na hasa hasa mifugo iliyopotea mikononi mwa polisi. Sasa Makamishna hawa waliahidi kufanya uchunguzi na kweli walifanya, walikuja mpaka maeneo ya matukio. Lakini taarifa hiyo mpaka leo hatujaipata. Sasa sina hoja kubwa kuhusu taarifa lakini nataka kujua je, wananchi ambao mifugo yao ilipotea mikononi mwa polisi wanaweza kufidiwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufafanua hoja ya Mheshimiwa Lwanji. Mimi ningeshauri kama atanikubalia na nina imani kwamba atanikubalia kwamba nitaipata hiyo ripoti maana yake kweli tulituma watu kule kutazama nini kilitokea na walikutana na wenyeji pale na nimeileta ile ripoti, tutaitazama hiyo ripoti na kuhakikishia na kabla Bunge hili halijaisha tutazungumza mimi na wewe na kama kuna uwezekano hata baada ya Bunge naweza kwenda kule kutegemeana na hiyo ripoti. Lakini nataka kukuhakikishia kwamba usiwe na wasiwasi Mheshimiwa Lwanji ni jambo ambalo tunalo na tutalitazama pamoja na tutatafuta suluhu ya jambo hili tukiwa pamoja kwa niaba ya wananchi wetu. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Ahsante sana Ndugu Mwenyekiti. Mimi katika karatasi yangu kwa Mheshimiwa Waziri niliomba kule Ziwa Tanganyika mwambao ujambazi umezidi sana. Vituo vidogo vya Korongwe na Mkinga wanaporwa watu mali mchana kweupe na majambazi kutoka *DRC* Congo. Pili nyongeza polisi wengi wameuawa katika kipindi kilichopita na vijana wangu wengi mapolisi wa Nkansi waliuawa. Lakini wananchi wa Bunge hawazungumzii polisi kuuawa na majambazi wanazungumzia tu raia kuuawa na majambazi. Hata polisi wameuawa wengi katika nchi hii na majambazi. Kwa hiyo, na ninyi muwadhibiti majambazi. Inaonyesha Wabunge wanawathamini sana majambazi kuliko polisi. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa ufafanuzi katika suala la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba hili suala la ujambazi na matukio mengine ya aina hiyo katika Ziwa Tanganyika ni suala ambalo tunalo na tunalishughulikia. Lakini kama nilivyosema katika jibu nililotoa hapa ni kwamba tunapata *boats* ambazo juzi tumepata *boat* mbili ambazo zipo *Lake Victoria* na tunategemea mwisho wa mwezi Oktoba tutapata boti zingine mbili. Kwa hiyo, tutakapopata ambazo ni *speed boat* na za kufanya *patrol* tutahakikisha kwamba ipi

ambayo itapelekwa kule *Lake Tanganyika* kwa sababu ya kufanya *patrol* na kutazama hali nyingine ya usalama, huo utakuwa ni mwanzo lakini tutaendelea. *(Makofi)*

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Mimi nataka kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri au Naibu wake kuhusu suala la madeni. Kwa kuwa suala hili lilikuja hapa Bungeni na nikauliza swali la nyongeza na kwa bahati njema Waziri mwenyewe Waziri wa Fedha akalichukulia dhamana. Hadi hii leo tunalisisitiza na kutaka kujua ni lini hasa wale askari 300 waliopata uhamisho mwaka 2008 kutoka Zanzibar kuja upande wa pili na wengine ambao wametoka huku kwenda upande wa Zanzibar watalipwa haki zao za uhamisho na haki zao nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa ufafanuzi katika hoja ya Mheshimiwa Sanya, ni kweli hili suala limechukua muda mrefu. Lakini kama tulivyosema hapa hizi pesa zimetoka Hazina kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha hapa tarehe 30 Juni zimetoka Hazina. Lakini kuanza kulipa tumeanza tangu tarehe 15 Julai na hivi wanakwenda Mkoa kwa Mkoa. Nataka nikuhakikishie itakapokuja kufika wiki ya kwanza ya mwezi huu unaokuja nadhani watakuwa wamemaliza katika maeneo mbalimbali.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Wakati nimetoa mchango wangu kwa njia ya maandishi niliipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuandaa mpango kabambe kwa kuwaelimisha kutii sheria pasipo shurti. Sasa napenda kujua Serikali yetu ina mkakati gani sasa kuhakikisha mpango huu unawafikia wananchi kikamilifu walio mjini na vijijini na hata kwetu sisi Wabunge? Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Jeshi letu la polisi limekuwa na huo mkakati wa kuwaelimisha wananchi katika maeneo mbalimbali ya Jamhuri ya Muungano juu ya kutii sheria bila ya kushurutishwa. Jeshi la Polisi limekuwa likienda katika maeneo mbalimbali. Lakini na mimi pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri na sisi tumekuwa tukifanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo. Kwa kupitia Bunge lako Tukufu Waheshimiwa Wabunge nao kama wawakilishi wa wananchi nao wana mchango maalumu katika kupeleka ujumbe huo kwa wananchi.

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge watusaidie tushirikiane ili tuwaelimishe wananchi juu ya jambo hili kwa sababu nchi yetu wananchi wakifuata Sheria, wananchi wakitii mamlaka bila shaka mahusiano kati ya vyombo vya dola na wananchi yataimarishwa. Mahusiano ya vyombo vya dola yakiimarisha nchi yetu itaendelea kuwemo katika amani na amani ikiwepo nchi yetu itaendelea. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia suala zima la wageni ambao wanaingia nchini, lakini hawafuati taratibu kwa ajili ya kupata kibali cha kuishi. Lakini mbaya zaidi wamekuwa wakifanya kazi katika makampuni mbalimbali. Lakini hata wale ambao wanapata fursa ya kupata kibali cha kuishi kinapoisha wanashindwa kufanya utaratibu wa ku-*renew* na moja ya makampuni ambayo yanalalamikiwa ni kampuni ya simu ya *Zantel.* Sasa nilikuwa nataka kujua kwamba je, Serikali inajua tatizo hilo na ina mkakati gani wa kuhakikisha wanalifanyia utatuzi suala hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi katika hoja ya Mheshimiwa Ester Bulaya kama ifuatavyo:-

Kwa kweli taarifa za Shirika kama *Zantel* kwamba ambayo sasa ni *Airtel* kwamba wana mchezo kama huo kwa kweli hatukuwa nao. Taarifa tumeipata baada ya kupata mchango wako wa maandishi, lakini ni jambo tunalifuatilia na kwa kawaida tunapopata taarifa kuhusu makampuni ama kuhusu waajiri ama kuhusu viwanda huwa tunaweka watu kule kwenda kuhakikisha kwamba kitu kama hicho kipo na pahala pengine tumefanikiwa, tumeweza kuwakamata watu kama hawa na kuweza kuwatoa ndani ya nchi na kuwaambia kwamba wanakaa katika nchi visivyo halali na tunapopata habari kama hizi taarifa kama hizi kwa kweli tunazifanyia kazi. Nataka nimwambie Mheshimiwa Ester Bulaya kwamba taarifa zake tumezipata na tutazifanyia kazi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua sera za Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hasa kuhusu viongozi na wananchi wanaopata majanga kutokana na kupambana na majambazi, unywaji wa gongo na bangi. Kule Vunjo kuna janga kubwa lilitokea nadhani sisi tunaita ulinzi shirikishi. Nashukuru *RPC* yule Marehemu na wenzake walifanya kazi nzuri, lakini tukapata athari kubwa sana. Mwenyekiti wangu wa kijiji cha Kiraracha, Andrea Anselem Lekule na ndugu yake Michael Anselem Lekule wale waasi tulikuwa tunapambana nao wakaenda wakachoma nyumba yake, mke wake mpenzi Catherine akafia ndani na mtoto Flora wa miaka sita. Nashukuru *IGP* amehangaika, lakini nilitaka kujua hapa kwamba kuna fungu gani la kumsaidia yule Mwenyekiti kwa sababu sisi tumechangisha shilingi milioni 22 na kweli nyumba mbili tumejenga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zimebaki kama shilingi milioni 16 kumalizia ile *finishing.* Mimi naomba moyo wa huruma na upendo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itafute fedha popote angalau isaidie ile familia ili kujenga *confidence* ya wananchi wa Vunjo kwamba kumbe ukipata janga Serikali inasaidia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza kwa makini Mheshimiwa Mrema, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi wa zamani. Nakubaliana naye kwamba wananchi ambao wanashirikiana na Jeshi la Polisi katika kudumisha ulinzi wa Taifa letu wanapaswa kuenziwa na kusaidiwa hasa wanapopata matatizo.

Nimelisikia na kwa moyo wa huruma tutalichukua jambo hili. Ni wajibu wetu tuwasaidie wenzetu hawa ambao na wao wametusaidia hasa wakati wa shida. Tutalitafakari na tutalichukua, bila shaka tutatafuta njia ya kuweza kusaidia.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi nilihoji ucheleweshwaji na usumbufu mkubwa unaoambatana na fidia kwa wahanga wa ajali mbalimbali pale inapobainika kwamba wanastahili kulipiwa fidia na nilitoa mfano wa ajali ya basi la *Buffalo* iliyotokea mwaka 2007 ambapo baadhi ya wanafunzi walipoteza maisha na ndugu zao bado wanahangaika hadi leo bila mafanikio yoyote. Naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi katika hoja ya Mheshimiwa Martha Umbulla kwamba kwa kweli ninalolisema ni ukweli kabisa. Nimekuja kupata taarifa juu ya kwamba kulikuwepo na wahanga na kulikuwa na masuala ya fidia. Lakini ni jambo ambalo tulikuwa hatujalipata. Lakini nimhakikishie kwa kuwa tumelipata hapa na tutazungumza naye, tutatazama ni jinsi gani tutaweza kumpatia ufumbuzi wa suala hili. Lakini pia kwa niaba ya Wizara na Waziri atufikishie pole zetu kwa wahanga hawa. *(Makofi)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru.

Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajaribu kuchambua hotuba ya Kambi ya Upinzani alisema kazi ya msingi ya Jeshi la Polisi ni kuchukua *commands.* Lakini Waziri pia alipokuwa na yeye anajaribu kufafanua nikamsikia akisema kwamba wale polisi wote wanaohusika na ukatili kwenye vituo vya polisi ama sehemu kadha wa kadha wanapaswa kuchukuliwa hatua. Swali, kwenye hotuba yetu tumesema kwamba polisi wote wadogo wawe makini, wasichukue *command* katili dhidi ya maisha ya mwanadamu. Je, Waziri anatuambia nini kwamba kwa sababu kazi ya polisi ni kuchukua *command,* polisi hao sasa wapo tayari kuchukua *command* yoyote hata kama ni kutesa haki za binadamu?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba si kazi ya Maafisa wa Jeshi la Polisi kupokea *command* katili, si kazi yao. Kazi yao kupokea *lawful order* wanazopewa na viongozi wao. Kwa hiyo, tunasisitiza kwamba wakipewa *lawful order* ni lazima watii kwa mujibu wa mamlaka. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilielezea ni jinsi gani ambapo baadhi ya polisi wamekuwa wanatumia nguvu kupita kawaida wanapotekeleza majukumu yao. Suala linalopekelea wananchi wasiokuwa na hatia kupata majeraha, kupata maumivu, wengine kupoteza maisha na wengine

wanapata ulemavu wa maisha. Naomba kujua kwamba na matokeo mengi yamekuwa yanatokea katika maeneo mbalimbali. Lakini cha kusikitisha ni kwamba sio Waziri, siyo *IGP,* siyo yeyote aliyewahi kusimama hapa Bungeni akakemea matukio haya. Naomba Serikali itoe ufafanuzi hapa Bungeni inatoa kauli gani kwa Watanzania juu ya matukio haya ya askari waliopoteza maadili na kutumia nguvu kupita kawaida wanapotekeleza majukumu yao? Ahsante.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika maelezo yangu ya majumuisho, wakati jeshi la polisi linapotekeleza majukumu yake ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Inawezekana sana wakati mwingine yakatokea madhara watu wakaumizwa na vikasababisha vifo. Lakini kama jambo hilo likitokea nimesema sisi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wenye jukumu la kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Tunalichunguza halafu tukishachunguza tunakusanya taarifa tunazipeleka kwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai.

Sasa yeye kwa taaluma yake, kwa weledi wake anapima hapa askari ametumia nguvu za ziada ama hakutumia nguvu za ziada, amefanya uzembe ama hakufanya uzembe. Akiridhika sasa ndiyo hatua zaidi zinachukuliwa ama huchukuliwa hatua za kinidhamu au kushitakiwa Mahakamani. Bila shaka kauli yangu ni kwamba sisi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tumesema kwamba hatuwezi kutetea mambo maovu, tunatetea mambo ya haki pale ambapo polisi wanatekeleza kazi zao kwa uaminifu na kufuata Sheria.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Kwenye mchango wangu wa maandishi ingawa Mheshimiwa Waziri hakunitaja kwenye orodha ya waliochangia kwa maandishi, niliandika kuwa Wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya ni moja kati ya Wilaya kongwe sana nchini hapa. Wilaya tatu kongwe, lakini kituo cha polisi cha Wilaya ya Chunya hamna. Polisi wamejibana kwenye maofisi machache ya jengo la Mkuu wa Wilaya. Kila mwaka tunaiomba Wizara itusaidie kutenga fedha kwa ajili ya kujenga kituo cha polisi Wilaya ya Chunya. Je, ni lini sasa pamoja na udogo wa sungura, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi Wilaya Chunya?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi au nijibu hoja ya Mheshimiwa Victor Mwambalaswa. Ni kweli ile hoja ya hali halisi katika Wilaya ya Chunya naielewa na tumewahi kuizungumza, lakini tatizo na ningeomba Mheshimiwa Mbunge, atuelewe tatizo ni ile kutoa ahadi ambayo hatuwezi tukaitimiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo katika utaratibu wa fedha ambazo tunazipata tunakwenda awamu kwa awamu katika maeneo mbalimbali ya nchi. Kubwa tu nimhakikishie kwamba hiyo tunayo ipo katika mpango wetu na tutafanya kila jitihada tuone kwamba tunafanya hili ambalo tunaweza kulifanya ili polisi ambao wapo katika Wilaya ya Chunya, wanaweza kupata ofisi na kadhalika.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu ambao nilichangia jana niliongelea jinsi ya ucheleweshaji wa haki za familia za askari ambapo mmoja anafariki, baba au mama akiwa askari; familia ambayo huwa inacheleweshewa haki zake. Nikamtaja huyu Marehemu *PC* Hamad Abeid Omar, mwenye namba *D 947* wa Mkoa wa Kusini Pemba, ambaye alifariki mwaka 2006 mwezi wa kwanza. Mpaka leo familia yake haijapatiwa urithi yaani haki zake. Naomba Mheshimiwa Waziri, anieleze ni lini urithi huo au haki hiyo itapatikana?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijaribu kutoa ufafanuzi kwa kumjibu Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar kuwa ile hoja sisi tumejaribu kuitizama na sijui yeye amecheki lini? Kwa sababu kufuatana na rekodi tulizonazo zinasema ameshalipwa! Itabidi labda sasa tukuoneshe zile rekodi tulizokuwanazo sisi na wewe labda utuoneshe ulizokuwanazo, labda wamemlipa mtu tofauti, lakini rekodi zinaonesha kwamba amekwishalipwa. Lakini hilo lisiwe tatizo ni jambo ambalo tutakutana na tutajaribu kuona tatizo liko wapi. *(Makofi)*

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye mchango wangu wa maandishi nimekuwa nikiulizia ujenzi wa nyumba za asakari pale kwenye Kituo cha Polisi cha

Magomeni. Jambo hili nimelisema kwa muda mrefu, tangu nimeingia Bungeni mwaka 2005, lakini mpaka leo hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa ikiwa ni pamoja na kumuomba Waziri, angalau atembelee akaangalie askari wanavyoishi katika hali duni na ya kusikitisha! Pamoja na kazi kubwa sana na nzuri wanayoifanya. Je, ni lini Serikali itawaonea huruma askari wa Kituo cha Polisi cha Magomeni, kwa kuwajengea nyumba? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Iddi Azzan, ameshanieleza kwamba hali ya nyumba wanazoishi askari polisi Magomeni, zipo katika hali mbaya sana na amenishauri kwamba nifanye ziara maalumu ili nijionee mwenyewe maana *seeing is believing* na mimi nimekubali kwamba nitafanya ziara hiyo, ni wajibu wetu kufanya hivyo na ninamuahidi basi Mwenyezi Mungu akipenda, tukijaliwa, baada ya kumaliza Bunge, nitafanya ziara hiyo. *(Makofi)*

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kikosi cha Zimamoto kimekuwa kikilamikiwa sana kwamba tukio la moto linatokea, watu wanatoa taarifa lakini mara nyingi wanafika wakati tayari madhara yameshatokea. Ningependa kupata kauli ya Waziri, inakuwaje hali hii imekuwa ikijirudia sehemu mbalimbali na mara nyingi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi katika hoja ya Mheshimiwa Regia Mtema, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la Zimamoto ni kweli kwamba wamekuwa wanapata taarifa na kwamba wamekuwa wanachelewa, lakini si jambo ambalo limekuwa linajirudia kote nchini! Wamekuwa wanajitahidi, wamekuwa wanafika sehemu za moto na kwa kweli kuna maeneo ambayo wamefanya kazi kubwa ya kuondosha madhara ya moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimwambie Mheshimiwa Mbunge kuwa kumekuwa na mara kadhaa ambapo wamekuwa wanapata simu za kwamba kuna moto na wamekuwa wanakwenda na wanakuta kwamba hakuna moto! Na hizi zimetokea mara kadhaa katika sehemu nyingi za nchi, lakini hiyo sio sababu! Kubwa ni kwamba hilo tumelichukua tutawahimiza, lakini pia kwa nyenzo ndogo ambazo wamekuwanazo, ndio maana wanatoa *service* kama hiyo ambayo haikuridhishi Mheshimiwa Mbunge, lakini tutafanya kila jitihada kuona kwamba wanakuwa katika *standard* za kuridhisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Muda uliobakia, sasa tunaenda katika utaratibu ule wa *guillotine.* Makatibu, tuendelee.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1001 - *Administration and General ... … …* Shs. 1,601,964,700
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts.... … … … ...* Shs. 259,253,200
Kifungu 1003 - *Policy and Planning… … … … … … …* Shs. 267,086,000
Kifungu 1004 - *Probation and Community Services Division…* ... ... ... ... ... ... ... ...Shs. 1,068,304,000
Kifungu 1005 - *Information, Education and Communication…* ... ... ... ... ... ... ... ... ... Shs. 79,270,000
Kifungu 1006 - *Management Information System Unit..* ... ... ... .... ... ... .... .... .... .... ...Shs. 75,395,000
Kifungu 1007 - *Internal Audit Unit … … … … … … … …*Shs. 109,144,000
Kifungu 1008 - *Procurement Management Unit … …*Shs. 130,063,000
Kifungu 1009 - *Complaints Division … … … … … … …* Shs. 393,742,000
Kifungu 1010 - *Legal Services Division… … … … … … …* Shs. 90,069,000
Kifungu 4001 - *Refugee Unit … … … … … … … … … …* Shs. 590,739,100

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji**

Kifungu 2001 - *Immigration Zanzibar…… ... … … …* Shs. 4,668,658,200
Kifungu 2002 - *Immigration Mainland… … ... … …* Shs. 35,094,333,300
Kifungu 2003 - *Regional Immigration Offices… …* Shs. 11,452,079,800
Kifungu 2004 - *TZ Regional Immigration Training Academy… ... ... ... ... ... ... ...*Shs. 1,991,858,700

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 28 – Polisi**

Kifungu 2001 - *Police Mainforce … … … ... … … …* Shs. 4,227,000,000
Kifungu 2002 - *Police Marine… ... ... ..... … … … … … … ... … …* Shs. 0
Kifungu 2004 - *Police Signals Branch… ... ... .... … … … … … …* Shs. 0
Kifungu 2005 - *Police Zanzibar… … … … … … … … …* Shs. 600,000,000
Kifungu 2006 - *Police Airwing… … … … ... ... … … … … … … …* Shs. 0
Kifungu 2017 - *Police Iringa… … … … … … … … … …* Shs. 750,000,000
Kifungu 2020 - *Police Kagera… … … … … … … … … …* Shs. 500,000,000
Kifungu 2022 - *Police Mwanza… … … … … … … … …* Shs. 500,000,000
Kifungu 2023 - *Police Mara… … … … … … … … … … …*Shs. 500,000,000
Kifungu 2027 - *Police Morogoro… … … … … … … … … … ... ...* Shs. 0
Kifungu 2041 - *Police Dodoma… … … … … … … … …* Shs. 417,169,000
Kifungu 3001 - *Police College Moshi… … … … … ... … … … ...* Shs. 0
Kifungu 3002 - *Police College… … … … … … … … ... … … ... ...* Shs. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 29 – Magereza**

Kifungu 1001 - *Prisons Headquarters … … … … ... …* Shs. 1,000,000,000
Kifungu 2002 - *Prisons Welfare and Rehabilitation*... Shs. 341,145,000
Kifungu 4001 - *Prison Building Brigade… … … … … …*Shs. 1,200,000,000
Kifungu 4002 - *Prison Industries… … … … … … … … …* Shs. 800,000,000
Kifungu 4003 - *Prisons farms… … … … … … … … …* Shs. 1,222,067,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1001 - *Administration and General… … ... … … … ... ...* Shs. 0
Kifungu 1003 - *Policy and Planning… … … … … … …* Shs. 1,000,000,000
Kifungu 4001 - *Refugee Unit … … … … … … … … …* Shs. 1,199,400,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji**

Kifungu 2002 - *Immigration Mainland… ... … … …* Shs. 26,808,667,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mheshimiwa Waziri, Taarifa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali na kuyapitisha makadirio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Bunge hili limepitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha ujao. Naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa niaba ya Bunge zima na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kazi kubwa mliyofanya humu ndani. Mheshimiwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, viongozi wetu wote wa Majeshi chini ya Wizara hii, tunawapongezeni sana kwa kazi nzuri, tunawatakia kila la heri katika mwaka ujao wa fedha na tunaamini mtaendelea kuwatumikia Watanzania vizuri kama ambavyo ni kawaida yenu. *(Makofi)*

Nina matangazo mawili, la kwanza ni Waheshimiwa Wabunge, hata kama tungeendelea na wakati ule wa kipindi kile cha Kamati ya Matumizi, tusingefika popote sana kwa sababu tulikuwa na Wabunge karibu 60 waliokuwa wamesimama na tulivyojitahidi tumeweza angalau kuwasikiliza 22, kwa hiyo hata kama tungeongeza muda wa nusu saa bado kuna wengine ambao kwa vyovyote vile wangebaki tu; kwa hiyo, tusameheane. Tungeanza kwa utaratibu ule wa mwanzo nina hakika kila mmoja wetu angepata fursa. *(Makofi)*

Tangazo la pili na la mwisho ni kwamba Mheshimiwa Godfrey Zambi anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote, walioombwa kuchangia mchango kutoka kwa vijana wa *Moravian* Mbeya, Usharika wa Mbeya Mjini ambao walitambulishwa na mimi hapa asubuhi, wanapenda kuwakaribisha Wabunge wote keshokutwa siku ya Jumapili katika tamasha la muziki wa injili litakalofanyika katika ukumbi wa Kilimani. Keshokutwa, Jumapili, tarehe 31 mwezi wa saba, kuanzia saa 7.00 mchana. Madhumuni ya tamasha hilo ni kukusanya mchango kwa ajili ya kujenga hosteli kwa ajili, ya watoto yatima, kwa hiyo, Wabunge wote mnakaribishwa Kilimani, tarehe 31 Julai, 2011. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, kwa kuwa shughuli zilizopangwa kwa siku ya leo katika *Order Paper* zimekamilika, naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi Jumatatu, terehe 1 Agosti, 2011 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.13 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, Tarehe 1 Agosti, 2011 Saa 3.00 asubuhi)*